Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Pili – Tarehe 7 Mei, 2014**

*(Mkutano Uilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):**

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2013 [*The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Financial Statement of Local Government Authorities for the Financial Year ended 30$^{th}$ June, 2013*].

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. N. MADELU):**

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuu kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2013 *[The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Financial Statement of the Central Government for the Year ended 30$^{th}$ June, 2013]*

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2013 [*The Annual General Report of the Controller and Auditor*

*General on the Audit of the Financial Statement of Donor Funded Project for the Financial Year ended 30th June, 2013]*.

Ripoti ya jumla ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi Maalum kwa kipindi kilichoishia tarehe 31 Machi 2014, *[The General Report on the Performance and Specialized Audits for the period ended 31 March 2014]*.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia mwaka 2012/2013 *[The General Report on the Audit of Public Authorities and other Bodies for the Financial Year ended 2012/2013]*.

*A study on cost control in the Public Procurement (A case study of Air Ticketing and Construction of Buildings) March 2014*.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Usimamizi wa Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu kwa kipindi kinachoishia Desemba, 2013 *[A Performance Audit Report on the Management of Wildlife in Game Reserves and Game Controlled Areas December, 2013]*.

**NAIBU WAZIRI WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII:**

*Performance Audit on the Management of Food Inspection and Surveillance at Processing Plants and at Ports of entry March 2014*.

*The Performance Audit Report on the Management of Identification and Provision of Services to most vulnerable children in Tanzania on December, 2013.*

*The Performance Audit Report on the Management of Health Care Waste March 2014*.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi na Usimamizi wa Ukaguzi wa Bidhaa Zinazoingia Nchini ya Machi, 2014 [*A Performance Audit Report and the Management of Inspection Of Imported Goods in Tanzania March, 2014]*.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge kama mtakavyoona hizi taarifa ni nyingi mtazikuta kwenye *pigeon holes* zenu. Mtumie nafasi kuweza kusoma kwa sababu zitawasaidia watu kujua nini kinachoendelea katika zile taarifa. Kwa hiyo, zipo nyingi sana na zitakuwa kwenye *pigeon* zenu.

Katibu tuendelee!

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Tunaanza maswali kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu na swali la kwanza litaulizwa na Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa.

Na. 10

**Usimamiaji wa Ugawaji Chakula kwa Mikoa yenye Njaa Nchini**

**MHE. MARIA I. HEWA** aliuliza:-

Tatizo la njaa limekuwa ni kilio cha Wabunge wengi katika Bunge hili la Kumi:

Je, ugawaji wa chakula kwenye Mikoa yenye njaa ulisimamiwaje?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa ikikumbwa na janga la mara kwa mara mathalan, kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2006 mpaka mwaka 2014, Serikali imetoa na kusimamia ugawaji wa jumla wa tani 406,571.13 za chakula zenye thamani ya sh. 163,636,538,300/=. Chakula hiki kilitolewa kwa waathirika katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Pwani, Morogoro, Iringa, Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Mara, Manyara, Mbeya, Kagera, Mtwara na Lindi ambayo ilikumbwa na ukame. Aidha, jumla ya Sh. 27,138,170,002.49 zimetolewa kwa ajili ya usafirishaji wa chakula hicho toka ghala la hifadhi hadi kwa walengwa. Ugawaji wa chakula umekuwa ukitolewa kwa kufuata mwongozo wa ugawaji wa chakula ambao ndio nyenzo ya kuhakikisha chakula kinatolewa kwa walengwa na kwa kufuata utaratibu maalum ambao unazingatia mahitaji ya makundi mbalimbali. Idadi ya Uratibu wa Maafa ina utaratibu wa kuanisha vijiji na idadi ya waathirika wanaostahili kupewa chakula hicho kulingana na matokeo ya tathmini zinazofanywa na taasisi/mamlaka mbalimbali ikiwa ni pamoja na Halmashauri au Sekretrieti za Mikoa. Halmashauri hupewa takwimu hizo za waathirika kabla ya zoezi la usambazaji wa chakula kufanyika ili zitumike katika mgao wa chakula hicho kwa kufuata mwongozo huu wa ugawaji wa chakula. Aidha, Idara ya Uratibu wa Maafa

inafanya ufuatiliaji kuhakikisha mwongozo unafuatwa na chakula kinawafikia walengwa katika kiwango sahihi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa swali la nyongeza.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Ahsante. Nina maswali mawili tu mafupi ya nyongeza. La kwanza, Kusini mwa nchi yetu Tanzania wanazalisha vyakula vingi sana katika Mikoa kama minne hivi, wanajiita *big four* mpaka wanavichezea vyakula hivi. Kwa nini Serikali isiwe na dhamira thabiti kabisa ya kwamba baada ya kufika wakati wa manunuzi ya chakula hiki kikanunuliwa mapema kabla ya watu wa Kusini hawajaanza kuhangaika na soko la chakula hiki?

Mheshimiwa Spika, la pili, Wilaya ya Kwimba eneo la Nkalalo huwa kuna eneo ambalo ndani ya Bunge hili Waziri wa kilimo huwa anahaidi kujenga ghala kwa maana ya Kanda ya Kaskazini. Je, hii ahadi itatimizwa lini katika eneo hilo la Nkalalo Kwimba ili na wananchi wa eneo lile wawe na eneo fupi la kuweza kupata chakula hiki cha njaa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika majibu!

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Ibeshi Hewa kama ifuatavyo:-

Kuhusu uzalishaji wa chakula ni kweli Mikoa hiyo imezalisha chakula cha kutosha na mwaka huu kwa kweli kwa mara ya kwanza tumenunua chakula mapema zaidi, maana yake Serikali ilitoa hela kufuatia Bunge hili kuidhinisha hela mapema kuanzia Januari tulianza kununua mahindi na mpaka mwisho wa msimu tulikuwa tumeshanunua tani 218,000.

Mheshimiwa Spika, lakini ni kwamba, isingewezekana kuendelea kununua mahindi yote yaliyozalishwa kwa sababu Hifadhi ya Taifa kazi yake ni kununua tu chakula kwa ajili ya hifadhi. Kwa kweli mwaka huu tumejitahidi na hivi sasa tunavyozungumza tunacho chakula cha kutosha katika Hifadhi ya Taifa. Tatizo ni kwamba mahindi ni mengi na tunachokifanya sasa tunaruhusu wananchi na wafanyabiashara kuuza mahindi yao ndani na nje ya nchi bila vikwazo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ghala la Kwimba, mimi mwenyewe nimekwenda kutembelea kule nimekwishaliona. Tunachokifanya mtaona baadaye katika hotuba yangu nitakayoitoa Serikali imejipanga kuanza kukarabati na kujenga maghala mengi katika nchi hii na kuweka mtawanyiko mzuri wa maghala ili yaweze kuhudumia wananchi. Kwa hiyo, hata hili la Kwimba nalo tutalifanyia utaratibu tulitazame.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Shekifu!

**MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja. Ni utaratibu wa kawaida kwamba maeneo yenye njaa yanaangaliwa mapema na yanajulikana. Je, Serikali inajua kwamba upo urasimu mkubwa sana wa kukipeleka chakula hiki katika maeneo yanayohitajika na inafikia mahali kwamba chakula kinapelekwa wakati tayari watu wamekwishaathirika na idadi ya watu wanaongezeka kila kinapopelekwa chakula. Je, Serikali inalitambua hili na kuna tatizo gani la urasimu mkubwa wa kugawa chakula hiki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu!

**NAIBU WAZIRI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa Sheria iliyopo ndiyo inayosababisha urasimu. Sisi kama Serikali tumeiona ile Sheria na sasa tunahangaika nayo ili tuje tufanye marekebisho hapa kwa sababu ni kweli kwamba maafa yakitokea huko lazima Wilaya iainishe, hata kama wakiainisha kwa namna gani, yakifika huku Makao Makuu kwa mujibu wa Sheria, lazima ile Kamati ya Maafa ikae ambayo Mwenyekiti wake ni Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu na Makatibu Wakuu wenzake na sisi wengine sio Wajumbe, wazungumze, waainishe, waidhinishe zile fedha zinazotakiwa na chakula kile kilichoombwa ndipo wapeleke mahitaji Wizara ya Kilimo, nayoe ijipange kusafirisha ili kupeleka katika maeneo hayo.

Lakini Hazina walete tena pesa, Ofisi ya Waziri Mkuu na Waziri Mkuu apeleke fedha kule kwenye maeneo yanayohusika kwa ajili ya usambazaji. Kwa hiyo, kuhusu urasimu ni kweli nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Shekifu kwamba utaratibu mzima wa kushughulikia maafa wala siyo ya chakula tu na njaa. Utaratibu mzima wa kushughulikia maafa una urasimu lakini urasimu huu umejengwa ndani ya Sheria. Kwa hiyo, kinachofanyika sasa tunataka kuandaa Sheria mpya ili tuipitie kwa sababu tumepata uzoefu wa kutosha ili tuweze kuweka Sheria ambayo haitakuwa na urasimu kwa sababu hatuwezi ku-*treat* maafa kwa urasimu wa Sheria iliyopo.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere.

Na. 11

**Uzinduzi wa Mradi wa Maji Mahiga**

**MHE. LETICIA M. NYERERE** aliuliza:-

Hivi karibuni Mheshimiwa Waziri Mkuu alitembelea Jimbo la Kwimba na kuzindua Mradi wa Maji wa Mahiga;

Je, mradi huo umefikia hatua gani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa Bwawa la umwagiliaji Mahiga unafanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba kwa ajili ya kilimo cha Mpunga sawa na eneo la hekta 300. Ujenzi wa mradi huu ulianza mwezi Agosti, 2010 ambapo ulitarajiwa kukamilika kwa muda wa miezi kumi kwa gharama ya shilingi bilioni 1.985. Utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 90 na gharama zilizotumika ni bilioni 1.47.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizofanyika na kukamilika ni ujenzi wa tuta na ujenzi wa mita 400 za mtaro. Katika bajeti ya mwaka 2013/2014, kazi zinazoendelea ni ujenzi wa mita 225 za mtaro, kulaza mawe ndani ya tuta na kukamilisha mtaro wa maji. Aidha, kwa sehemu ambazo mradi umekamilika wananchi wapatao 195 wameanza kilimo cha umwagiliaji katika eneo la hekta 200. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2014. Mradi ukikamilika utawezesha, upatikanaji wa maji ya uhakika kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji pamoja na shughuli nyingine za kunyweshea mifugo na kuanzisha sekta ya ufugaji wa samaki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Leticia Nyerere, swali la nyongeza!

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake.

Mheshimiwa Spika, mwaka juzi nilimpelekea Mheshimiwa Waziri Mkuu ombi maalum kwa ajili ya mradi huu wa Mahiga. Nampongeza na namshukuru kwa utekelezaji wake mzuri alioufanya na ndiyo maana mradi huu umefikia hatua hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa mradi huu wa Mahiga kwamba, mradi huu utakapokamilika wananchi wa Kwimba sasa tutaondokana na utegemezi wa chakula cha msaada. Kwa sababu hiyo basi, wananchi wa Kwimba wameniomba nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu atuzindulie mradi mwingine kama huo maeneo ya Kiliaboya na baada ya kufanya hivyo atapewa tuzo itakayoitwa *N'zagamba Makoba* maana yake ni tegemeo la kila mtu. Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa tayari kutuzindulia

huo mradi ili hatimaye sisi wananchi wa Kwimba tumkabidhi hiyo tuzo inayoitwa *N'zagamba Makoba*?

Swali la pili, je, Mheshimiwa Waziri Mkuu atakuwa tayari kufuatana na mimi baada ya kikao hiki ili twende tukayabaini maeneo niliyoyataja likiwemo Kiliaboya na Ilumba?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Shughuli hapa! Tuzo inaanza kabla hujafanya kazi, tuendelee. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, Wabunge wote watatu Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mheshimiwa Mansoor, Mheshimiwa Richard Ndassa wamekuwa wakifuatilia miradi hii kwa karibu sana na napenda kuwapongeza kwa kazi nzuri wanayoifanya, hilo ni jambo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, lakini kama mmesikiliza Waziri Mkuu jana alipokuwa anatoa hotuba hapa na Mheshimiwa Hawa Ghasia, kiongozi wetu katika Wizara, anazungumza kitu kinachoitwa Fursa na Vikwazo, *Opportunities and Obstacles to Development (O&OD)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida miradi hii yote anayoizungumza Mheshimiwa Leticia, inapoanza huwa inaanza na wananchi kutoka kule chini kwenye Kitongoji inakwenda kwenye Kijiji mpaka kwenye Kata. Nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, huu mradi wa pili anaoutaja hapa kama utafuata utaratibu huo kwa maana ya kwamba utakuwa umependekezwa na ukaja ukafuata hatua hizo zote, sisi kama Ofisi ya Waziri Mkuu hatuna tatizo na hilo, lakini uzingatie huu utaratibu unaosema wa fursa na vikwazo na sisi tutaendelea kushirikiana naye.

Mheshimiwa Spika, swali la pili analoliuliza hapa, ratiba ya Waziri Mkuu haipo hivyo kama anavyotaka kuiweka, siwezi kujibu hapa sasa hivi nikasema ndiyo. Nikitoka hapa huyu Mzee ananiuliza bwana wewe nimekusikia umesema mimi nitakwenda kule. Kwa hiyo, ni utaratibu maalum, lakini nataka nimhakikishie kwamba nitafikisha ombi hili kwake ili sasa Waziri Mkuu aone atakavyofanya kwa kadri itakavyompendeza.

**SPIKA:** Alivyoomba ni vizito. Mheshimiwa Susan Lyimo kwa kifupi tafadhali!

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Ni ukweli ulio wazi kwamba maji ni uhai na nashukuru kwamba kumekuwa na miradi mingi, lakini pia miradi mingi ya maji bado haitekelezwi na naomba kujua kule Moshi Vijijini, Kijiji cha Korini Kusini, mradi wa maji ilikuwa uzinduliwe toka mwezi wa Nane, mwaka jana na Naibu Waziri aliyekuwepo analijua hii, lakini mpaka leo ninavyoongea bado mradi huo haujazinduliwa na hakuna dalili na wananchi wanalalamika sana kwa sababu wameshafanya kila kitu, wameshachangia, pia Serikali imeshachangia lakini mradi huo haujazinduliwa.

Naomba tamko kutoka kwa Serikali ni lini huu utazinduliwa ili wananchi wa vijiji vya Korini Kusini waweze kupata maji kama ambavyo waliahidiwa mwaka juzi?

**SPIKA:** Swali lako ni *very specific*, maswali ya nyongeza yanatakiwa yawe ni *general* ya sera, lakini kwa sababu mnajuana ujibu na swali hili Mheshimiwa Susan anauliza mara zote akisimama.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli unavyosema tunajuana, kwa sababu hata Azimio la Umwagiliaji lilipitia Moshi, yaani azimio lote la utaratibu wa kumwagilia ni Azimio ambalo lilitokea Moshi. Mradi huu anaouzungumza Mheshimiwa Susan naufahamu, ni kweli kwamba haujazinduliwa, lakini kazi hii tunaifanya sisi pamoja na wenzetu Mheshimiwa Chiza na wenzake Wizara ya Kilimo na masuala ya *Irrigation* yapo kwao.

Naomba nimthibitishie Mbunge kwamba, nitawasiliana na Mheshimiwa Waziri na bahati nzuri wamo humu ndani wanasikia ili basi tuweze kuweka utaratibu wa kuweza kuzindua na kuona kwamba ni Kiongozi gani atakayefanya kazi hiyo.

**SPIKA:** Ahsante. Wakati ni ukuta, kwa hiyo, nakwenda na *speed* kwa sababu nataka saa nne tuwe tumemaliza maswali yote, muda hautoshi leo. Tunakwenda Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Kabati atauliza swali linalohusika.

Na. 12

**Matumizi ya Mashine za Kielekitroniki (EFD)**

**MHE. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Mfumo wa kutumia mashine za kielekitroniki (*EFD*) ni mpya katika nchi yetu na bado haujaeleweka vizuri kwa wafanyabiashara wetu na ndio maana

kumekuwa na migomo ya wafanyabiashara kwenye baadhi ya maeneo nchini:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kutoa elimu ya kutosha kwa walengwa kabla ya kuanza kutumia mashine hizo?

(b) Kwa kuzingatia malalamiko ya wafanyabiashara juu ya bei za mashine hizo; je, kwa nini Serikali isiwe na mpango wa makusudi wa kupunguza bei ya mashine hizo au kutoa ruzuku katika ununuzi ili wafanyabiashara wa hali zote waweze kununua bila kuathiri mitaji yao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. M. NCHEMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mungu na namshukuru Mheshimiwa Rais kwa fursa hii na nawaahidi tu vijana wa Tanzania kwamba sitawaangusha.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mfumo wa kutumia mashine za kieletroniki za kutolea risiti (*EFD*) ulianza rasmi hapa nchini mwezi Julai, mwaka 2010 ukitekelezwa kwa awamu. Katika kuanzisha mfumo huu Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* ilianza kwa kutoa elimu kwa wafanyabiashara waliolengwa kwa kutumia mfumo huu katika awamu ya kwanza ambao walikuwa ni wafanyabiashara waliosajiliwa katika kulipa kodi ya ongezeko la thamani *(VAT)*. *TRA* pia ilitoa elimu kabla ya kuanza awamu ya pili inayowahusu wafanyabiashara waliosajiliwa kwa mfumo wa *VAT*, wenye biashara zilizo rasmi zenye mzunguko wa mauzo (*turnover)* kati ya shilingi milioni kumi na nne na milioni thelathini na tisa (milioni 14-milioni 39) kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili ilipangwa kuanza rasmi tarehe 1 Oktoba, 2013. Baada ya watumiaji kuonesha kuwa walihitaji elimu zaidi, tarehe ya kuanza rasmi ilisogezwa mbele mpaka tarehe 31 Januari, 2014. Katika kipindi chote hiki, *TRA* imeendelea kutoa elimu kwa wafanyabiashara kwa kutumia njia mbalimbali kama vile semina, runinga, redio, machapisho mbalimbali pamoja na semina za ujumla, makundi mbalimbali yenye biashara zinazofanana yaliwekwa pamoja na kuelimishwa katika kila Mkoa na Wilaya. Aidha, watumiaji hupata pia mafunzo ya kina kwa kutumia mashine kutoka kwa msambazaji mara anapoinunua. Elimu hii ni endelevu, kutoka *TRA* na kwa wauzaji mashine.

(b) Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara kuhusu bei ya mashine za *EFDs*. Serikali imeyafanyia kazi

malalamiko hayo na hivyo kushusha bei za mashine kutoka shilingi kati ya 600,000/= na 800,000/= za awali hadi kufikia shilingi kati ya 600,000/= na 690,000/= kulingana na aina ya mashine.

Mheshimiwa Spika, ili kuleta unafuu zaidi, Serikali kupitia Bunge lako Tukufu imeondoa kodi ya *VAT* kwenye ununuzi wa mashine za *EFDs*. Aidha, kuanzia Julai Mosi, Serikali itaanza kutoza kiwango cha ushuru wa forodha cha asilimia sifuri kwenye uingizaji wa mashine hizi, hatua ambayo itapunguza bei zaidi ukilinganisha na bei za awali.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa nafasi aliyoipata kwa sababu leo ndiyo siku yake ya kwanza kujibu maswali yetu. Vile vile nimpongeze kwa majibu ambayo ametupatia, lakini naomba nimuulize maswali madogo mawili.

Kwa kuwa, mashine hizi za *EFDs* zimekuwa zikilalamikiwa sana na wafanyabiashara wadogo wadogo karibu nchi nzima kwa kuwa na gharama kubwa na kwa kuwa, kuwauzia wafanyabiashara wenye mitaji midogo ni kuua mitaji yao. Kwa nini Serikali isiweke utaratibu wa kuwakopesha ama kuwapatia bure ili kukuza mitaji ya biashara zao na kupata kodi kubwa zaidi?

Swali la pili, kwa nini Serikali isiruhusu wafanyabiashara kununua mashine hizi za *EFDs* popote zinapopatikana ili mradi zinakidhi viwango badala ya kulazimisha kununua mashine hizo kutoka kwa Mawakala wa TRA?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. M. NCHEMBA)** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Ritta Kabati kwa *concern* yake kwa wafanyabishara hasa wa Iringa Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme, suala alilosema la kuwakopesha, utaratibu unaotumiwa na Serikali kwa namna moja ni kama kuwakopesha kwa sababu gani? Utaratibu uliowekwa tulisema kwamba kama mfanyabiashara atanunua mashine hii na akaitumia, mathalani kama amenunua kwa shilingi laki sita atakapoitumia watakapokwenda ku-*calculate* kodi yake mwisho wa mwaka, atarudishiwa kwanza gharama aliyotumia kununulia mashine ile.

Kwa hiyo, kama atakuwa amenunua kwa bei kubwa kuliko ile kodi yake, maana yake atakata gharama ya mwaka huu anayotakiwa kulipa kodi na mwaka unaofuata atakata tena. Utaratibu uliotumika ni vile tu kwamba, tuna ufinyu wa bajeti, Serikali ikaona ni vema wakanunua kwanza halafu wakarudisha kupitia kwenye kodi ili tusiharibu fedha ambazo zingekwenda kutoa huduma sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili alilosema kuhusu kuwaruhusu wanunue popote, hili ni jambo ambalo lingeweza kufanyika, lakini mamlaka ya mapato pamoja na Wizara ilizingatia uhitaji wa mashine hizi. Mashine hizi ni tofauti na *calculator* ambazo unaweza ukawa na *varieties* na bado zikatoa majibu yale yale. Mashine hizi zinakuwa *programmed* ili kuweza kufikia lengo lililokusudiwa. Kwa hiyo, kuweka utaratibu wa kuagiza kwa pamoja tuliona zitaweza kufikia lile lengo kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, pili, katika utaratibu wa kisasa ukiacha wafanyabishara milioni moja na nusu mpaka milioni mbili kila mmoja akaifuata Dubai, utaratibu mpaka ukamilike ungechukua muda mrefu zaidi. Pia kuleta kwa pamoja kuliwezesha watu wanaosambaza kupewa kazi ya kufundisha, vilevile kutengeneza punde zinapoharibika.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Swali langu limeshaulizwa na Mheshimiwa Ritta na nimeridhika na jawabu.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Spika nashukuru. Naomba kuuliza swali lingine la nyongeza kuhusiana na hizi mashine za *EFDs*. Tumesikia majibu ya Naibu Waziri, lakini swali langu ni moja kwamba, ni kwa nini kwa sababu ukiangalia nchi za nje ambako mashine za *EFDs* zimechukuliwa kwa mfano kama China, gharama yake ni kati ya dola hamsini mpaka dola mia moja, lakini zinapokuja nchini wafanyabiashara wanauziwa kwa shilingi laki sita mpaka wengine shilingi laki nane. Kwa nini Serikali ama Wizara isingenunua au kuziagiza yenyewe, halafu ikazitoa kwa wafanyabiashara kwa bei ndogo zaidi tofauti na zinapochukuliwa nje na wafanyabiashara na wale wafanyabiashara wanakuja kuziuza kwa wafanyabiashara wetu kwa gharama kubwa zaidi kwa sababu ya kutengeneza faida? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU L. M. NCHEMBA)** Mheshimiwa Spika, hiki anachokisema Mbunge ni kitu ambacho kingewezekana, lakini kwa upande wa bei ni tofauti na maeneo mengine kufuatana na mahitaji. Kama tulivyosema mashine za aina hii ambazo zingeweza kutoa risiti peke yake, bei yake ingewezakuwa tofauti, lakini mashine hizi kwa jinsi zilivyotengenezwa, mahitaji yake ni mengi. Kwanza, utunzaji wa kumbukumbu zake ni mkubwa, lakini vile vile zina uwezo wa kufanya mawasiliano kwa *sms* ya Mamlaka ya Mapato pamoja na mtumiaji.

Vilevile zina uwezo mkubwa wa kutunza kumbukumbu ambazo zitamsaidia hata mfanyabiashara kupunguza gharama ambazo angezitumia kwa risiti.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kwa nini Serikali isingefanya yenyewe, unatambua kwamba Serikali haifanyi biashara na utaratibu wa kisasa duniani kote ni namna ya kugawa kazi zifanywe na watu, lakini kwa utaratibu ambao tumeuweka wa Sheria za Manunuzi. Kuhusu namna ya kushusha bei nimetoka tu kuielezea hapa ambazo ni hatua zinazochukuliwa na Serikali za kikodi, lakini vile vile za kuwabana wauzaji ili waweze kuwauzia wafanyabiashara kwa bei ambayo ni nafuu kwa ajili ya kuweza kuleta tija.

**SPIKA:** Swali linalofuata Mheshimiwa Maida, hapana kwanza Mheshimiwa Waziri wa Fedha!

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nampongeza sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ya ufasaha kabisa.

Mheshimiwa Spika, kuongezea tu hili swali la mwisho, utaratibu ambao tumeufanya katika ku-*acquire* hizi mashine za *EFDs* ilikuwa ni kutazama pale ambapo mashine hizi zitakuwa *compatible* na mifumo yote ya kwetu hapa Tanzania. Hivyo mifumo hii kutokana na *TRA, EWURA, SUMATRA* kwa sababu yote sasa baadaye tutaingia katika kuiweka pamoja hii mfumo iwe inazungumza kwa mfanyabiashara kwa sababu hatutakwenda tu kwa mfanyabishara yule ambaye anauza biashara, lakini kwenye vituo vya mafuta, hivyo itabidi lazima tuunganishe na *EWURA* na vitu vingine kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mashine za Tanzania siyo zile ambazo unaweza ukaenda China ukanunua kwa dola hamsini ukaja nayo, *these are so special* na Serikali inajua umuhimu wa mashine hizi na najua kwamba wafanyabiashara watapata faida. Ndiyo maana kama Naibu Waziri alivyoeleza kwamba, tupo katika hatua mbalimbali za kuhakikisha kwamba bei ya mashine inapungua na mfanyabiashara awe anaimiliki kama vile anavyomiliki kalamu yake na karatasi na vitu vingine kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, hilo linatambulika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Naomba tuendelee na swali linalofuata Mheshimiwa Maida Hamadi Abdallah, kwa niaba yake Mheshimiwa Sereweji!

Na.13

**Pato la Siku kwa kila Mtanzania**

**MHE. JUMA HAJI SEREWEJI (K.n.y. MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH)** aliuliza:-

Katika Bajeti ya mwaka 2013/2014, Serikali ilitumia vigezo kwa pato la kila Mtanzania kufikia sh. 1,025,038/= kwa siku kutokana na Takwimu za Sense ya Watu na Makazi za mwaka 2012:-

Je, Serikali ilitumia vigezo gani kiuchumi na kuona kwamba wananchi wa Tanzania wanapata pato hilo kwa kila siku?

**MHE. JUMA HAJI SEREWEJI (K.n.y. MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Maida anaomba swali lake lifutwe kwa sababu ni swali la zamani na limepitwa na wakati.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Nashukuru tunaendelea na swali linalofuata Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali.

Na. 14

**Ujenzi wa Soko la Kimataifa Mkalazi**

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI** aliuliza:-

Mwaka 2011 Serikali iliahidi kujenga Soko la Kimataifa mpakani katika Kijiji cha Mkalazi (Mabamba):-

(a) Je, ujenzi wa soko hilo utaanza na kukamilika lini?
(b) Je, Serikali inachukua hatua gani ili ujenzi uanze mara moja?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunifikisha hapa nilipo. Namshukuru pia Rais kwa kunibadilisha kituo, hili ni swali langu la kwanza katika Wizara hii, namwomba Mwenyezi Mungu anisaidie.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mbunge wa Muhambwe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa mwaka 2011 Serikali iliahidi kujenga soko la Kimataifa mpakani kati ya Tanzania na Burundi katika Kijiji cha Mkalazi, Mabamba. Katika kufanikisha azma hiyo Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo kwa kushirikiana na wananchi wa Kijiji cha Mkalazi wametenga eneo la ekari 149.7 litakalotumika kujenga soko hilo.

Soko hilo mpaka kukamilika kwake limekadiriwa kugharimu shilingi bilioni 2.4, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 2.1 ni mkopo kutoka Benki ya Rasilimali ya Tanzania (*TIB*) na shilingi milioni mia mbili arobaini na moja ni mchango wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo.

Mheshimiwa Spika, kigezo kimojawapo kitakachotumika kwa Benki ya Rasilimali (*TIB*) kuidhinisha mkopo kwa ajili ya ujenzi wa soko hilo ni hati miliki ya ardhi ya eneo husika. Mpaka sasa eneo limepimwa na michoro imekwishapelekwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ajili ya kupatiwa hati miliki. Aidha, mpango wa biashara (*business plan)* na ramani ya soko vilikwishawasilishwa *TIB* kwa ajili ya hatua zaidi ya kupata mkopo.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa ujenzi wa soko unaharakishwa, Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo inafuatilia hatua kwa hatua mchakato wa upatikanaji wa mkopo huo na kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Halmashauri imetenga shilingi milioni 120 ikiwa ni malipo ya awali kwa *TIB* kwa lengo la kumpata Mshauri Elekezi atakayeandika mpango wa biashara mahsusi na mtalaam atakayesimamia ujenzi wa soko hilo.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika nakushukuru. Nina maswali mawili lakini kwa urahisi kwa sababu swali la kwanza niliuliza ujenzi huu utaanza lini na kukamilika lini, kwa hiyo Waziri kama alikuwa hajui kwamba ujenzi huu utaanza lini na kukamilika lini, angenijibu tu kwamba Serikali haijui ujenzi utaanza lini na kukamilika, ndiyo ustaarabu kuliko kuandika maneno mengi, halafu unaliacha swali pembeni. Sasa naomba arudi kujibu hapa kama nilivyouliza kwenye swali ujenzi unaanza lini na kukamilika lini, ndiyo swali namba moja na ndiyo ustaarabu.

Mheshimiwa Spika, namba mbili, swali hili nililiuliza mwaka 2011 ndani ya Bunge hili na nikajibiwa kwamba kuna hatua na mchakato wa upatikanaji wa mkopo na nini unaendelea, sasa leo nimeuliza hatua gani zinachukuliwa ujenzi uanze mara moja, nimejibiwa vilevile kama mwaka 2011. Sasa nataka arudie kujibu swali la (b) tena kwamba Serikali inachukua hatua gani ili ujenzi uanze mara moja, hajajibu!

Mheshimiwa Spika, sijaona hili jibu, sijui kama wewe Spika, umeliona nakushukuru. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Nimeliona, nimeona kwamba kuna mchakato wa benki na vitu kama hivyo, Mheshimiwa Naibu Waziri ujibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Mkosamali kistaarabu kuwa mchakato huu ukimalizika, kwanza hati ikipatikana ili Benki ya Rasilimali itoe pesa ndipo ujenzi utakapoanza.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa hiyo ukasaidie kupata hati. Mheshimiwa Ntukamazina!

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kama ilivyo kwa Kibondo, katika bajeti ya mwaka jana Waziri wa Viwanda na Biashara aliahidi kwamba Serikali ingejenga soko la mpakani la Murusagamba ambako kuna biashara kubwa kati ya Warundi na wananchi wetu. Je, soko hilo litajengwa lini?

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. Hilo ni swali jipya kwa kweli. Kwa hiyo, kama wewe hujafika huko na ni mara yako ya kwanza unaweza kushindwa kujibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, hilo soko analolitamka sina taarifa kamili hapa. Nitalifanyia kazi na nitarudi kumpa jibu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante, tunaendelea na swali linalofuata. Mheshimiwa Herbert James Mntangi atauliza swali hilo.

Na. 15

**Kiwanda cha Usindikaji Matunda-Muheza**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kikundi cha Ushirika Muheza kilimiliki na kuendesha Kiwanda Kidogo cha Usindikaji wa Matunda, lakini sasa kimekosa uwezo wa kukiendesha kiwanda hicho.

(a) Je, Serikali inatoa ushauri gani na msaada gani ili wananchi wa kikundi hicho waweze kuendesha kiwanda hicho?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia Wilaya ya Muheza kupata mwekezaji wa Kiwanda cha Usindikaji wa Matunda?

**SPIKA:** Wizara ya Viwanda swali linalofuata. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda swali linalofuata ni la kwako swali namba 15 limeulizwa na Mheshimiwa James Herbert Mntangi. Unayo majibu huna?

**WABUNGE FULANI:** Aaa ni namba 15. *(Makofi)*

Mkosamali umeuliza maswali magumu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Samahani sana Mheshimiwa Mkosamali kanichanganya kidogo, kanichangamsha kidogo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ili kikundi cha Ushirika cha Muheza kiweze kupata msaada na ushauri unaotakiwa, Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara itatuma wataalam mwanzoni mwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, kwa lengo la kubaini uwezo wa kiwanda husika na changamoto zilizopo na hatimaye kutoa ushauri muafaka utakaowezesha kikundi hicho kuendelea na uzalishaji. Matokeo ya utafiti mdogo utakaofanywa na Wataalam hao na mapendekezo yatakayotolewa ndiyo itakuwa msingi wa kikundi hicho kupata msaada.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kukamilisha azma ya Wilaya ya Muheza kuwa na Kiwanda cha Kusindika Matunda, Halmashauri ya Muheza tayari ilishaanza kutekeleza mkakati wa kuwa na mbegu bora za miche ya michungwa isiyo na mbegu inayofaa kwa ajili ya usindikaji wa *juice* na bidhaa nyingine kama ilivyoshauriwa na wataalam wa Kilimo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo katika mwaka wa fedha 2013/2014, Halmashauri ya Muheza kupitia Baraza lake la Madiwani katika kikao kilichofanyika tarehe 11 na tarehe 12 Desemba, 2013 kiliidhinisha kiasi cha shilingi milioni 85 kwa ajili ya ununuzi wa miche ya michungwa laki moja isiyo na mbegu. Aidha, katika kongamano la uwekezaji ambalo lilifanyika Mkoa wa Tanga tarehe 26 hadi 27 Septemba, 2013 kila Halmashauri ziliandaa fursa mbalimbali za uwekezaji na wawekezaji wengi walionesha nia ya kuwekeza katika Mkoa wa Tanga. Hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wakiwemo wa Muheza, tushirikiane kuwahamasisha wawekezaji ili waweze kuwekeza katika kilimo cha matunda na Viwanda vya Usindikaji wa Matunda. Ahsante.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa Wizara kuona umuhimu wa kupeleka Watalaam pale Muheza. Nawashukuru sana. Ushauri wangu ni kwamba watakapofikia wakati huo, basi wanishauri na mimi ili niweze kwenda kushirikiana nao. Hata hivyo, naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Ili uwekezaji, wawekezaji tulizungumza nao Tanga. Ili wawekezaji waweze kuwekeza inahitajika miundombinu maalum ikiwemo umeme, barabara na kikubwa zaidi ni maji, je Wizara itakubali kuishauri Serikali kutekeleza mpango wa maji wa Muheza ambao Mheshimiwa Rais aliahidi katika mwaka wa fedha huu tuliokuwa nao ili wawekezaji waweze kuja kuwekeza?

Swali la pili, Mkoa wa Tanga ulikuwa na mpango wa ujenzi wa soko kubwa la matunda katika eneo la Segera pale Mkoani Tanga. Je, Serikali inasema nini juu ya utekelezaji wa mpango huo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Silinde naomba urudi ulikotoka. Mheshimiwa Silinde rudi ulikotoka. Mheshimiwa Mntangi endelea!

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, nimemaliza. Labda kama Mheshimiwa Waziri hakusikia vizuri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la kuhamasisha Wizara husika katika masuala ya kuweka miundombinu hasa miundombinu ya maji naahidi kuwa tutaongea na wahusika ili waweze kuharakisha miundombinu hiyo ili kusudi kiwanda kitakapojengwa kiwe kina uhakika wa kupata maji na miundombinu husika.

Kuhusiana na swali la pili la soko la Segera, hilo ni soko ambalo vile vile liko katika mipango ya Wizara kwa ajili ya kulijenga kwa ajili ya soko la matunda na mboga kama ambavyo ilikuwa imeainishwa.

**SPIKA:** Tunaendelea, sikuona mtu mwingine, Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile atauliza swali hilo.

Na. 16

**Matumizi ya Tiketi za Kielekitroniki Kivukoni**

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE** aliuliza:-

Wizara ya Ujenzi inayoendesha vivuko viwili kati ya Magogoni na Kigamboni imeanzisha mfumo wa udhibiti wa mapato kwa kutumia matumizi ya tiketi za kielekitroniki:-

(a) Je, ni nini mapato ya Kivuko hiki kwa siku na kwa mwezi, kabla na baada ya kuanzisha mfumo huu mpya?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza kivuko kingine ili kuhimili mahitaji makubwa ya wananchi wa Kigamboni wanaotegemea usafiri huo?

(c) Je, ni nini mkakati wa Serikali katika kuboresha mafao ya watumishi wa kivuko wanaolalamikia maslahi madogo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kabla ya kuweka mfumo wa kielekitroniki, mapato ya kivuko kwa kipindi cha Januari hadi Aprili, 2013 yalikuwa ni wastani wa sh. 14,556,399/= kwa siku, sawa na sh. 436,691,970/= kwa mwezi. Baada ya kuanzisha mfumo wa tiketi za kielekitroniki, wastani wa makusanyo kwa siku katika kipindi cha Juni, 2013 hadi Machi, 2014 ni sh. 17,279,289/=, sawa na wastani wa sh. 525,290,386 kwa mwezi. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 20.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kuhimili mahitaji makubwa ya wananchi wa Kigamboni wanaotumia kivuko, Serikali inaendelea na ujenzi wa daraja la Kigamboni ambalo linategemewa kukamilika ifikapo Januari 2015. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Serikali imepanga kununua kivuko kipya chenye uwezo wa kubeba watu 1,000 na magari magari madogo 40 kwa mara moja. Kukamilika kwa ujenzi wa wa daraja na kivuko kutaondoa msongamano katika kivuko cha Magogoni kwa kiasi kikubwa.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuboresha maslahi ya watumishi wa vivuko pamoja na watumishi wote wa *TEMESA* ikiwemo kupandisha mishahara yao. Kuanzia mwezi Julai, 2013 kima cha chini cha mshahara wa wafanyakazi wa *TEMESA* kimeongezwa kutoka shilingi 170,000 mpaka shilingi 240,000/= kwa mwezi. Kiasi hicho hakitoshi, lakini Wakala itaendelea kuboresha mishahara na marupurupu mengine ya watumishi wake kadri mapato ya Wakala yatakavyozidi kuongezeka.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Namshukuru sana Mheshimiwa NaibuWaziri kwa majibu mazuri na kama hicho kivuko ambacho amekisema kitanunuliwa kitasaidia sana kuondoa kero pale Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa wananchi takribani laki moja na sitini ambao wanakaa katika Tarafa ya Kigamboni wanategemea kivuko hiki kwa ajili ya mahitaji yao na kwenda mjini kwa ajili ya kazi na shughuli nyingine za maendeleo; na kwa kuwa kwa upande wa Kigamboni eneo la kusubiria abiria ni dogo sana kiasi cha kuhatarisha usalama na afya ya wananchi ambao wanaishi Kigamboni. Kwa kuwa mwaka jana Serikali ilipanga bajeti kwa ajili ya kufanya upanuzi katika lile eneo la kusubiria abiria upande wa Kigamboni. Je, ni lini kazi hii itaanza?

Swali la pili, kwa kuwa Serikali ina Sheria nzuri na Sera nzuri za ushirikishwaji wa sekta binafsi *(public private partnership)*. Je, Serikali ina mpango gani kwa

kushirikisha sekta binafsi katika kuendesha huduma za vivuko hasa pale Kigamboni?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu eneo la kusubiria abiria, fedha hizi ambazo tumetamka kwamba zinakusanywa kwa ajili ya kuendesha kivuko, hizi hatuzitumii kwa ajili ya kufanya maendeleo kama hivi kujenga maeneo ya kusubiria. Haya Serikali itatafuta katika mipango yake ya maendeleo kuweza kujenga, kwa mfano, haya maegesho na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, kwa mwaka huu wa fedha tutaangalia namna ya kuboresha eneo hilo ambalo abiria wanasubiri.

Katika kushirikisha sekta binafsi, kama nilivyosema sasa hivi Serikali bado kwa sababu tumeanzisha Wakala wa *TEMESA*, hatujashindwa kuendesha vivuko. Kwa hiyo, hatuoni sababu ya kushirikisha sekta binafsi katika kuendesha vivuko kwa sababu hiyo kazi tunaifanya kwa ufanisi mkubwa.

**SPIKA:** Wakati haujafika. Haya tunaendelea na swali linalofuata Mheshimiwa Ignas Malocha atauliza swali hilo.

Na. 17

**Ahadi ya Kutengeneza Barabara Kadhaa Kwela**

**MHE. IGNAS A. MALOCHA** aliuliza:-

Katika uchaguzi wa mwaka 2010 Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya kutengeneza barabara za Kalambanzite hadi Ilemba yenye urefu wa kilomita 12; Miangulua hadi Chombe kilomita 16 kwa lami ili barabara hizo ziweze kupitika wakati wowote kwani ni barabara zinazopita kwenye milima mikali:-

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mbunge wa Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kalambanzite hadi Ilemba yenye wa kilomita 23.9 na barabara ya Miangulua hadi Chombe yenye urefu wa kilomita 18.6 ni barabara za Wilaya na zinahudumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga. Kutokana na barabara hizi kupita katika miinuko mikali Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi imekuwa ikitenga fedha kila mwaka kwa ajili ya ujenzi wa sehemu zenye miinuko mikali kwa kiwango cha zege.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka wa fedha 2011/2012 hadi 2013/2014 jumla ya sh. Milioni 326.8 zilitengwa kwa barabara ya Miangulua hadi Chombe kwa ajili ya kujenga mita 600 ya sehemu ya milima mikali kwa kiwango cha zege. Hadi sasa mita 400 zimekamilika ambapo mita 200 zingine zinaendelea kujengwa katika bajeti ya 2013/2014. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga pia imejenga mita 700 za zege katika barabara hiyo. Hivyo kutakuwa na jumla ya kilomita 1.3 ya barabara ya zege baada ya kukamilika kazi zinazoendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara ya Kalambanzite hadi Ilemba, jumla ya shilingi milioni 90 zimetengwa na kukamilika ujenzi wa mita 200 kwa kiwango cha zege katika mwaka wa fedha 2012/2013. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, jumla ya shilingi milioni 110 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa mita 200 kwenye maeneo ya milima kwa kiwango cha zege. Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga imejenga pia mita 505, na katika mwaka wa fedha 2013/2014, mita 320 zipo katika ujenzi. Kazi zinazoendelea zikikamilika jumla ya kilomita 1.225 zitakuwa zimejengwa kwa kiwango cha zege.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi hizi zilizokwisha kufanywa kati ya Wizara yangu na Halmashauri husika, namshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Halmashauri husika ili ajue kama imeingizwa katika mipango yao ya maendeleo kwa kujengwa kwa lami.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza nasikitika swali langu liliulizwa juu ya utekelezaji wa ahadi ya Mheshimiwa Rais kuziwekea lami barabara hizo. Majibu niliyojibiwa ni tofauti na swali langu. Hata hivyo, ninayo maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Kutokana na Serikali kutoa fedha nusu nusu na kwa kiwango kidogo, haziwezi kuleta tija kwa utengenezaji wa barabara sugu kama zile. Kwa nini Serikali isiheshimu ahadi ya Mheshimiwa Rais na kwa nini isitoe fedha za kutosha na kwa wakati ili kukamilisha ujenzi wa barabara hizo? *(Makofi)*

Swali la pili, kutokana na barabara hizo kuhitaji fedha nyingi, kushinda uwezo wa mapato ya Halmashauri ndiyo maana Halmashauri na Kikao cha Ushauri cha Mkoa wa Rukwa *(RCC)* kiliziombea zichukuliwe na *TANROAD* na Mtaalam kutoka Ofisi ya Wizara ya Ujenzi alifika kushuhudia sifa za kuchukuliwa na barabara hizo, toka mwaka 2012. Kwa nini Wizara ya Ujenzi haitaki kuzipandisha daraja barabara hizo zichukuliwe na *TANROAD*? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu jibu kwamba ungetaka kuona utekelezaji wa ahadi za Rais. Kwa utaratibu ambao tunao ni kwamba, mipango yote ambayo tunafanya katika kujenga barabara

za lami tunazingatia Ilani ya Uchaguzi. Tunazingatia pia ahadi za viongozi ikiwepo ahadi ya Rais na viongozi wengine wa Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, lakini barabara hizi katika mitandao ambayo tunayo, tuna barabara ambazo zinahudumiwa na Wizara ya Ujenzi na kuna barabara ambazo zinahudumiwa na Halmashauri. Barabara inayotajwa hapa ni ya Halmashauri ya Wilaya husika ambayo Mheshimiwa Mbunge ni Mjumbe wa Halmashauri ile. Sasa Rais akishaahidi barabara anaahidi kwa maana ya Serikali, lakini mpango inatakiwa ifanywe aidha kwenye Halmashauri au ifanywe kwenye Serikali Kuu.

Kwa hiyo, ndiyo maana tumekujibu hivyo. Lakini kwa sababu ya ugumu wa ile barabara, tumekuwa tunasaidia kujenga katika maeneo ambayo ni korofi kwa kiwango cha zege ili kusudi barabara ile iweze kupitika pamoja na kwamba iko chini ya Halmashauri ya Wilaya.

Sasa katika swali lako la pili kuhusu kupandishwa hadhi barabara ile. Kwa utaratibu tunayo Kamati ambayo Wizara huwa inapitia. Kwa hiyo, suala hilo bado linaendelea kushughulikiwa. Itakapokuwa tayari, Serikali itaona uwezo wa kuangalia kama inakidhi vigezo vinavyotakiwa na barabara itaweza kupandishwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Njwayo swali la nyongeza. Nina wasiwasi mnakwenda vijijini kwenu, haya!

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Matatizo ya kutokamilika kwa ahadi yaliyoko kwenye barabara ya Kalambanzite hadi Ilemba yanafanana kabisa na tatizo la kutokamilika kwa ahadi iliyopo kati ya Ndundu na Somanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa ninavyoongea hivi leo tangu juzi Watanzania wanaotumia barabara ya Dar es Salaam kwenda Lindi wamekwama kwa kiasi kikubwa; kuna magari zaidi ya 200 yako pale maeneo ya Manzese, wananchi wanapata shida, maradhi yanawakabili, lakini hakuna suluhisho pale. Naomba kupata maelezo ya Serikali wanafanya nini kama hatua za dharura kuwakomboa wananchi waliokwama pale Manzese? *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ingawa havifanani, ile ni barabara kuu na ile ni ya, oooh Waziri wa Ujenzi, unaulizwa hiyo barabara nyingine hiyo.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa alilouliza kuhusu sehemu ya Ndundu – Somanga. Ni kweli kabisa juzi palikuwa na lori lililokuwa linapita pale likakwama na baadaye tukapeleka malori yaliyokuwa yamebeba mawe nayo yakakwama na hii ni kulingana na

hali halisi ya mvua zinazonyesha katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi na maeneo mengine mbalimbali.

Napenda kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Mtwara na Lindi ambao wamekwama pale, suala hili tunalishughulikia na ikiwezekana leo suala hili litakuwa limeshapata ufumbuzi ili wananchi hao waendelee kupita salama kuelekea maeneo yao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya tunaendelea na Wizara inayofuata, watu wanasubiri barabara, kwa hiyo, Mheshimiwa Mangungu swali lako limejibiwa, hutapata nafasi ya kujieleza kuhusu hoja binafsi, maana hakuna lingine. Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Haroub Mohamed Shamis atauliza swali.

Na. 18

**Makampuni ya Simu Kutapeli na Kukera Wateja**

**MHE. HAROUB MOHAMMED SHAMIS** aliuliza:-

Baadhi ya Makampuni ya Simu yamekuwa na tabia za kitapeli na kukera wateja wao kama vile kutoa ofa ya kuongea kwa dakika tatu na badala yake simu kukatwa baada ya dakika mbili, kuwapigia wateja simu hata usiku wa manane na kutoa matangazo yao ya biashara na kadhalika:-

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya tabia hiyo ya Makampuni ya Simu?

**WAZIRI WA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haroub Mohammed Shamis, Mbunge wa Chonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa kulinda haki za watumiaji wa huduma za mawasiliano *(consumers),* mwaka 2011 ilitunga Kanuni za Kulinda Watumiaji wa huduma, yaani *Electronic and Postal Communications Regulations,* ambazo zinabainisha haki na wajibu wa watumiaji wa huduma hizo. Kanuni hizo zimeweka bayana taratibu za kuwasilisha malalamiko, ili yaweze kupatiwa ufumbuzi kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, kwa mujibu wa Sheria ni kosa kwa Kampuni ya Simu kuwalipisha watumiaji wa huduma kwa huduma ambazo hawajatumia au hawajaziomba. Aidha, Kanuni hizo pamoja na mambo mengine zinaelezea kwamba, mtoa huduma

hatajihusisha na kutangaza biashara kupitia maongezi au ujumbe mfupi wa simu ya mteja bila ridhaa ya mteja husika.

Mheshimiwa Spika, pale ambapo itathibitishwa kwamba, Kampuni ya Mawasiliano ya Simu imekiuka Masharti ya Mkataba wa Huduma kwa Mteja, Kampuni husika hupaswa kulipa fidia kwa mteja husika. Hata hivyo, changamotio iliyopo ni kwamba, ingawa wateja wengi wanakumbana na matatizo haya, hawawasilishi malalamiko yao katika ngazi husika kama Sheria zinavyoagiza. Kwa mantiki hiyo, Wizara kwa kushirikiana na *TCRA* inaendelea na mpango wa kuwaelimisha watumiaji kuhusu haki na wajibu wao.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwasihi watumiaji wa huduma za mawasiliano kuwa, wawe wanawasilisha malalamiko pindi yanapotokea, ili yashughulikiwe Kikanuni. Utaratibu wa kulalamika ni kwamba, mteja anatakiwa kulalamika kwa mtoa huduma ya mawasiliano husika na endapo hataridhika na majibu ya mtoa huduma husika, anashauriwa kupeleka malalamiko husika Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania au Baraza la Watumiaji wa Mawasiliano Tanzania.

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa sababu Serikali imekiri kwamba, matatizo haya katika Makampuni ya Simu ya kuibia wananchi yapo, pale Mheshimiwa Waziri aliposema kwamba, naomba nimnukuu:

> *"Ingawa Wateja wengi wanakumbana na matatizo haya, lakini hawawasilishi malalamiko yao katika ngazi husika kama Sheria zinavyoagiza."*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Watanzania wengi ni maskini na hawawezi kushughulikia hizo kesi za kudai haki zao au hawajui kama haki zao zimedhulumiwa. Je, Serikali inawasaidiaje wananchi hao masikini, ili wasiendelee kudhulumiwa na Mkampuni haya ya Simu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Serikali inachukua hatua gani kwa Makampuni haya ya Simu dhidi ya wizi wanaoufanya kwa Watanzania maskini ambao baada ya miaka 50 ya uhuru wanaishi katika Dunia ya Nne na sio ya tatu tena kwa umaskini na shida?

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano imeanzisha mpango wa kuendesha elimu ili kuwafahamisha utaratibu Watanzania wote jinsi ya kupeleka malalamiko yao. Hilo la kwanza.

La pili, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano tena inashirikiana na watoa huduma kuwakutanisha baina ya watoa huduma ya mawasiliano na walalamikaji ili kutatua matatizo ambayo yanajitokeza na kwa utaratibu huu, tumeweza kufanikiwa kutatua matatizo mengi kabisa ambayo yanawakabili wananchi.

Mheshimiwa Spika, vile vile Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano iko mbioni kufungua Kituo Maalum, ambacho kazi yake itakuwa ni kupokea malalamiko kwa wananchi saa 24, siku saba kwa wiki, mwaka mzima saa zote na wananchi wanatakiwa wapige namba ambazo zitapatikana bure ama watume ujumbe wao kwa kutumia namba ambazo zitapatikana bure. Kituo hicho kitaanza kufanya kazi mwishoni mwa mwezi wa Juni mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, pia kama swali lake la nyongeza je, Serikali inafanyaje kuhakikisha kwamba, wale wanaofanya wizi huu wanapata adhabu inayostahili? Ni kwamba, iko Kanuni yetu ambayo inaeleza kwamba, mtoa huduma yeyote ambaye atakiuka mikataba na mteja, anatakiwa alipe faini si chini ya milioni tano ama aende kifungo cha miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

Na. 19

**Eneo Lililokuwa Shamba la *NAFCO* Namtumbo**

**MHE. VITA R. M. KAWAWA** aliuliza:-

Namtumbo ina eneo la ardhi lililokuwa shamba la Namtumbo na tangu shamba hilo lisitishwe shughuli zake ni zaidi ya miaka (20) sasa na ardhi hiyo imebaki kama haina mwenyewe; na ardhi hiyo kwa sasa imeangukia ndani ya eneo la Mamlaka ya Halmashauri ya Namtumbo. Je, maombi ya Halmashauri ya Namtumbo kutaka kuachiwa eneo hilo yamefikia wapi baada ya kuleta vielelezo na maombi ya eneo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni mara ya kwanza kwangu kusimama hapa kujibu maswali tangu niteuliwe, naomba nichukue dakika moja tu nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa imani kubwa aliyoonesha kwangu ya kuniteua. Naomba tu niwaahidi wana Mbozi, wana Mbeya na Watanzania kwamba, nitawatumikia kwa kadiri ya uwezo wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi naomba sasa kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, nijibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shamba la Namtumbo ni kati ya mashamba yaliyokuwa chini ya Shirika la Taifa la Kilimo na Chakula *(NAFCO)* ambapo shamba hilo liliainishwa kwa ajili ya ubinafsishaji chini ya iliyokuwa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(Parastatal Sector Reform Commission – PSRC)*. Aidha, Serikali ilitangaza kubinafsisha Shamba la Namtumbo mara kadhaa bila kupata Mwekezaji makini, hivyo, shamba hilo kwa sasa lipo chini ya usimamizi wa Shirika Hodhi la Mashirika ya Umma *(CHC)*.

Mheshimiwa Spika, tunakiri kupokea maombi kutoka Taasisi mbalimbali, ikiwemo Halmaashauri ya Wilaya ya Namtumbo na Kikundi cha Kukuza Uchumi wa Namtumbo *(KUNA)* kuhusu kutumia shamba hilo kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia maombi hayo, Wizara kwa kushirikiana na wadau, imeandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri wenye mapendekezo mbalimbali kuhusu matumizi ya shamba hilo kwa ajili ya maamuzi ya Serikali. Maombi ya wadau ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo na Kikundi cha Kukuza Uchumi wa Namtumbo *(KUNA)* yatazingatiwa. Aidha, kwa sasa Wizara imetuma timu ya Wataalam kwa ajili ya kuhakiki Taarifa mbalimbali kuhusu shamba hilo, ili kuapata hali halisi ya sasa ambayo itaiwezesha Serikali kufanya maamuzi kwa kuzingatia maslahi ya wadau.

**MHE. VITA R. M. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, shamba lile limeachwa karibu robo karne sasa bila kufanyiwa shughuli za kimaendeleo zilizokusudiwa na sasa eneo hilo liko ndani ya Ramani ya Mamlaka ya Mji ya Halmashauri ya Namtumbo na kwa kuwa, Wajumbe wa Baraza la Mawaziri wako hapa, naiomba tena Serikali itupe kipaumbele Halmashauri na wananchi wa Namtumbo kutupatia shamba hilo, ili tuweze kuendeleza kukuza uchumi wa wananchi wa Namtumbo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, katika Kijiji cha Suruti, Namtumbo kuna mashamba na majengo ya Kituo cha Utafiti ya *branch* ya Kituo cha Utafiti cha Uyole yaliyokuwa yanafanyiwa kazi kubwa ya utafiti wa mbegu katika maeneo ya hali ya hewa ya mazingira ya kusini, lakini Kituo hicho kimetelekezwa kama hakina mwenyewe na kwa kuwa, Serikali au nchi inategemea 70% ya mbegu kutoka nje, je, Serikali haioni ipo haja sasa kukiendeleza Kituo kile ili kiweze kutupatia mbegu hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza kama nilivyojibu kwenye majibu ya msingi, tumesema kwamba, tumeandika Waraka kwa ajili ya Baraza la Mawaziri, ili waweze kufanya maamuzi juu ya shamba hilo ambalo kama alivyosema yeye limekaa muda mrefu, lakini pia shamba lenyewe baada ya jitihada zote za kutaka kulibinafsisha kushindikana, tumeandika Waraka huo ili upelekwe kwenye Baraza la Mawaziri ili liweze kufanya maamuzi juu ya matumizi ya shamba hilo. Kama nilivyosema, tutakapokuwa tunafanya maamuzi hayo, basi maombi ya Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo yatazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili; naomba tu niseme kwamba, ni kweli Kijiji alichokisema kwamba, kuna Kituo kidogo cha Kilimo cha Suruti ambacho ni *sub-station* ya Uyole. Kituo hicho ni kwamba, ni kweli kinakabiliwa na matatizo mengi, lakini sisi kama Wizara tumejipanga sasa tuhakikishe kwamba, moja tunaweza kuimarisha shughuli za utafiti kwa kupeleka Watafiti. Tunajua kabisa kwamba, watumishi waliopo ni wachache na mmoja amestaafu mwezi Januari na mwingine anastaafu mwezi wa Tano, kwa maana hiyo tutakuwa tunabaki na mtumishi mmoja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mipango ya Wizara ni kuajiri na kwa sababu, tumepata pia kibali cha kuajiri baadhi ya watumishi, tutaangalia namna ya kuwapanga vizuri ili kile Kituo kisibaki peke yake. Pia tuna mpango wa kuimarisha shughuli za utafiti, ili baadhi ya mazao kwa mfano, maharage, soya na mengine, ambayo mbegu zake zilikuwa zinatafitiwa hapo, basi shughuli za utafiti ziweze kuendelea.

Mheshimiwa Spika, tunachoomba ni Waheshimiwa Wabunge kutupitishia Bajeti ya Wizara yetu ambayo itasomwa siku ya Ijumaa na kujadiliwa Jumamosi, ili maamuzi yakishafanyika basi haya mambo mengine ya kukirekebisha Kituo cha Suruti yaweze kufanyika vizuri. Ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha. Nafurahi kwamba, tumetumia dakika zile tulizostahili, saa moja bila kuongeza, leo tuna kazi nyingi.

Kwanza niwatambue wageni waliopo, mtakumbuka kwamba, tumeweka Mezani Taarifa nyingi za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali na yeye yupo. Huyu anaitwa Ndugu Ludovick Uttoh, ndio Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Naomba asimamame, ahsante. *(Makofi)*

Pia ameambatana na Manaibu Wakaguzi Wakuu wa Serikali watano kutoka Ofisi yake. Naomba nao pia wasimame, Manaibu wote, ahsante. Tulikuwa tunaangalia kama *Gender has been taken care of,* yuko mmoja, sio *one third* wala sio nini. *(Makofi)*

Halafu kuna Wakuu wa Idara watano na Wakaguzi Wakazi watano kutoka Ofisi ya *CAG*. Pia naomba wasimame walipo, hawa wapo hapa katika upande wa pili. Ahsante sana. Halafu kuna Maafisa wengine watano kutoka Ofisi ya *CAG* na wengine; wasimame hao wengine. Ahsante, Maafisa wengine, tunashukuru. *(Makofi)*

Tuna Wageni wawili kutoka Shirika la Misaada la Ujerumani *(GIZ)* ambao ndio Wafadhili wa miradi mbalimbali ya maendeleo, wameambatana pamoja na *CAG* nafikiri ndio hawa Wageni wetu. Ahsante karibu Wageni kutioka *GIZ,* ahsante sana. *(Makofi)*

Halafu kuna ndugu Kodula Mula, ndio wenyewe? *Ok,* Kodula Mula na ndugu Akim Biame, tunawakaribisheni sana na Mkaguzi tunakuhakikishia kwamba, kazi yako nzuri itaendelea kusimamiwa na Bunge letu. Hata kama tuna matatizo ya kuweka ratiba, lakini tutaweka nafasi Taarifa zako ziweze kupata kujadiliwa kwa mujibu wa taratibu na Sheria zetu.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wapo wageni wa Mheshimiwa Mary Nagu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Uwekezaji na Uwezeshaji, ambao ni ndugu Aluu Segamba, Katibu wa *CCM* Wilaya ya Hanang. Ahsante, asimame alipo.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Henry Shekifu. Yuko mke wake Mrs. Joyce *Shekifu,* naomba asimame alipo. Ahsante na wale wageni wengine wasimame? Ahsante nashukuru sana. *(Makofi)*

Tuna wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya Mafunzo. Kuna Ndugu Senga Sungura na Ndugu Latifah Hussein, wako wapi? *Okay,* ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, leo liko tatizo la muda.

Tangazo la Kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa William Ngeleja, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa 8.15 mchana, wakutane katika Ukumbi wa Hazina Ndogo. Sijui kwa nini saa 8.00 maana sisi tunaahirisha saa 7.00; utajua wewe hapo sasa, lakini mkutane kwenye Hazina Ndogo.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, leo asubuhi yote hii tutatumia muda kuwasikiliza Wenyeviti wa Kamati mbalimbali pamoja na Wasemaji wa Kambi ya Upinzani mbalimbali. Katibu!

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014/2015 – Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Kama nilivyosema, tutaanza na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Atafuatiwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na atafuatiwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Katiba Sheria na Utawala! Kwa niaba yake Mheshimiwa Fakharia!

### Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kama ilivyosomwa Bungeni

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (K.n.y. MHE. WILLIAM M. NGELEJA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu Kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za 99 (5) na (9) na 114(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha katika Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu inajumuisha Mafungu matano ambayo ni kama ifuatavyo:-

Fungu 25 – Waziri Mkuu; Fungu 27 – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa; Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu; Fungu 42 – Mfuko wa Bunge na Fungu 61 – Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 2 Mei, 2014 Kamati ilipata fursa ya kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014. Katika kupitia

utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**SPIKA:** Waheshimiwa mnaotoka naomba mpunguze sauti, Waheshimiwa wanaotoka watoke kimya kimya maana sisi hatusikilizani hapa. Mheshimiwa endelea!

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (K.n.y. MHE. WILLIAM M. NGELEJA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Spika, Kamati ilitaka kujiridhisha kama maoni na ushauri wa Kamati uliotolewa wakati wa kupitisha makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 ulizingatiwa. Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Bunge; Kamati yangu ilipokea maelezo kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge pamoja na Taasisi zote zilizo chini yake. Maelezo na ufafanuzi huo uliwasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), Mheshimiwa William Lukuvi. Katika maelezo yake, pamoja na mambo mengine Waziri aliieleza Kamati kuhusu makusanyo ya maduhuli hadi kufikia mwezi Machi, 2014 na matumizi kwa mafungu yote.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014. Kwa kuzingatia umuhimu na unyeti wa Ofisi ya Waziri Mkuu ambaye ndiye Msaidizi Mkuu wa Rais, Mratibu na Msimamizi Mkuu wa shughuli na mipango yote ya Serikali katika sekta zote na ndani ya Bunge. Kamati ilitoa maoni na ushauri mbalimbali kwa Ofisi hii wakati wa kupitisha makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka 2013/2014. Kamati inatambua na kuthamini juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu katika kuleta maendeleo na ustawi wa nchi yetu. Hivyo basi, Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada hizo zinazolenga kuwakwamua wananchi wetu na kutoka kwenye umaskini na kuhakikisha kuwa wanapata maisha bora.

**SPIKA:** Jamani kuna kelele nyingi zinaendelea, *Hansard* hairipoti vizuri. Kuna kelele nyingi, kwa nini mnaongea?

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (K.n.y. MHE. WILLIAM M. NGELEJA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ulizingatiwa na utekelezaji wa mambo yaliyotolewa ushauri unaendelea.

Yafuatayo ni baadhi ya maeneo yaliyofanyiwa kazi kutokana na ushauri uliotolewa na Kamati:-

(1) Serikali kuwalipa fedha Wenyeviti wa Vijiji, Mitaa na Vitongoji walioshiriki katika zoezi la Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012.

Kamati ilielezwa na Serikali kuwa watendaji wote wamekwishalipwa stahili zao ambapo ilitumia kiasi cha sh. 4,292,501,555/=.

(2) Ili kuepuka maafa makubwa kama mafuriko, majanga ya moto yanayotokana na ujenzi holela, Serikali itoe elimu ya kutosha kwa wananchi. Serikali imeiagiza Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ili kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kuzingatia taratibu za mipango miji kwani taasisi hizo ndizo zinazohusika moja kwa moja na kusimamia taratibu za mipango miji.

(3) Uanzishwaji wa Idara ya Maafa katika ngazi ya kila Wilaya ili kurahishisha uratibu wa shughuli za maafa nchini. Serikali imekwishaunda Kamati za Menejimenti ya maafa na kuainisha majukumu ya menejimenti hizo katika ngazi ya Mikoa, Wilaya, Kata na Vijiji katika mikoa yote ya Tanzania Bara inayoratibu shughuli za maafa. Aidha, kila Halmashauri imeteua Mratibu ambaye anayewajibika kuratibu shughuli za maafa na kuwasiliana na Idara ya Maafa iliyoko Ofisi ya Waziri Mkuu ngazi ya Taifa kwa muda wote.

(4) Ofisi ya Bunge kutoa elimu kuhusu utaratibu wa matibabu kwa Waheshimiwa Wabunge pamoja na familia zao. Kamati imeelezwa kwamba Ofisi ya Bunge imeingia Mkataba wa mwaka mmoja na Jubilee *Insurance* kuanzia Januari, 2014 ambapo utaratibu wa matibabu kwa Waheshimiwa Wabunge na familia zao umekwishaanza.

(5) Ofisi ya Bunge kujenga Ofisi za Waheshimiwa Wabunge katika Majimbo yote na kuziwekea samani. Kamati ilielezwa kwamba TAMISEMI walijenga Ofisi 75 za Wabunge na kuzikabidhi Ofisi ya Bunge. Baada ya kukabidhiwa Ofisi hizo, Ofisi ya Bunge iliingia Mkataba na Jeshi la Magereza ili kutengeneza samani ambapo samani hizo zimekamilika na utaratibu wa kuzisambaza unaandaliwa. Aidha, Ofisi ya Bunge imeingia Mkataba na *NSSF* wa kujenga Ofisi za Wabunge 178 kwa mkupuo katika Majimbo yote ya Bunge yasiyo na Ofisi za Wabunge.

(6) Serikali kutenga fedha za kutosha ili kuiwezesha Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuboresha Daftari la Kudumu la Mpiga Kura. Kamati ilielezwa kuwa Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 39 kwa ajili ya maandalizi ya maboresho hayo.

(7) Ofisi ya Bunge iangalie uwezekano wa kununua mabasi mengine badala ya kukodisha. Ofisi ya Bunge imefanya utafiti na kubaini kuwa njia zote mbili za kununua na kukodisha magari zinafaa kulingana na mazingira husika. Mathalani Waheshimiwa Wabunge wanaposafiri safari za mbali hutumia usafiri

wa ndege na wanapofika mahali wanakokwenda, Ofisi ya Bunge huwakodia magari ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao. Aidha, Ofisi ya Bunge imeazimwa magari manne na Wizara ya Mambo ya Nje ili kusaidia kurahisisha usafiri.

(8) Serikali kuongeza bajeti ya Msajili wa Vyama vya Siasa ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Bajeti ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa imeongezwa kutoka Sh. 1,167,287,000/= katika mwaka wa fedha 2013/2014 hadi kufikia sh. 2,167,287,000/= likiwa ni ongezeko la sh. 500,000,000/=.

(9) Kwa ujumla utekelezaji wa ushauri na maoni ya Kamati umekuwa mgumu hasa katika miradi ya maendeleo kutokana na fedha za miradi kuchelewa kutolewa na kutolewa kidogo ikilinganishwa na kiasi kinachotengwa au kutotolewa kabisa. Suala hili linafanya miradi mingi kushindwa kutekelezwa inavyotakiwa. Ili kuhakikisha miradi hii inatekelezwa kwa ufanisi, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha fedha za miradi zinatolewa zote na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazoikabili Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zilizo chini yake. Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zilizo chini yake katika utekelezaji wa majukumu yake imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge. Katika Mwaka wa Fedha 2013/2014, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge ilikabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ukusanyaji hafifu wa maduhuli ya Serikali katika taasisi mbalimbali ikilinganishwa na makadirio yanayofanywa katika taasisi hizo. Katika Mwaka wa Fedha 2013/2014, Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zilizo chini yake ilikadiriwa kukusanya maduhuli ya jumla ya Sh. 5,284,713, 079/=, hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2014, Ofisi ya Waziri Mkuu ilikuwa imekusanya kiasi cha sh. 1,329,596,919/= sawa na asilimia 25 tu. Kiasi hiki ni kidogo sana ikilinganishwa na makisio yaliyotarajiwa.

(ii) Mfumo wa ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa fedha zinazotolewa na Serikali kwa ajili ya maendeleo kutokuwa madhubuti hivyo kusababisha malengo ya ukusanyaji na utekelezaji wa mipango kutokufikiwa.

(iii) Idara ya Maafa na Mpiga chapa Mkuu wa Serikali pamoja na unyeti na umuhimu wake kwa Taifa, zinakabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi hivyo kuathiri utendaji na ufanisi.

(iv) Hazina kuchelewa kupeleka fedha zinazoidhinishwa na Bunge katika Ofisi na Taasisi za Serikali. Mathalani, mradi wa ujenzi wa makazi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, ulitengewa kiasi cha sh. 1,500,000,000/= hadi kufikia 30 Machi, 2014, Ofisi ya Waziri Mkuu ilikuwa haijapokea kiasi chochote cha fedha kutoka Hazina. Aidha, mradi wa kuendeleza eneo la Makaburi ya Viongozi Dodoma kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, ulitengewa kiasi cha sh. 1,000,000,000/= lakini hadi wakati Kamati inaandaa taarifa hii, hakuna kiasi chochote cha fedha kilichokuwa kimetolewa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa ambayo inahusika na usajili na usimamizi wa mienendo ya Vyama vya Siasa inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

Sheria ya Usajili wa Vyama vya Siasa (*The Political Parties Act, Cap* 258) kuwa na upungufu mkubwa na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu yake.
Kutokana na mabadiliko ya Sheria ambapo jukumu la kukagua hesabu za Vyama vya Siasa limehamishiwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali toka Makampuni ya Ukaguzi, Msajili wa Vyama vya Siasa hakuweza kutoa taarifa kwa umma kuhusu hesabu zilizokaguliwa kwa Vyama vya Siasa vinavyopata ruzuku kutoka Serikalini kuanzia Mwaka 2009 hadi 2013.

Mheshimiwa Spika,Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Taasisi hii ni muhimu katika Taifa kutokana na wajibu mkubwa wa kuratibu na kusimamia chaguzi mbalimbali nchini. Katika kutekeleza majukumu haya, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inakabaliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Tume ya Taifa ya Uchaguzi haina jengo la ofisi hivyo imeendelea kupanga katika kipindi chote toka mfumo wa Vyama Vingi uanzishwe. Jambo hili linasababisha Tume kutumia gharama kubwa katika kulipia pango la ofisi.

(ii) Serikali bado haijaipatia fedha Tume ili iweze kulipa madeni yake likiwemo deni la sh. 2,254,323,693/= zilizotokana na gharama za uchaguzi za Mwaka 2010. Deni hili linaisababishia usumbufu na kupunguza uaminifu kutoka kwa watu na taasisi zinazoidai Tume.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali inafanya kazi muhimu ya kuchapisha nyaraka mbalimbali za Serikali hapa nchini. Katika kutekeleza majukumu hayo, idara inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ina mtambo mmoja wenye uwezo wa kuchapa rangi nne tu katika upande mmoja wa karatasi. Kutokana na hali hiyo kunahitajika mashine nyingine ndogo sita ili kuweza kuchapa pande zote nne. Aidha, Idara ina upungufu wa mtambo mmoja

mkubwa wa umaliziaji. Changamoto hii inasababisha kutotekelezwa majukumu ya uchapaji kwa ufanisi na kwa wakati.

(ii) Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kupokea fedha kidogo za *retention* ambazo hazikidhi gharama za uzalishaji. Aidha, fedha za *retention* hazitolewi kwa wakati na Hazina, mathalani kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara haikupewa fedha ilizokusanya takribani shilingi milioni 809. Hali hii inakwamisha ukusanyaji wa maduhuli kwani Idara inashindwa kununua malighafi ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 imetengewa jumla ya sh. 224, 932, 198,000 mgawanyo wake ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, fungu 25 - Waziri Mkuu, shilingi 6,358,738,000/= zinaombwa kwa matumizi ya kawaida; Fungu 27 - Msajili wa Vyama vya Siasa kiasi cha sh. 20,732,781,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida; Fungu 37- Ofisi ya Waziri Mkuu kiasi cha sh. 36,081,195,000/= **(39,574,195,000)** kinaombwa kwa matumizi ya kawaida na sh. 18,498,285,000/= kwa miradi ya maendeleo. Fungu 42 - Mfuko wa Bunge unaomba jumla ya sh. 123,941,455,000/=, kati ya fedha hizo sh. 15,520,327,000/= zinaombwa kwa ajili ya mishahara ya Wabunge na watumishi, sh. 108,421,128,000 zitatumika kuendeshea mikutano ya Bunge na Kamati pamoja na shughuli zingine za kiutawala. Vile vile sh. 8,755,439,000/= zinaombwa kwa ajili ya mpango wa maendeleo. Fungu 61-Tume ya Taifa ya Uchaguzi kiasi cha sh. 4,371,895,000/= kinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati. Kwa kuzingatia taarifa iliiyowasilishwa mbele ya Kamati mnamo Tarehe 2 Mei, 2014, pamoja na maombi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 kama yalivyoainishwa kwa kila fungu, Kamati inatoa maoni na mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia unyeti wa Ofisi ya Waziri Mkuu ambaye ndiye msaidizi mkuu wa Rais, mratibu na msimamizi mkuu wa shughuli na mipango yote ya Serikali katika sekta zote nchini na ndani ya Bunge, mhimizaji mkuu wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya wananchi mijini na vijijini katika misingi ya utawala bora, kwa mantiki hii Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Ofisi hii itengewe fedha za kutosha na kuajiri watumishi wenye taaluma stahiki ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

(ii) Kwa kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu ni msimamizi wa shughuli za Serikali ikiwemo mapambano dhidi ya rushwa, ni vema watumishi katika Ofisi hii wawe mfano kwa jamii kwa kutojihusisha na vitendo vya rushwa.

(iii) Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kutekeleza majukumu yake, hufanya ziara katika sehemu mbalimbali nchini. Kwa kufanya hivyo, wakati mwingine hulazimika kutoa ahadi ili kutatua kero na changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi. Kamati imebaini kwamba baadhi ya ahadi zinazotolewa hazitekelezwi kwa wakati. Hivyo basi Kamati inashauri kwamba, ipo haja ya kuwepo na mfumo mzuri wa kubainisha ahadi zote zinazotolewa na Waziri Mkuu katika maeneo mbalimbali na kuzitekeleza kwa wakati.

(iv) Kuhusu mradi wa kuendeleza eneo la Makaburi ya Viongozi, Kamati inashauri Serikali itilie maanani uwepo wa mradi huu kwa kuendelea kuutengea fedha na kuhakikisha kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya Mradi huu zinatolewa ili zifanye kazi inayokusudiwa. Kamati inasisitiza kuwa kiasi cha shilingi bilioni moja zilizotengwa kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 zitolewe kabla ya mwaka wa fedha haujakwisha.

(v) Kwa kuwa Serikali inajenga Ofisi na Makazi ya Waziri Mkuu Dodoma, Kamati inashauri kasi ya utoaji wa fedha zinazotengwa kwa ajili ya ujenzi huo iongezwe ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa fedha zilizotengwa kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, zinatolewa kabla ya kuisha kwa mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Ustawishaji Makao Makuu Dodoma. Uanzishwaji wa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kuwa Mji wa Dodoma unapangwa na kuendelezwa ili kuufanya kuwa na sura na hadhi ya Makao Makuu ya Nchi. Aidha, Kamati inashauri kuwa Serikali, Idara na Taasisi zote za Serikali ziweke mipango ya ujenzi wa ofisi zao Dodoma ili kuhakikisha kuwa azma ya Serikali ya kuhamia Dodoma inatimia.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Maafa. Katika kuimarisha Idara ya Maafa, Kamati inatoa ushauri na mapendekezo kama ifuatavyo:-

(i) Pamoja na Serikali kutekeleza ushauri wa kuanzisha Idara ya Maafa katika kila Wilaya hapa nchini Kamati inashauri Idara hii iboreshwe kwa kujengewa uwezo wa fedha na rasilimali watu, ujuzi na vifaa kwa lengo la kuisaidia nchi yetu kukabiliana na maafa ya aina mbalimbali yatakayoweza kujitokeza kama ilivyokusudiwa.

(ii) Katika jitihada za uokoaji pale maafa yanapojitokeza, ni vyema vyombo vya ulinzi na usalama kama Jeshi la wananchi washirikishwe kikamilifu kwani wao wana ujuzi na utaalam wa kutosha katika masuala ya uokoaji. Aidha, kwa kuwa taratibu za kulishirikisha Jeshi la Wananchi lina masharti

magumu, Kamati inashauri Ofisi ya Waziri Mkuu ifanye mazungumzo na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la wananchi ili walegeze masharti ya taratibu za Jeshi na kuruhusu Jeshi na vyombo vya Jeshi vitumike kuokoa maisha ya wananchi pale maafa yanapojitokeza hasa maafa ya baharini.

(iii) Serikali iandae utaratibu utakaowezesha fedha na misaada inayotolewa na Serikali na wananchi kwa ajili ya kusaidia watu waliokumbwa na maafa inawafikia walengwa kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Wakati wa kupitia utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2013/014 na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, Kamati ilibaini kuwa Idara ya Mpiga Chapa wa Serikali imekuwa haitekelezi majukumu yake kwa ufanisi, ili kuboresha utendaji wa Idara hii Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali iboreshe Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kununua Mashine zinazoweza kuchapa rangi nne pande mbili za karatasi kwa wakati mmoja na kwa haraka.

(ii) Idara iruhusiwe kupokea kazi za nje za wateja wengine wa nje mbali na kazi za Serikali ili kuiwezesha kujiendesha kibiashara badala ya kutegemea ruzuku kutoka Serikalini.

(iii) Kamati inaendelea kutoa rai kwa Serikali kuwa tozo la 26% ya mapato ya Idara yanayotokana na shughuli za upigaji chapa lipunguzwe hadi kufikia 5% kwani bajeti inayotengewa Idara haikidhi mahitaji.

Mheshimiwa Spika, Msajili wa Vyama vya Siasa fungu namba 27.

(i) Msajili wa Vyama vya Siasa ahakikishe kuwa taarifa za fedha za Vyama Vya Siasa zinatangazwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa katika gazeti la Serikali ili kuwezesha umma kupata taarifa sahihi juu ya ruzuku inayotolewa kwa Vyama vya Siasa pamoja na namna inavyotumika.

(ii) Kamati imepata taarifa kwamba Serikali inakusudia kuleta Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa *(The Political Parties Act, CAP* 258 *R.E* 2002*)*. Kamati inaona lengo hilo ni jema na Kamati inashauri mchakato wa kuleta marekebisho hayo Bungeni uharakishwe ili wadau wa Vyama vya Siasa wanufaike na maboresho hayo.

(iii) Msajili wa Vyama Vya Siasa aendelee kuratibu kwa karibu zaidi masuala ya maridhiano kwa Vyama vya Siasa kupitia Baraza la Demokrasia

Nchini *(Tanzania Centre for Democracy)* ili kukuza na kuimarisha demokrasia kwa lengo la kudumisha amani na utulivu nchini.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Bunge, Fungu 42. Kuhusu Mfuko wa Bunge Kamati inaipongeza Ofisi ya Mheshimiwa Spika pamoja na Tume ya Utumishi wa Bunge kwa kuendelea kutoa ushauri na mapendekezo kwa Mheshimiwa Rais ya kuboresha maslahi ya Waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Bunge ili kuhakikisha kuwa Wabunge na watumishi wa Bunge wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kuleta tija kwa Taifa. Hata hivyo ili kuhakikisha Bunge linatekeleza majukumu yake ipasavyo Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Kwa kuwa Ofisi ya Bunge imeingia mkataba na mkandarasi wa kujitegemea *(Jubilee Insurance)* ili kutoa matibabu kwa waheshimiwa Wabunge na familia zao, Kamati inashauri kuwa Ofisi ya Bunge imwelekeze mkandarasi huyo atoe elimu kwa Waheshimiwa Wabunge kuhusu utaratibu wa utoaji huduma, aina ya matibabu na hopitali zinazohusika na mkataba huo na mahali zinakopatikana.

(ii) Ofisi ya Bunge iharakishe Mchakato wa makabidhiano ya Ofisi 75 zilizojengwa na TAMISEMI kwa ajili Wabunge katika Majimbo husika na kuziwekea samani ili kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kuanza kuzitumia katika kuwahudumia wananchi kwa karibu na kwa ufanisi zaidi.

(ii) Kamati imepewa taarifa kuwa ofisi ya Bunge imeingia mkataba na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) kujenga ofisi 178 za Waheshimiwa Wabunge katika Majimbo ambayo hayana ofisi, Kamati inaona ni jambo jema, hivyo inashauri kazi hiyo ianze na kukamilishwa mapema iwezekanavyo ili ofisi hizo zianze kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

(iii) Ofisi ya Bunge iangalie uwezekano wa kuwapatia Waheshimiwa Wabunge wote Ofisi za kufanyia kazi wanapokuwepo Dodoma ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa umakini na ufanisi.

(v) Ofisi ya Bunge ihakikishe inaingia mikataba na mabenki yanayotoa mikopo yenye bima ili kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza kutokana na deni la mkopo huo kwa familia za Wabunge hao endapo watapoteza maisha kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Fungu 61. Kamati inatoa ushauri na mapendekezo yafuatayo kuhusu Tume ya Taifa ya Uchaguzi:-

(i) Tume ya Taifa ya Uchaguzi ndiyo iliyopewa majukumu ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Mpigakura mara mbili kati ya kipindi kimoja cha

uchaguzi na kipindi kingine. Ili kutekeleza jukumu hili lililoainishwa na sheria, Kamati inashauri fedha zinazotengwa kwa ajili ya kazi hiyo zitolewe kwa wakati.

(ii) Kwa kuwa fedha za Tume za kulipa deni hazikutolewa kama kamati yangu ilivyoshauri katika bajeti ya Mwaka 2013/2014, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Serikali itoe kiasi cha sh. 2,254,323,693 /= zilizotokana na gharama mbalimbali wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala. Napenda nitumie nafasi hii pia kukupongeza kwa dhati kwa jinsi unavyoliongoza Bunge hili ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ili kuhakikisha kuwa ustawi wa wananchi ndio kipaumbele cha kwanza.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania: Kwanza, kwa jinsi anavyoratibu vizuri na kufuatilia kwa karibu shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Wizara zote katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwani sote tunatambua kuwa changamoto zinazoikabili Serikali yetu ni nyingi hivyo…

**SPIKA:** Mheshimiwa kengele imegonga.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (K.n.y. MHE. WILLIAM M. NGELEJA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** *Okay*, ahsante. Nashukuru nimeshamaliza.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea Mwenyekiti…

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (K.n.y. MHE. WILLIAM M. NGELEJA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Haya yote, majina ya Wajumbe wa Kamati na wengine wa kuwashukuru….

**SPIKA:** Huna muda wa kuongeza.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (K.n.y. MHE. WILLIAM M. NGELEJA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante, huna muda wa kuongeza ikigonga kengele basi.

Mheshimiwa ahsante kwa kusoma vizuri.

**Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Sheria, Katiba na Utawala kama ilivyowasilishwa Mezani**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA WAZIRI MKUU KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni za 99 (5)&(9) na 114 (11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili 2013, naomba kuwasilisha katika Bunge lako tukufu Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**Mheshimiwa Spika** Ofisi ya Wazri Mkuu inajumuisha Mafungu matano ambayo ni kama ifuatavyo: Fungu 25 – Waziri Mkuu; Fungu 27 – Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa; Fungu 37 – Ofisi ya Waziri Mkuu; Fungu 42 – Mfuko wa Bunge; na Fungu 61 – Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 2 Mei,2014 Kamati ilipata fursa ya kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014. Katika kupitia utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, Kamati ilitaka kujiridhisha kama maoni na ushauri wa Kamati uliotolewa wakati wa kupitisha makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 ulizingatiwa.

### 1.1 OFISI YA WAZIRI MKUU SERA, URATIBU NA BUNGE

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu ilipokea maelezo kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge pamoja na Taasisi zote zilizo chini yake. Maelezo na ufafanuzi huo uliwasilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Bunge, Mheshimiwa William V. Lukuvi. Katika maelezo yake, Pamoja na mambo mengine Waziri aliieleza Kamati kuhusu makusanyo ya maduhuli hadi kufikia mwezi Machi, 2014 na matumizi kwa mafungu yote. Aidhachangamoto zinazoikabili Ofisi hii na Taasisi zilizo chini yake katika kutekeleza majukumu, kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 ziliwasilishwa.

## 2.2 UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia umuhimu na unyeti wa Ofisi ya Waziri Mkuu ambaye ndiye Msaidizi Mkuu wa Rais, Mratibu na Msimamizi Mkuu wa shughuli na mipango yote ya Serikali katika sekta zote na ndani ya Bunge. Kamati yangu ilitoa maoni na ushauri mbalimbali kwa Ofisi hii wakati wa kupitisha makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka 2013/2014. Ushauri huo ulilenga kuboresha utendaji wa Ofisi hii ili kuhakikisha kuwa huduma bora na yenye ufanisi mkubwa kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua na kuthamini juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu katika kuleta maendeleo na ustawi wa nchi yetu. Hivyo basi, Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada hizo zinazolenga kuwakwamua wananchi wetu na kutoka kwenye umasikini na kuhakikisha kuwa wanapata maisha bora.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ulizingatiwa na utekelezaji wa mambo yaliyotolewa ushauri unaendelea. Yafuatayo ni baadhi ya maeneo yaliyofanyiwa kazi kutokana na ushauri uliotolewa na Kamati:-

(i) **Serikali kuwalipa fedha Wenyeviti wa Vijiji, Mitaa na Vitongoji walioshiriki katika zoezi la Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012.**

Kamati ilielezwa na serikali kuwa watendaji wote wamekwishalipwa stahili zao ambapo ilitumia kiasi cha shilingi **4,292,501,555.**

(ii) **Ili kuepuka maafa makubwa kama mafuriko, majanga ya moto yanayotokana na ujenzi holela, Serikali itoe elimu ya kutosha kwa wananchi.**

Serikali imeiagiza Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(TAMISEMI) pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ili kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kuzingatia taratibu za mipango miji kwani taasisi hizo ndizo zinazohusika moja kwa moja na kusimamia taratibu za mipango miji.

**(iii) Uanzishwaji wa Idara ya maafa katika ngazi ya kila Wilaya ili kurahishisha uratibu wa shughuli za maafa Nchini.**

Serikali imekwishaunda kamati za menejimenti ya maafa na kuainisha majukumu ya menejimenti hizo katika ngazi ya mikoa, wilaya, kata na vijiji katika mikoa yote ya Tanzania Bara zinazoratibu shughuli za maafa. Aidha kila Halmashauri imeteua mratibu ambaye anayewajibika kuratibu shughuli za maafa na kuwasiliana na Idara ya Maafa iliyoko Ofisi ya Waziri Mkuu ngazi ya taifa kwa muda wote.

**(iv) Ofisi ya Bunge kutoa elimu kuhusu utaratibu wa matibabu kwa Waheshimiwa Wabunge pamoja na familia zao.**

Kamati imeelezwa kwamba Ofisi ya Bunge imeingia Mkataba wa Mwaka mmoja na Jubilee Insurance kuanzia Januari, 2014 ambapo utaratibu wa matibabu kwa Waheshimiwa Wabunge na familia zao umekwishaanza.

**(v) Ofisi ya Bunge kujenga Ofisi za Waheshimiwa Wabunge katika majimbo yote na kuziwekea samani.**

Kamati ilielezwa kwamba TAMISEMI walijenga Ofisi 75 za Wabunge na kuzikabidhi Ofisi ya Bunge. Baada ya kukabidhiwa Ofisi hizo, Ofisi ya Bunge lilingia Mkataba na Jeshi la Magereza ili kutengeneza samani ambapo samani hizo zimekamilika nautaratibu wa kuzisambaza unaandaliwa. Aidha, Ofisi ya Bunge imeingia Mkataba na NSSF wa kujenga Ofisi za Wabunge 178 kwa mkupuo katika majimbo yote ya Bunge yasiyo na Ofisi za Wabunge.

**(vi) Serikali kutenga fedha za kutosha ili kuiwezesha Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuboresha Daftari la Kudumu la Mpiga Kura.**

Kamati ilielezwa kuwa Serikali imetoa jumla ya shilingi Bilioni 39kwa ajili ya maandalizi ya maboresho hayo**.**

**(vii) Ofisi ya Bunge iangalie uwezekano wa kununua mabasi mengine badala ya kukodisha.**

Ofisi ya Bunge imefanya utafiti na kubaini kuwa njia zote mbili za kununua na kukodisha magari zinafaa kulingana na mazingira husika.Mathalani Waheshimiwa Wabunge

wanaposafiri safari za mbali hutumia usafiri wa ndege na wanapofika mahali wanakokwenda, Ofisi ya Bunge huwakodia magari ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao. Aidha Ofisi ya Bunge imeazimwa magari manne na Wizara ya Mambo ya Nje ili kusaidia kurahisisha usafiri.

**(viii) Serikali kuongeza bajeti ya Msajili wa Vyama vya Siasa ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo**.

Bajeti ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa imeongezwa kutoka Shilingi 1,167,287,000 katika mwaka wa fedha 2013/2014 hadi kufikia shilingi 2,167,287,000 likikwa ni ongezeko la shilingi 500,000,000.

**(ix) Mheshimiwa Spika,**Kwa ujumla utekelezaji wa ushauri na maoni ya Kamati umekuwa mgumu hasa katika miradi ya maendeleo kutokana na fedha za miradi kuchelewa kutolewa, kutolewa kidogo ikilinganishwa na kiasi kinachotengwa au kutotolewa kabisa. Suala hili linafanya miradi miradi mingi kushindwa kutekelezwa inavyotakiwa. Ili kuhakikisha miradi hii inatekelezwa kwa ufanisi, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha fedha za miradi zinatolewa zote na kwa wakati.

## 2.2 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI OFISI YA WAZIRI MKUU PAMOJA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zilizo chini yake katika utekelezaji wa majukumu yake imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:-

### 1.3.1 Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Bunge:

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2013/2014 Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge ilikabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Kumekuwa na ukusanyaji hafifu wa maduhuli ya Serikali katika taasisi mbalimbali ikilinganishwa na makadirio yanayofanywa katika taasisi hizo. Katika Mwaka wa Fedha 2013/2014 Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na taasisi zilizo chini yake ilikadiriwa kukusanya maduhuli ya Jumla ya Shilingi **5,284,713, 079**, hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2014, Ofisi ya Waziri Mkuu ilikuwa imekusanya kiasi cha shilingi **1,329,596,919** sawa na asilimia 25 tu. Kiasi hiki ni kidogo sana ikilinganishwa na makisio yaliyotarajiwa.

(ii) Mfumo wa ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa fedha zinazotolewa na Serikali kwa ajili ya maendeleo kutokuwa madhubuti hivyo kusababisha malengo ya ukusanyaji na utekelezaji wa mipangokutokufikiwa.

(iii) Idara ya Maafa na Mpigachapa Mkuu wa Serikali pamoja na unyeti na umuhimu wake kwa taifa, zinakabiliwa na upungufu mkubwa wa watumishi hivyo kuathiri utendaji na ufanisi.

(iv) Hazina kuchelewa kupeleka fedha zinazoidhinishwa na Bunge katika Ofisi na taasisi za serikali.Mathalani, mradi wa ujenzi wa makazi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 ulitengewa kiasi cha shilingi 1,500,000,000 hadi kufikia Machi 30,2014 Ofisi ya Waziri Mkuu ilikuwa haijapokea kiasi chochote cha fedha kutoka Hazina.

Aidha, mradi wa kuendeleza eneo la Makaburi ya Viongozi Dodoma kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 ulitengewa kiasi cha shilingi 1,000,000,000 lakini hadi wakati Kamati inaandaa taarifa hii, hakuna kiasi chochote cha fedha kilichokuwa kimetolewa.

**1.3.2 Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa;**

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa ambayo inahusika na usajili na usimamizi wa mienendo ya Vyama vya Siasa inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Sheria ya Usajili wa Vyama vya Siasa ( The Political Parties Act Cap 258) kuwa na mapungufu makubwa na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu yake.

(ii) Kutokana na mabadiliko ya Sheria ambapo jukumu la kukagua hesabu za Vyama vya Siasa limehamishiwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali toka Makampuni ya Ukaguzi, Msajili wa Vyama vya siasa hakuweza kutoa taarifa kwa Umma kuhusu hesabu zilizokaguliwa kwa vyama vya siasa vinavyopata ruzuku kutoka serikalini kuanzia Mwaka 2009 hadi 2013.

**1.3.4 Tume ya Taifa ya Uchaguzi:**

**Mheshimiwa Spika**,Taasisi hii ni muhimu katika Taifa kutokana wajibu mkubwa wa kuratibu na kusimamia chaguzi mbalimbali nchini. Katika kutekeleza

majukumu haya, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inakabaliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Tume ya Taifa ya Uchaguzi haina jengo la ofisi hivyo imeendelea kupanga katika kipindi chote toka mfumo wa Vyama Vingi uanzishwe. Jambo hili linasababisha Tume kutumia gharama kubwa katika kulipia pango la ofisi.

(ii) Serikali bado haijaipatia fedha Tume ili iweze kulipa madeni yake likiwemo deni la shiling**i 2,254,323,693** zilizotokana na gharama za uchaguzi za Mwaka 2010. Deni hili linaisababishia usumbufu na kupunguza uaminifu kutoka kwa watu na taasisi zinazoidai Tume.

Tume kutokuwa na watumishi wake wa kutosha na hivyo kutegemea watumishi wa Serikali katika Halmashauri kusimamia chaguzi mbalimbali, hali inayo sababisha wadau wa uchaguzi kuilalamikia kwa dhana kwamba kwa kutumia watumishi wa serikali katika zoezi la kusimamia uchaguzi kama vile walimu kunaifanya Tume kutokuwa huru.

### 1.3.5 Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali:

**Mheshimiwa Spika**, Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali inafanya kazi muhimu ya kuchapisha nyaraka mbalimbali za Serikali hapa nchini. Katika kutekeleza majukumu hayo, idara inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali inamtambo mmoja wenye uwezo wa kuchapa rangi nne tu katika upande mmoja wa karatasi. Kutokana na hali hiyo kunahitajika Mashine nyingine ndogo sita ili kuweza kuchapa pande zote nne.Aidha idara ina upungufu wa mtambo mmoja mkubwa wa umaliziaji. Changamoto hiiinasababisha kutotekelezwa majukumu ya uchapaji kwa ufanisi na kwa wakati.

(ii) Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kupokea fedha kidogo za "Retention" ambazo hazikidhi gharama za uzalishaji.Aidha fedha za Retention hazitolewi kwa wakati na Hazina, mathalani kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 Idara haikupewa Fedha ilizokusanya takribani shilingi milioni **809.** Hali hii inakwamisha ukusanyaji wa maduhuli kwani Idara inashindwa kununua malighafi ya kutosha.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 imetengewa jumla ya sh **224,932**, **198,000**. Mgawanyo wake ni kama ifuatavyo; Fungu 25-Waziri Mkuu, sh 6,358,738,000 zinaombwa kwa matumizi ya kawaida. Fungu 27-Msajili wa Vyama vya Siasa kiasi cha sh, **20,732,781,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida, Fungu 37-Ofisi ya Waziri Mkuu kiasi cha sh **36, 081,195,000** kinaombwa kwa matumizi ya kawaida na **sh 18,498,285,000** kwa miradi ya maendeleo, Fungu 42-Mfuko wa Bunge unaomba jumla ya Sh. **123,941,455,000** kati ya fedha hizo Sh. **15,520,327,000 z**inaombwa kwa ajili ya mishahara ya Wabunge na watumishi, Sh.108,421,128,000 zitatumika kuendeshea mikutano ya Bunge na Kamati pamoja na shughuli zingine za kiutawala. Vilevile sh**, 8,755,439,000** zinaombwa kwa ajili ya mpango wa maendeleo.Fungu 61-Tume ya Taifa ya Uchaguzi kiasi cha **shilingi 4,371,895,000** kinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kwaida.

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia taarifa iliiyowasilishwa mbele ya Kamati mnamo Tarehe 2 Mei 2014 ,pamoja na maombi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 kama yalivyoainishwa kwa kila fungu, Kamati inatoa maoni na mapendekezo yafuatayo:

### 3.1 WAZIRI MKUU NA OFISI YA WAZIRI MKUU: fungu 25 na 37

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia unyeti wa Ofisi ya Waziri Mkuu ambaye ndiye msaidizi mkuu wa Rais,mratibu na msimamizi mkuu wa shughuli na mipango yote ya Serikali katika sekta zote nchini na ndani ya Bunge,mhimizaji mkuu wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya wananchi mijini na vijijini katika misingi ya utawala bora, kwa mantiki hii Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Ofisi hii itengewe fedha za kutoshana kuajiri watumishi wenye taaluma stahiki iliiweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

(ii) Kwa kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu ni msimamizi wa shughuli za serikali ikiwemo mapambano dhidi ya rushwa, ni vema watumishi katika ofisi hii wawe mfano kwa jamii kwa kutojihusisha na vitendo vya rushwa.

(iii) Mheshimiwa Waziri Mkuu katika kutekeleza majukumu yake, hufanya ziara katika sehemu mbalimbali nchini. Kwa kufanya hivyo wakati mwingine hulazimika kutoa ahadi ili kutatua kero na

changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi. Kamati imebaini kwamba baadhi ya ahadi zinazotolewa hazitekelezwi kwa wakati. Hivyo basi, Kamati inashauri kwamba, ipo haja ya kuwepo na mfumo mzuri wa kubainisha ahadi zote zinazotolewa na Waziri Mkuu katika maeneo mbalimbali na kuzitekeleza kwa wakati.

(iv) Kuhusu mradi wa kuendeleza eneo la Makaburi ya Viongozi, Kamati inashauri Serikali itilie maanani uwepo wa mradi huu kwa kuendelea kuutengea fedha na kuhakikisha kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya Mradi huu zinatolewa ili zifanye kazi inayokusudiwa. Kamati inasisitiza kuwa kiasi cha shilingi bilioni moja zilizotengwa kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 zitolewe kabla ya mwaka wa fedha haujaisha.

(v) Kwa kuwa Serikali inajenga Ofisi na Makazi ya Waziri Mkuu Dodoma, Kamati inashauri kasi ya utoaji wa fedha zinazotengwa kwa ajili ya ujenzi huo iongezwe ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa fedha zilizotengwa kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 zinatolewa kabla ya kuisha kwa mwaka wa fedha. Vilevile bajeti ya kutosha itengwe ili kukamilisha azma hiyo.

### 3.1.1 Ustawishaji Makao Makuu Dodoma.

**Mheshimiwa Spika**,Uanzishwaji wa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kuwa Mji wa Dodoma unapangwa na kuendelezwa ili kuufanya kuwa na sura na hadhi ya Makao Makuu ya Nchi.

Kamati inatambua juhudi zinazofanywa na Serikali katika kutimiza azma yake. Hata hivyo Kamati inashauri kuwalli kutimiza azma hii Serikali iweke kipaumbele kwa kutenga bajeti ya kutosha na kuhakikisha fedha zinazotengwa kwa ajili ya kuendeleza mji zinatolewa ikiwa ni pamoja na Fedha zilizotengwa kwa Mwaka 2013/2014 kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi ambao maeneo yao yalichukuliwa kwa ajili ya miradi ya kupima viwanja ili kuwezesha Mamlaka hiyo kutekeleza Majukumu yake.

Aidha Kamati inashauri kuwa Serikali, Idara na Taasisi zote za Serikali ziweke mipango ya ujenzi wa ofisi zao Dodoma ili kuhakikisha kuwa azma ya Serikali ya kuhamia Dodoma inatimia.

### 3.1.2 Idara ya Maafa

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha Idara ya Maafa, Kamati inatoa ushauri na mapendekezo kama ifuatavyo:-

(i) Pamoja na Serikali kutekeleza ushauri wa kuanzisha idara ya maafa ,katika kila Wilaya hapa nchini,Kamati inashauri idara hii iboreshwe kwa kujengewa uwezo wa fedha na rasilimali watu, ujuzi na vifaa, kwa lengo la kuisaidia nchi yetu kukabiliana na maafa ya aina mbalimbali yatakayoweza kujitokeza kama ilivyokusudiwa.

(ii) Katika jitihada za uokoaji pale maafa yanapojitokeza, ni vyema vyombo vya ulinzi na usalama kama Jeshi la wananchi washirikishwe kikamilifu kwani wao wana ujuzi na utaalamu wa kutosha katika masuala ya uokoaji. Aidha, kwa kuwa taratibu za kulishirikisha jeshi la Wananchi lina masharti magumu, ,kamati inashauri Ofisi ya Waziri Mkuu ifanye mazungumzo na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la wananchi ili walegeze masharti ya taratibu za Jeshi na kuruhusu Jeshi na vyombo vya Jeshi vitumike kuokoa maisha ya wananchi pale maafa yanapojitokeza hasa maafa ya baharini.

(iii) Serikali iandae utaratibu utakaowezesha fedha na misaada inayotolewa na Serikali na wananchi kwa ajili ya kusaidia watu waliokumbwa na maafa inawafikia walengwa kama ilivyokusudiwa.

(iv) Kamati inashauri pia kwamba Idara ya maafa ihakikishe inachukua hatua za haraka katika kuokoa na kutoa misaada pale maafa yanapojitokeza.

### 3.1.3 Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika**,Wakati wa kupitia utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2013/014 na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 ,Kamati ilibaini kuwa Idara ya Mpiga Chapa wa Serikali imekuwa haitekelezi majukumu yake kwa ufanisi, ili kuboresha utendaji wa Idara hii Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali iboreshe Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kununua Mashine zinazoweza kuchapa rangi nne pande mbili za karatasi kwa wakati mmoja na kwa haraka. Aidha Mtambo Mmoja Mkubwa wa umaliziaji(print-finishing) ili kuwezesha kukusanya na kufunga vitabu na majarida mbalimbali yanayochapishwa kwa haraka na ufanisi.

(ii) Kwa kuwa ofisi ya mpiga chapahukusanya maduhuli ya kutosha na kuyapeleka hazina,Kamati inashauri Idara hii ipewe fedha za "retention" ili kuiwezesha Idara kununua malighafi na kufanyakazi kwa tija kwa lengo la kujiendesha yenyewe.

(iii) Idara iruhusiwe kupokea kazi za wate wengine nje ya kazi za Serikali ili kuiwezesha kujiendesha kibiashara badala ya kutegemea ruzuku kutoka serikalini.

(iv) Kamati inaendelea kutoa rai kwa Serikali kuwa tozo la 26% ya mapato Idara yanayotokana na shughuli za upigaji chapa lipunguzwe hadi kufikia 5% kwani bajeti inayotengewa idara haikidhi mahitaji.

### 4.0 MSAJILI WA VYAMAVYA SIASA: Fungu 27

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Msajili wa Vyama Vya Siasa nchini ni muhimu kwa ustawi na ushamiri wa demokrasia hapa nchini. Kwa kutambua umuhimu wa Ofisi hii ili kuhakikisha kuwa demokrasia inaendelezwa, Kamati inatoa maoni na ushauri ili kuiimarisha ofisi hii kama ifuatavyo:-

(i) Msajili wa Vyama vya Siasa ahakikishe kuwa taarifa za fedha za vyama vya siasa zinatangazwa kwa mujibu wa sheria ya vyama vya siasa katika gazeti la serikali ili kuwezesha umma kupata taarifa sahihi juu ya ruzuku inayotolewa kwa vyama vya siasa pamoja namna inavyotumika.

(ii) Kamati imepata taarifa kwamba serikali inakusudia kuleta Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa- The Political Parties Act, CAP 258 R.E 2002. Kamati inaona lengohilo ni jema na Kamati inashauri mchakato wa kuleta marekebisho hayo Bungeni uharakishwe ili wadau wa Vyama vya Siasa wanufaike na maboresho hayo.

(iii) Msajili wa Vyama Vya Siasa aendelee kuratibu kwa karibu zaidi masuala ya maridhiano kwa Vyama vya Siasa kupitia Baraza la Demokrasia Nchini( Tanzania Centre for Democracy) ili kukuza na kuimarisha demokrasia kwa lengo la kudumisha amani na utulivu nchini.

### 5.0 MFUKO WA BUNGE: Fungu 42

**MheshimiwaSpika,**Kuhusu Mfuko wa Bunge Kamati inaipongeza Ofisi ya Mheshimiwa Spika pamoja na Tume ya Utumishi wa Bunge kwa kuendelea kutoa ushauri na mapendekezo kwa Mheshimiwa Rais ya kuboresha maslahi ya

Waheshimiwa Wabunge na watumishi wa Bunge ili kuhakikisha kuwa Wabunge na watumishi wa Bunge wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kuleta tija kwa taifa. Hata hivyo ili kuhakikisha Bunge linatekeleza majukumu yake ipasavyo Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Kwa kuwa Ofisi ya Bunge imeingia mkataba na mkandarasi wa kujitegemea ''Jubilee Insurance"ili kutoa matibabu kwa waheshimiwa Wabunge na familia zao,Kamati inashauri kuwa Ofisi ya Bunge imuelekeze mkandarasi huyo atoe elimu kwa Waheshimiwa Wabunge kuhusu utaratibu wa utoaji huduma,aina ya matibabu na hopitali zinazohusika na mkataba huo na mahali zinakopatikana.

(ii) Ofisi ya Bunge iharakishe Mchakato wa makabidhiano ya Ofisi 75 zilizojengwa na TAMISEMI kwa ajili Wabunge katika Majimbo husika na kuziwekea samani ili kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kuanza kuzitumia katika kuwahudumia wananchi kwa karibu na kwa ufanisi zaidi.

(iii) Kamati imepewa taarifa kuwa ofisi ya Bunge imeingia mkataba na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii(NSSF) kujenga ofisi 178 za Waheshimiwa Wabunge katika majimbo ambayo hayana ofisi ,Kamati inaona ni jambo jema,hivyo inashauri kazi hiyo ianze na kukamilishwa mapema iwezekanavyo ili ofisi hizo zianze kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

(iv) Ofisi ya Bunge kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ziweke vigezo sahihi vya kuyatambua na kutenga maeneo ya ujenzi wa Ofisi za Waheshimiwa Wabunge. Lengo ni kuhakikisha kuwa Ofisi hizo zinajengwa katika maeneo stahiki kwa maslahi wa wananchi ili ziweze kutumika kwa miaka mingi inayokuja.

(v) Ofisi ya Bunge iangalie uwezekano wa kuwapatia Waheshimiwa Wabunge wote Ofisi za kufanyia kazi Wanapokuwepo Dodoma ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa umakini na ufanisi.

(vi) Ofisi ya Bunge ihakikishe inaingia mikataba na mabenki yanayotoa mikopo yenye bima ili kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza kutokana na deni la mkopo huo kwa familia za Wabunge hao endapo watapoteza maisha kwa namna moja au nyingine.

**6.0 TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI: Fungu 61**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatoa ushauri na mapendekezo yafuatayo kuhusu Tume ya Taifa ya Uchaguzi**.**

I) Tume ya Taifa ya Uchaguzi ndiyo iliyopewa majukumu ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Mpiga kura mara mbili kati ya kipindi kimoja cha uchaguzi na kipindi kingine .Ili kutekeleza jukumu hili lililoainishwa na sheria,Kamati inashauri fedha zinazotengwa kwa ajili ya kazi hiyo zitolewe kwa wakati.

II) Kwa kuwa fedha za Tume za kulipa deni hazikutolewa kama kamati yangu ilivyoshauri katika bajeti ya Mwaka 2013/2014,Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Serikali itoe kiasi cha sh **2,254,323,693** zilizotokana na gharama mbalimbali wakati wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010.

III) Kamati imeelezwa kuwa Tume imepewa kiasi cha shilingi **Bilioni 39** ili kuboresha Daftari la Kudumu la Mpiga Kura. Hata hivyo Kamati inashauri taratibu za maandalizi ya Uboreshaji huo zitekelezwe mapema iwezekanavyo kwani Daftari hilolinategemewa kutumika wakati wa upigaji wa kura ya maoni kuhusu Katiba Mpya.

IV) Tume kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iendelee kutoa elimu ya uraia na umuhimu wa kupiga kura ili kuwahamasisha wananchi kujitokeza kupiga kura katika chaguzi mbalimbali hapa nchini.

V) Serikali itenge fedha ili kuiwezesha Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuanza mchakato wa ujenzi wa jengo la Ofisi yake ili kupunguza gharama za upangaji pamoja na kuiwezesha kufanya kazi katika mazingira bora na ya kisasa.

VI) Kwa kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatakiwa kuwa huru katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati inashauri Tume ipewe kibali ili iweze kuajiri watumisi wa kutosha watakaoweza kufanya kazi hadi katika ngazi ya Halmashauri na kuondoa dhana kwamba kwa kutumia watumishi wa Halmashauri katika chaguzi kunaifanya tume kutokuwa huru.

VII) Tume ya Taifa ya Uchaguzi iwezeshwe kifedha ili iweze kupeleka watumishi wengi zaidi kwenda kushuhudia chaguzi mbalimbali zinazofanyika katika nchi mbalimbali jirani kwani kwa kufanya hivyo Tume itajifunza namna bora ya kusimamia chaguzi.

## 7.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** mwisho, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala. Napenda nitumie nafasi hii pia kukupongeza kwa dhati kwa jinsi unavyoliongoza Bunge hili ambalo ni chombo cha uwakilishi wa Wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali ili kuhakikisha kuwa ustawi wa wananchi ndio kipaumbele cha kwanza.

**Mheshimiwa Spika,** nimpongeze pia Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania: Kwanza, kwa jinsi anavyoratibu vizuri na kufuatilia kwa karibu shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Wizara zote katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwani sote tunatambua kuwa changamoto zinazoikabili Serikali yetu ni nyingi hivyo kuzisimamia shughuli zote hizo ni mzigo mkubwa.

Pili, kwa kuwa karibu na Ofisi ya Bunge kwa kuwa tayari kuyashughulikia matatizo ya Kamati za Bunge wakati zinapotekeleza majukumu yake kwa niaba ya Bunge.Aidha, namshukuru kwa ushirikiano wake mkubwa kwa Kamati yangu wakati wa uchambuzi wa Bajeti kwani amekuwa mwepesi wa kupokea ushauri na kutuwezesha kufikia hapa tulipo.

**Mheshimiwa Spika,**pia napendanimshukuru Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge na , Makatibu Wakuu, Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi, Idara na vitengo pamoja na Maafisa wote, kwa maelezo na ufafanuzi wa kina walioutoa kwa Kamati wakati wa kuchambua bajeti ya Wizara hii na kukubali kufanya kazi hadi nyakati za usiku kutokana na ufinyu wa muda.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio haya. Umahiri na uzalendo wao kwa Nchi yetu uliwafanya kuvumilia na kufanya kazi hata katika mazingira magumu ili kukamilisha. Kwa heshima naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

(i) Mhe. William M.Ngeleja, Mb - Mwenyekiti
(ii) Gosbert B. Blandes, Mb - M/Mwenyekiti
(iii) Mhe. Abbas Zuberi Mtemvu, Mb - Mjumbe
(iv) Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mb - Mjumbe
(v) Mhe. Nimrod Elirehema Mkono, Mb- Mjumbe
(vi) Mhe. Halima J. Mdee, Mb - Mjumbe
(vii) Mhe. Fakharia K. Shomar, Mb - Mjumbe
(viii) Mhe. Rukia Kassim Ahmed, Mb - Mjumbe
(ix) Mhe. Ali Khamis Seif, Mb - Mjumbe

(x) Mhe. Felix Francis Mkosamali, Mb - Mjumbe
(xi) Mh, Abdallah Sharia Ameir, Mb - Mjumbe
(xii) Mhe. Mustapha B. Akunaay, Mb - Mjumbe
(xiii) Mhe. Mariam Reuben Kasembe, Mb-Mjumbe
(xiv) Mhe. Tundu A. Mughwai Lissu, Mb - Mjumbe
(xv) Mhe. Deogratias A. Ntukamazina, Mb-Mjumbe
(xvi) Mhe. Jason S. Rweikiza, Mb - Mjumbe
(xvii) Mhe.Nyambari C.M.Nyangwine.Mb - Mjumbe
(xviii) Mhe. Ramadhan Haji Saleh - Mjumbe
(xix) Mhe. Zahra Ali Hamad, Mb - Mjumbe
(xx) Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb - Mjumbe

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa makini na madhubuti wa Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, nawashukuru ndugu Charles Mloka, ndugu Matamus Fungo, Maria Mdulugu, Mark Tanda na Abdallah Selemani kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Taasisi zake kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

William Mganga Ngeleja, (Mb.)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA**
Mei, 2014

**SPIKA:** Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Yuko wapi Mwenyekiti wa Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa? Jamani! Haya anayefuata ni Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara!

**Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara kama ilivyosomwa Bungeni**

**MHE. DUNSTAN LUKA KITANDULA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara kuhusu

utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 37 – Uwekezaji na Uwezeshaji) kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema ambaye ametuwezesha kuendelea kuwa wazima wenye afya njema.

Mheshimiwa Spika, wakati wa vikao vya Kamati vilivyofanyika Bagamoyo, Kamati ilipokea Taarifa kuhusu Utekelezaji wa Shughuli za Uendeshaji wa Sekta Binafsi, Uwekezaji na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa mwaka wa Fedha 2013/2014 na Makadirio ya Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2014/2015. Kamati ilipokea na kujadili kwa kina taarifa hiyo na hatimaye kuishauri Ofisi hiyo ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Majukumu kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014. Serikali ina jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa sekta binafsi inakuwa mhimili wa Uchumi wa Taifa kupitia kuweka mazingira wezeshi, sambamba na kusimamia utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa na Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Jitihada za kukuza Uwekezaji, kuendeleza sekta binafsi na kuwezesha wananchi kiuchumi ni masuala muhimu yanayohitaji msukumo wa kipekee ili Taifa liweze kuwa na uchumi imara. Katika kufanikisha haya Serikali ilijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kuratibu na kusimamia maendeleo ya sekta binafsi nchini chini ya Uratibu wa Taasisi ya Sekta Binafsi *(TPSF)*;

(ii) Kuandaa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Sekta Binafsi na Sheria ya Sekta Binafsi;

(iii) Kuweka mfumo thabiti wa kisera, kisheria na kitaasisi kama hatua muhimu ya utekelezaji wa Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

(iv) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa azma ya Kilimo Kwanza na Mpango wa kukuza Kilimo Ukanda wa Kusini *(SAGCOT)*.

(v) Kuendelea kuboresha mazingira ya wezeshi ya Biashara na uwekezaji nchini.

(vi) Kuhamasisha na kuvutia uwekezaji wa ndani na nje nchi kupitia Kituo cha Uwekezaji *(TIC)*.

(vii) Kuratibu na kusimamia programu na mifuko mbalimbali ya uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio haya, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi) inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Kuwepo kwa Sera, Sheria na Mifumo ya Kitaasisi inayokinzana na mazingira wezeshi kwa sekta binafsi.

(ii) Mtazamo potofu katika jamii kuwa lengo la uwekezaji ni kupora rasilimali za nchi.

(iii) Kukosekana kwa Miundombinu ya msingi kama vile maji, umeme, barabara, reli na bandari hali inayoongeza kwa kiasi kikubwa gharama za kufanya biashara na kuwekeza nchini.

(iv) Mahakama kuchukua muda mrefu katika kutoa hukumu za kesi zinazohusu masuala ya biashara na uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015. Kimsingi Kamati inakubaliana na misingi na shabaha ya Ofisi ya Waziri Mkuu katika utekelezaji wa Bajeti kwenye Fungu la 37; ambazo zinalenga kutatua changamoto zinazokwamisha jitihada za Serikali katika masuala ya Uwekezaji na Uwezeshaji ambayo ni maeneo ya kimkakati katika kukuza uchumi wa nchi na kupunguza umaskini wa kipato.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2014/2015, unaonesha kuwa mwenendo wa Hali ya Uchumi katika mwaka 2013, Pato halisi la Taifa lilikuwa kwa kiwango cha asilimia 7.0% ikilinganishwa na asilimia 6.9% mwaka 2012. Kiwango cha juu cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi kilikuwa katika shughuli za sekta ya mawasiliano iliyokua kwa asilimia 22.8%; ujenzi asilimia 8.6%; biashara ya jumla na rejareja asilimia 8.3%; hoteli na migahawa asilimia 6.3%.

Mheshimiwa Spika, aidha, wakati ambapo kwa upande wa sekta ya kilimo ukuaji ulibakia kama ulivyokuwa mwaka 2012 yaani asilimia 4.3%; sekta ya Uvuvi, kasi ya ukuaji imepungua hadi asilimia 2.2% kutoka asilimia 2.9% kwa mwaka 2012. Sekta ya mifugo ilikua kwa asilimia 3.8% kutoka asilimia 3.1% kwa mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu hizi zinaonesha kuwa bado tuna safari ndefu ya kumkomboa mwananchi mwenye kipato cha chini ili aweze kufaidika na Rasilimali za Taifa. Hii ni kutokana na ukweli kwamba kwa muda mrefu sasa

shughuli za kiuchumi ambazo zimekuwa zikiongoza katika ukuaji zipo katika sekta zinazogusa wananchi wachache.

Kamati inaendelea kuishauri Serikali kwamba kuna haja ya kuongeza msukumo mkubwa zaidi kwenye shughuli za sekta ya Kilimo, Uvuvi na Ufugaji ambazo zinaajiri na kutegemewa na Watanzania wengi. Kuimarika kwa sekta hizi kutasaidia kuleta uwiano kati ya ukuaji wa uchumi na kipato cha wananchi. Kamati inahoji ni lini kama Taifa tutaona umuhimu wa kuwekeza katika ufugaji wa samaki kwa ukanda wa bahari kama moja ya mkakati wa kuwa na usalama wa chakula na kuinua uchumi wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Fedha ni eneo lingine linalopaswa kupewa kipaumbele; hususan katika suala la upatikanaji wa mikopo na hatua nyingine za uwezeshaji. Ni maoni ya Kamati kuwa pamoja na kuongezeka kwa fursa za upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi, sehemu kubwa ya mikopo hiyo bado haiwafikii walengwa na hivyo kushindwa kutoa matokeo tarajiwa katika kumwezesha mwananchi wa kawaida. Aidha, hata pale mikopo hii inapowafikia walengwa kwa uchache, bado mikopo hiyo inakuwa na riba kubwa na hivyo kuwa kikwazo kikubwa katika kupunguza umasikini na kuongeza chachu ya ukuaji wa uchumi.

Ripoti ya utafiti uliofanyika hivi karibuni (*FINSCOP)* ya mwaka 2013 inaonesha kuwa asilimia 35 ya wakulima wadogo waliopo vijijini hawapati huduma za kifedha, licha ya kuwepo kwa huduma za mitandao ya simu. Kamati inashauri Serikali kuwa umakini unahitajika katika kuhakikisha kuwa huduma za kifedha zinazotolewa nchini zinalenga mahitaji halisi ya wananchi; hususan wananchi wenye kipato cha chini na kwa masharti nafuu.

Kamati imebaini kuwa, kuna tatizo kubwa la urejeshaji wa mikopo hapa nchini, jambo ambalo linarudisha nyuma jitihada za uwezeshaji wananchi. Takwimu zinaonesha kuwa idadi kubwa ya mifuko inayotoa mikopo hapa nchini inakabiliwa na tatizo la mikopo kutorejeshwa kwa wakati, takriban asilimia 20; kiwango hiki ni kikubwa mno kuachwa kupotea. Serikali inashauriwa ifanye tathmini ya fedha za mikopo inayotolewa kupitia mifuko mbalimbali ili kubaini kiwango halisi cha upotevu wa fedha na hatimaye kuweka mikakati ya kurejeshwa kwa fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, Ripoti ya Benki ya Dunia (*Doing Business)* ya mwaka 2014, inaonesha kwamba nchi yetu bado inakabiliwa na gharama kubwa za kufanya biashara na kuwekeza ikilinganishwa na nchi kadhaa za Afrika Mashariki. Aidha, kati ya nchi 189 zilizofanyiwa utafiti, nchi yetu imeshika nafasi ya 145 na hivyo kuzidi kuporomoka ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo tulikuwa tunashika nafasi ya 136.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa hatutaweza kuendelea bila ya kuwa na msukumo wa hali ya juu wa kuboresha mazingira ya kufanyia biashara na kuwekeza ili kuongeza kasi ya kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Hatua hii lazima iambatane na kuondoa urasimu, ucheleweshaji au kutokutoa maamuzi kwa wakati pamoja na kurekebisha baadhi ya sheria zetu na kuimarisha miundombinu ya msingi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza kuwa, bado idadi kubwa ya Watanzania hawajafaidika na mikakati mbalimbali ya Serikali ya kuwawezesha wananchi kiuchumi. Licha ya kuwepo programu mbalimbali kama vile Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Mpango wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi na Kuongeza Ajira; Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wafanyabiashara Wadogo *(NEDF)* na mingine mingi yenye lengo la kuwasaidia na kuwawezesha wananchi wengi wenye kipato cha chini, bado jitihada hizi hazijaweza kuwanufaisha wananchi kikamilifu kutokana na tatizo la *targeting* na utekelezaji wake kutosimamiwi ipasavyo.

Vile vile baadhi ya Mifuko hii mitaji yake ni midogo kuweza kutosheleza mahitaji ya wananchi na baadhi inaongozwa na watu wasio na ujuzi stahiki kwenye eneo la taaluma ya mikopo na elimu ya ujasiriamali. Kamati inashauri Serikali kufuatilia suala hili ili kuhakikisha kwamba, malengo ya *program* hizo yanafikiwa ikiwemo kusaidia kuongeza mitaji ya Mifuko hiyo, kwa mfano, Mfuko wa Vijana; pamoja na kuhakikisha kuwa inaongozwa na watu wenye ujuzi na uzoefu stahiki katika masula ya mikopo na ujasiriliamali.

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi imeendelea kuwa changamoto kubwa katika uchumi wetu. Pamoja na lengo zuri la misamaha hiyo ambalo ni kuvutia na kuhamasisha uwekezaji hapa nchini; ili hatimaye Serikali iweze kupata kodi baada ya uzalishaji kukua na ajira kuongezeka, Kamati inaona kuwa misamaha hii imekuwa uchochoro mkubwa wa kukwepea kodi hapa nchini. Kamati inaishauri  Serikali kufanya tathmini ya kina kuona kwanini misamaha hii iendelee.

Mheshimiwa Spika, aidha, tathmini ioneshe kwa uwazi faida na hasara za misamaha hiyo kwenye uchumi wetu. Inashauriwa vile vile kuwa tathmini hii isilenge misamaha inayotolewa kupitia Kituo cha Uwekezaji (*TIC*) pekee, bali pia maeneo yote ikiwemo misamaha inayotolewa kupitia *TRA*.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inashuhudia uwekezaji mkubwa katika maeneo ya uchimbaji wa madini, utafutaji gesi, mahoteli, na viwanda. Hata hivyo, jambo la kusikitisha ni kwamba mahitaji muhimu kwa matumizi katika maeneo haya hususan nyama, matunda na hata mbogamboga huagizwa kutoka nje ya nchi badala ya mazao hayo kununuliwa hapa nchini kwa lengo la kukuza uchumi. Hali hii sio tu kwamba inazorotesha uchumi bali pia

inawanyima wananchi fursa zitokanazo na uwekezaji huu. Kamati inaishauri Serikali kuweka mkakati madhubuti wa kuwaunganisha wazalishaji wanaoishi katika maeneo yanayozunguka miradi hii kupitia mikataba maalum ya uzalishaji, kuwapatia huduma za ugani na mitaji ili waweze kuzalisha bidhaa na mazao yenye ubora unaohitajika na hivyo kulikamata soko husika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali juu ya umuhimu wa ushiriki wa Serikali katika ngazi ya Mkoa na Wilaya pamoja na ushiriki wa sekta binafsi kupitia miradi ya *PPP* katika shughuli za uwekezaji na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Pamoja na makongamano ya uwekezaji yanayoendelea katika mikoa mbalimbali kwa sasa, ni vyema makongamano hayo yakaandaliwa kitaalam zaidi ili yaweze kuwa na tija zaidi kuliko ilivyo sasa. Mfumo uliopo sasa wa kubaini fursa za uwekezaji katika ngazi za Mikoa na Wilaya uboreshwe kwa Serikali kutenga fedha ili kuwezesha upembuzi yakinifu kufanyika kwa miradi inayoibuliwa ili kuwezesha ushiriki wa wananchi kupitia Halmashauri zao kwa njia ya ubia na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Nchi; Uwekezaji na Uwezeshaji Dkt. Mary Michael Nagu, Katibu Mkuu, pamoja na wataalamu wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuwa tayari kutoa ufafanuzi na kupokea maoni na ushauri wa Wajumbe wa Kamati yangu wakati wote wa mjadala wa makadirio haya. Ni matarajio ya Kamati kuwa ushirikiano huu utaendelea katika mwaka ujao wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara kwa ushirikiano na uzalendo walionyesha katika kufanya mambo ya kusimamia shughuli za Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana wewe mwenyewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kutupatia maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah. Halikadhalika, napenda kuwashukuru Ndugu James Warburg, Ndugu Lawrence Robert Makigi na Ndugu Pauline Mavunde kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 37-Uwekezaji na Uwezeshaji, yenye maombi ya jumla ya sh. 10,158,193,800/=. Kati ya fedha hizo sh. 8,118,193,800/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na sh. 2,040,000,000/= ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara kama ilivyowasilishwa Mezani**

## TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA WAZIRI MKUU, FUNGU 37- UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

### 1.0. UTANGULIZI:

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kanuni ya 99(9) ya Kanuni za kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Fungu 37 – Uwekezaji na Uwezeshaji) kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa vikao vya Kamati vilivyofanyika Bagamoyo, Kamati ilipokea Taarifa kuhusu Utekelezaji wa Shughuli za Uendelezaji wa Sekta Binafsi, Uwekezaji na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa mwaka wa Fedha 2013/2014 na Makadirio ya Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2014/2015. Kamati ilipokea na kujadili kwa kina taarifa hiyo na hatimaye kuishauri Ofisi hiyo ipasavyo.

### 2.0. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ina jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa sekta binafsi inakuwa mhimili wa Uchumi wa Taifa kupitia kuweka mazingira wezeshi, sambamba na kusimamia utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa na Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Jitihada za kukuza Uwekezaji, kuendeleza sekta binafsi na kuwezesha wananchi kiuchumi ni masuala muhimu yanayohitaji msukumo wa kipekee ili Taifa liweze kuwa na uchumi imara. Katika kufanikisha haya Serikali ilijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

- Kuratibu na kusimamia maendeleo ya sekta Binafsi nchini chini ya uratibu wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF)
- Kuandaa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Sekta Binafsi na Sheria ya Sekta Binafsi
- Kuandaa Sera ya Ushiriki na Umiliki wa Uchumi kwa Uwekezaji Unaofanyika Nchini (The National Local Content Policy)
- Kuweka mfumo thabiti wa kisera, kisheria na kitaasisi kama hatua muhimu ya utekelezaji wa Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

- Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Azma ya KILIMO KWANZA na Mpango wa kukuza Kilimo Ukanda wa Kusini (SAGCOT).
- Kuendelea kuboresha mazingira ya wezeshi ya Biashara na uwekezaji nchini.
- Kuhamasisha na kuvutia uwekezaji wa ndani na nje nchi kupitia kituo cha Uwekezaji (TIC).
- Kuratibu na kusimamia programu na mifuko mbalimbali ya uwezeshaji wananchi kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio haya, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi) inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- Kuwepo kwa Sera, Sheria na Mifumo ya Kitaasisi inayokinzana na mazingira wezeshi kwa sekta binafsi.
- Mtazamo potofu katika jamii kuwa lengo la uwekezaji ni kupora rasilimali za nchi.
- Kukosekana kwa Miundombinu ya msingi kama vile maji, umeme, barabara, reli na bandari hali inayoongeza kwa kiasi kikubwa gharama za kufanya biashara na kuwekeza nchini.
- Mahakama kuchukua muda mrefu katika kutoa hukumu za kesi zinazohusu masuala ya biashara na uwekezaji nchini.

## 3.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

**3.1 Mheshimiwa Spika,** Kimsingi kamati inakubaliana na misingi na shabaha ya Ofisi ya Waziri Mkuu katika utekelezaji wa Bajeti kwenye Fungu la 37; ambazo zinalenga kutatua changamoto zinazokwamisha jitihada za Serikali katika masuala ya Uwekezaji na Uwezeshaji ambayo ni maeneo ya kimkakati katika kukuza uchumi wa nchi na kupunguza umaskini wa kipato.

**3.2 Mheshimiwa Spika**, Mapitio ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2014/2015 unaonesha kuwa mwenendo wa Hali ya Uchumi katika mwaka 2013, Pato halisi la Taifa lilikuwa kwa kiwango cha asilimia 7.0 ikilinganishwa na asilimia 6.9 mwaka 2012. Kiwango cha juu cha ukuaji wa shughuli za kiuchumi kilikuwa katika shughuli za sekta ya mawasiliano iliyokua kwa asilimia 22.8; ujenzi asilimia 8.6; biashara ya jumla na rejareja asilimia 8.3; hoteli na migahawa asilimia 6.3. Aidha, wakati ambapo kwa upande wa sekta ya kilimo ukuaji ulibakia kama ilivyokuwa mwaka 2012 yaani asilimia 4.3; sekta ya Uvuvi kasi ya ukuaji imepungua hadi asilimia 2.2 kutoka asilimia 2.9 kwa mwaka 2012. Sekta ya mifugo ilikua kwa asilimia 3.8 kutoka asilimia 3.1 mwaka 2012. **Takwimu hizi zinaonyesha** kuwa bado tuna safari ndefu ya kumkomboa mwananchi mwenye kipato cha chini ili aweze kufaidika na Rasilimali ya Taifa. Shughuli za sekta mbalimbali zinazofanyika kusaidia Uwekezaji na Uwezeshaji

bado hazijaweza kuwasaidia wananchi walio wengi hasa wa vijijini katika kuwapunguzia makali ya maisha. Hii inatokana na ukweli kwamba shughuli za Sekta hizo zinawagusa wananchi wachache tu. **Kamati inaendelea kuishauri Serikali** kwamba kuna haja ya kuongeza msukumo mkubwa zaidi kwenye shughuli za sekta ya Kilimo, Uvuvi na Ufugaji ambazo zinaajiri na kutegemewa na watanzania wengi. Kuimarika kwa sekta hizi kutasaidia kuleta uwiano kati ya ukuaji wa uchumi na kipato cha wananchi.

**3.3 Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Fedha ni eneo lingine linalopaswa kupewa kipaumbele; hususan katika suala la upatikanaji wa mikopo na hatua nyingine za uwezeshaji. Ni maoni ya kamati kuwa pamoja na kuongezeka kwa fursa za upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi, sehemu kubwa ya mikopo hiyo bado haiwafikii walengwa na hivyo kushindwa kutoa matokeo tarajiwa katika kumwezesha mwananchi wa kawaida. Aidha, hata pale mikopo hii inapowafikia walengwa kwa uchache, bado mikopo hiyo inakuwa na riba kubwa na hivyo kuwa kikwazo kikubwa katika kupunguza umasikini na kuongeza chachu ya ukuaji wa uchumi. Ripoti ya utafiti uliofanyika hivi karibuni (FINSCOP 2013) inaonesha kuwa asilimia 35 ya wakulima wadogo waliopo vijijini hawapati huduma za kifedha licha ya kuwepo kwa huduma za mitandao ya simu. **Kamati inashauri Serikali** kuwa umakini unahitajika katika kuhakikisha kuwa huduma za kifedha zinazotolewa nchini zinalenga mahitaji halisi ya wananchi; hususan wananchi wenye kipato cha chini na kwa masharti nafuu.

Kamati imebaini kuwa kuna tatizo kubwa la urejeshaji wa mikopo hapa nchini, jambo ambalo linarudisha nyuma jitihada za uwezeshaji wananchi. Takwimu zinaonesha kuwa idadi kubwa ya mifuko inayotoa mikopo hapa nchini inakabiliwa na tatizo la mikopo kutorejeshwa kwa takriban asilimia 20; kiwango hiki ni kikubwa mno kuachwa kupotea. Serikali inashauriwa ifanye tathmini ya fedha za mikopo inayotolewa kupitia mifuko mbalimbali ili kubaini kiwango halisi cha upotevu wa fedha, na hatimaye kuweka mikakati ya kurejeshwa kwa fedha hizo.

**3.4 Mheshimiwa Spika,** Ripoti ya Benki ya Dunia (Doing Business 2014) inaonesha kwamba nchi yetu bado inakabiliwa na gharama kubwa za kufanya biashara na kuwekeza ikilinganishwa na nchi kadhaa za Afrika Mashariki. Aidha, kati ya nchi 189 zilizofanyiwa utafiti, nchi yetu imeshika nafasi ya 145 na hivyo kuzidi kuporomoka ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo tulikuwa tunashika nafasi ya 136. Ni dhahiri kuwa hatutaweza kuendelea bila ya kuwa na msukumo wa hali ya juu wa kuboresha mazingira ya kufanyia biashara na kuwekeza ili kuongeza kasi ya kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Hatua hii lazima iambatane na kuondoa urasimu, ucheleweshaji au kutokutoa maamuzi kwa wakati pamoja na kurekebisha baadhi ya sheria zetu na kuimarisha miundombinu ya msingi.

**3.5** **Mheshimiwa Spika**, **Kamati inasisitiza** kuwa, bado idadi kubwa ya Watanzania hawajafaidika na mikakati mbalimbali ya Serikali ya kuwawezesha kiuchumi. Licha ya kuwepo programu mbalimbali kama vile Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; Mpango wa Uwezeshaji wa Wananchi kiuchumi na Kuongeza Ajira; *Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wafanyabiashara Wadogo (NEDF);* Mfuko wa Maendeleo ya Vijana; Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake; Mfuko wa Rais wa Kusaidia Wananchi; Mradi wa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo (SELF); Mpango wa Udhamini wa Mikopo kwa Mauzo ya Nje (Export Credit Gurantee Scheme); Mpango wa Kudhamini Miradi Midogo na ya Kati (Small and Medium Enterprises Credit Gurantee Scheme – SME-CGS); Mradi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (BEST project) na mingine mingi yenye lengo la kuwasaidia na kuwawezesha wananchi wengi wenye kipato cha chini, bado jitihada hizi hazijaweza kuwanufaisha wananchi kikamilifu kutokana na tatizo la **targeting** na utekelezaji wake kutosimamiwi ipasavyo vilevile, baadhi ya mifuko hii mitaji yake ni midogo kuweza kutosheleza mahitaji ya wananchi; na baadhi inaongozwa na watu wasio na ujuzi stahiki kwenye eneo la taaluma ya mikopo na elimu ya ujasiriamali. **Kamati inashauri Serikali** kufuatilia suala hili na kuhakikisha malengo ya programu hizo yanafikiwa ikiwemo kusaidia kuongeza mitaji ya mifuko hiyo pamoja na kuhakikisha kuwa inaongozwa na watu wenye ujuzi na uzoefu stahiki katika masula ya mikopo na ujasiriliamali.

**3.6** **Mheshimiwa Spika,** misamaha ya kodi imeendelea kuwa changamoto kubwa katika uchumi wetu. Pamoja na lengo zuri la misamaha hiyo ambalo ni kuvutia na kuhamasisha uwekezaji hapa nchini; ili hatimaye Serikali iweze kupata kodi baada ya uzalishaji kukua na ajira kuongezeka, kamati inaona kuwa misamaha hii imekuwa uchochoro mkubwa wa kukwepea kodi hapa nchini. Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya kina kuona kwanini misamaha hii iendelee. Aidha, tathmini ioneshe kwa uwazi faida na hasara za misamaha hiyo kwenye uchumi wetu. Inashauriwa vile vile kuwa tathmini hii isilenge misamaha inayotolewa kupitia kituo cha Uwekezaji (TIC) pekee, bali pia maeneo yote ikiwemo misamaha inayotolewa kupitia TRA.

**3.7** **Mheshimiwa Spika,** nchi yetu inashuhudia uwekezaji mkubwa katika maeneo ya uchimbaji wa madini, utafutaji gesi, mahoteli, na viwanda. Hata hivyo jambo la kusikitisha ni kwamba mahitaji muhimu kwa matumizi katika maeneo haya hususan nyama, matunda, na hata mboga mboga huagizwa kutoka nje ya nchi badala ya mazao hayo kununuliwa hapa nchini kwa lengo la kukuza uchumi. Hali hii sio tu kwamba inazorotesha uchumi bali pia inawanyima wananchi fursa zitokanazo na uwekezaji huu. Kamati inaishauri Serikali kuweka mkakati madhubuti wa kuwaunganisha wazalishaji wanaoishi katika maeneo yanayozunguka miradi hii kupitia mikataba maalum ya uzalishaji, kuwapatia huduma za ugani na mitaji ili waweze kuzalisha bidhaa na mazao yenye ubora unaohitajika na hivyo kulikamata soko hilo.

**8.8** **Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kuishauri Serikali juu ya umuhimu wa ushiriki wa Serikali katika ngazi ya Mkoa na Wilaya pamoja na ushiriki wa sekta binafsi kupitia miradi ya *PPP* katika shughuli za uwekezaji na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Pamoja na makongamano ya uwekezaji yanayoendelea katika mikoa mbali mbali kwa sasa; ni vyema makongamano hayo yakaandaliwa kitaalamu zaidi ili yaweze kuwa na tija zaidi kuliko ilivyo sasa. Mfumo uliopo sasa wa kubaini fursa za uwekezaji katika ngazi za Mikoa na Wilaya uboreshwe kwa Serikali kutenga fedha ili kuwezesha upembuzi yakinifu kufanyika kwa miradi inayokabiliwa ili kuwezesha ushiriki wa wananchi kupitia halmashauri zao kwa njia ya ubia na sekta binafsi.

## 4.0 HITIMISHO:

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Nchi; Uwekezaji na Uwezeshaji Dkt. Mary Michael Nagu (MB), Katibu Mkuu, pamoja na wataalamu wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuwa tayari kutoa ufafanuzi na kupokea maoni na ushauri wa Wajumbe wa Kamati yangu wakati wote wa mjadala wa makadirio haya. Ni matarajio ya Kamati kuwa ushirikiano huu utaendelea katika mwaka ujao wa Fedha.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara ambao wameweza kutoa maoni na michango ya mawazo yao mbali mbali katika kuboresha makadirio haya ili hatimaye yaletwe mbele ya Bunge hili tukufu. Naomba nitumie nafasi hii kuwatambua wajumbe wote kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Luhaga Joelson Mpina, MB, — Mwenyekiti
2. Mhe. Dunstun Luka Kitandula, MB, — M/Mwenyekiti
3. Mhe. Margareth Agness Mkanga, MB, — Mjumbe
4. Mhe. Aieshi Khalfan Hilary, MB, — Mjumbe
5. Mhe. Ester Lukago Minza Midimu, MB, — Mjumbe
6. Mhe. Hussein Nassor Amar, MB — Mjumbe
7. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, MB, — Mjumbe
8. Mhe. Joyce John Mukya, MB, — Mjumbe
9. Mhe. David Zakaria Kafulila, MB, — Mjumbe
10. Mhe. Shawana Bukhet Hassan, MB, — Mjumbe
11. Mhe. Said Mussa Zubeir, MB, — Mjumbe
12. Mhe. Vicky Pascal Kamata, MB — Mjumbe
13. Mhe. Naomi Ami Mwakyoma Kaihula, MB — Mjumbe
14. Mhe. Khatibu Said Haji, — Mjumbe
15. Mhe.Freeman Aikael Mbowe, MB — Mjumbe
16. Mhe. Josephine Jonson Genzabuke, MB — Mjumbe
17. Mhe. Eng. Habib Juma Mnyaa, MB — Mjumbe

18. Mhe. Mohamed Hamis Misanga , MB Mjumbe
19. Mhe. Dkt. Terezya Luoga Huvisa, MB Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, naomba nikushukuru sana wewe mwenyewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kutupatia maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah. Halikadhalika, napenda kuwashukuru Ndugu James Warburg, Ndugu Lawrence Robert Makigi na Ndugu Pauline Mavunde kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 37-Uwekezaji na Uwezeshaji, yenye maombi ya jumla ya shilingi **10,158,193,800.** Kati ya fedha hizo shilingi **8,118,193,800** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **2,040,000,000**/= ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**Mhe. Luhaga Joelson Mpina Mb.**
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA**
**6 MEI, 2014**

**Hotuba ya Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Kama ilivyosomwa Bungeni**

**MHE. DKT. KHAMIS ANDREA KIGWANGALA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013 naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Pamoja na Makadirio ya Mapato na matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, kuanzia tarehe 27 Aprili hadi 4 Mei, 2014 katika Ukumbi wa Julius Nyerere *International Convention Centre, Dar es Salaam*, Kamati ilichambua pia ilipitia Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 kwa Mikoa yote ya Tanzania Bara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nisiitaje.

Mheshimiwa Spika, kwa umakini na kwa kujitolea kufanya kazi kwa masaa mengi, Wajumbe wa Kamati yako hii walichambua taarifa za utekelezaji na bajeti za Mikoa na kutoa maoni na maagizo mahsusi kwa kila Mkoa. Ni matarajio ya Kamati hii kuwa maoni, ushauri na maagizo hayo yatafanyiwa kazi katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2014/2015 na pia katika maandalizi ya bajeti zitakazofuata.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya Mwaka 2013/2014 Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ilikadiriwa kukusanya maduhuli ya Sh. 10,500,000/= ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2014 jumla ya Sh. 39,197,800/= zilikusanywa ikiwa ni sawa na asilimia 373 ya makadirio. Kamati ilielezwa kwamba sababu ya kuvukwa kwa lengo la ukusanyaji katika Ofisi hii ilikuwa ni mauzo ya zabuni na vitabu na madawati ya fedha za *BAE* ambazo hazikuwepo katika makisio ya awali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Taasisi zilizo chini ya Fungu 56 – Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ilikadiriwa kuwa zingekusanya maduhuli ya jumla ya Sh. 10,190,381,355/= ambapo hadi kufikia Machi, 2014 Taasisi hizo zilikuwa zimekusanya kiasi cha Sh. 5,091,410,695/= ikiwa ni sawa na asilimia 50 ya makisio.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2013/2014, Fungu 56 - Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) pamoja na Taasisi zilizo chini yake, ambazo ni Shirika la Elimu Kibaha, Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa *(LAPF),* Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo na Wakala wa Wakala wa Usafiri wa Haraka Dar es Salaam ziliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya Sh. 278,686,064,802/=. Kati ya fedha hizo, Sh. 194,359,133,000/= ziliidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh. 84,326,931,802/= ziliidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo *(Development Budget)*.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2014, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) pamoja na Taasisi zilizo chini yake ilikuwa imepokea jumla ya Sh. 176,628,908,702/= sawa na asilimia 63.4 tu ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge ili kutekeleza shughuli zake.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa ujumla wake ziliidhinishiwa kiasi cha Sh. 4,079,140,624,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Miradi ya maendeleo hadi kufikia Machi, 2014, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zilipokea na kukusanya kiasi kisichozidi asilimia 60 tu.

Mheshimiwa Spika, lingine ni utekelezaji wa maoni ya Kamati ya kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuchambua bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha, Kamati ilitoa ushauri na maoni katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa kazi za Ofisi hii. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa sehemu, maoni na ushauri wa Kamati yetu umezingatiwa kama ifuatavyo:-

Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kuboresha muundo wa bajeti ili asilimia 40 ya bajeti yake ielekezwe katika miradi ya maendeleo na mahususi kwa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, asilimia 60 ya bajeti yake ielekezwe katika miradi ya maendeleo. Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ilitoa maelekezo kwa Sekretariet za Mikoa na Halmashauri kutenga asilimia 40 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Hazina, wadau wa maendeleo, Mikoa pamoja na Halmashauri, imeelekezwa na Kamati ifanye tathmini juu ya uwezo wa kukusanya mapato ili malengo ya makusanyo yanayokadiriwa yatolewe kwa wakati, Mamlaka hizo pia ziweze kufikia malengo hayo kwa ufanisi ili kuongeza pato la Taifa.

Hata hivyo, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) imefanya utafiti katika Halmashauri 30 ili kutambua uwezo wao wa mapato wa Halmashauri kutokana na hali ya uchumi wa mamlaka husika, yaani *revenue potential* pamoja na changamoto zinazokabili Halmashauri katika usimamizi.

Kamati inaishauri Serikali ibuni njia mpya za ukusanyaji wa mapato na kuongeza vyanzo vya mapato ili kufikia malengo yake.

Mheshimiwa Spika, hatua za kufunga mfumo wa *LGRIS* katika Jiji la Arusha ambapo makusanyo yameongezeka kwa kiwango kikubwa na kwa haraka, pia mfumo huu unafungwa katika Miji ya Mwanza, Mbeya na Tanga, Manispaa ya Mtwara, Kigoma na Dodoma na upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Kamati inapongeza Serikali kwa kuchukua hatua za kutumia mbinu za kisasa za ukusanyaji wa mapato ya majengo, yaani *Property Tax* katika Majiji na Miji midogo. Kamati inaomba mpango huo uendelee kutekelezwa kwa kasi na kwa ufanisi wa hali ya juu. *(Makofi)*

Vile vile Halmashauri zote kujifunza kutoka kwa Halmashauri zilizofanikiwa kukusanya kikamilifu ushuru wa huduma, yaani *Service Levy* kutoka kwa Makampuni makubwa yanayoendesha shughuli zao katika maeneo ya Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ilitoa maelekezo au Mwongozo kwa Halmashauri zote nchini kupitia kwa Makatibu Tawala wa Mikoa

kuhusu Halmashauri zote kuhakikisha zinazingatia marekebisho mapya ya Sheria Na.8 ya mwaka 2012, kwa kutoza ushuru wa huduma na aidha Makampuni yote yakiwemo matawi ya Makampuni hayo au watu binafsi wenye leseni katika maeneo yao.

Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo inaelekezwa na Kamati kuandaa mfumo wa uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo kwa kuzingatia vipaumbele vichache na vya haraka ili kutoa matokeo makubwa kwa haraka.

Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Serikali ya Ubelgiji inatafuta fedha kwa ajili ya kuandaa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini utakaotumika Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika utekelezaji wa fedha za miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida. Mfumo huu ukikamilika, utaisaidia Serikali kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kuona thamani ya fedha ikipatikana.

Aidha, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, kutafuta mbinu za kupata fedha, hata kwa mikopo ya nje, ili kuweza kujenga barabara za juu, yaani *fly-overs* katika makutano makubwa ya barabara ili kupambana na msongamano wa magari.

Mheshimiwa Spika, Serikali inasema kwamba ujenzi wa barabara za juu kwenye makutano makubwa ya barabara za Dar es Salaam unashughulikiwa. *TANROADS* imepata fedha kutoka Serikali ya Japan kwa ajili ya ujenzi wa *fly over* kwenye makutano ya Tazara, yaani makutano ya barabara ya Nyerere na Nelson Mandela . Ujenzi huo unatarajiwa kuanza mwaka huu, 2014.

Aidha, kwenye makutano ya Ubungo (makutano ya barabara za Morogoro na Sam Nujoma) *TANROADS* imeshapata mtaalamu mshauri ambaye amekwishaanza kazi ya usanifu wa kina wa ujenzi wa barabara za juu. Kazi ya usanifu inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2014. Ujenzi wa barabara za juu kwenye eneo hilo umepangwa ufanyike haraka na kukamilishwa ifikapo mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, ni maelezo ya Kamati kwamba, pamoja na kwamba Serikali imetekeleza maoni ya Kamati, lakini bado kuna maeneo machache ambayo bado utekelezaji wake haukuwa mzuri. Kwa mfano, bado kuna taarifa kwamba baadhi ya Halmashauri hazinufaiki kikamilifu na mapato yatokanayo na ushuru wa huduma, yaani *service levy* kwa kukosekana kwa sheria ndogo za kusimamia makusanyo hayo.

Aidha, agizo kwa Halmashauri zote kutenga asilimia 60 ya fedha itokanayo na makusanyo ya ndani, yaani *own source* kutekeleza miradi *ya* maendeleo halikutekelezwa kikamilifu na baadhi ya Halmashauri. Kamati itazidi kuwa mstari wa mbele kuhakikisha kuwa suala hili linakuwa sehemu ya mipango ya bajeti za Halmashauri zote nchini na itakagua utekelezaji wa miradi hiyo.

Kamati yetu inaamini kwamba, lengo la ugatuaji wa madaraka kutoka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa, yaani *Decentralisation by Devolution (D by D)*, lilikuwa kupeleka siyo tu maamuzi na usimamizi karibu zaidi na wananchi, lakini pia kuzielekeza Halmashauri zetu kuanza harakati za kujitegemea katika utendaji wake kwa kukusanya mapato yao wao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilitegemewa kuwa Serikali Kuu atabaki kuwa mlezi wa kudumu wa Halmashauri hizi kwa kuzipa Sera na Miongozi mbalimbali ya kutekeleza majukumu yake na pia kupeleka ruzuku ya mishahara na ya miradi ya maendeleo kwa kipindi fulani tu. Kila mtu, kati yetu wale tunaoamini na tunaopenda nyongeza ya mamlaka zaidi ya wananchi na ushirikishwaji wa karibu zaidi katika kujiletea maendeleo yao, tulidhani huu ni uelekeo sahihi. Tulijua ipo siku mchango wa Serikali Kuu utakuwa ni mdogo sana kwenye Serikali za Mitaa. Leo hii hali ni tofauti na haileti matumaini kabisa. *(Makofi)*

Sura ya Mipango na Maumbile ya Bajeti za Halmashauri za Wilaya kwa kiasi kikubwa, katika kipindi cha miaka miwili hii ya kuanzishwa rasmi kwa Kamati yetu na Utekelezaji wake wa majukumu, tumejifunza na kubaini uwepo wa hali ya juu wa dhana ya utegemezi uliokithiri kwa Serikali Kuu, badala ya Serikali za Mitaa kuanza kujifikiria zaidi katika uelekeo sahihi wa kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, utegemezi huu, kwa bahati mbaya sana, haujawahi na kamwe hautokuja kuzisaidia Halmashauri zetu kwenye eneo la miradi ya maendeleo; na sababu ziko wazi kabisa kwamba, kama Taifa, tuna utegemezi mkubwa sana kwenye mikopo ya kibiashara yaani *concessional loans* kutoka kwa marafiki zetu ama michango ya wahisani kwenye bajeti. Hivyo ikitokea kuwa wahisani hawajaleta fedha hizi ama wameleta nusu, kwa hakika, mpango wetu wa bajeti hautatekelezeka kama tulivyotaka.

Mheshimiwa Spika, tunaamini kuna miradi midogo midogo ya wananchi, ambayo kwa kiasi kikubwa haihitaji mapesa mengi kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ruzuku kwa Serikali za Mitaa.

Miradi ya aina ya kumalizia majengo ya madarasa, majengo ya Zahanati na Vituo vya Afya, nyumba za Walimu, nyumba za Wauguzi vijijini, barabara za vijijini, kuchimba visima na kadhalika, inaweza kabisa kutekelezwa kwa fedha zinazotokana na mapato ya ndani.

Mheshimiwa Spika, hili la kunyimwa mikopo ama wahisani na wabia wetu wa maendeleo kuacha, kupunguza kiwango ama kuchelewesha fedha kwa ajili ya kutusaidia kutekeleza mpango wetu wa bajeti, lina maana moja kubwa kwamba, tumepigiwa simu ya kutuamsha kutoka kwenye usingizi mzito, yaani *wake-up call* kuwa tuanze kufikiria kujitegemea kwenye bajeti yetu sasa, na kwamba ni ngumu sana kutegemea kuleta maendeleo ndani ya nyumba yetu kwa kutegemea msaada wa rafiki ama jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miaka takriban 20 iliyopita, Prof. Abdulrahman Mohamed Babu aliliona hili na aliandika kwenye kitabu chake kinachojulikana kama *An Economic Strategy for the Second Liberation of Africa,* kilichopigwa chapa na Mkuki na Nyota mwaka 1994, kuwa, na ninaomba nimnukuu:

> *"The situation is so bad that no "reforms", whether inspired by the World Bank or IMF (International Monetary Fund), or initiated locally, can get us out of the mess. For what is needed is not reform but a different outlook which calls for a decisive change of direction, a change of the primitive colonial structure of the economy to a national economy; above all, a change in the structure of production. This entails a change from an outward-motivated to an inward-motivated development strategy, whose guiding principle must be based on the recognition that external causes are only a condition of change, whereas internal causes are the basis of change." (Makofi)*

Ambayo inatafsirikia, kwa tafsiri isiyo rasmi kama *"Hali ni mbaya sana kiasi kwamba hakuna 'mabadiliko' yatakayofanyika, ama kwa kuhamasishwa na Benki ya Dunia au Shirikia la Fedha la Kimataifa, au mabadiliko yatakayoanzishwa kutokea ndani, yanayoweza kutunasua kutoka hapa tulipo. Kwa kuwa kinachohitajika siyo mabadiliko, bali mtazamo mpya kabisa ambao utahitaji uamuzi mahsusi wa kubadili uelekeo, kubadili muundo wa uchumi wa kikoloni kwenda kwenye uchumi wa kiTaifa; na juu ya yote, mabadiliko kwenye muundo wa uzalishaji.*

*Hii inamaanisha mabadiliko kutoka kwenye mkakati wa maendeleo unaotokea nje kwenda kwenye ule unaotokea ndani yetu wenyewe, ambao msingi wake mkubwa unaoongoza ni lazima uwe umejikita kwenye kutambua kwamba sababu za nje ni masharti tu ya mabadiliko, wakati sababu za ndani ni msingi wa mabadiliko." (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kwa msingi huu, Kamati iliamua, kwenye vikao vya Bajeti mwaka jana, 2013, kupendekeza kuondoa utaratibu wa kufanya kazi kwa mazoea, yaani *Business as usual* ili kuendana na dhana ya ugatuaji wa madaraka na kufanikisha uwepo wa Halmashauri na uendeshaji wake

unaolenga kufuata misingi iliyozianzisha badala ya kuendesha Halmashauri kwa mtindo wa kizamani usioendana na matakwa ya mfumo huu mpya. *(Makofi)*

Katika vikao vya Bajeti ya mwaka 2013/2014, Kamati iliazimia kuiagiza Wizara ya TAMISEMI kuziagiza Halmashauri zote nchini, kwanza, kuongeza ubunifu na jitihada kwenye ukusanyaji wa mapato mbalimbali ya Halmashauri; pili, kutenga asilimia 60 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Agizo hili lilionekana gumu na kwamba halitekelezeki. Visingizio vilikuwa vingi, hata hivyo, Kamati haikutetereka, imeendelea kushikilia msimamo wake kwa faida ya nchi na wananchi wake. Kwa sababu tunaamini kabisa kuwa tukiboresha Serikali za Mitaa tutayagusa maisha ya watu wote. Maana hakuna aliye nje ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kupongeza juhudi za Wizara katika kuwawajibisha Watendaji wasio waaminifu katika matumizi ya fedha na inazitaka Tawala za Mikoa kufuata nyayo hizo. Kamati inatambua mamlaka hizo zina uwezo wa kuanzisha mfumo madhubuti wa usimamizi ili kuziba mianya ya matumizi mabaya ya fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inaomba kuidhinishiwa Jumla ya Sh. 4,978,576,426,000/= kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI (Makao Makuu), Tawala za Mikoa na katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mchanganuo ulioandikwa hapo.

Mheshimiwa Spika, sasa ni maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2014/2015 pamoja na utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, naomba yote niliyoyaruka yaingie kwenye *Hansard* kama taarifa kamili ilivyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita kumekuwepo na makusanyo yasiyoridhisha katika Halmashauri nyingi ambayo kwa sehemu kubwa imesababishwa ama na udhaifu katika ukusanyaji wa mapato au makisio ya chini katika bajeti ya makusanyo ya ndani.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kusisitiza kwamba Sekretarieti za Mikoa zikiongozwa na Wakuu wa Mikoa, kuimarisha ufuatialiaji kwa kuzisimamia Halmashauri na kuhakikisha kuwa Fedha za Miradi ya Maendeleo zitokanazo na makuanyo ya ndani, pamoja na zile ambazo zinatoka nje, zinatumika

kuwaletea wananchi maendeleo na kwa wakati na kwa viwango stahiki na thamani ya fedha iweze kuonekana.

Mheshimiwa Spika, kwa msisitizo na kwa umuhimu wa suala hili, Kamati inaendelea kuzishauri Halmashauri zote nchini, kuhakikisha kuwa katika bajeti zake, asilimia isizopungua 60; narudia tena, kwa msisitizo na kwa umuhimu wa suala hili, Kamati inaendelea kuzishauri Halmashauri zote nchini kuhakikisha kuwa katika bajeti zake, asilimia isiyopungua 60 kutoka katika makusanyo ya ndani *(own source)* inatengwa kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wananchi. Kamati haitakuwa tayari kukubaliana na Bajeti ya Halmashauri yoyote ile kama haijakidhi matakwa ya agizo hili.

Aidha, Kamati inaitaka Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kuhakikisha agizo hili la Kamati linatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kwamba Serikali iweke mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa mapato ya majengo, yaani *property tax* katika Majiji, Manispaa, Miji na Miji midogo, kwani fedha nyingi zinapotea kwa kutokusanywa kwa kodi hii.

Kamati inatambua kuwa agizo, hata hivyo kwa yale maeneo ambayo yameainishwa kutakiwa kufanyiwa tathmini kuhusu thamani halisi ya majengo hayo kwa ajili ya kutozwa kodi ya majengo, Kamati inasisitiza tena kwamba, fedha maalum itengwe ili kuwezesha tathmini hiyo kukamilika kwa haraka ikiwa sahihi ili kodi hiyo ikusanywe katika mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, ushiriki wa wananchi pia utasaidia katika zoezi zima la kuchangia ujenzi wa miradi ya maendeleo hasa pale ambapo Serikali kuu pamoja na Serikali za Mitaa zitakapokuwa zinatoa mchango wake kikamilifu katika miradi husika na hivyo nguvu ya wananchi kutopotea.

Aidha, Kamati inazitaka Halmashauri zote nchini kuacha kuwabughudhi na kuwanyanyasa wananchi wenye kipato cha chini kabisa kwa kuwalazimisha walipe kodi kubwa kuliko hata mtaji na thamani ya mali zao wanazouza, hususan wafanyabiashara ndogo ndogo, mfano wale wanaotembeza bidhaa za mikononi, maarufu kama Wamachinga na Mama Lishe, ambao mara kadhaa wamekuwa wakinyang'anywa biashara zao na Mgambo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kama wezi ndani ya nchi yao. Mgambo hao kinyume kabisa na maadili ya kiafrika wakizitupa, wakihodhi ama kumwaga chini bidhaa hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, binafsi nimewahi kushuhudia Mgambo wakimwaga chakula cha Mama Lishe aliyekaidi agizo la Mkuu wa Wilaya la kuondoka

kwenye eneo walikozoea kufanyia biashara yao kwa sababu Serikali haikuwa imewaandalia eneo lingine mahsusi la kufanyia biashara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kikwetu sisi kumwaga chakula chini bila sababu ya msingi ni kitendo kinachoondoa baraka kutoka kwa Mungu. Ndiyo maana sisi huwa tunakula viporo hadi vya ugali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vitendo vya kinyama dhidi ya watu wa aina hii ni vingi na kwa namna yoyote ile havikubaliki katika Taifa letu na hivyo basi, Kamati inaitaka Serikali itekeleze Sera yake nzuri ya kuwalinda na kuwawezesha wananchi wenye uchumi wa chini kwa vitendo ili nao wajikwamue na umaskini, wakidhi mahitaji yao na waendelee kuiheshimu na kuipenda nchi yetu na Serikali yake.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inaiagiza Serikali kutoa maelekezo sahihi kwa Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kuwajengea mazingira mazuri, wezeshi na ya kisheria wafanyabiashara wote wanaohangaika kutafuta mkate wao wa kila siku kwa uchuuzi wa bidhaa zinazohesabika kwa macho tu bila matumizi ya nguvu ili kulinda haki ya wananchi kujifanyia kazi zao za kujipatia kipato chao cha kujikimu kila siku na familia zao bila kuingiliwa. *(Makofi)*

Kama inavyosema Sera ya CCM ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi, Sura ya Tano ya Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2010, Ukurasa wa 89, Sera Na. 75 (b), na naomba ninukuu:

*"75. Kwa kutambua kwamba kila raia wa Tanzania anayo fursa ya kumiliki ardhi na kuendesha shughuli za maendeleo pale anapoishi, Chama cha Mapinduzi kinaendelea kutoa wito kwa wananchi kwamba sera ya uwezeshaji itafanikiwa tu katika maisha yao kama kila mwenye uwezo wa kufanya kazi atafanya yafuatayo:-*

*(b) Kutambua kwamba, ardhi, cherehani, mgahawa, duka, mashine ya kufyatulia matofali anayomiliki na kadhalika, ni msingi imara wa maendeleo yake na kwamba uwezeshaji ni njia ya kumuunga mkono. Kila mwananchi mwenye shughuli halali ya kufanya, azame katika kujiletea maendeleo kwa kuendeleza shughuli hiyo."*

Mheshimiwa Spika, haikubaliki kisera na hata kibinadamu kuwaondoa wananchi kwenye maeneo yao ya shughuli bila kuwalipa fidia, ama kwa kuwapunja fidia, kuwadhulumu mali zao kwa kisingizio cha matumizi ya sheria ama kuwafukuza Mama Lishe na Wamachinga kwenye maeneo waliyozoea kufanyia biashara bila kuwaandalia mazingira mengine mazuri zaidi ya kufanyia kazi. Haikubaliki, haikubaliki, haikubaliki! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatutofanikiwa kudumisha amani, mshikamano na upendo katika Taifa letu kama tutaendelea kufanya vitendo kama vinavyojitokeza kwenye mradi mkubwa wa kupima viwanja kule Lindi unaoendeshwa na Taasisi ya *Unity Trust of Tanzania (UTT),* vya kuwanyang'anya wananchi maeneo yao ya asili bila ridhaa yao, kuyapima na kuyauza kwa ujanja ujanja huku mwenye ekari 20 za ufukweni akijikuta anapewa fidia kwa ekari nne tu na nyingine kuandikishwa majina ya watu wasiojulikana.

Mheshimiwa Spika, Kamati imesikitishwa na hili na imeazimia kuitaka Serikali kuwasilisha ndani ya wiki moja taarifa ya namna ilivyolishughulikia jambo hili na hatua ilizochukua dhidi ya udhalimu huu mkubwa kwa wananchi. Sambamba na hilo, Kamati imeiagiza Serikali isitishe zoezi hili kwa muda mpaka ukweli wa namna jambo hili lilivyotekelezwa utakapopatikana.

Aidha, Kamati imefurahishwa hatua za awali na za haraka zilizochukuliwa na Serikali kutii agizo la Kamati na hapa natumia fursa hii kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kwa kuguswa na jambo hili na kulitolea uamuzi wa mara moja kwa kuuagiza Mkoa kutekeleza maazimio ya Kamati bila kuchelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusikubali kuvunja misingi imara ya Taifa letu kwa kuukubali ubepari na ubeberu kuingia nchini na hadi kwa wananchi wetu huko vijijini, bila kuweka mifumo ya kulinda maslahi yao na kuyasimamia ilhali tunaujua uwezo wao kielimu, kiuchumi na kisheria, kuwa ni mdogo unaopaswa kuongozwa na Sera, Sheria na huruma ya Wataalamu na Viongozi wetu kule Mikoani.

Mheshimiwa Spika, ubepari una sura nyingi na una njia nyingi za kupenya na kujitengenezea himaya. Tufumbue macho yetu, tuwahurumie watu wetu, tuzijue shida na kero zao, tuzingatie malalamiko yao, tutafute ufumbuzi wa shida, kero na malalamiko yao kwa nguvu zetu zote. Hata siku moja tusisahau kuwa tunatoka kwenye utamaduni wa kijamaa ambao ni asili yetu sisi waafrika. Tusiukubali ukweli wa usemi kuwa "Mwenye shibe hamjui mwenye njaa." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam ni tatizo kubwa linalohitaji kupatiwa ufumbuzi wa haraka na wa makusudi kabisa.

Madhara ya msongamano ni mengi ikiwemo kuleta hasara kubwa katika uchumi kwa kupunguza masaa ya kazi *(man hours)* na kuchelewesha watu kwenda kupata huduma za kijamii. Pamoja na jitihada za Serikali na watu binafsi kujenga makazi, maofisi na sehemu za masoko makubwa nje ya Jiji, bado tatizo hili halijapatiwa ufumbuzi.

Ili kupata ufumbuzi wa tatizo la msongamano wa magari Jijini Dar es Salaam, mwaka 2007 Serikali ilibuni Mradi wa Usafiri wa Mabasi Yaendayo Kasi na kwa mujibu wa mpango huo, mradi huu ukikamilika inakadiriwa utakuwa umetatua tatizo la usafiri wa umma katika Jiji la Dar es Salaam na pia kupunguza msongamano wa magari Jijini humo mpaka kufikia miaka ya 2030/2031.

Hata hivyo, Kamati ya TAMISEMI imebaini kuwa kungepaswa kuwe na usanifu ambao ungezingatia angalau utatuzi wa tatizo hili kwa miaka 50 na hata 100 baadaye kwa kutazama maoteo ya idadi ya watu katika miaka hiyo. Usanifu, yaani *design* ya mradi ingepaswa kuzingatia uwepo wa njia mbalimbali mchanganyiko za kutatua tatizo hili, hata kama kwa sasa tuna uwezo wa kujenga miundombinu ya mabasi yaendayo kasi tu.

Hii ingetoa fursa kwa Serikali kuongeza njia moja baada ya nyingine kukamilika ama kadri ambavyo pesa zinapatikana bila kuathiri bajeti za fidia ama kubomoa bomoa miundo mipya na imara inayojengwa sasa, na zaidi bila kuongeza msongamano katika kipindi chote cha ujenzi wa mradi.

Mheshimiwa Spika, Waingereza wana methali moja *kuwa "chance favours a prepared mind",* kwamba 'fursa hupendelea kwenda kwa mtu aliyejiandaa kuipokea.' Hivyo, ni ushauri wa Kamati yetu kuwa, tujipange kwa kuwa na mpango kabambe wa kutatua kero za msongamano wa watu na magari katika Jiji la Dar es Salaam kwa kuwa linakua kwa kasi sana. Tusishindwe kujenga leo na tukakubali kushindwa hata kupanga tu.

Mheshimiwa Spika, kusanifu mpango mzuri siyo kujenga, ni kusanifu tu. Kuna uwezekano mkubwa wa kufanya usanifu unaozingatia idadi ya watu na maoteo ya idadi ya magari miaka 50 mbele, yaani kutengeneza *simulation model* ya kipindi hicho na hivyo kubuni njia mbalimbali zitakazohitajika kuwepo kipindi hicho. Kufanya hivi itasaidia kupunguza bomoa bomoa kila mara inapohitajika kujenga awamu nyingine ya mfumo kutokana na mahitaji ya wakati huo.

Mheshimiwa Spika, nina dakika ngapi?

**SPIKA:** Zimekwisha.

**MHE. DKT. KHAMIS ANDREA KIGWANGALLA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Oooh!

Mheshimiwa Spika, pendekezo lingine, ili tuendane na uchumi wa kisasa na tuweze kuyafikia malengo tuliyojiwekea kama Taifa, hususan lile kubwa la kufikia kuwa nchi yenye uchumi wa kiwango cha kati, yaani *Mid-Income*

*country* ifikapo mwaka 2025, ni lazima tuwe na rasilimali watu ya kutosha na yenye weledi wa hali ya juu. Kamati inakiri na kupongeza mafanikio makubwa katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa kuhakikisha tuna Shule za Sekondari kwenye kila Kata, tuna Zahanati kwenye kila Kijiji na Kituo cha Afya kwenye kila Kata. Kwa kiasi kikubwa malengo ya kujenga majengo na mahali pengine kuanzisha utoaji wa huduma yameweza kufikiwa.

Hata hivyo, Kamati imebaini changamoto kubwa kwenye ubora wa huduma kutokana na kuwa na nguvu kazi kubwa ya watumishi ambayo haina motisha ya kujitoa. Kwa kuzingatia nia yetu kama Taifa ya kutaka kuyafikia malengo yetu, ni lazima kubuni mbinu mahsusi za kutoa motisha kwa watoa huduma wetu ili tuweze kufikia malengo yetu bila shida. Tunaweza kutazama mifumo ya kutoa motisha kwa kutazama umbali wa kijiografia ama kwa kuzingatia utofauti wa kimajukumu na kutoa motisha stahiki, yaani *differential incentives.*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Bahati yako mbaya, muda umekwisha.

**MHE. DKT. HAMISI ANDREA KIGWANGALA-MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Uliniambia nina dakika tatu.

**SPIKA:** Muda umekwisha. Naomba tukubaliane, muda umekwisha.

**MHE. DKT. HAMISI ANDREA KIGWANGALA-MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba ni-*wind up.*

**SPIKA:** Hakuna cha ku-*wind up*, muda umekwisha! Siyo utaratibu wetu.

**MHE. DKT. HAMISI ANDREA KIGWANGALA - MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba hotuba hii iingie yote kwenye *Hansard* kama ilivyo. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**Hotuba ya Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Kama ilivyowasilishwa Mezani**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015**

## 1.0 UTANGULIZI

1.1 **Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013 naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

1.2 **Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 26 Aprili, 2014 katika Ukumbi wa Karimjee, Dar es Salaam, Kamati ilianza kazi ya uchambuzi wa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kufanya mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 56 - Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) na taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014. Aidha, Kamati ilipokea maelezo ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

1.3 **Mheshimiwa Spika,** kuanzia tarehe 27 Aprili – 04 Mei, 2014 katika Ukumbi wa Julius Nyerere International Convention Centre, Dar es Salaam, Kamati ilichambua pia ilipitia Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 kwa Mikoa yote ya Tanzania Bara kama ifuatavyo:-

1. Fungu 70 – Mkoa wa Arusha
2. Fungu 88 – Mkoa wa Dar es Salaam
3. Fungu 72 – Mkoa wa Dodoma
4. Fungu 63 – Mkoa wa Geita
5. Fungu 73 – Mkoa wa Iringa
6. Fungu 87 – Mkoa wa Kagera
7. Fungu 36 – Mkoa wa Katavi
8. Fungu 74 – Mkoa wa Kigoma
9. Fungu 75 – Mkoa wa Kilimanjaro

10. Fungu 76 – Mkoa wa Lindi
11. Fungu 95 – Mkoa wa Manyara
12. Fungu 77 – Mkoa wa Mara
13. Fungu 78 – Mkoa wa Mbeya
14. Fungu 79 – Mkoa wa Morogoro
15. Fungu 80 – Mkoa wa Mtwara
16. Fungu 81 – Mkoa wa Mwanza
17. Fungu 54 – Mkoa wa Njombe
18. Fungu 71 – Mkoa wa Pwani
19. Fungu 89 – Mkoa wa Rukwa
20. Fungu 82 – Mkoa wa Ruvuma
21. Fungu 83 – Mkoa wa Shinyanga
22. Fungu 47 – Mkoa wa Simiyu
23. Fungu 84 – Mkoa wa Singida
24. Fungu 85 – Mkoa wa Tabora na
25. Fungu 86 – Mkoa wa Tanga

**1.1 Mheshimiwa Spika,** kwa umakini na kwa kujitolea kufanya kazi kwa masaa mengi, Wajumbe wa Kamati walichambua taarifa za utekelezaji na bajeti za mikoa na kutoa maoni na maagizo mahsusi kwa kila mkoa. Ni matarajio ya Kamati hii kuwa maoni, ushauri na maagizo hayo yatafanyiwa kazi katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2014/2015 na pia katika maandalizi ya bajeti zitakazofuata.

## 2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2013/2014

### Fungu 56 – Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI)

#### Makusanyo ya Maduhuli

**2.1 Mheshimiwa Spika,** katika bajeti ya Mwaka 2013/2014 Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ilikadiriwa kukusanya maduhuli ya Sh. 10,500,000 ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2014 jumla ya Sh. 39,197,800 zilikusanywa ikiwa ni sawa na asilimia mia tatu sabini na tatu (373%) ya makadirio. Kamati ilielezwa kwamba sababu ya kuvukwa kwa lengo la ukusanyaji katika Ofisi hii ilikuwa ni mauzo ya zabuni na vitabu na madawati ya fedha za BAE ambazo hazikuwemo katika makisio ya awali.

**2.2 Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa taasisi zilizo chini ya Fungu 56 – Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ilikadiriwa kuwa zingekusanya maduhuli ya jumla ya Sh. 10,190,381,355 ambapo hadi kufikia Machi, 2014 taasisi hizo zilikuwa zimekusanya kiasi cha Sh. 5,091,410,695 ikiwa ni sawa na asilimia hamsini (50%) ya makisio.

**Matumizi**

**2.3 Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2013/2014, Fungu 56 - Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) pamoja na taasisi zilizo chini yake, ambazo ni Shirika la Elimu Kibaha, Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (LAPF), Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo (LGTI) na Wakala wa Wakala wa Usafiri wa Haraka Dar es Salaam (DART) ziliidhinishiwa na Bunge lako tukufu jumla ya Shilingi Bilioni 278,686,064,802. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 194,359,133,000.000 ziliidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Reccurent Budget) na Shilingi Bilioni 84,326,931,802 ziliidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo (Development Budget).

**2.4 Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2014, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) pamoja na taasisi zilizo chini yake ilikuwa imepokea jumla ya Shilingi Bilioni 176, 628,908,702 sawa na asilimia sitini na tatu nukta nne (63.4%) ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge ili kutekeleza shughuli zake.

**2.5 Mheshimiwa Spika,** kwa muhtasari, Kamati ilipewa taarifa kwamba shughuli zifuatazo zilifanyika katika utekelezaji wa bajeti hiyo:-

(a) Uwezeshaji wa Tawala za Mikoa na Halmashauri zake;
(b) Usimamizi wa utekelezaji wa shughuli za Elimu ya Msingi na Sekondari;
(c) Kufanya tathmini juu ya ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Mikoa na Halmashauri;
(d) Usimamizi wa utawala bora katika ngazi zote;
(e) Kusimamia na kuendesha mifumo ya habari, teknolojia na mawasiliano; na
(f) Kusimamia shughuli za Taasisi, Mfuko wa Barabara na Miradi ya Maendeleo iliyopo chini ya Ofisi.

**Tawala za Mikoa na Halmashauri**

**2.6 Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa ujumla wake ziliidhinishiwa kiasi cha Sh. 4,079,140,624,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, miradi ya maendeleo na makusanyo. Hadi kufikia Machi, 2014, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zilipokea na kukusanya kiasi kisichozidi asilimia sitini (60%) kwa wastani.

**2.7 Mheshimiwa Spika,** kwa muhtasari utekekezaji wa bajeti za mikoa na halmashauri zake ulijikita katika kutetekeleza majukumu yafuatayo:-

(a) Kuendesha shughuli za ofisi za kila siku ambazo ni pamoja na kulipia gharama za simu, umeme na maji;

(b) Kuendesha vikao vya kisheria ikiwa ni pamoja na kamati ya Ushauri za Mkoa, Kamati Maalum za Ajira, Kamati za Ulinzi na Usalama na Bodi za Ajira za Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(c) Sekretarieti za Mikoa zilifanya ufuatiliaji na tathimini za shughuli zinazoelekezwa kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa na kutoa ushauri.

(d) Kufuatilia na kukagua miradi ya Maendeleo katika Halmashauri.

**2.8** **Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa bajeti ya Mwaka 2013/2014, Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kulikuwepo na changamoto mbalimbali. Baadhi ya changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

(a) Kuchelewa kwa fedha toka hazina na wakati mwingine kutokutolewa kabisa au kuletwa nusu ya kiasi kilichoombwa. Hii ni pamoja na kutolewa kwa "ex-chequer issues" bila fedha kuonekana kwenye mtandao kwa muda mrefu. Hivyo kupelekea kuchelewa kuanza kwa utekelezaji wa miradi husika;

(b) Kuwepo kwa madeni makubwa ya watumishi (walimu na wasio walimu). Watumishi walio katika sekretariati ya mkoa na Halmashauri zake wanadai serikali kwa muda mrefu, malimbikizo ya posho za uhamisho, posho za kukaimu, "Arreaas" za Mishahara, uendeshaji wa ofisi na baadhi ya watoa huduma na wazabuni;

(c) Baadhi ya sekretarieti za mikoa bado zina uhaba wa washauri/wataalamu mbalimbali.pia baadhi ya tarafa zina uhaba wa watumishi, wakiwemo wataalamu wa usimamizi wa utekelezaji wa miradi katika ngazi za vijiji.

(d) Uhaba wa vitendea kazi na vifaa muhimu katika ngazi zote tarafa, wilaya na mkoa. Mfano, Halmashauri nyingi za mikoa wana uhaba wa vifaa muhimu vya ujenzi wa barabara na vifaa vya kusafishia miji;

(e) Kuwepo kwa miundombinu isiyokidhi mahitaji halisi hivyo kusababisha msongamano katika vituo vya kutolea huduma ikiwemo shule, Hospitali, Maji, Barabara n.k.

(f) Baadhi ya Mikoa imekuwa ikikumbwa na majanga ikiwemo mafuriko. Majanga haya yanasababisha athari kubwa kwa miundombinu ya kijamii na kiuchumi, hivyo kutumika fedha ambazo zilitengwa kwa malengo mengine.

## 3.0 UTEKELEZAJI WA MAONI YA KAMATI YA KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

**3.1** **Mheshimiwa Spika,** wakati wa kuchambua bajeti ya Ofisi ya waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha, Kamati ilitoa ushauri na maoni katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa kazi za Ofisi hii. Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa sehemu, maoni na ushauri wa Kamati umezingatiwa kama ifuatavyo:-
**OWM-Tamisemi kuboresha muundo wa bajeti ili 40% ya bajeti yake ielekezwe katika miradi ya maendeleo na mahususi kwa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, 60% ya bajeti yake ielekezwe katika miradi ya maendeleo.**

3.2 Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ilitoa maelekezo kwa Sekretariti za Mikoa na Halmashauri kutenga 40% ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

**Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI kwa kushirikiana na HAZINA, wadau wa maendeleo, Mikoa pamoja na Halmashauri, ifanye tathmini juu ya uwezo wa kukusanya mapato ili malengo ya makusanyo yanapowekwa, mamlaka hizo ziweze kufikia malengo hayo kwa ufanisi ili kuongeza pato la taifa.**

**3.3** **OWM – TAMISEMI** imefanya utafiti katika Halmashauri 30 ili kutambua uwezo wao wa mapato wa Halmashauri kutokana na hali ya uchumi wa mamlaka husika (revenue potential) pamoja na changamoto zinazokabili Halmashauri katika usimamizi.

**Serikali ibuni njia mpya za ukusanyaji wa mapato na kuongeza vyanzo vya mapato.**

**3.4** Serikali imekwishaanza kuimarisha mifumo ya usimamizi na ufuatiliaji wa ukusanyaji wa Mapato ya Halmashauri. Katika mpango wa Tekeleza Sasa kwa matokeo makubwa (BRN) kodi ya Majengo na kodi ya Ardhi zimewekewa mikakati madhubuti ili kuongeza mapato yatokanayo na vyanzo hivyo.

**Serikali iweke mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa mapato ya majengo (property tax) katika majiji na miji midogo.**

**3.5** Hatua za kufunga mfumo wa LGRIS katika Jiji la Arusha ambapo makusanyo yameongezeka kwa kiwango kikubwa na kwa haraka.Pia mfumo huu unafungwa katika miji ya Mwanza,Mbeya, na Tanga,Manispaa ya Mtwara, Kigoma, na Dodoma upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji

**Halmashauri zote kujifunza kutoka kwa halmashauri zilizofanikiwa kukusanya kikamilifu ushuru wa huduma (service levy) kutoka kwa makampuni makubwa yanayoendesha shughuli zao katika maeneo yao.**

**3.6** OWM – TAMISEMI ilitoa maelekezo au mwongozo kwa Halmashauri zote Nchini kupitia kwa Makatibu Tawala wa Mikoa kuhusu Halmashauri zote kuhakikisha zinazingatia marekebisho mapya ya Sheria Namba 8 ya mwaka 2012, kwa kutoza ushuru wa huduma, Makampuni yote yakiwemo matawi ya Makampuni hayo au watu binafsi wenye leseni katika maeneo yao.

**OWM – TAMISEMI kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo kuandaa mfumo wa uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo kwa kuzingatia vipaumbele vichache na vya haraka kutoa matokeo makubwa kwa haraka.**

**3.7** OWM – TAMISEMI kwa kushirikiana na shirika la Maendeleo la Serikali ya Ubelgiji inatafuta fedha kwa ajili ya kuandaa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini utakaotumika OWM – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika utekelezaji wa fedha za miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida. Mfumo huu ukikamilika utaisaidia Serikali kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kuona thamani ya fedha.

**Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, kutafuta mbinu za kupata fedha, hata kwa mikopo ya nje, ili kuweza kujenga barabara za juu (fly-overs) katika makutano makubwa ya barabara.**

**3.8** Ujenzi wa barabara za juu kwenye makutano makubwa ya barabara za Dar es salaam unashughulikiwa. TANROADS imepata fedha kutoka Serikali ya Japan kwa ajili ya ujenzi wa "fly over" kwenye makutano ya Tazara (makutano ya barabara ya Nyerere na Nelson Mandera). Ujenzi huo unatarajiwa kuanza mwaka huu (2014).

**3.9** Aidha, kwenye makutano ya Ubungo (makutano ya barabara za Morogoro na Sam Nujoma) Tanroads imeshapata mtaalamu mshauri ambaye amekwishaanza kazi ya usanifu wa kina wa ujenzi wa barabara

za juu (flyover). Kazi ya usanifu inatarajiwa kukamilika mwezi June 2014. Ujenzi wa barabara za juu kwenye eneo hilo umepangwa ufanyike haraka na kukamilishwa mwaka 2016.

**3.10** **Mheshimiwa Spika,** pamoja na kwamba Serikali imetekekeleza maoni ya Kamati lakini bado kuna maeneo machache ambayo bado utekelezaji wake haukuwa mzuri. Kwa mfano, bado kuna taarifa kwamba baadhi ya halmashauri hazinufaiki kikamilifu na mapatao yatokanayo na ushuru wa huduma (service levy) kwa kukosekana kwa sheria ndogo za kusimamia makusanyo hayo.

**3.11** Aidha, ***agizo kwa halmashauri zote kutenga asilimia isiyopungua sitini (60%) ya fedha itokanayo na makusanyo ya ndani (own source) kutekeleza miradi ya*** maendeleo halikutekelezwa kikamilifu na baadhi ya halmashauri. Kamati itazidi kuwa mstari wa mbele kuhakikisha kuwa suala hili linakuwa sehemu ya mipango ya bajeti za halmashauri zote nchini na itakagua utekelezaji wa miradi hiyo.

**3.12** Kamati yetu inaamini kwamba, lengo la **Ugatuaji wa Madaraka kutoka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa, yaani 'Decentralisation by Devolution (D by D)'**,lilikuwa kupeleka si tu maamuzi na usimamizi karibu zaidi na wananchi, lakini pia kuzielekeza Halmashauri zetu kuanza harakati za kujitegemea katika utendaji wake kwa kukusanya mapato yao wao wenyewe. Na ilitegemewa kuwa Serikali Kuu atabaki kuwa mlezi wa kudumu wa Halmshauri hizi kwa kuzipa Sera na Miongozi mbali mbali ya kutekeleza majukumu yake, na pia kupeleka ruzuku ya misharahara na ya miradi ya maendeleo kwa kipindi fulani. Kila mtu, kati yetu wale tunaoamini na tunaopenda nyongeza ya mamlaka zaidi ya wananchi na ushirikishwaji wa karibu zaidi katika kujiletea maendeleo yao, tulidhani huu ni uelekeo sahihi, na tulijua ipo siku mchango wa Serikali Kuu utakuwa ni mdogo sana kwenye Serikali za Mitaa. Leo hii hali ni tofauti na haileti matumaini kabisa. Sura ya Mipango na Maumbile ya Bajeti za Halmashauri za Wilaya kwa kiasi kikubwa, katika kipindi cha miaka miwili hii ya kuanzishwa rasmi kwa Kamati Yetu na Utekelezaji wake wa majukumu, tumejifunza na kubaini uwepo wa wa hali ya juu wa ***"dhana ya utegemezi"*** uliokithiri kwa Serikali Kuu, badala ya Serikali za Mitaa kuanza kujifikiria zaidi katika uelekeo sahihi wa ***"kujitegemea".***

**3.13** **Mheshimiwa Spika,** Utegemezi huu, kwa bahati mbaya sana, haujawahi na kamwe hautokuja kuzisaidia Halmashauri zetu kwenye eneo la miradi ya maendeleo; na sababu ziko wazi kabisa: kwamba, kama Taifa tuna utegemezi mkubwa sana kwenye mikopo ya kibiashara ***"concessional loans"*** kutoka kwa marafiki zetu ama michango ya wahisani kwenye bajeti, hivyo ikitokea kuwa wahisani hawajaleta fedha hizi ama wameleta

nusu, kwa hakika, mpango wetu wa bajeti hautotekelezeka kama tulivyotaka. Lakini tunaamini kuna miradi midogo midogo ya wananchi, ambayo, kwa kiasi kikubwa haihitaji 'mapesa mengi' kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ruzuku kwa Serikali za Mitaa. **Miradi ya aina ya kumalizia majengo ya madarasa, majengo ya zahanati na vituo vya afya, nyumba za walimu, nyumba za wauguzi vijijini, mabarabara ya vijijini, kuchimba visima n.k., inaweza kabisa kutekelezwa kwa fedha zinazotokana na mapato ya ndani!**

**3.14** **Mheshimiwa Spika,** hili la kunyimwa mikopo ama wahisani na wabia wetu wa maendeleo kuacha, kupunguza kiwango ama kuchelewesha fedha kwa ajili ya kutusaidia kutekeleza mpango wetu wa bajeti, lina maana moja kubwa; kwamba,'***tumepigiwa simu ya kutuamsha kutoka kwenye usingizi mzito (wake-up call!)'*** kuwa tuanze kufikiria ***"kujitegemea"*** kwenye bajeti yetu, na kwamba ni ngumu sana kutegemea kuleta maendeleo ndani ya nyumba yetu kwa kutegemea msaada wa rafiki ama jirani. Mheshimiwa Spika, miaka takriban 20 iliyopita, **Prof. Abdulrahman M. Babu**[1] aliliona hili na aliandika kwenye kitabu chake kinachojulikana kama **"An Economic Strategy for the Second Liberation of Africa**[2]**"** kilichopigwa chapa na Mkuki na Nyota Publishers Ltd, Mwaka 1994, kuwa, na ninaomba nimnukuu:

***"The situation is so bad that no "reforms", whether inspired by the World Bank or IMF (International Monetary Fund), or initiated locally, can get us out of the mess. For what is needed is not reform but a different outlook which calls for a decisive change of direction, a change of the primitive colonial structure of the economy to a national economy; above all, a change in the structure of production. This entails a change from an outward-motivated to an inward-motivated development strategy, whose guiding principle must be based on the recognition that external causes are only a condition of change, whereas internal causes are the basis of change."***

Ambayo inatafsirikia, kwa tafsiri isiyo rasmi kama:
***"Hali ni mbaya sana kiasi kwamba hakuna 'mabadiliko' yatakayofanyika, ama kwa kuhamasishwa na Benki ya Dunia au Shirikia la Fedhaa la Kimataifa, au mabadiliko yatakayoanzishwa kutokea ndani, yanayoweza kutunasua kutoka hapa tulipo.***

---

1 Prof. A. M. Babu alikuwa Mwanasiasa, Mwanazuoni na Mwanaharakati maarufu Tanzania, Afrika na Duniani Kote. Aliwahi kuwa Waziri kwenye Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Muungano. Pia aliwahi kuwa mwandishi

wa habari maarufu sana Tanzania, Africa na Duniani Kote. Umauti ulimkuta tarehe 7 Agosti 1996, akiwa Zanzibar. Mawazo yake yanaendelea kuishi.

2 A. M. Babu (1994). An economic strategy for the second liberation of Africa. Mkuki na Nyota Publishers Ltd. Revised Edition, 2010.

> ***Kwa kuwa kinachohitajika siyo mabadiliko bali mtazamo mpya kabisa ambao utahitaji uamuzi mahsusi wa kubadili uelekeo, kubadili muundo wa uchumi wa kikoloni kwenda kwenye uchumi wa kitaifa; na juu ya yote, mabadiliko kwenye muundo wa uzalishaji. Hii inamaanisha mabadiliko kutoka kwenye mkakati wa maendeleo unaotokea nje kwenda kwenye ule unaotokea ndani yetu wenyewe, ambao msingi wake mkubwa unaoongoza ni lazima uwe umejikita kwenye kutambua kwamba sababu za nje ni masharti tu ya mabadiliko, wakati sababu za ndani ni msingi wa mabadiliko.“***

**3.15** **Mheshimiwa Mwenyekiti,** Ni kwa misingi hii, Kamati iliamua, kwenye vikao vya Bajeti mwaka jana, kupendekeza kuondoa utaratibu wa kufanya kazi kwa mazoea, yaani ***‘Business as usual‘*** ili kuendana na dhana ya ugatuaji wa madaraka na kufanikisha uwepo wa Halmashauri na uendeshaji wake unaolenga kufuata misingi iliyozianzisha badala ya kuendesha Halmshauri kwa mtindo wa kizamani usioendana na matakwa ya mfumo huu mpya.

**3.16** Katika vikao vya Bajeti ya mwaka 2013/14, Kamati iliazimia kuiagiza Wizara ya TAMISEMI kuziagiza Halmashauri zote nchini, kwanza, kuongeza ubunifu na jitihada kwenye ukusanyaji wa mapato mbalimbali ya Halmashauri, pili, kutenga asilimia 60 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Agizo hili lilionekana gumu na kwamba halitekelezeki, visingizio vilikuwa vingi, Kamati, hata hivyo haikutetereka, imeendelea kushikilia msimamo wake kwa faida ya nchi na wananchi wake. Kwa sababu tunaamini kabisa kuwa tukiboresha Serikali za Mitaa tutayagusa maisha ya watu wote. Maana hakuna aliye nje ya Serikali za Mitaa!

**3.17** **Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kupongeza juhudi za Wizara katika kuwawajibisha Watendaji wasio waaminifu katika matumizi ya fedha, na inazitaka Tawala za Mikoa kufuata nyayo hizo. Kamati inatambua mamlaka hizo zina uwezo wa kuanzisha mfumo madhubuti wa usimamizi ili kuziba mianya ya matumizi mabaya ya fedha.

## 4.0 MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

4.1 **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inaomba kuidhinishiwa Jumla ya Shilingi Trilioni **Sh. 4,978,576,426,000** kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI (Makao Makuu), Tawala za Mikoa na katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mchanganuo ufuatao:-

- OWM (TAMISEMI) na Taasisi zilizo chini yake kiasi cha **Shilingi Bilioni 479,224,062,000** kinaombwa ambapo kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 273,065,895,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Mishahara na Matumizi Mengineyo) na Shilingi Bilioni 206,158,167,000 kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo; na

- Tawala za Mikoa na Halmashauri zake kiasi cha **Shilingi Trilioni 4,231,442,974,000** ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi Trilioni 3,292,680,594,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Mishahara na Matumizi Mengineyo), **Shilingi Bilioni 458,470,622,000** ikiwa ni Mapato yatokanayo na Makusanyo, na **Shilingi Bilioni 748,201,148,000** ikiwa ni fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

4.2 **Mheshimiwa Spika,** katika ngazi ya Tawala za Mikoa, fedha inayoombwa inategemewa kuanzisha ujenzi wa miundombinu ya Mikoa na Wilaya mpya pamoja na kukamilisha miradi ya ujenzi na ukarabati wa Ofisi, Nyumba za Wakuu wa Mikoa na Wilaya pamoja na Hospitali za Mikoa.

4.3 **Mheshimiwa Spika,** katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, fedha inayoombwa inategemewa kukamilisha ujenzi wa Shule za Sekondari ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mabweni, maabara na kupanua baadhi ya shule kwa ajili ya kuongeza kidato cha tano na sita.

4.4 **Mheshimiwa Spika,** napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba Kamati ilichambua randama ya Fungu – 56 OWM (TAMISEMI) pamoja na randama za mafungu ya mikoa yote na kutoa maelekezo mahsusi katika kila mkoa juu ya uatekelezaji wa fedha inayoombwa.

## 5.0 MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA WAZIRI MKUU KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 PAMOJA NA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YAKE

### Mapato ya Serikali za Mitaa (Halmashauri)

5.1 **Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita kumekuwepo na makusanyo yasiyoridhisha katika Halmashauri nyingi ambayo kwa sehemu kubwa imesababishwa ama na udhaifu katika ukusanyaji wa mapato yatokanayao na vyanzo vilivyopo au makisio ya chini katika bajeti ya makusanyo ya ndani.

5.2 **Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua kuwa moja ya jukumu la Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI ni kuziwezesha Tawala za Mikoa, Kamati inaishauri Ofisi hiyo kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa kuhakikisha kwamba, katika Bajeti ya Mwaka 2014/2015 inazisimamia halmashauri zote nchini katika kutambua uwepo wa vyanzo vya mapato ili halmashauri hizo ziweze kuandaa makadirio kulingana na uwezo wa ukusanyaji lakini pia kuhakikisha kuwa mikakati madhubuti inawekwa kukusanya mapato na kufikia malengo yatakayowekwa.

5.3 **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kusisitiza kwamba sekretarieti za mikoa zikiongozwa na wakuu wa mikoa, kuimarisha ufuatiliaji kwa kuzisimamia halmashauri na kuhakikisha kuwa fedha za miradi ya maendeleo zitokanazo na makusanyo ya ndani pamoja na zile ambazo zinatoka nje zinatumika kuwaletea wananchi maendeleo, kwa wakati na kwa viwango stahiki na thamani ya fedha iweze kuonekana.

5.4 **Mheshimiwa Spika**, kwa msisitizo na kwa umuhimu wa suala hili, Kamati inaendelea kuzishauri halmashauri zote nchini, kuhakikisha kuwa katika bajeti zake, ***asilimia isizopungua sitini (60%) kutoka katika makusanyo ya ndani (own source) inatengwa kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wananchi. Kamati haitokuwa tayari kukubaliana na bajeti ya Halmashauri yoyote ile kama haijakidhi matakwa ya agizo hili. Aidha Kamati inaitaka Ofisi ya Waziri Mkuu (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) kuhakikisha agizo hili la Kamati linatekelezeka.***

5.5 **Mheshimiwa Spika,** Kamati inapendekeza kwamba Serikali iweke mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa mapato ya majengo **(property tax)** katika majiji, manispaa, miji na miji midogo kwani fedha nyingi zinapotea kwa kutokusanywa kwa kodi hii. Kamati inatambua kuwa agizo hili limeshaanza kutekelezwa na Serikali, hata hivyo kwa yale maeneo ambayo yameainishwa kutakiwa kufanyiwa tathimini kuhusu thamani halisi ya majengo hayo kwa ajili ya kutozwa kodi ya majengo, Kamati

inasisitiza tena kwamba, fedha maalum itengwe ili kuwezesha tathmini hiyo kukamilika kwa haraka ikiwa sahihi ili kodi hiyo ikusanywe katika Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**Ubunifu wa Vyanzo Vipya vya Mapato**

**5.6** **Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa bado kuna changamoto kwa halmashauri kuendelea kutegemea vyanzo vile vile vya mapato mwaka hadi mwaka ambavyo endapo kunapokuwa kumetokea jambo linaloathiri chanzo kimojawapo, makusanyo ya halmashauri hushuka.

**5.7** Kwa mfano, halmashauri ambazo zinazotegemea mapato yatokanayo na kilimo, pale ambapo wakulima wanapokosa mazao ya kutosha kutokana na uharibifu utokanao na majanga kama mafuriko, halmashauri hizo pia hutetereka kwa kukosa mapato. Hivyo basi, ubunifu wa vyanzo vipya vya mapato, sio tu kwamba utazisaidia kufikia malengo ya ukusanyaji lakini pia utaziezesha halmashauri kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa haraka.

**Usimamizi wa Matumizi**

**5.8** **Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba kukosekana kwa mapato kwa kiasi kikubwa kumechangiwa na kutokuwepo kwa mfumo mzuri wa usimamizi na ufuatiliaji. Aidha kumekuwepo na udanganyifu katika makusanyo, ambao kwa kiasi kikubwa umechangia kupotea kwa fedha nyingi. Kamati inaishauri Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI, kwa kushirikiana na wadau wengine, kuandaa mfumo wa uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo.

**Ushiriki wa Wananchi**

**5.9** **Mheshimiwa Spika,** Kamati inazitaka Sekretarieti za mikoa na halmashauri zote nchini kuhakikisha kwamba inawashirikisha wananchi kikamilifu katika maandalizi ya bajeti zao hususan katika mipango ya maendeleo na pia katika kubuni vyanzo vya mapatao na pia katika utungaji wa sheria ndogo za ukusanyaji ili kurahisisha zoezi la makusanyo bila manung'uniko.

**5.10** **Mheshimiwa Spika,** ushiriki wa wananchi pia utasaidia katika zoezi zima la kuchangia ujenzi wa miradi ya maendeleo hasa pale ambapo Serikali kuu pamoja na Serikali za Mitaa zitakapokuwa zinatoa mchango wake kikamilifu katika miradi husika na hivyo nguvu ya wananchi kutopotea.

**5.11** Aidha kamati inazitaka Halmashauri zote nchini kuacha kuwabughudhi na kuwanyanyasa wananchi wenye kipato cha chini kabisa kwa kuwalazimisha walipe kodi kubwa kuliko hata mtaji na thamani ya mali

zao wanazouza, hususan wafanya biashara ndogo ndogo, mfano wale wanaotembeza bidhaa za mikononi (maarufu kama wamachinga) na mama lishe, ambao mara kadhaa wamekuwa wakinyang'anywa biashara zao na migambo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kama wezi ndani ya nchi yao na migambo hao kinyume kabisa na maadili ya kiafrika wakizitupwa, wakihodhi ama kumwaga chini.

**5.12** **Mheshimiwa Spika,** mimi binafsi, nimewahi kushuhudia Mgambo wakimwaga chakula cha Mama Lishe aliyekaidi agizo la Mkuu wa Wilaya la kuondoka kwenye eneo walilozoea kufanyia biashara yao kwa sababu Serikali haikuwa imewaandalia eneo jingine mahsusi la kufanyia biashara hiyo – kikwetu kumwaga chakula chini bila sababu ya msingi ni kitendo kinachoondoa Baraka kutoka kwa Mungu, ndiyo maana sisi huwa tunakula viporo hadi vya ugali!

**5.13** **Mheshimiwa Spika,** vitendo vya kinyama dhidi ya watu wa aina hii ni vingi na kwa namna yoyote ile havikubaliki katika Taifa letu na hivyo basi Kamati inaitaka Serikali itekeleze Sera yake nzuri ya kuwalinda na kuwawezesha wananchi wenye uchumi wa chini kwa vitendo ili nao wajikwamue na umaskini, wakidhi mahitaji yao na waendelee kuiheshimu na kuipenda nchi yetu na Serikali yake.

**5.14** **Mheshimiwa Spika,** aidha, Kamati inaiagiza Serikali kutoa maelekezo sahihi kwa Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kuwajengea mazingira mazuri, wezeshi na ya kisheria wafanyabiashara wote wanaohangaika kutafuta mkate wao wa kila siku kwa uchuuzi wa bidhaa zinazohesabika kwa macho tu bila matumizi ya nguvu ili kulinda haki ya wananchi kujifanyia kazi zao za kujipatia kipato chao cha kujikimu kila siku na familia zao bila kuingiliwa, kama inavyosema **Sera ya CCM ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi, Sura ya Tano ya Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2010[3], Ukurasa wa 89, Sera Na. 75 (b.),** na naomba ninukuu:

***"75. Kwa kutambua kwamba kila raia wa Tanzania anayo fursa ya kumiliki ardhi na kuendesha shughuli za maendeleo pale anapoishi, Chama Cha Mapinduzi kinaendelea kutoa wito kwa wananchi kwamba sera ya uwezeshaji itafanikiwa tu katika maisha yao kama kila mwenye uwezo wa kufanya kazi atafanya yafuatayo:-***

***(b.) Kutambua kwamba, ardhi, cherehani, mgahawa, duka, mashine ya kufyatulia matofali anayomiliki n.k. ni msingi imara wa maendeleo yake na kwamba uwezeshaji ni njia ya kumuunga mkono. Kila mwananchi mwenye shughuli halali ya kufanya azame katika kujiletea maendeleo kwa kuendeleza shughuli hiyo."***

**5.15** **Mheshimiwa Spika,** haikubaliki kisera na hata kibinadamu kuwaondoa wananchi kwenye maeneo yao ya shughuli bila kuwalipa fidia, ama kwa kuwapunja fidia, kuwadhulumu mali zao kwa kisingizio cha matumizi ya sheria ama kuwafukuza mama lishe na wamachinga kwenye maeneo waliyozoea kufanyia biashara bila kuwaandalia mazingira mengine mazuri zaidi ya kufanyia kazi. Haikubaliki.

**5.16** **Mheshimiwa Spika,** Hatutofanikiwa kudumisha amani, mshikamano na upendo katika Taifa letu kama tutaendelea kufanya vitendo kama vinavyojitokeza kwenye mradi mkubwa wa kupima viwanja kule Lindi unaoendeshwa na taasisi ya Unity Trust of Tanzania (UTT), vya kuwanyang'anya wananchi maeneo yao ya asili bila ridhaa yao, kuyapima na kuyauza kwa ujanja ujanja huku mwenye ekari 20 za ufukweni akijikuta anapewa fidia kwa ekari 4 tu na nyingine kuandikishwa majina ya watu wasiojulikana. Mheshimiwa Spika, Kamati imesikitishwa na hili na imeazimia kuitaka Serikali kuwasilisha ndani ya wiki moja taarifa ya namna ilivyolishughulikia jambo hili na hatua ilizochukua dhidi ya udhalimu huu mkubwa kwa wananchi, na sambamba na hilo Kamati imeiagiza Serikali isitishe zoezi hili kwa muda mpaka ukweli wa namna jambo hili lilivyotekelezwa utakapopatikana. Aidha, Kamati imefurahishwa hatua za awali na za haraka zilizochukuliwa na Serikali kutii agizo la Kamati na hapa natumia fursa hii kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mhe. Hawa Abdulrahmani Ghasia, kwa kuguswa na jambo hili na kulitolea uamuzi wa mara moja kwa kuuagiza Mkoa kutekeleza maazimio ya Kamati bila kuchelewa.

**5.17** **Mheshimiwa Spika,** tusikubali kuvunja misingi imara ya Taifa letu kwa kuukubali ubepari na ubeberu kuingia nchini, na hadi kwa wananchi wetu huko vijijini, bila kuweka mifumo ya kulinda maslahi yao na kuyasimamia ilhali tunaujua uwezo wao kielimu, kiuchumi na kisheria – kuwa ni mdogo unaopaswa kuongozwa na Sera, Sheria na Huruma ya Wataalamu na Viongozi wetu kule Mikoani. Ubepari una sura nyingi, na una njia nyingi za kupenya na kujitengenezea himaya; tufumbue macho yetu, tuwahurumie watu wetu, tuzijue shida na kero zao, tuzingatie malalamiko yao, tutafute ufumbuzi wa shida, kero na malalamiko yao kwa nguvu zetu zote, na hata siku moja tusisahau kuwa tunatoka kwenye utamaduni wa kijamaa ambao ni asili yetu sisi waafrika. Tusiukubali ukweli wa usemi kuwa ***'Mwenye shibe hamjui mwenye njaa.'***

**Maoni ya Jumla**

**5.18** **Mheshimiwa Spika,** msongamano wa magari katika jiji la Dar es salaam ni tatizo kubwa linalohitaji kupatiwa ufumbuzi wa haraka na wa maksudi kabisa. Madhara ya msongamano ni mengi ikiwemo kuleta hasara kubwa katika uchumi kwa kupunguza masaa ya kazi (man hours) na

kuchelewesha watu kwenda kupata huduma za kijamii. Pamoja na jitihada za serikali na watu binafsi kujenga makazi, maofisi na sehemu za masoko makubwa nje ya jiji, bado tatizo hili halijapatiwa ufumbuzi. Ili kupata ufumbuzi wa tatizo la msongamano wa magari jijini Dar es salaam, mwaka 2007 Serikali ilibuni mradi wa Usafiri wa mabasi yaendayo kasi (Bus Rapid Transit, BRT), na kwa mujibu wa mpango huo, mradi huu ukikamilika inakadiriwa utakuwa umetatua tatizo la usafiri wa umma katika jiji la Dar es salaam na pia kupunguza msongamano wa magari jijini humo mpaka kufikia miaka ya 2030/31. Hata hivyo, Kamati ya TAMISEMI imebaini kuwa kungepaswa kuwe na usanifu ambao ungezingatia walau utatuzi wa tatizo hili kwa miaka 50 na hata 100 baadaye kwa kutazama maoteo ya idadi ya watu katika miaka hiyo. Usanifu (design) ya mradi ingepaswa kuzingatia uwepo wa njia mbalimbali mchanganyiko za kutatua tatizo hili, hata kama kwa sasa tuna uwezo wa kujenga miundombinu ya mabasi yaendayo kasi tu. Hii ingetoa fursa kwa serikali kuongeza njia moja baada ya nyingine kukamilika ama kadri ambavyo pesa zinapatikana bila kuathiri bajeti za fidia ama kubomoa bomoa miundo mipya na imara inayojengwa sasa, na zaidi bila kuongeza msongamano katika kipindi chote cha mradi.

**5.19** **Mheshimiwa Spika,** waingereza wana methali moja kuwa **"chance favours a prepared mind",** kwamba 'fursa hupendelea kwenda kwa mtu aliyejiandaa kuipokea.' Hivyo, ni ushauri wa Kamati yetu kuwa, tujipange kwa kuwa na mpango kabambe wa kutatua kero za msongamano wa watu na magari katika jiji la Dar es salaam kwa kuwa linakua kwa kasi sana. Tusishindwe kujenga leo na tukakubali kushindwa hata kupanga tu! Kusanifu mpango mzuri si kujenga, ni kusanifu tu. Kuna uwezekano mkubwa wa kufanya usanifu unaozingatia idadi ya watu na maoteo ya idadi ya magari miaka 50 mbele, yaani **"simulation model"** ya kipindi hicho na hivyo kubuni njia mbalimbali zitakazohitajika kuwepo kipindi hicho. Kufanya hivi itasaidia kupunguza bomoa bomoa kila mara inapohitajika kujenga awamu nyingine ya mfumo kutokana na mahitaji ya wakati huo.

**5.20** **Mheshimiwa Spika,** Kamati pia imebaini kuwa miradi ya mabasi yaendayo kasi, kujenga reli, ama kuweka seabuses na ama treni nyepesi za umeme mijini, kwa mujibu wa sheria zetu na mgawanyiko wa madaraka uliopo, inaangukia juu ya mamlaka tofauti tofauti za kiutawala; kuna ambayo inaangukia moja kwa moja ofisi ya waziri mkuu (TAMISEMI), mingine ipo chini ya Wizara ya Uchukuzi na mingine chini ya Wizara ya Ujenzi. Hivyo, ni lazima ufanyike uratibu ndani ya Serikali ili katika hatua hii, ikamilishwe hatua ya usanifu wa njia mchanganyiko za mfumo wa usafiri jijini **(multi-modal city transit systems)** ili kukidhi mahitaji mapana ya baadaye.

**5.21** Hivyo basi, Kamati inaiagiza Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kuratibu zoezi la kusanifu kwa pamoja na Wizara za Uchukuzi, Wizara ya Ujenzi, na Ofisi ya Rais – Tume ya Mipango ili kupata picha ya Dar es salaam ya miaka 50 ijayo na miaka 100 ijayo, yaani ***"Simulation Model"*** kwa lengo la kupata Mfumo wa Usafiri Mchanganyiko **(Multi – Model Transport System):** ambao utaunganisha mfumo wa mabasi yaendayo kasi **(Bus Rapid Transit),** treni za umeme za mjini **(TRAMS),** treni kasi mjini juu kwa juu na chini ya ardhi na chini ya maji **(RAPID TRANSIT TRAINS – RTT)** na mabasi ya juu ya maji **(sea buses).**

**5.22** **Mheshimiwa Spika,** mipango hii iende sambamba na usanifu wa mipango ya barabara za juu **(flyovers)** na Reli ya *Trams* iwe mule mule kwenye barabara za mabasi yaendayo kasi **(Bus Rapid Transit)**. Aidha kwenye usanifu huu mpya, hata kama miradi haitekelezwi leo, pafanyike utaratibu wa kuaandaa mazingira na nafasi ya mahali ambapo nguzo za treni za hewani na barabara za juu zitapita. Hii ikifanyika leo, itaokoa pesa nyingi huko mbeleni. Maana sote tutakubaliana kuwa, kazi ya kujenga miundo mbinu hii haikwepeki katika siku za usoni.

**5.23** Mpango uwe wa mwaka 2014 – 2050 na wataalam wanaweza kutengeneza sinema ikizingatia ongezeko na msongamano wa watu na magari. Trams na Treni zitumie umeme kupunguza uchafuzi wa hewa na kelele katika Jiji. Mabasi ya majini yaende Posta – Tegeta – Bagamoyo. Tukiwa na usanifu wa aina hii na kwa kuzingatia ujio wa utajiri wa gesi, tutaweza kuja kuitekeleza miradi yote hii wakati fedha zitakapopatikana kupitia mfuko wa utajiri wa Taifa, yaani **"sovereign wealth fund."**

**5.24** **Mheshimiwa Spika,** tumebaini kuwa wananchi wakiunganishwa katika ushirika wanaongeza tija na ufanisi katika shughuli zao lakini pia inakuwa rahisi kuwafikia na kuwahudumia ikiwemo kuwajengea uwezo zaidi. Kamati imebaini uwepo wa ushirika wa wakulima kwenye mazao mbalimbali makubwa, lakini kwa bahati mbaya sana kumekuwa na migogoro na matatizo yasiyoisha kwenye ushirika huu, jambo ambalo limepelekea Serikali kulazimika kila leo kuingilia kati uendeshaji wa ushirika ili kuwanusuru wananchi walio wengi vijijini ambao ni wanachama wafaidika wa vyama mbalimbali vya ushirika.

**5.25** **Mheshimiwa Spika,** ushirika ni nguzo imara sana ya uchumi wa watu maskini katika mifumo ya kijamaa, hivyo ni lazima tuulinde ushirika kwa nguvu zetu zote. Huku kulegalega kwa ushirika kunatakiwa kutazamwe kwa jicho la 'tatu' kama kweli tuna nia ya dhati ya kuwatumikia wananchi waliotuweka madarakani. Sababu kubwa ya kulega lega huku ni kuingia kwa mfumo mpya wa kiuchumi katika nchi yetu. Hatujawa tayari kukiri, lakini ni wazi kabisa, ubepari na ubeberu unatamalaki katika

uchumi wetu na siwezi kushangaa kuona ushirika wa kijamaa unapata taabu kustawi kwa kushindana na nguvu za mabwanyenye waliounyemelea uchumi wetu. Kwa msingi huu, ni lazima Serikali, ili kutatua kero za ushirika zilizodumu kwa muda mrefu na kuhakikisha wakulima na haki zao wanalindwa na uwepo wa ubepari na mabepari wasio na huruma kwa maskini bali nia na tamaa ya kutaka kukidhi haja yao ya kukuza mitaji na kuongeza faida kwao binafsi tu, ibuni mfumo mpya na wa kisasa wa ushirika unaoendana na mfumo huu mpya wa soko huria ambamo mapepari, mabeberu na wajamaa wanatangamana na kushindana kuzalisha, kununua na kuuza bidhaa.

**5.26** Ofisi ya waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ziajiri wafanyakazi wa ngazi mbalimbali kulingana na upungufu kwa kila Halmashauri na kwa wakati, ili shughuli mbalimbali za Halmashauri ziweze kutekelezeka.

**5.27** Tawala za Mikoa kuwa na mipango ya muda mfupi na muda mrefu kulingana na mabadiliko ya ongezeko la watu nchini, ili kuepuka tatizo la miundombinu kutokidhi mahitaji halisi hivyo kusababisha msongamano katika vituo vya kutolea huduma kama vile mashuleni, katika shule, hospitalini n.k.

**5.28** Serikali iboreshe miundombinu ya sasa na kutekeleza miradi inayoendelea kwa ufanisi na kiwango bora, ili kuepusha kuharibika kwa miundombinu muda mfupi tangu mradi husika kukamilika kuepusha upotevu wa fedha ya serikali.

**5.29** Aidha, Halmashauri zitenge fedha zao wenyewe ili kununua vifaa mbalimbali na mitambo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu na miradi mbalimbali ya mendeleo katika Halmashauri zao na kutumia wataalam wa ndani katika kutekeleza miradi hiyo na hivyo kuokoa gharama itokanayo na wazabuni.

**5.30** **Mheshimiwa Spika,** Ili tuendane na uchumi wa kisasa na tuweze kuyafikia malengo tuliyojiwekea kama Taifa, hususan lile kubwa la kufikia kuwa nchi yenye uchumi wa kiwango cha kati (yaani **Mid-Income country)** ifikapo mwaka 2025, ni lazima tuwe na raslimali watu ya kutosha na yenye weledi wa hali ya juu. Kamati inakiri na kupongeza mafanikio makubwa katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa kuhakikisha tuna Shule za Sekondari kwenye kila Kata, tuna zahanati kwenye kila kijiji na Kituo cha Afya kwenye kila Kata. Kwa kiasi kikubwa malengo ya kujenga majengo na mahala pengine kuanzisha utoaji wa huduma yameweza kufikiwa.

**5.31** Hata hivyo, Kamati imebaini changamoto kubwa kwenye ubora wa huduma kutokana na kuwa na nguvu kazi kubwa ya watumishi ambayo haina motisha ya kujitoa. Kwa kuzingatia nia yetu kama Taifa ya kutaka kuyafikia malengo yetu, ni lazima tubuni mbinu mahsusi za kutoa motisha kwa watoa huduma wetu ili tuweze kufikia malengo yetu bila shida. Tunaweza kutazama mifumo ya kutoa motisha kwa kutazama umbali wa kijiografia ama kwa kuzingatia utofauti wa kimajukumu na kutoa motisha stahiki **(differential incentives).** Mfumo wa motisha unataka katika hatua hii tuwe na kipengele chenye mkakati wa kujenga nyumba za watumishi vijijini, kuboresha mazingira ya kazi kwa kuhakikisha vitendea kazi vyote vipo na vinapatikana kadri vinavyohitajika na uwepo wa posho za ziada kutokana na vigezo vya utofauti wa kimazingira ama kimajukumu (mfano: wanaofanya kazi vijijini zaidi wanakuwa na posho yao maalum, na mfano mwingine ni kwa wale wenye majukumu maalum kama kufundisha masomo ya Hisabati na Sayansi ama kuwa Daktari Bingwa na kukubali kufanya kazi kwenye hospitali zilizo mbali na majiji).

**5.32** **Mheshimiwa Spika,** ni jambo gumu sana kwa Diwani kule kwenye Kata ama Mbunge kumshawishi Mwalimu afanye kazi yake kwa bidii wakati Mwalimu huyo anaishi kwenye nyumba isiyo na madirisha ama wavu, isiyo na maji wala umeme, na kijiji kisicho na mawasiliano ya simu wala ya intaneti, na anaishi kwenye nyumba hiyo kwa kuchangia na walimu wenzake wanne. Ama anapaswa kwa siku kufundisha masomo matatu, kidato cha kwanza hadi cha nne; na pamoja na mzigo huu wa kazi, hana posho ya ziada na ana mshahara sawa na Mwalimu mwenye kipindi kimoja tu kwa siku, ana nyumba nzuri ya kuishi, ana umeme, maji, mtandao wa simu na inteneti, na mshahara wao ni sawa!

**5.33** Mheshimiwa Spika, sababu za kutokuwa na pesa haziwezi kutosha kukidhi kiu ya majibu wanayoyatarajia walimu, manesi, ma-afisa ugani, na madaktari kule vijijini. Hazitoshi hata kidogo. Ni lazima tufumbuke, tujipange upya tutafute suluhu ya namna tutakavyoongeza motisha kwa watoa huduma wetu vijijini. Kuwaeleza madaktari kuwa hatuna fedha za kuwalipa posho ya kufanya kazi usiku, yaani **'on-call allowance'** wakati tunaweza kuwalipa wataalamu wengine kwenye serikali posho ya masaa ya ziada, yaani **'extra-duty allowance'** ni jambo lisiloingia akilini, na linalokatisha tamaa sana. **Kama tunakubaliana hakuna uwezo wa kulipa posho kwa baadhi ya makundi ya watumishi, ingekuwa busara ya kawaida kabisa kuamua kwa pamoja kufuta posho ya vikao kwetu sote *(sitting allowance ya Wabunge ikiwemo)* na kufuta posho za kufanya kazi masaa ya ziada kwenye mfumo wetu wa utawala na sote tukajitolea.**

**5.34** **Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kusisitiza kwamba, ili kuleta maendeleo ya kweli na ya haraka kwa Wananchi, ni lazima yafanyike mageuzi makubwa katika maeneo makuu yafuatayo:-

i. **Mabadiliko ya kifikra (change of mind set)** kwa Watendaji wa Serikali waliopewa dhamana ya kusimamia rasilimali zilizopo. Hatuwezi kufanya kazi kwa kuendelea kuamini kuwa maendeleo yanatokea juu au nje. Ni vyema Sera ya Ugatuaji Madaraka kwa Umma (D by D) iwe msingi mkuu wa kuziwezesha halmashauri kujitegemea na kuwaletea wananchi maendeleo.

ii. **Uwajibikaji: -** Madiwani na Wabunge, wanao uwezo na dhamana ya kuwasimamia watendaji wasiotekeleza majukumu yao kwa maendeleo ya Wananchi kwa kuhakikisha kuwa wanashiriki kikamilifu katika vikao vyote na hasa vile vya Kamati za Fedha (Finance Committees) na Baraza la Madiwani (Full Council).

**Mheshimiwa Spika**, aidha kwa upande wa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, wasiache kutekeleza jukumu la usimamizi unaochochea maendeleo. Kamati hii kwa niaba ya Bunge, haitasita kufika eneo lolote ambalo lina harufu ya kutowajibika ili kufanya uchunguzi na kupendekeza hatua za kinidhamu kuchukuliwa kwa wale watakaobainika kukiuka Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo.

**Mheshimiwa Spika,** hatuwezi kuleta ustawi wa Taifa letu bila uwajibikaji, na uwajibikaji unakuja pamoja na maumivu. Aidha, maumivu yatokanayo na kufanya kazi kwa bidii na kwa kujitolea ili kutimiza majukumu yako kwa ufanisi au maumivu yatokanayo na kuwajibishwa kwa kutotekeleza majukumu yako kikamilifu. Maumivu yote haya mawili ni lazima ili maendeleo yapatikane.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasisitiza na kuishauri Serikali kuanzisha Mfuko Maalum wa Miradi ya Ujenzi wa Hospitali za Rufaa kwa kuzingatia Kanda za Kiutawala ili kutengwe fedha za kutosha kukamilisha miradi mingi kwa muda mfupi.

iii. **Vipaumbele katika kukuza uchumi**: Wananchi washirikishwe kikamilifu katika kutambua fursa walizo nazo ambazo zitachochea ustawi na maendeleo ili kukabiliana na umaskini.

## 6.0 HITIMISHO

**6.1** **Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati ninamshukuru Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala

za Mikoa na Serikali za Mitaa akisaidiwa na Mhe. Aggrey Deaisile Joshua Mwanri (Mb) na Mhe. Majaliwa Kassim Majaliwa (Mb), Naibu Mawaziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Watendaji wa Ofisi hiyo wakiongozwa na Ndg. Jumanne A. Sagini, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa jinsi walivyoshirikiana na Kamati katika kutoa majibu ya hoja za Waheshimiwa Wabunge kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**6.2** **Mheshimiwa Spika,** vilevile napenda kutoa shukrani za kipekee kwa wakuu wa mikoa yote ya Tanzania Bara pamoja na sekretarieti za miko na halmashauri zote kwa mawasilisho ya taarifa za utekelezaji wa bajeti zilizopita na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 na kwa kuzingatia mapendekezo ya Kamati katika maeneo mbalimbali.

**6.3** **Mheshimiwa Spika,** namshukuru sana Mhe. John Paul Lwanji (Mb) Makamu Mwenyekiti wa Kamati, kwa msaada anaonipa kuiongoza Kamati wakati ninapokuwa natekeleza majukumu mengine ya kitaifa. Aidha, kwa umuhimu mkubwa nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa uzalendo wao, maoni, busara, mahudhurio, utayari wao wa kufanya kazi bila kuchoka na ushauri uliosaidia kuwasilishwa kwa taarifa hii mbele ya Bunge lako.

**6.4 Mheshimwa Spika,** kwa heshima na taadhima, na kwa kutambua mchango wao katika kuipitia na kuijadili Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI, naomba niwatambue wajumbe wa kamati kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. John Paul Lwanji, Mb – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Highness Samson Kiwia, Mb
4. Mhe. Benardetha Kasabago Mushashu, Mb
5. Mhe. Asha Mohamed Omari, Mb
6. Mhe. Rosweeter Faustine Kasikila, Mb
7. Mhe. Christopher Olonyokie Ole-Sendeka, Mb
8. Mhe. Eugen Elishiriga Mwaiposa, Mb
9. Mhe. Rashid Ali Abdallah, Mb
10. Mhe. Mhandisi Athuman Rashid Mfutakamba, Mb
11. Mhe. Pauline Philipo Gekul, Mb
12. Mhe. Sabreena Hamza Sungura, Mb
13. Mhe. Mkiwa Adam Kimwanga, Mb
14. Mhe. Mariam Salum Mfaki , Mb
15. Mhe. Moses Joseph Machali, Mb
16. Mhe. Sylvester Massele Mabumba, Mb

17. Mhe. Conchesta Leonce Rwamlaza, Mb

**6.1** **Mheshimiwa Spika,** napenda kuishukuru Ofisi ya Bunge hasa Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah na Makatibu wa Kamati Ndg. Yona Kirumbi na Ndg. Mwajuma Ramadhan wakisaidiwa na Ndg. Cletty Urassa, kwa uratibu wa shughuli zote za Kamati. Pia nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuihudumia Kamati mpaka kukamilika kwa taarifa hii.

**6.2** **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 jumla ya **Shilingi Trilioni 4,978,576,426,000.**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA**
**NA SERIKALI ZA MITAA**
6 Mei, 2014

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa wa Kamati ya Ukimwi! Mwenyekiti wa Kamati ya UKIMWI! Hakuna, mwakilishi wake? *Okay!*

**MHE. OMARY AHMAD BADWEL (k.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASWALA YA UKIMWI):** Mheshimiwa Spika, ifuatayo ni taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya masuala ya Ukimwi kuhusu utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya Fungu 91 na Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania, Fungu 92 kwa mwaka wa fedha 2013/2014 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kwa Tume hizo.

Mheshimiwa Spika, utangulizi, kwa mujibu wa kanuni ya 99(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2013, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu na bajeti ya Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya Fungu 91 na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania Fungu 92 kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu ya Bunge kwa mujibu wa Ibara ya 63 (2) na 63 (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya

mwaka 1977, pamoja na majukumu mengine, Bunge lina jukumu la kuidhinisha mapato na makadirio ya fedha za Serikali na kufuatilia utekelezaji na usimamizi wa shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Aprili, 2013, inaelekeza kwamba Kamati za Bunge za kisekta zinatakiwa kufanya ukaguzi wa miradi iliyoombewa fedha za maendeleo na kuidhinishiwa kwa mwaka wa fedha unaomalizika.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu hayo ya kikatiba na kikanuni, Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi kuanzia tarehe 28 Januari hadi tarehe 6 Februari, 2014 kwenye Mikoa ya Iringa na Pwani.

Aidha, Tarehe 1 Mei hadi tarehe 2 Mei, 2014, Kamati ilifanya Kazi ya kupitia taarifa ya Utekelezaji wa bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 pamoja na kuchambua Makadirio ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2014/2015 kwa Tume hizo mbili.

Mheshimiwa Spika, kufuatia maelekezo hayo, Taarifa ya Kamati ninayoiwailisha mbele ya Bunge lako, imegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza inahusu Taarifa ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, sehemu ya pili inahusu Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, na sehemu ya tatu inahusu maombi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kutembelea miradi hii, ulilenga kupata picha halisi ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2013/2014 pamoja na kujiridhisha na hali halisi ya matumizi ya fedha za Umma na hatimaye kuishauri Serikali katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Moja, Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya**;** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2013/2014 Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya iliomba na kuidhinishiwa fedha za miradi ya maendeleo jumla ya Sh. 2,651,738,800/=. Fedha hizi zilijumuisha pesa za ndani Sh. 350,000,000/= kwa ajili ya Mradi wa Ujenzi wa Ghala la Kuhifadhia Vielelezo vya Kesi za Dawa za Kulevya na Sh.2,798,000,000/= fedha za nje kwa ajili ya Mradi wa Kudhibiti Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI miongoni mwa watumiaji wa Dawa za kulevya kwa kujidunga sindano.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa kiasi kikubwa fedha za miradi ya maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge kwa wakati na Mradi wa Ujenzi wa Ghala la Kuhifadhia Vielelezo vya Kesi za Dawa za Kulevya imetolewa na Kamati ilipotembelea mradi huu ilikuta ujenzi wa ghala hiyo ukiendelea na kuridhishwa na kazi iliyofanyika.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kutenga fedha zake za ndani kwa ajili ya ujenzi wa Ghala la Kuhifadhia Vielelezo vya Kesi za Dawa za Kulevya. Kamati inaamini hatua hii muhimu itasaidia kuboresha mazingira ya kufanyia kazi pamoja na kuharakisha hukumu za kesi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pili, Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania. Katika Mwaka wa Fedha 2013/2014 Tume ya Kudhibiti UKIMWI iliomba na kuidhinishiwa jumla ya Sh.15,334,335,000/= kwa ajili ya kutekeleza afua za UKIMWI na mwitikio wa kitaifa kupitia miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2014 kiasi cha Shilingi 9,939,107,213.40 sawa na asilimia 71 zilikuwa zimeshatolewa. Kamati inaamini mpaka kufikia Juni 30 kiasi cha fedha ambazo hazijatolewa sawa na asilimia 29 kitatolewa na kukamilisha kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kufuatilia utekelezaji wa fedha hizo, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa matumizi ya fedha hizo kwa Mikoa ya Pwani na Iringa kwa muda wa siku saba kuanzia 28 Januari hadi 6 Februari, 2014.

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa kufanya ziara Mikoani, Mikoa hiyo ilifikiwa kufuatia Ripoti ya Utafiti wa Viashiria vya VVU na UKIMWI kwa Mwaka 2011/2012 ambao unaonyesha Mkoa wa Iringa ni wa pili wa maambukizi makubwa kiTaifa na Mkoa wa Pwani ulitembelewa kwa kuwa ni moja kati ya Mikoa inayoongoza kwa maambukizi makubwa.

Aidha, Mkoa wa Njombe unaoongoza kwa kuwa na maambukizi makubwa ya Virusi vya UKIMWI ulishatembelewa na Kamati na taarifa yake ilitolewa kwenye Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa shughuli za Kamati iliyowasilishwa Bungeni Desemba, 2013.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hizo, Kamati iliweza kubaini mambo mbalimbali yafuatayo:-

Mambo muhimu yaliyojitokeza katika ziara ya Mkoa wa Pwani.

Moja, Kamati inaupongeza Mkoa wa Pwani kwa kufanya janga la UKIMWI na tatizo la Dawa za kulevya kuwa ajenda ya kudumu katika mipango ya Mkoa huo.

Pili, Watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI wameweza kwa kusaidiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha kuanzisha umoja wa watu wanaoishi na UKIMWI ambapo Wilaya imeweza kuwapatia mtaji wa kuendesha biashara ndogo ndogo ili kujiongezea kipato na kupata lishe bora.

Tatu, Kamati inaupongeza Uongozi wa Mkoa na hususan Halmashauri ya Kibaha kwa kutenga mapato ya ndani kwa ajili ya afua za UKIMWI na dawa za kulevya.

Nne, Mkoa umeweza kuwasaidia vijana walioacha kutumia dawa za kulevya kwa kuwapatia mtaji na kuanzisha mradi wa kuosha magari. Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha imeweza kununua mashine mbili za kuosha magari kwa ajili ya vijana hao ambazo zimewasaidia vijana hao kuongeza kipato na kuweza kujitegemea.

Tano, Kamati inaupongeza Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* kwa kuanzisha mpango wa kunusuru kaya masikini ambapo mpango huu umesaidia kuboresha maisha ya watu masikini.

Mheshimiwa Spika, changamoto. Moja, Kamati imebaini kuwepo na tatizo kubwa la ucheleweshaji wa fedha kutoka Wizara ya Fedha na Tume ya kudhibiti UKIMWI hali inayochangia miradi mingi na mipango mbalimbali dhidi ya UKIMWI kushindwa kutekelezekwa na kukamilika kwa wakati.

Pili, kukosekana kwa mpango mkakati wa kupambana na UKIMWI na dawa za kulevya katika ngazi ya Mkoa na Halmashauri.

Tatu, mipango mingi ya mapambano ya UKIMWI inategemea fedha za wadau wa maendeleo.

Nne, vijana walioacha kutumia dawa za kulevya kukosa fedha za kutosha na maeneo ya kufanyia shughuli mbalimbali za kuwaingizia kipato.

Tano, miradi ya kusaidia kaya masikini unaoendeshwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* kupitia mpango wa kunusuru kaya maskini, inakabiliwa na tatizo la wataalam wa ugani kutowafikia walengwa.

Sita, Halmashauri kutowasimamia wataalam wa ugani ili kuwajengea wananchi uwezo wa uendeshaji bora wa miladi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maagizo na ushauri wa Kamati kwa Mkoa wa Pwani na Wilaya zake.

Moja, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inatoa fedha zilizoizinishwa na Bunge kwa wakati.

Pili, Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania ishirikiane na Sekretarieti za Mikoa na Wilaya na kuandaa Mpango kazi wa kupambana na UKIMWI katika ngazi zote.

Tatu, Kamati inazishauri Sekretarieti na Mikoa kutenga fedha za kuwahudumia WAVIU na waathirika wa dawa za kulevya kutoka mapato yake ya ndani.

Nne, Kamati inashauri Uongozi wa Mkoa wa Pwani kuwasaidia vijana walioacha kutumia dawa za kulevya na umoja wa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI kwa kuwapatia elimu ya ujasiriamali, mitaji na maeneo kwa ajili ya kuendeshea biashara zao pamoja na kuwatafutia masoko ya bidhaa zao.

Tano, ili miradi ya kunusuru kaya masikini iwe endelevu, ni vyema wasaidiwe kuanzisha Vyama vya Kuweka na Kukopa, yaani *SACCOS* na *VICOBA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya ziara Mkoa wa Iringa na kutembelea Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Manispaa ya Iringa, Wilaya ya Mufindi, Halimashauri ya Wilaya ya Kilolo na baadhi ya Vijiji, pamoja na shughuli ya ukaguzi wa miradi. Kamati pia ilipokea Taarifa ya Mkoa na Wilaya zake kuhusu mapambano dhidi ya UKIMWI na dawa za kulevya.

Mambo muhimu yaliyojitokeza katika ziara ya Mkoa wa Iringa ni kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mafanikio, Kamati imeridhishwa na inaupongeza Uongozi wa Mkoa kwa jinsi Mkoa ulivyojipanga kupambana na tatizo la UKIMWI. Mkoa wa Iringa una mpango makakati wa kupambana na UKIMWI. Mpango mkakati huu ulitokana na Azimio lililopitishwa kwenye kikao cha ushauri cha Mkoa, *RCC*. Hii inaonyesha kuwa, kuna utashi wa kisiasa wa kupunguza maambukizi ya UKIMWI. Mkoa huu unafaa kuwa Mkoa wa mfano na wa kuigwa. *(Makofi)*

Pili, Kamati inaupongeza Uongozi wa Mkoa wa Iringa kwa kutekeleza Sera ya mwaka 2010 ya *Private Public Partnership (PPP),* ambapo Mkoa umeweza kushirikiana na sekta binafsi na wadau mbalimbali katika kupambana na UKIMWI na hivyo kusaidia kupunguza unyanyapaa. *(Makofi)*

Tatu, Kamati inaupongeza Uongozi wa Mkoa wa Iringa kwa kutekeleza kwa vitendo mwongozo wa uundaji wa Kamati za kudhibiti UKIMWI za Wilaya, Kata, Vijiji na Vitongoji, ambazo kwa asilimia kubwa zimekuwa zikikutana na kufanya kazi kama mwongozo ulivyowaelekeza. *(Makofi)*

Nne, Vijiji 67 zaidi ya Vijiji 123 vya Halmashauri ya Wilaya ya Iringa vimeweza kuanzisha mifuko ya kusaidia watoto yatima pamoja na kupunguza madhara yatokanayo na UKIMWI.

Tano, Mkoa unafanya kazi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Aidha, Mkoa unao utaratibu wa kuainisha kila mdau na shughuli anazofanya pamoja na fedha alizochangia katika shughuli anazozifanya. Utaratibu huu ni wa kupongezwa na kuigwa kwa kuwa unaisaidia Serikali kuweza kuratibu vizuri shughuli za mapambano dhidi ya UKIMWI na unapunguza mwingiliano wa kazi na unaokoa muda na fedha.

Sita, Kamati inaupongeza Halmashauri ya Wilaya ya Iringa Manispaa ya Iringa kwa kushirikiana na Taasisi isiyo ya Kiserikali ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto Vijiji ***(TAWOK)*** kwa kuanzisha kituo cha kuwahudumia waathirika wa vitendo vya ukatili wa kijinsia, wengi wao wakiwa ni wananwake na watoto. Kuanzishwa kwa kituo hiki kimesaidia kuwahifadhi kwa muda waathirika wa ukatili wa kijinsia na hivyo kupunguza tatizo la watoto wa mitaani kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Kamati inapongeza juhudi ya mapambano dhidi ya UKIMWI zinazofanywa na Shirika la Ma-*sister* Wa-*missionary* wa *Consolatha* kwa kuanzisha Kituo cha Lamano, ambacho kinatoa huduma mbalimbali kama ushauri nasaha na upimaji, *clinic* ya tiba na dawa, huduma ya wagonjwa nyumbani na huduma ya watoto waishio katika mazingira hatarishi na yatima.

Huduma hizi hutolewa na kituo cha ufadhiri cha *USAID Paper* na *Africare*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto zilizopo ni kama ifuatavyo:-

Mkoa wa Iringa ni miongoni mwa Mikoa inayoongoza KiTaifa kwa maambukizi ya UKIMWI. Maambukizi hayo yanachangiwa kwa kiasi kikubwa na mwingiliano wa watu kutoka ndani na nje ya nchi hususan wafanyabiashara wanaofanya shughuli za biashara katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, unywaji wa pombe uliokithiri na ukatili wa kijinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pili, Kamati imebaini baadhi ya Wajumbe wa Kamati za Kudhibiti UKIMWI katika ngazi za Kata na Vijiji hawajajengewa uwezo, hivyo hawajui wajibu wao. Aidha, Kamati imebaini kuna ukiukwaji mkubwa wa mwongozo wa upatikanaji wa Wajumbe wa Kamati hizi.

Tatu, kutopatikana kwa wakati fedha za ruzuku zilizotengwa kwa ajili ya utekelezajio wa afua za UKIMWI na uhaba wa rasilimali fedha katika kutekeleza mipango ya UKIMWI.

Nne, upungufu wa vitendanishi vya kupimia *VVU, DBS, DETRTAMINE* na *UNIGOLD* katika bohari ya madawa. Aidha, hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi inakabiliwa na tatizo la *CD4 machine*. *CD4 machine* iliyopo ni ndogo na hivyo kuzidiwa uwezo wa kupima sampuli kutokana wingi wa wananchi wanaohitaji huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maagizo na ushauri Kamati kwa Mkoa wa Iringa na Wilaya zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mkoa wa Iringa ni miongoni mwa Mikoa inayoongoza kwa maambukizi ya virusi vya UKIMWI kiTaifa, na kwa kuwa ukishusha maambukizi kwenye Mkoa huu maambukizi kiTaifa yatashuka pia, Kamati inashauri kuwa utaratibu unaotumika sasa wa ugawaji fedha kulingana na wingi wa idadi ya watu upitiwe upya na kuboreshwa ambapo kipaumbele kiwe kwenye Mikoa/ maeneo yenye maambukizi makubwa ya UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ili kushusha maambukizi ya UKIMWI kiTaifa, ni lazima kushusha maambukizi ya UKIMWI katika Mikoa kumi yenye maambukizi makubwa. Kamati inashauri Tume ya kudhibiti UKIMWI *(TACAIDS)* kuanzisha mpango mkakati maalum wa kupambana na UKIMWI kwenye Mikoa hiyo ikiwa ni pamoja na kutengewa fedha. *(Makofi)*

Tatu, mfumo wa uendeshaji wa Kamati za kudhibiti UKIMWI ngazi ya Kata, Vijiji na Vitongoji uangaliwe upya. Mfumo ulioko sasa umepitwa na wakati na hauendani na hali halisi ya tatizo. Kwa mfano, vigezo vinavyotumika kuteua Wajumbe wa Kamati hizi havizingatii mwongozo uliopo.

Nne, ili kuleta ufanisi wa utekelezaji wa mapambano dhidi ya UKIMWI katika ngazi ya Kata, Vijiji na Vitongoji, Kamati inazishauri Halmashauri na Manispaa zote nchini kuzijengea uwezo Kamati za kudhibiti UKIMWI kwa kuwapa mavunzo ya aina mbalimbali ambazo zitajumuisha ziara za mafunzo kwenye maeneo ambayo Kamati za aina hii zimefanikiwa.

Tano, kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ina kiwango cha juu cha maambukizi ya UKIMWI yanayotokana na mwingiliano wa wageni ambao ni wafanyabiashara, Kamati inashauri Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na Mkoa wa Iringa kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi kuandaa mpango mkakati wa kupambana na UKIMWI wa Mkoa utakaoshirikisha wadau na wafanyabiashara wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ukatili wa kijinsia ni moja ya kichocheo kikubwa cha maambukizi ya virusi vya UKIMWI katika Mkoa wa Iringa. Kamati inaishauri Serikali kuanzisha *program* maalum zitakazosaidia kupunguza tatizo la ukatili wa kijinsia. *Program* hizi zihusishe madawati ya ukatili wa kijinsia yaliyoko Vituo vya Polisi, kuanzisha vituo/sehemu za kuwahifadhi waathirika wa ukatili wa kijinsia na kushirikisha mashirika yasiyo ya kiselikali katika kushughulikia tatizo hili.

Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuona uwezekano wa kutoa ruzuku kwa mashirika yasiyo ya Kiserikali ambayo yamekuwa yakifanya kazi kubwa na nzuri ya kuwahudumia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, unywaji pombe wa kupindukia ni chanzo kingine cha maambukizi ya UKIMWI Mkoani Iringa ambapo mnywaji wa pombe hupungukiwa uwezo wa kufanya maamuzi ya busara. Kamati inashauri, ili kuweza kukabiliana na tatizo la unywaji wa pombe uliokithiri Halmashauri za Miji na Wilaya zisaidie Uongozi wa Kata na **Vijiji** kutunga sheria ndogo ndogo za kupambana na ulevi kwenye maeneo yao. Aidha, ni vyema elimu kuhusu pombe na madhara yake itolewe mashuleni.

Nane, Kamati inaiagiza Wizara ya Afya kuhakikisha vifaa tiba na vitendanishi vya kupimia *VVU* vinapatikana kwa wakati na vinaendana na mahitaji halisi ya sehemu husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu/bajeti ya Tume ya Kuratibu Udhibiti Dawa za Kulevya na Tume ya Kudhibiti Ukimwi kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza juhudi za Serikali katika kushughulikia tatizo la biashara ya Dawa za kulevya. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa, kuendelea kucheleweshwa kwa uaandaaji na ukamilishwaji wa sheria mpya ya Kudhibiti Dawa za Kulevya kunakofanywa na Serikali kunapelekea kuendelea kushamiri kwa biashara haramu ya dawa za kulevya.

Kamati inaamini ikiwa Sheria mpya itakamilika mapema iwezekanavyo juhudi za kupambana na biashara ya dawa za kulevya zitafanikiwa kwa kiasi kikubwa na kurudisha taswira na heshima ya Tanzania nchi za nje. Aidha, Kamati inatambua uwezo wa Serikali ikiwa itadhamiria kwa dhati kupambana na tatizo la dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa nafasi ya Kamishna wa Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya imekuwa ikikaimiwa na Watendaji mbalimbali. Kukosekana kwa Kamishina wa Tume kumepelekea hukumu za kesi za dawa za kulevya kusimama.

Kusimama kwa kesi hizo kunatokana na matakwa ya kisheria kwamba Kamishina wa Tume ndiye anayehitajika kisheria kusaini kesi zote zinazohusu dawa za kulevya. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha uteuzi wa Kamishina wa Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, Tume ya kudhibiti UKIMWI inaendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupungua na kuchelewa kutolewa kwa fedha ziliotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na utegemezi mkubwa wa fedha za miradi ya maendeleo kutoka kwa wadau wa maendeleo. Licha ya changamoto hizo, Kamati imebaini pia kuwa muundo wa Tume ni moja ya changamoto kubwa inayokwamisha utendaji bora wa Tume hiyo.

Mheshimiwa Spika, muundo wa Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania unakinzana na miongozo ya utawala bora kwa kuwa Mwenyekiti Mtendaji wa Tume ndiye Mwenyekiti wa Kamisheni na Kiongozi wa Sekretarieti ya Tume. Muundo huu unapunguza ufanisi na uwajibikaji. Kamati inaendelea kuishauri Serikali ilete marekebisho ya sheria ili kuweza kutofautisha majukumu ya Mkurugenzi Mtendaji na Mwenyekiti wa Tume.

Mheshimiwa Spika, Maombi ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya tume ya kuratibu udhibiti wa dawa za kulevya na Tume ya Kudhibiti Ukimwi kwa mwaka wa fedha 2014/2015

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015, Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh. 9,999,577,000/= kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida na Mishahara ni Sh. 4,658,291,000/=. Sh. 5,341,268,000/= zinaombwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Mandeleo.

Mheshimiwa Spika, ilielezwa kwamba katika mwaka wa fedha 2014/2015 fedha inayoombwa imepangiwa kutekeleza kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuimarisha mazungumzo na majadiliano na wadau wa VVU na UKIMWI kupitia utaratibu na muundo wa majadiliano ya MKUKUTA. Kuimarisha upatikanaji wa huduma bora na za kutosha za UKIMWI, kuimarisha utetezi na uratibu wa *program* za mawasiliano ya mabadiliko ya tabia na kusaidia kuingizwa masuala ya jinsia kwenye mikakati ya mipango mbalimbali ya Taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya na Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa, Serikail kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu iongeze fedha kwa ajili ya uwezeshaji na upambanaji wa biashara haramu ya dawa za kulevya kwani biashara hii imekuwa ikifanywa na watu wenye fedha nyingi na mtandao mkubwa duniani ambao wana mbinu za kisasa za kukabiliana na juhudi za Serikali za kupambana na dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua na kupongeza jitihada za Serikali katika kuwashughulikia na kuwapatia matibabu waathirika wa dawa za kulevya kwa kuwapatia tiba ya dawa ya *methadone*. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupanua wigo wa matibabu ya *methadone* ili iweze kutolewa kwenye Miji yote Mikuu na Majiji ambako kuna ongezeko kubwa la vijana wanaotumia dawa za kulevya. Kwa sasa tiba hiyo hutolewa katika Mkoa wa Dar es Salaam pekee.

Mheshimiwa Spika, vilevile kumekuwepo na ongezeko la vijana wanaotumia dawa za kulevya, bangi na mirungi. Ili kukabiliana na ongezeko hilo, Kamati inaishauri Serikali ishirikiane na vyombo vya habari vya umma na vya binafsi ili kuweka utaratibu wa kutangaza athari za UKIMWI na dawa za kulevya kwa mwaka mzima na siyo kama ilivyo sasa ambapo matangazo hayo yanasubiria Siku ya UKIMWI Duniani na Siku ya Dawa za Kulevya Duniani.

Hatua hii itasaidia kuwakumbusha vijana athari za UKIMWI na dawa za kulevya na hivyo kuwaepusha na tabia hatarishi.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2014/2015, Tume ya kudhibiti UKIMWI inakadiria kutumia kiasi cha Sh. 5,341,286/= fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Ili kuweza kupunguza utegemezi wa wadau wa maendeleo katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kuharakisha uanzishwaji wa mfuko wa UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Kamati inataka kupata uhakika ni lini Serikali italeta Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya UKIMWI ya mwaka 2008 ili Mfuko wa UKIMWI uweze kuanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wataalam wa afya wamethibitisha uhusiano mkubwa ulipo kati ya UKIMWI na utumiaji wa dawa za kulevya, na kwa kuwa masuala haya ni mtambuka, Kamati inashauri Kamati za Kudhibiti UKIMWI ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata, Vijiji na Vitongoji ambazo zimeundwa kwa muundo uliotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, ziongezewe jukumu na kuhusisha masuala ya dawa za kulevya katika utendaji wake wa kazi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa, fedha za matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2014/2015 zilizotengwa kwa Tume ya Kudhibiti UKIMWI zitumike vizuri na kwa uaminifu ili ziweze kuwafikia walengwa na hasa katika

masuala ambayo yanaleta tija na siyo kama ilivyozoeleka kwamba fedha za UKIMWI zimekuwa zikitumika kulipana posho za vikao, Semina na Makongamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati, namshukuru Mheshimiwa Vangimembe Lukuvi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Dkt. Florence Turuka na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Wazairi Mkuu Ndugu Regina Kikuli. Mwenyekiti Mtendaji Tume ya kudhibiti UKIMWI Dkt. Fatuma Mrisho, Kaimu Kamishna Tume ya kuratibu udhibiti wa dawa za kulevya pamoja na watendaji wa Tume hizo kwa jinsi walivyoshirikiana na Kamati katika kutoa majibu na hoja za Waheshimiwa Wabunge kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Tume hizo kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na mapitio ya bajeti ya mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo (Mb) Makamu Mwenyekiti, kwa msaada anaonipa kuiongoza Kamati wakati ninapokuwa natekeleza majukumu mengine ya kiTaifa.

Aidha, kwa umuhimu mkubwa nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa maoni, busara, utayari wao wa kufanya kazi bila kuchoka na ushauri uliosaidia kuwasilishwa kwa taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimwa Spika, kwa heshima na taadhima na kwa kutambua mchango wao katika kuipitia na kuijadili Bajeti ya Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya na Tume ya Kudhibiti UKIMWI, naomba *Hansard* iwaorodheshe Wajumbe wote wa Kamati hii kama sehemu ya taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Ofisi ya Bunge hasa Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah na Makatibu wa Kamati Ndg. Rachel Nyega kwa uratibu shughuli za Kamati. Pia nawashukuru wafanyakazi wote wa shughuli za Bunge kwa kuihudumia Kamati mpaka kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 91 – Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya na Fungu 92 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015, Jumla ya Sh.18, 498, 706,000/=.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha, na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kama ilivyowasilishwa Mezani**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASWALA YA UKIMWI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI YA TUME YA KURATIBU UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA FUNGU 91 NA TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA FUNGU 92 KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/15 KWA TUME HIZO**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kanuni ya ....... () ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Maswala ya UKIMWI, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu na bajeti ya Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya Fungu 91 na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania Fungu 92 kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/15

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa majukumu ya Bunge kwa mujibu wa ibara ya 63 (2) na 63 (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na majukumu mengine, Bunge lina jukumu la kuidhinisha mapato na makadirio ya fedha za Serikali na kufuatilia utekelezaji na usimamizi wa shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la April, 2013,inaelekeza kwamba Kamati za Bunge za kisekta zinatakiwa kufanya ukaguzi wa miradi iliyoombewa fedha za maendeleo na kuidhinishiwa kwa mwaka wa fedha unaomalizika .

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza majukumu hayo ya kikatiba na kikanuni, Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI ilifanya ziara ya ukaguzi wa miradi kuanzia tarehe 28 Januari hadi tarehe 06 Februari, 2014 kwenye mikoa ya Iringa na Pwani. Aidha, Tarehe 01 Mei hadi tarehe 02 Mei, 2014, Kamati ilifanya Kazi ya kupitia taarifa ya Utekelezaji wa bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 pamoja na kuchambua makadirio ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2014/2015 kwa Tume hizo mbili.

**Mheshhimiwa Spika,** kwa mukutadha huo, Taarifa ya Kamati ninayoiwailisha mbele ya Bunge lako, imegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya

kwanza itahusu taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania na Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, taarifa ya pili itahusu ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 kwa tume hizo na sehemu ya tatu itahusu maombi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 kwa Tume hizo mbili.

## 2.0 TAARIFA YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

**Mheshimiwa Spika,** uamuzi wa kutembelea miradi hii, ulilenga kupata picha halisi ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 pamoja na kujiridhisha na hali halisi ya matumizi ya fedha za umma na hatimaye kuweza kujenga hoja na kuishauri Serikali katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2014/2015 hususan katika miradi ya maendeleo.

1. **TUME YA KURATIBU UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA**

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2013/2014 Tume ya Kuratibu udhibiti wa Dawa za Kulevya iliomba na kuidhinishiwa fedha za miradi ya maendeleo jumla ya shilingi 2, 651,738,800.00. Fedha hizi zilijumuisha pesa za ndani shilingi 350,000,000.00 kwa ajili ya Mradi wa Ujenzi wa Ghala la Kuhifadhia Vielelezo vya Kesi za Dawa za Kulevya na shilingi 2,798,000,000.00 fedha za nje kwa ajili ya Mradi wa Kudhibiti Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI miongoni mwa watumiaji wa Dawa za kulevya kwa kujidunga sindano.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa fedha zote za miradi ya maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge ilitolewa kwa wakati na Kamati ilitembelea Mradi wa Ujenzi wa Ghala la Kuhifadhia Vielelezo vya Kesi za Dawa za Kulevya ilikuta ujenzi wa ghala unaendelea na kuridhishwa na kazi inayofanyika.

**Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kutenga fedha zake za ndani kwa ajili ya kujenga Ghala la Kuhifadhia Vielelezo vya Kesi za Dawa za Kulevya. Kamati inaamini hatua hii ni muhimu na itasaidia kuharakisha hukumu za kesi na maamuzi sahihi ya kesi yatapatikana.

## 2. TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2013/2014 Tume ya Kudhibiti UKIMWI iliomba na kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 15,334,335,000.00** kwa ajili ya kutekeleza afua za UKIMWI na mwitikio wa kitaifa kupitia miradi mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi, 2014 kiasi cha **shilingi 9,939,107,213.40** sawa na asilimia 71 zilikuwa zimeshatolewa. Kamati inaamini mpaka kufikia June 30 kiasi cha fedha ambazo hazijatolewa sawa na asilimia 29 kitatolewa.

**Mheshimiwa Spika,** katika kufuatilia utekelezaji wa fedha hizo Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa matumizi ya fedha hizo kwa mikoa ya Pwani na Iringa kwa muda wa siku saba kuanzia 28 Januari hadi 06 Februari, 2014.

**Mheshimiwa Spika ,** uamuzi wa kufanya ziara mikoa hiyo ulifikiwa kufuatia Ripoti ya Utafiti wa Viashiria vya VVU/ UKIMWI kwa Mwaka 2011/2012 ambao unaonyesha mkoa wa Iringa ni wa pili kitaifa kwa kuwa na maambukizi ya juu (asilimia 9.1) na mkoa wa Pwani ulitembelewa kwa kuwa umeweza kushusha maambukizi kutoka asilimia ........ hadi asilimia 5.9. Aidha, Mkoa wa Njombe unaoongoza kwa kuwa na maambukizi makubwa ya Virusi vya UKIMWI kwa asilimia 14.8 ulishatembelewa na Kamati na taarifa yake ilitolewa na kusomwa kwenye Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa shughuli za Kamati iliyowasilishwa Bungeni Desemba 2013.

**Mheshimiwa Spika,** katika ziara hizo, Kamati iliweza kubaini mambo mbalimbali yafuatayo:-

### MAMBO MUHIMU YALIYOJITOKEZA KATIKA ZIARA YA MKOA WA PWANI

### MAFANIKO

1. Kamati inapongeza Mkoa wa Pwani kwa kufanya janga la UKIMWI na tatizo la Dawa za kulevya kuwa ajenda ya kudumu katika mipango ya mkoa.

2. Kamati inaupongeza uongozi wa mkoa na hususan halmashauri ya Kibaha kwa kutenga mapato ya ndani kwa ajili ya afua za UKIMWI na dawa za kulevya.

3. Mkoa umeweza kuwasaidia vijana walioacha kutumia dawa za kulevya kwa kuwapatia mtaji na kuanzisha mradi wa kuosha magari. Hii ni kutokana na halimashauri ya Wilaya ya Pwani kununua mashine mbili za kuosha magari kwa ajili ya vijana hao.

4. Watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI wameweza kwa kusaidiwa na halmashauri ya wilaya ya Kibaha kuanzisha umoja wa watu wanaoishi na UKIMWI ambapo wilaya imeweza kuwapatia mtaji wa kuendesha biashara ndogondogo.

5. Kamati inaipongeza TASAF kwa kuanzisha mpango wa kunusuru kaya maskini ambapo, mpango huu umesaidia kuboresha maisha ya watu maskini, aidha Kamati inapongeza pia vigezo vilivyoyumika kufanya utambuzi kwa kaya maskini.

**CHANGAMOTO**

1. Kutokuwepo kwa mkakati wa kupambana na UKIMWI na dawa za kulevya katika ngazi ya Mkoa na Halmashauri.

2. Kamati imebaini kuwepo na tatizo kubwa la ucheleweshaji wa fedha kutoka Wizara ya Fedha (HAZINA) na Tume ya kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) hali inayochangia miradi mingi na mipango ya mapambano ya UKIMWI kushindwa kutekelezeka na kukamilika kwa wakati.

3. Mipango mingi ya mapambano ya UKIMWI inategemea fedha za wadau wa maendeleo.

4. Vijana walio acha kutumia dawa za kulevya kukosa fedha za kutosha na maeneo ya kufanyia shughuli mbalimbali za kuwaingizia kipato.

5. Miadi ya ufugaji kuku na bata inayoendeshwa na mpango wa kunusuru kaya maskini (TASAF) inaendeshwa bila utaalam na hivyo manufaa yake kwa walengwa ni kidogo.

**MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI KWA MKOA WA PWANI NA WILAYA ZAKE**

1. Tume ya kudhibiti UKIMWI Tanzania bara (TACAIDS) ishirikiane na sekretariet za mikoa na wilaya na kuandaa Mpango kazi wa kupambana na UKIMWI katika ngazi zote.

2. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inatoa fedha zilizoizinishwa na Bunge kwa wakati.

3. Kamati inazishauri sekretarieti na mikoa kutenga fedha za kuwahudumia WAVIU na waathirika wa dawa za kulevya kutoka mapato yake ya ndani.

4. Kamati imeagiza uongozi wa mkoa wa Pwani kuwasaidia vijana walioacha kutumia dawa za kulevya na umoja wa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI mkoani Pwani kwa maana ya kuwapatia mitaji na maeneo kwa ajili ya kuendeshea biashara zao.

5. Kuhusu mpango wa kunusuru kaya maskini na hususan miradi ya kuku na bata, Kamati ina shauri sekretariet ya mkoa kupitia maafisa ugani kuwajengea uwezo kwa kuwafundisha wananchi njia bora za ufugaji wa kisasa. Aidha, ili miradi hii iwe endelevu ni vyema kaya hizi maskini zisaidiwe kuanzisha vikundi vya saccos.

**MKOA WA IRINGA**

Kamati ilifanya ziara mkoa wa Iringa na hususani Halmashauri ya Wilaya ya Iringa Vijijini, Wilaya ya Mufindi na Halimashauri ya Wilaya ya Kilolo Pamoja na shughuli ya ukaguzi wa miradi, Kamati pia ilipokea taarifa ya mkoa na wilaya zake kuhusu mapambano dhidi ya UKIMWI na dawa za kulevya.

**MAMBO MUHIMU YALIYOJITOKEZA KATIKA ZIARA YA MKOA WA IRINGA**

**MAFANIKIO**

1. Kamati imeridhishwa na jinsi mkoa ulivyojipanga kupambana na tatizo la **UKIMWI. Mkoa wa Iringa** ndio mkoa unaongoza kwa maambukizi ya UKIMWI kitaifa kwa mujibu wa taarifa za TMHS 2012/2013.

2. Mkoa una mkakati wa mkoa wa kupambana na UKIMWI, na mkakati huu ulitokana na azimio lililopitishwa kwenye RCC.

3. Vijiji 67 vya halmashauri ya Wilaya ya Iringa vijijini vimeweza kuanzisha mifuko ya kusaidia kupambana na UKIMWI na madhara yatokanayo na UKIMWI.

4. Mkoa unafanya kazi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Aidha, mkoa unao utaratibu wa kuainisha kila mdau na shughuli zake pamoja na fedha anzochangia katika shughuli anazozifanya. Utaratibu huu ni wa kupongezwa na kuigwa kwa kuwa unaisaidia Serikali kuweza kuratibu vizuri shughuli za mapambano dhidi ya UKIMWI na unapunguza mwingiliano wa kazi na unaokoa muda na fedha.

**CHANGAMOTO**

1. Mkoa wa Iringa ndio mkoa unaongoza kitaifa kwa maambukizi ya UKIMWI. Maambukizi hayo yanachangiwa kwa kiasi kikubwa na mwingiliano wa watu kutoka ndani na nje ya nchi hususan wafanyabiashara wanaofanya shughuli za biashara katika halmashauri ya wilaya ya Mufindi.

2. Kamati za kudhibiti UKIMWI za wilaya zinakutana na zinafanyakazi kama muongozo unavyoelekeza kwa kuwa Kamati hizi zinajumuisha mabaraza ya madiwani na hivyo zinatengewa fedha, tatizo kubwa liko kwenye Kamati za kudhibiti UKIMWI katika ngazi ya kata/ vijiji ambazo hazikutani kwa kuwa hakuna pesa inayotengwa. Aidha, Kamati imebaini Wajumbe wa Kamati hizi hawajui wajibu wao na hakuna vigezo sahihi vinavyotumika kupata Wajumbe wa Kamati za kudhibiti UKIMWI katika ngazi ya kata/ vijiji.

3. Kutopatikana kwa wakati fedha za ruzuku zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza afua za UKIMWI na uhaba wa rasilimali fedha katika kutekeleza mipango ya UKIMWI.

4. Upungufu wa vitendanishi vya kupimia VVU (DBS, *DETRTAMINE*, na *UNIGOLD* katika bohari ya madawa. Aidha, hospitali ya halmashauri ya wilaya ya Mufindi inakabiliwa na tatizo la CD4 machine, CD4 machine iliyopo ni ndogo na hivyo kuzidiwa uwezo wa kupima sampuli kutokana wingi wa wateja wanao hitaji huduma hiyo.

**MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI KWA MKOA WA IRINGA NA WILAYA ZAKE**

1. Kwa kuwa mkoa wa Iringa ndio mkoa unaongoza kwa maambukizi ya UKIMWI kitaifa na kwa kuwa ukishusha maambukizi kwenye mkoa huu maana yake ni kwamba maambukizi kitaifa yatashuka pia,Kamati inashauri kuwa utaratibu unaotumika sasa

wa ugawaji fedha kulingana na wingi wa idadi ya watu upitiwe upya na kuboreshwa ambapo kipaumbele kiwe kwenye mikoa/ maeneo yenye maambukizi makubwa.

2. Ili kushusha maambukizi ya UKIMWI kitaifa, ni lazima kushusha maambukizi ya UKIMWI katika mikoa kumi (10) yenye maambukizi makubwa Mkoa wa Iringa ukiwa unaongoza, Kamati inaishauri Tume ya kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) kuanzishwa kwa Mkakati maalum wa kupambana na UKIMWI kwenye mikoa hiyo.

3. Mfumo wa uendeshaji wa Kamati za kudhibiti UKIMWI ngazi ya kata, vijiji na vitongoji uangaliwe upya. Mfumo ulioko sasa hauendani na hali halisi ya tatizo, kwa mfano kuna baadhi ya Wajumbe wa Kamati hizo wamechaguliwa bila ya kuwa na dhamira ya dhati ya kupambana na UKIMWI.

4. Waratibu wa UKIMWI ngazi ya mikoa wasaidie kuzijengea uwezo Kamati za UKIMWI katika ngazi za Kata/ vijiji na vitongoji.

5. Kwa kuwa maambukizi makubwa ya UKIMWI mkoani Iringa yanachangiwa na mwingiliano wa wafanyabiashara hususan katika halmashauri ya wilaya ya Mufindi, Kamati inashauri Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na mkoa wa Iringa kupitia halmashauri ya wilaya ya Mufindi kuandaa mkakati wa kupambana na UKIMWI wa Mkoa utakaoshirikisha wadau na wafanyabiashara wa halmashauri ya wilaya ya Mufindi.

6. Tatizo la Ukatili wa kijinsia ni moja ya kichocheo kikubwa cha maambukizi ya UKIMWI katika Mkoa wa Iringa, Kamati inaishauri Serikali kuanzisha program maalum zitakazo saidia kupunguza tatizo la ukatili wa kijinsia. Program hizi zihusishe dawati la ukatili wa kijinsia katika vituo vya polisi, kuanzisha vituo/ sehemu za kuwahifadhi waathirika wa ukatili wa kijinsia na kushirikisha mashirika yasiyo ya kiselikali (*NGO'S*).

7. Unywaji pombe wa kupindukia ni chanzo kingine cha maambukizi ya UKIMWI mkoani Iringa ambapo mlevi wa pombe hupungukiwa uwezo wa kufanya maamuzi ya busara ikiwa ni pamoja na kushindwa kutumia mipira ya kujikinga na UKIMWI (*condoms*) wakati wa kujamiana. Kamati inashauri ili kuweza kukabiliana na tatizo la unywaji pombe uliokithiri,

Halmashauri za miji na Wilaya zisaidie uongozi wa Kata na Vijiji kutunga sheria ndogo ndogo za kupambana na ulevi kwenye maeneo yao.

## 3.0 MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU/BAJETI YA TUME YA KURATIBU UDHIBITI DAWA ZA KULEVYA NA TUME YA KUDHIBITI UKIMWI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza juhudi za Serikali katika kushughulikia tatizo la biashara ya Dawa za kulevya, hata hivyo Kamati imebaini kuwa, kuendelea kucheleweshwa kwa uaandaaji na ukamilishwaji wa Sheria Mpya ya Kudhibiti Dawa za Kulevya kunakofanywa na Serikali kunapelekea kuendelea kushamiri kwa biashara haramu ya dawa za kulevya. Kamati inaamini ikiwa Sheria Mpya itakamilika mapema iwezekanavyo juhudi za kupambana na biashara ya dawa za kulevya zitafanikiwa kwa kiasi kikubwa na kurudisha taswaira na heshima ya Tanzania kwa nchi za nja. Aidha, Kamati inatambua uwezo wa Serikali ikiwa itadhamiria kwa dhati kupambana na tatizo la dawa za kulevya.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muda mrefu sasa nafasi ya Kamishina wa Tume ya kuratibu Udhibiti wa Dawa za kulevya imekuwa ikikaimiwa na watendaji mbalimbali. Kukosekana kwa Kamishina wa Tume kumepelekea hukumu za kesi za dawa za kulevya kusimama nah ii inatokana na matakwa ya kisheria kwamba kamishina wa Tume pekee ndiye anaehitajika kisheria kusaini kesi zote zinazohusu dawa za kulevya. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha uteuzi wa Kamishina wa Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya mapema iwezekanavyo.

**Mheshimiwa Spika,** Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kikao cha Baraza la Mawaziri kimeridhia kuanzishwa kwa Mfuko wa UKIMWI Tanzania, hatua ambayo itasaidia kupunguza utegemezi wa fedha za UKIMWI. Ili Mfuko wa UKIMWI uweze kuanza inahiti Bunge lifanye marekebisho ya Sheria ya UKIMWI ya Mwaka 2008, Kamati imebaini wingi wa shughuli za Bunge unakwamisha Sheria hii kuwasilishwa Bungeni ili iweze kujadiliwa. Kamati inaitaka Serikali kuwasilisha marekebisho ya Sheria hii kwenye kikao kijacho cha Bunge ili Mfuko huu uanze kufanya kazi na kuzisaidia katika mapambano dhidi ya UKIMWI.

## 4.0 MAOMBI YA FEDHA KWA AJILI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TUME YA KURATIBU UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA NA TUME YA KUDHIBITI UKIMWI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015, Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya inaombakuidhinishiwa Jumla ya Shilingi Bilioni 9,999,577,000/= kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida, na Mishahara ni Shilingi Bilioni 4,658,291,000/= zinaombwa kwa ajili na Shilingi Bilioni 5,341,268,000/= zinaombwa kwa ajili ya ya utekelezaji wa Miradi ya Mandeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kwamba, katika Mwaka wa Fedha 2014/2015, fedha inayoombwa imepangiwa kutekeleza kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Kuimarisha mazungumzo na majadiliano na wadau wa VVU na UKIMWI kupitia utaratibu na muundo wa majadiliano wa MKUKUTA, Kuimarisha upatikanaji wa huduma bora na za kutosha za UKIMWI, Kuimarisha utetezi na uratibu wa programu za mawasiliano ya mabadiliko ya tabia na kusaidia kuingizwa maswala ya jinsia kwenye mikakati na mipango mbalimbali ya taasisi.

## 5.0 MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA TUME YA KURATIBU UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA NA TUME YA KUDHIBITI UKIMWI TANZANIA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kuwa, fedha za Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, zitumike vizuri na kwa uaminifu ili ziweze kuwafikia walengwa na hasa katika masuala ambayo yanaleta tija na siyo kama ilivyozoeleka kwamba fedha za UKIMWI zimekuwa zikitumika kulipana posho za vikao, semina na makongamano yasiyo kwisha;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kuwa Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, iongeze fedha kwa ajili ya uendeshaji na upambanaji wa biashara haramu ya Dawa za kulevya kwani biashara hii imekuwa ikifanywa na matajiri tena wenye mtandao mkubwa duniani ambao wana pesa na mbinu za kisasa za kukabiliana na kikosi cha kupambana na dawa za kulevya;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua na kupongeza jitihada za Serikali katika kuwashughulikia na kuwapatia matibabu waathirika wa dawa za kulevya kwa kuwapatia tiba ya dawa ya methadone. Hata hivyo Kamati inaishauri Serikali kupanua wigo wa matibabu ya methadone ili iweze kutolewa kwenye miji yote mikuu na majii, kwa sasa tiba hiyo hutolewa katika Mkoa wa Dar es salaam na halmashauri na manispaa zake tu.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile kumekuwepo na ongezeko la vijana wanaotumia dawa za kulevya, bangi na mirungi, ili kukabiliana na ongezeko hilo, Kamati inaishauri Serikali ishirikiane na vyombo vya habari vya umma na vya binafsi ili kuweka utaratibu wa kutangaza athari za UKIMWI na dawa za kulevya kwa mwaka mzima na sio kama ilivyo sasa ambapo matangazo hayo yanasubiria siku ya UKIMWI duniani na siku ya dawa za kulevya duniani. Hatua hii itasaidia kuwakumbusha vijana athari za UKIMWI na dawa za kulevya na hivyo kuwaepusha na tabia hatarishi.

**Mheshimiwa Spika,** kuna uhusino mkubwa kati ya UKIMWI na utumiaji wa dawa za kulevya, na kwa kuwa maswala haya ni mtambuka, Kamati inashauri Kamati za Kudhibiti UKIMWI ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata, Vijiji na Vitongoji ambazo zimeundwa kwa muongozo uliotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI ziongezewe jukumu na kuhuisha maswala ya Dawa za Kulevya katika utendaji kazi zake

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati ninamshukuru Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. Mkurugenzi na Mwenyekiti Mtendaji Tume ya Kudhibiti UKIMWI, Kaimu Kamishina Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya pamoja na Watendaji wa Tume hizo wakiongozwa na Dkt. Florence Turuka Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu na Ndugu Regina Kikuli, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa jinsi walivyoshirikiana na Kamati katika kutoa majibu ya hoja za Waheshimiwa Wabunge kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Tume hizo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, na Mapitio ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**Mheshimiwa Spika,** namshukuru sana Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo (Mb) Makamu Mwenyekiti, kwa msaada anaonipa kuiongoza Kamati wakati ninapokuwa natekeleza majukumu

mengine ya kitaifa. Aidha, kwa umuhimu mkubwa nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa maoni, busara, utayari wao wa kufanya kazi bila kuchoka na ushauri uliosaidia kuwasilishwa kwa taarifa hii mbele ya Bunge lako.

**Mheshimwa Spika,** kwa heshima na taadhima, na kwa kutambua mchango wao katika kuipitia na kuijadili Bajeti ya Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya na Tume ya Kudhibiti UKIMWI, naomba niwatambue wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Ledian Mafuru Mng'ong'o , Mb. - Mwenyekiti
2. Mhe. Diana Mkumbo Chilolo, Mb.- Makamu Mwenyekiti
3. Mhe.Maida Hamad Abdallah, Mb.
4. Mhe.Said Suleman Said, Mb.
5. Mhe. Chiku Aflan Abwao, Mb.
6. Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb.
7. Mhe. Mbarouk Salim Ali, Mb.
8. Mhe. Anna MaryStella John Mallack, Mb.
9. Mhe. Maria Ibeshi Hewa, Mb.
10. Mhe. Rashid Ali Omar, Mb.
11. Mhe. Lameck Okambo Airo, Mb.
12. Mhe. Lucy Thomas Mayenga, Mb.
13. Mhe. Mch. Luckson Ndaga Mwanjale, Mb.
14. Mhe. Mwanamrisho Taratibu Abama, Mb.
15. Mhe. Dkt. Engelbert Faustine Ndungulile , Mb.
16. Mhe. Ignatus Aloyce Malocha, Mb.
17. Mhe. Selemani Saidi Bungara, Mb.
18. Mhe. Neema Mgaya Hamid, Mb.
19. Mhe. Sara Msafiri Ali, Mb.
20. Mhe. Maulida Anna Valerian Komu, Mb.
21. Mhe. Ahmed Ally Salim, Mb.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuishukuru Ofisi ya Bunge hasa Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah na Makatibu wa Kamati Ndg. Rachel Nyega na Ndg. Abdallah Hancha wakisaidiwa na Ndg. Halima Laizer, kwa uratibu wa shughuli zote za Kamati. Pia nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuihudumia Kamati mpaka kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 91 – Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya

na Fungu 92 Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania, kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015, Jumla ya Shilingi Bilioni 18, 498, 706,000/=.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha, na naunga mkono hoja.

Lediana Mafuru Mng'ong'o (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA MASWALA YA UKIMWI**
06 Mei, 2014

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kufuatana na makubaliano tuliyofanya, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani anapewa saa moja kusoma hotuba yake, na sijui kwa nini hazijapatikana lakini mimi nimeiona moja kwangu. Sasa nyingine kwa nini hazijapatikana mimi sijui.

Sasa nakuita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**Hoja ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kama ilivyosomwa Bungeni**

**MSEMAJI MKUU KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU – MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mawazo ya Kambi ya Upinzani katika bajeti ya mwaka huu kwa Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuzungumzia mchakato wa Katiba mpya na mustakabali wa Taifa.

Mheshimiwa Spika nchi yetu ipo katika kipindi tete cha kikatiba na kisiasa. Mchakato wa kutunga Katiba mpya kwa ajili ya nchi yetu ulioanza kufuatilia hotuba ya Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete mwaka mpya 2011 uko katika hatari kubwa ya kuanguka na kuparaganyika.

Sehemu muhimu ya Wabunge wa Bunge maalum, yaani baadhi yao wale wanaounda Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) wamesusia vikao vya Bunge Maalum kutokana na kile wanachoona kama njama za kulitumia Bunge Maalum kama chombo cho kupitishia matakwa ya kikatiba ya Chama cha Mapinduzi (CCM) na kutupa jalalani matakwa ya wananchi kama yalivyoainishwa na Rasimu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano iliyoandaliwa na kuwasilishwa Bungeni na Tume ya Mabadiliko ya Katiba. *(Makofi)*

Kwa sababu ya njama hizo, Bunge Maalum limegeuzwa kuwa uwanja wa matusi, vijembe, kejeli, kauli za kibaguzi na vitisho dhidi ya wananchi wanaotaka mabadiliko ya msingi ya kikatiba na ya kisiasa na ya muundo wa Muungano kati ya nchi mbili zinazounda Muungano huo, yaani Tanganyika na Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati akitangaza kuanza kwa mchakato wa Katiba mpya katika wa hotuba yake ya tarehe 31 Desembam 2010, Rais Kikwete alisema maneno yafuatayo ambayo kwa umuhimu wake, tunaomba kuyanukuu kwa kirefu.

*"Mwaka 2011 nchi yetu itatimiza miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara, miaka 47 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar na miaka 47 ya Muungano wa nchi zetu mbili. Kwa ajili hiyo, ni vyema kuwa na Katiba inayoendana na mabadiliko na matakwa ya hali halisi ya siasa; Katiba ambayo italipeleka Taifa letu miaka 50 ijayo kwa salama, amani, umoja na kuwepo maendeleo makubwa zaidi. Ndiyo maana tukaamua kuanzisha mchakato huu na kwa ajili hiyo nimeamua kuunda Tume maalum ya Katiba itakayoongozwa na mwanasheria aliyebobea. Itakuwa na Wajumbe watakaowakilisha makundi mbalimbali katika jamii yetu kutoka pande zetu mbili za Muungano.*

*Jukumu la msingi la Tume hiyo litakuwa ni kuongoza na kuratibu mchakato utakaowashirikisha wananchi wote bila kubagua vyama vya siasa, wanasiasa, wafanyabiashara, asasi za kiraia, mashirika ya dini, wanataaluma na makundi mbalimbali ya watu wa nchi yetu kote nchini katika kutoa maoni yao juu ya wayatakayo kuhusu Katiba ya nchi yao.*

*Baada ya kukamilisha kukusanya maoni, Tume itatoa mapendekezo yake yatakayofikishwa kwenye vyombo stahiki vya kikatiba kwa kufanyiwa maamuzi. Baada ya makubaliano kufikiwa, Taifa letu litapata Katiba Mpya kwa siku itakayoamuliwa ianze kutumika.*

*Ni matumaini yetu kuwa mchakato huo utaendeshwa vizuri, kwa amani na utulivu kama ilivyo sifa ya nchi yetu na mazoea yetu ya kujadiliana bila kugombana. Pasiwepo kutukanana, kudharauliana, kushutumiana, kubezana, kuzomeana wala kushinikizana. Naomba washiriki waongozwe kwa hoja badala ya jazba. Tukiwa na jazba, hasira na kushinikizana kamwe hatutaweza kutengeneza jambo jema; na inapohusu Katiba ya nchi itakuwa hasara tupu, haitakuwa endelevu na kulazimika kufanyiwa marekebisho mengine mwanzoni tu baada ya kutungwa." (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza ahadi hiyo, Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria ya Mabadiliko ya Katiba sura ya 83 ya Sheria za Tanzania mnamo Novemba, 2011. Baadaye sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho mara tatu

kati ya Februari, 2012 na Desemba, 2013. Aidha, Bunge lako Tukufu lilitunga Shera ya Kura ya Maoni mwaka 2013. Vile vile katika kipindi hicho hicho Rais Kikwete aliteua Tume ya mabadiliko ya Katiba. Kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais, Tume hiyo iliongozwa na Mwanasheria aliyebobea na ambaye aliwahi pia kuwa Mwanasheria Mkuu na Waziri wa Katiba na Sheria na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba.

Kama alivyoahidi Mheshimiwa Rais, Wajumbe wa Tume hiyo walitoka katika makundi mbalimbali ya jamii kutoka nchi zote mbili zilizounda Jamhuri ya Muungano. Wajumbe hao walijumuisha wanataaluma waliobobea, Wanasheria, Viongozi na Watumishi wa Umma waliotumikia Taifa katika nafasi za juu, Viongozi wa kidini na Wawakilishi wa Vyama vya Siasa na Asasi za Kiraia.

Mheshimiwa Spika, kati ya Mei Mosi, 2012 wakati Tume ya Mabadiliko ya Katiba ilipoanza kazi rasmi na tarehe 21 Machi, 2014 Tume hiyo ilipovunjwa rasmi, Bunge lako Tukufu liliidhinisha jumla ya Shilling bilioni 74.463 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Tume. Katika kipindi hicho, Tume ilitembelea nchi nzima kukusanya maoni ya Watanzania juu ya Katiba Mpya waitakayo. Tume pia ilifanya rejea ya nyaraka nyingi kama zilivyoorodheshwa katika kifungu cha 17 (4) cha Sheria; pamoja na kupitia taarifa mbalimbali zilizoandaliwa na wataalam walioteuliwa na Tume kwa ajili hiyo.

Baadaye kwa kuzingatia vyanzo hivyo vya taarifa, tarehe 3 Juni, 2013 Tume ilitoa rasimu ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Rasimu hiyo nayo ilipelekwa kwa wananchi kwa ajili ya kutolewa maoni na wananchi, Taasisi za Kiserikali, Asasi za Kiraia, Vyama vya Siasa na watu mashuhuri. Aidha, Tume iliunda Mabaraza ya Katiba ya Wilaya, na ya Kitaasisi ili kutoa fursa kwa wananchi katika umoja huo kutoa maoni yao juu ya rasimu ya kwanza. Matokeo yake, Tume iliandaa Rasimu ya Pili ya Katiba ambayo iliwasilishwa katika Bunge Maalum na Mwenyekiti wa Tume, Jaji Warioba.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vya habari mbalimbali hasa nchini vimemnukuu Waziri wa fedha Mheshimiwa Saada Salum Mkuya akisema kwamba, hadi kuahirishwa kwake Bunge Maalum limetumia zaidi ya Shilingi bilioni 27. Kama taarifa hizo ni za kweli, itakuwa na maana kwamba katika kipindi cha miaka miwili iliyopita mchakato wa Katiba umetumia zaidi ya Shilingi bilioni 102. Hiki ni kiasi kikubwa mno cha fedha katika nchi ambayo shughuli mbalimbali za maendeleo na huduma za jamii zenye umuhimu mkubwa kwa ustawi wa wananchi zimekwama kwa kukosa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, licha ya matumizi haya makubwa ya fedha za umma kwa ajili ya mchakato wa Katiba na licha ya maneno ya Rais kwamba Wajumbe wa Bunge Maalum wajadili Rasimu kwa hoja badala ya

jazba, Rais Kikwete mwenyewe ndiye aliyeongoza Mawaziri wake na Viongozi wengine waandamizi na Wajumbe wa CCM wa Bunge Maalum katika kujadili Rasimu kwa kutukanana, kudharauliana, kushutumiana, kubezana, kuzomeana na hata kushinikizana. Kauli na vitisho hivi vimetolewa hadharani siyo ndani ya ukumbi wa Bunge tu, bali pia hata katika nyumba za Ibada bila kujali athari zake kwa jamii yetu yenye imani tofauti tofauti za kidini. *(Makofi)*

Wajumbe wanaounda UKAWA wamekataa kuwa sehemu ya Bunge Maalum la aina hii na hawatarudi Bungeni hadi hapo dhima halisi ya Bunge hilo itakapopatiwa ufumbuzi. *(Makofi)*

**MJUMBE FULANI:** Sawa, tokeni!

**MSEMAJI MKUU KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU – MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, kama dhima hiyo itakuwa ni kutumia mwavuli wa Bunge Maalum ili kuendeleza mfumo wa kikatiba na muundo wa Muungano uliopo kwa sasa, basi Wajumbe wa UKAWA hawatakuwa sehemu ya usaliti huo wa Watanzania. Hata hivyo, kama dhima ya Bunge Maalum itakuwa ni kujadili na kuboresha matakwa ya wananchi kama yalivyodhihirishwa na Rasimu ya Katiba na Taarifa ya Tume, basi wanachama wa UKAWA watakuwa tayari kurudi kwenye Bunge Maalum ili kuendelea na mjadala wa Rasimu hiyo.

Mheshimiwa Spika, madai ya Katiba mpya yana historia ndefu ikianzia miaka ya mwisho wa mwaka 1980. Mwaka 1990 Rais Ali Hassan Mwinyi aliunda Tume ya Rais ya mfumo wa Chama kimoja cha siasa au Vyama vingi iliyoongozwa na aliyekuwa Jaji Mkuu wa Tanzania, Marehemu Francis Nyalali. Pamoja na mapendekezo mengine, Tume ya Nyalali ilipendekeza kutungwa kwa Katiba mpya kwa ajili ya nchi yetu. Tume hiyo ilipendekeza pia muundo wa Muungano wa Serikali tatu.

Baada ya mfumo wa Siasa wa Vyama Vingi kurejeshwa mwaka 92 Vyama vya Upinzani na makundi mbalimbali ya kijamii yaliendelea kudai kutungwa kwa Katiba mpya. Hii ilitokana na kutoridhishwa na mfumo wa uchaguzi ambao haukuwa huru na wa haki, madaraka makubwa ya Rais. Mfumo mzima wa usimamizi wa rasilimali za Taifa pamoja na upungufu mwingi katika mifumo yetu ya utawala na uendeshaji wa Serikali.

Kwa kiasi kikubwa mapendekezo ya Rasimu ya Katiba iliyowasilishwa na Tume inakidhi mahitaji haya ya mabadiliko ya msingi katika mfumo wa utawala, usimamizi wa rasilimali za Taifa na uendeshaji wa Serikali. Ni wazi, Kwa hiyo, kwamba Rasimu hii inatoa fursa muhimu ya kutibu majeraha yetu kama Taifa.

Kwa Viongozi wa CCM, wakiongozwa na Rais Kikwete kupotosha, kubeza na kukejeli mapendekezo haya ni kuthibitisha yale ambayo yaliwahi kusemwa na aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Celina Kombani na baadaye kurudiwa na Mwanasheria Mkuu, Mheshimiwa Frederick Werema kwamba Serikali ya CCM haioni haja ya kuwa na Katiba Mpya kwani iliyopo inatosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu mchakato huu wa Katiba Mpya ulipoanza mwanzoni mwa 2011, CCM ilionyesha dalili zote za kutaka kuuteka na kuupotosha mchakato mzima. Suala la nafasi na ushiriki wa Zanzibar katika mchakato huu, na muundo wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba na utaratibu wa uteuzi wa Wajumbe wa Tume yalikuwa masuala yaliyoleta mvutano mkubwa. Baadaye suala la muundo, idadi na utaratibu wa kuwapata Wajumbe wa Bunge Maalum nayo yalileta mvutano mkubwa ndani na nje ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, hofu ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba CCM ingetumia mamlaka ya Rais ya uteuzi wa Wajumbe wa Bunge Maalum kujaza makada wengi wa CCM katika Bunge hilo, imethibitika kuwa ya kweli. Kwa utafiti wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kati ya Wajumbe 201 wa Bunge Maalum walioteuliwa na Rais Kikwete, zaidi ya Wajumbe 160 ni Wanachama na Viongozi waandamizi wa CCM waliochomekwa kwenye Bunge Maalum kwa kutumia kivuli cha Waganga wa Kienyeji, Taasisi za Kidini, Asasi za Kiraia, Taasisi za Kitaaluma, watu wenye malengo yanayofanana, na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri hatua hizi basi zimechangia kujenga mazingira ya kutokuaminiana na hivyo kuweka msingi mbaya kwa mchakato wenyewe.

Mheshimiwa Spika, hata baada ya Bunge Maalum kuitishwa na kuanza kazi, CCM iliendelea kufanya hila za kuchakachua Kanuni za Bunge Maalum ili kupitisha hoja zao kirahisi. Hila hizo ziliposhindwa, CCM ilitumia mabavu ya wazi kwa kulazimisha Mwenyekiti wake wa Taifa atumie kivuli cha Urais kusisitiza msimamo wa CCM na kutisha Wajumbe wa Bunge Maalumu kwamba wakipitisha muundo wa Serikali Tatu, kama ilivyopendekezwa na Tume aliyoiteua yeye mwenyewe, basi Jeshi la Wananchi wa Tanzania litapindua Serikali. *(Makofi)*

Hilo liliwezekana tu baada ya Mwenyekiti wa Bunge Maalum kuchakachua Kanuni za Bunge Maalum ili kumwezesha Rais kuhutubia Bunge hilo baada ya Mwenyekiti wa Tume, kama njia ya kumwezesha Rais kuijibu Tume na kupinga Rasimu yake hadharani na kulazimisha maoni na msimamo wa Chama chake cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kadri ya ufahamu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, haijawahi kutokea kwa Mkuu wa Nchi na Amiri Jeshi Mkuu kuchochea Jeshi lake kufanya mapinduzi ya kijeshi ili kuzuia matakwa ya wananchi juu ya Katiba Mpya kutekelezwa. Haijawahi kutokea kwa Rais na Mkuu wa Nchi kuwaasa Wajumbe wa Bunge la Katiba kujadili hoja badala ya jazba, halafu Rais na Mkuu wa Nchi huyo huyo kugeuka na kukejeli na kubeza Tume aliyoiteua yeye mwenyewe na hivyo kujenga mazingira ya Wajumbe wa Bunge hilo kutukanana, kudharauliana, kushutumiana, kubezana, kuzomeana na kushinikizana. Hapa ndipo CCM ilikoifikisha nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji, kama Rais Kikwete hakuwa tayari kukubali maoni ya wananchi katika mchakato wa mabadiliko ya Katiba, kwa nini yeye na Serikali yake wameliingizia Taifa hasara ya kutumia mabilioni ya fedha za walipa kodi wa Tanzania kugharamia mchakato wa Katiba Mpya ambao ni wazi yeye na Chama chake hawako tayari kukubali matokeo yake?

Mheshimiwa Spika, fedha zote zilizotumika kwa ajili ya gharama mbalimbali za Bunge Maalum hazikuidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Ukweli ni kwamba hadi sasa Bunge lako Tukufu halijui bajeti yote ya Bunge Maalum. Halijui fedha kiasi gani zimetumika kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya miundombinu ya Bunge hili, au kwa ajili ya posho, mishahara na stahili mbalimbali za Wajumbe na Watumishi wa Bunge Maalum hadi lilipoahirishwa tarehe 25 Aprili, 2014. Aidha, Bunge lako Tukufu halina ufahamu wowote juu ya gharama za Bunge Maalum pale litakaporudi tarehe 5 Agosti, 2014, kuendelea kujadili Rasimu ya Katiba Mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu halina ufahamu huu kwa sababu, licha ya madai ya Wabunge, Serikali hii ya CCM haijawahi kuleta makadirio ya matumizi kwa ajili ya shughuli mbalimbali za Bunge Maalum. Mwaka jana (2013) wakati Bunge lako Tukufu linajadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala iliagiza kwamba bajeti ya Bunge Maalum, nanukuu: *"iletwe Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa."* Mwisho wa kunukuu.

Agizo hilo la Kamati ya Bunge siyo tu lilipuuzwa mwaka 2013 na Serikali hii ya CCM kutokuleta bajeti hiyo, bali hata mwaka huu 2014 agizo hilo limepuuzwa kwani bajeti ya Bunge Maalum haipo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mabadiliko ya Katiba inatamka wazi kwamba fedha zote zitakazogharamia mchakato wa Katiba Mpya zitatoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali. Ibara ya 136(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatamka kwamba, nanukuu: *"Fedha hazitatolewa*

*kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa ajili ya matumizi, isipokuwa fedha hizo ziwe kwa ajili ya matumizi ambayo yameidhinishwa yatokane na fedha zilizomo katika Mfumo Mkuu wa Hazina ya Serikali na idhini hiyo iwe imetolewa na Katiba hii au Sheria nyingine yoyote; na fedha hizo ziwe kwa ajili ya matumizi ambayo yameidhinishwa ama na Sheria ya Matumizi ya Serikali iliyotungwa mahususi na Bunge au Sheria iliyotungwa kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 140 ya Katiba hii." (Makofi)*

Aidha, kwa mujibu wa Ibara ya 136(3) ya Katiba, nanukuu: *"fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali hazitatolewa kutoka Mfuko huo kwa ajili ya matumizi ila mpaka matumizi hayo yawe yameidhinishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na pia kwa sharti kwamba fedha hizo ziwe zimetolewa kwa kufuata utaratibu uliowekwa kwa ajili hiyo kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge."*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa vifungu tajwa vya Katiba, fedha kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya Bunge Maalum zilitakiwa kuidhinishwa na Katiba au Sheria nyingine yoyote. Masharti haya yalitekelezwa kwa Bunge lako Tukufu kutunga Sheria ya Mabadiliko ya Katiba iliyoidhinisha matumizi ya fedha zilizopo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

Pili, fedha kwa ajili ya matumizi ya Bunge Maalum zilitakiwa kuidhinishwa na ama Sheria ya Matumizi ya Serikali iliyotungwa mahususi na Bunge au Sheria iliyotungwa kwa mujibu wa Ibara ya 140 ya Katiba. Ibara ya 140 inahusu Mfuko wa Matumizi ya Dharura unaoanzishwa kwa ajili ya mambo ya haraka na dharura ambayo hayakutazamiwa kutokea na ambayo hayakupangiwa fedha zozote za matumizi. Sharti hili nalo halikutekelezwa.

Tatu, hata kama fedha za matumizi ya Bunge Maalum zingeidhinishwa kama inavyotakiwa na Katiba, bado matumizi hayo yalitakiwa kuidhinishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hili nalo halikutekelezwa. Ukweli ni kwamba ingekuwa ajabu sana kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kuidhinisha matumizi ya fedha za Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali wakati matumizi hayo hayakuidhinishwa kwa mujibu wa Katiba.

Kwa sababu zote hizi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kupata majibu ya maswali yafuatayo:-

(i) Je, bajeti ya matumizi ya Bunge Maalum ni kiasi gani na kwa ajili ya matumizi gani? *(Makofi)*

(ii) Je, ni kiasi gani cha fedha hizo kimeshatumika hadi sasa na kwa ajili ya matumizi gani? *(Makofi)*

(iii) Je, ni nani aliyejadili na kupitisha bajeti hiyo? *(Makofi)*

(iv) Je, ni Sheria gani iliyotungwa na Bunge lipi lilioidhinisha matumizi haya ya fedha za Umma? *(Makofi)*

(v) Je, ni lini na kwa waraka gani Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliidhinisha matumizi haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majibu ya maswali haya ni muhimu ili kuliepusha Taifa letu na balaa la ufisadi na wizi mkubwa wa fedha za Umma kama ilivyotokea mwaka 2005. Mwaka huo, kama inavyojulikana, mabilioni ya fedha za Umma yaliibiwa kutoka katika akaunti ya kulipa madeni ya nje *(EPA)* ya Benki Kuu ya Tanzania kwa ajili ya kugharamia Kampeni za Uchaguzi Mkuu za CCM na Mgombea wake wa Urais. Makada wa CCM na Viongozi waandamizi wa CCM na Serikali yake walishiriki katika ufisadi huo. *(Makofi)*

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM itoe kauli rasmi mbele ya Bunge lako rasmi kuhusu giza hili lililogubika fedha za matumizi ya Bunge Maalum. Hii ni muhimu, siyo tu kwa sababu ni muhimu kuwa na uwazi katika matumizi ya fedha za Umma, bali pia ili kuzuia wizi na ufisadi wa fedha za Umma kwa kutumia kivuli cha mchakato wa Katiba Mpya ambao tayari umevurugwa na CCM, Serikali yake na Viongozi wake Waandamizi.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira ambayo Bunge Maalum limegeuzwa na CCM kuwa uwanja wa kuwazomea, kuwatukana, kuwatisha, kuwadhalilisha na kuwabagua kidini na kiasili yao Wajumbe wa Bunge hilo wanaotetea maudhui ya Rasimu ya Katiba iliyowasilishwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba. Katika hali ambayo CCM imejaza makada wake ndani ya Bunge Maalum kwa kutumia kofia na vivuli mbalimbali vya kitaasisi ili kuhakikisha agenda yake ya kuendeleza mfumo wa kikatiba na muundo wa Muungano uliopo inatekelezwa. *(Makofi)*

Katika mazingira ambayo CCM inatumia wingi wake huo kupindua Rasimu ya Katiba iliyoandaliwa na Tume kufuatana na maoni ya wananchi, katika hali ambayo Wajumbe wa CCM katika Bunge Maalum wamebadilisha Kanuni za Bunge Maalum ili kuwawezesha kuchakachua maoni ya wananchi kama yalivyoakisiwa na Rasimu ya Tume, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuweka wazi msimamo wa Wajumbe wake na Wanachama wa UKAWA kwamba haitakuwa busara kwake kuendelea na mjadala wa Bunge Maalum wenye lengo la kupitisha mapendekezo ya kundi la Viongozi wa CCM.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na Wanachama wa UKAWA hawako tayari kuendelea kushiriki katika Bunge Maalum ambalo limejaa kauli za kibaguzi, kashfa, vijembe na matusi dhidi ya Wajumbe wa UKAWA na dhidi ya

Wajumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, hasa Mwenyekiti wake Jaji Joseph Sinde Warioba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mjadala wowote utakaoendelea kuanzia sasa katika Bunge Maalum hautakuwa na uhalali wowote mbele ya macho ya Watanzania. Ni mchakato wa CCM, unaoendeshwa kwa fedha za Umma na wana-CCM, kwa faida na matakwa ya CCM. Kinachoendelea sasa katika Bunge Maalum hakitajibu matatizo mbalimbali ya Muungano ambao umeigeuza Zanzibar kuwa koloni la Tanganyika na ambao umeivalisha Tanganyika joho la Jamhuri ya Muungano na ambao unatishia mahusiano kati ya wananchi wa nchi hizi mbili. *(Makofi)*

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kwa niaba ya Wanachama wa UKAWA, itaendeleza harakati za kudai Katiba Mpya yenye kujibu haja, matakwa na matumaini ya Watanzania walio wengi nje ya Bunge Maalum ambalo limetekwa nyara na CCM. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni itaendeleza harakati, nje ya Bunge Maalumu, zitakazowezesha kubadilishwa kwa muundo wa Muungano kwa kuivua Tanganyika koti la Muungano, kuipatia Zanzibar mamlaka kamili ndani ya Muungano na kujenga mahusiano ya hadhi na haki sawa baina ya Tanganyika na Zanzibar. *(Makofi)*

Kama ilivyoonekana wazi wakati wa mjadala katika Kamati mbalimbali za Bunge Maalum, licha ya kujaza makada na Washirika wake, CCM haiwezi kupitisha matakwa yake ndani ya Bunge hilo kwa vile haiwezi kupata theluthi mbili ya idadi ya Wajumbe wa kuiunga mkono kama inavyotakiwa na kifungu cha 26(1) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba na Ibara ya 98(1) ya Katiba. Hii ndiyo sababu pekee iliyosababisha kuahirishwa kwa Bunge Maalum hadi mwezi Agosti ijayo bila ya kupiga kura ya maamuzi juu ya Sura za Kwanza na Sita zinazohusu muundo wa Muungano. *(Makofi)*

Kama CCM haijaweza kupata idadi ya Wajumbe iliyotakiwa na Sheria na Katiba ndani ya Bunge Maalum inayolitawala, itakuwa ni ndoto kupata idadi inayotakiwa ya Sheria wakati wa kura ya maoni ya kuhalalisha Katiba Mpya isiyotokana na matakwa ya wananchi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawataka Watanzania wote wenye nia njema na nchi yetu, kujiandaa kwa ajili ya kura hiyo ili kuhakikisha kwamba ndoto na matumaini yao kuhusu Katiba Mpya hayapotezwi kutokana na hila za CCM na washirika wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kauli za Uchochezi na Ubaguzi Nje ya Bunge Maalum. Pamoja na kuhamisha mjadala wa Bunge Maalum la Katiba usijadili Rasimu ya Katiba iliyowasilishwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba na badala yake kujadili Rasimu ya Katiba ya Chama kimoja, yaani Chama cha Mapinduzi nje ya Bunge Maalum, imeendeleza kauli za kichochezi na kibaguzi zinazoweza kuvunja amani.

Katika Mkutano wa Katibu Mkuu wa CCM Abdrahamani Kinana Unguja wa tarehe 4 Mei, 2014, naomba kunukuu: *"Mnadhimu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar (BLW), Salmin Awadh Salmin ambaye ni Mjumbe wa Bunge maalum la Katiba, amesema Wawakilishi wa CCM wanajiandaa kuwasilisha hoja binafsi kwenye Baraza hilo ili kuwapa nafasi wananchi waulizwe iwapo wanataka kuendelea na Serikali ya Umoja wa KiTaifa."*

Madhumuni ya mchakato huo ni kuvunja Serikali ya Umoja wa KiTaifa ambayo iliamuriwa iwepo na kura ya maoni ya Wazanzibari wote na imesaidia kuleta amani na utulivu nchini Zanzibar.

Aidha, kauli ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Idd katika Mkutano huo wa CCM kuwa Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu, Mwakilishi wa Mji Mkongwe kuwa siyo raia wa Zanzibar ni ya kibaguzi, kichochezi na yenye kupandikiza chuki dhidi ya jamii watu wenye asili ya Kihindi. Ni kauli inayopaswa kulaaniwa na kila mpenda amani popote alipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama hii sasa ndiyo Sera Mpya ya CCM na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuivunja Serikali ya Umoja wa KiTaifa Zanzibar na kuibua hisia za ubaguzi? *(Makofi)*

Jeshi la Polisi lilishiriki katika mauaji yaliyotokea Zanzibar Januari, 2001 na kwa mara ya kwanza kusababisha wakimbizi zaidi ya 2000 kutoka Zanzibar kwenda Kenya. Kauli za kuchochea kuivunja Serikali ya Umoja wa KiTaifa Zanzibar zitatonesha vidonda na zinapandikiza mbegu ya chuki na vurugu inayoweza kusababisha maafa makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe Baraza la Wawakilishi kwa pamoja lilipeleka waraka kwenye Tume ya Mabadiliko ya Katiba na kupendekeza kuwepo kwa mamlaka huru ya Zanzibar, mamlaka huru ya Tanganyika na mamlaka ya Muungano na iwekwe wazi maeneo, uwezo, nguvu, utendaji na mipaka ya kila mamlaka."

Kwa Kiswahili rahisi, mamlaka huru ya Zanzibar, mamlaka huru ya Tanganyika na mamlaka ya Muungano maana yake Serikali ya Zanzibar, Serikali ya Tanganyika na Serikali ya Muungano.

Kwa CCM na Serikali ya Muungano kuwabana Wawakilishi wa Zanzibar kubadilisha msimamo wao wakati wa Bunge Maalum la Katiba ni kuendeleza taswira kuwa mambo ya Zanzibar yanaamuliwa Dodoma na kwa hiyo, kuendelea kuudhoofisha Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mizunguko ya Mikutano ya CCM na maandamano ya pikipiki kuhusiana na mchakato wa Katiba ndani ya Tanganyika na Zanzibar, kumeendelea kutolewa kauli za kutukana, kudhalilisha na hata kubeza Viongozi mbalimbali wa Vyama vingine na hata wasio na Vyama wanaotofautiana kimsimamo au kimtazano na Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, Viongozi wa juu wa CCM na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanawajibika kukemea kauli hizi, lakini hawafanyi hivyo na badala yake kuonekana ama kuzitoa wenyewe, kuzikoleza au kuzishabikia bila kutathmini nafasi na wajibu wao wa kuliunganisha Taifa. Kitendo hiki siyo tu ni fedheha kwa Chama Tawala, bali ni ushuhuda wa aina gani ya Viongozi tulio nao. Vikiruhusiwa kuendelea vitendo vya CCM vitaliingiza Taifa letu katika mgogoro mkubwa wa kisiasa na hata maafa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nielezee kuhusu mchakao wa Katiba Mpya na Chaguzi za Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu wa 2015.

Mheshimiwa Spika, iliyoonekana awali dhamira njema ya kupata Katiba aliyokuwanayo Rais Jakaya Kikwete ilikuwa itupatie Katiba Mpya kwa Watanzania katika mwaka 2014. Sheria ya Mabadiliko ya Katiba inalitaka Bunge Maalumu kujadili Rasimu ya Katiba Mpya na Maudhui yake kama ilivyowasilishwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba na si vinginevyo.

Ni bahati mbaya kwamba, Rasimu ya Katiba Mpya imewekwa kando na mjadala katika Bunge Maalumu umejikita katika Mapendekezo ambayo hayamo katika Rasimu. Hali hii inapoteza uhalali wa Bunge Maalumu la Katiba, siyo tu kwa kuwa linakwenda kinyume na Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kifungu cha 25, lakini kwa sababu linakwenda kinyume na matakwa ya wananchi ambayo kwa ujumla wao yako katika Rasimu ya Katiba Mpya iliyowasilishwa na Tume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni bahati mbaya zaidi kwamba baadhi ya Wajumbe wa Bunge Maalumu la Katiba hasa kutoka kundi la walio wengi wamejivika jukumu lililokuwa la Tume ya Mabadiliko ya Katiba wakidai kupokea maoni mbadala ya wananchi, kitendo hiki ni kinyume na Sheria na ukiukwaji wa kiasi kikubwa wa haki ya wananchi ambao kwa ujumla wao walitoa maoni yao kwa Tume ya Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inapaswa kuingia katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani Mwaka 2015. Ndoto ya Watanzania ilikuwa kutumia Katiba Mpya katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Kama tutakwenda katika uchaguzi Mkuu wa Mwakani bila Katiba Mpya tutaliingiza Taifa katika mgogoro mkubwa wa kikatiba yaani "*Constitutional crisis*" ambao utakuwa rahisi kuzaa machafuko hasa katika kipindi cha uchaguzi.

Katiba inayotumika sasa, ya Mwaka 1977, ina upungufu mwingi na haiwezi kutupatia uchaguzi ulio huru na haki katika mazingira ya sasa yanayojengwa na uzoefu wa chaguzi nne zilizopita chini ya mfumo wa Vyama vingi.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri vilevile kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kufikia chaguzi zilizo mbele yetu bila kukamilisha upatikanaji wa Katiba Mpya yenye maridhiano. Kwa vyovyote vile, uhalali wa Katiba itakayokuwepo wakati huo wa uchaguzi, ndiyo njia pekee ya kutokugeuza chaguzi za mbele kuwa kichocheo cha mpasuko mkubwa wa KiTaifa.

Tukienda katika Uchaguzi Mkuu mwakani tukiwa katika mazingira tuliyonayo leo, tutakwenda tukiwa tumegawika kama Taifa pengine kuliko wakati mwingine wowote katika historia ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuna uwezekano mkubwa wa Uchaguzi Mkuu ujao wa 2015 kuwa chanzo cha machafuko makubwa ya kisiasa hapa nchini ikiwa Serikali itaendelea kupuuza mapendekezo ya marekebisho ya Sheria na Kanuni mbalimbali za Uchaguzi zilizolalamikiwa kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Miongoni mwa mambo yaliyolalamikiwa na Vyama vya Siasa ni pamoja na Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 1985 ambayo imepitwa na wakati na hivyo kutokidhi mahitaji ya kisiasa ya sasa, na kuundwa kwa Tume Huru ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na kutofanyika kwa marekebisho hayo, chaguzi zimekuwa zikifanywa kiholela bila utaratibu unaoeleweka kwa kutumia mwanya wa udhaifu au upungufu uliopo katika sheria na kanuni mbalimbali za uchaguzi ili mradi udhaifu au upungufu huo unakipa Chama cha Mapinduzi ushindi.

Mheshimiwa Spika, mara kadhaa Serikali ilipoulizwa kuhusu marekebisho ya Sheria na Kanuni mbalimbali za Uchaguzi imekuwa ikijibu kwamba tusubiri Katiba Mpya ambayo itatatua kero hizo.

Ni kweli kwamba mchakato wa Katiba Mpya unaendelea, lakini umegubikwa na wingu zito la mivutano jambo ambalo ni kiashiria kimojawapo kwamba tunaweza tusipate Katiba Mpya kwa muda uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna dalili na viashiria vya kutopata Katiba Mpya kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, na kwa kuwa hatutakuwa tayari kuingia katika Uchaguzi Mkuu kwa kutumia Katiba ya sasa ambayo ndiyo chimbuko la matatizo ya kiuchaguzi tuliyonayo sasa, hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza mbele ya Bunge hili, ina mpango gani wa kuweka utaratibu wa mpito *(transitional arrangement)* kuelekea Uchaguzi Mkuu wa 2015 ikiwa uchaguzi huo utafanyika kabla ya Katiba Mpya kupatikana. *(Makofi)*

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri kwa dhati kabisa kwamba, taratibu za mpito za kushughulikia masuala yote ya Uchaguzi Mkuu ziendelee kufanyika ili kama Uchaguzi Mkuu utafika kabla ya kuwa na Katiba Mpya, basi kuwe na "*fall-back position*" ili kuinusuru nchi kuingia katika mtanziko ambao unaweza kuwa chanzo cha machafuko ya kisiasa.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuingia Uchaguzi wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa kwa utaratibu uliopo leo. Hatuwezi kwenda kwenye uchaguzi Mkuu mwakani na Tume ya Uchaguzi kama ilivyo leo ambayo haijawekewa vyombo vya kikatiba ikiwemo mifumo ya utendaji ambayo itahakikisha uhuru wa Tume unalindwa na haki kutendeka kwa wadau wote.

Hatuwezi tena kwenda kwenye Uchaguzi Mkuu mwakani wakati Matokeo ya Uchaguzi wa Rais hayawezi kuhojiwa Mahakamani na hoja ya mgombea huru haijapatiwa majibu. Hatuwezi kuingia katika uchaguzi ujao na Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lililopo leo.

Hatuwezi kulikubali daftari jipya litakalotengenezwa kama wadau wote hatutashirikishwa kikamilifu katika hatua zake zote za upatikanaji wake ikiwemo mifumo itakayotumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kurudia. Ni kweli kama ilivyo kawaida, Serikali ya CCM inaweza kupuuza tahadhari hizi na kulazimisha kwenda katika chaguzi hizi katika mazingira ambayo hayana muafaka kama inavyoonekana sasa katika Mchakato wa Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, uchaguzi wa Serikali za Vitongoji, Vijiji na Mitaa. Mwezi Machi, 2014 Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda alizungumza na vyombo vya habari na kueleza kwamba ameona dhahiri hatari ya kusogezwa mbele kwa Uchaguzi wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa kutoka Oktoba, 2014 mpaka mwaka 2015. Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda alieleza kwamba Uchaguzi huo umesogezwa mbele kutoa nafasi kwa kazi nyingine kuendelea hususan mchakato wa mabadiliko ya Katiba. Waziri Mkuu Pinda alieleza kwamba angemwomba Rais Jakaya Kikwete kusogeza mbele uchaguzi huo.

Hata hivyo, wakati kauli hizo zikitolewa Kambi Rasmi ya Upinzani inazo taarifa kwamba maandalizi ya uchaguzi huo yanaendelea chini kwa chini kwa ajili ya uchaguzi huo kufanyika Oktoba, 2014. Maandalizi hayo ni pamoja na mapitio ya Kanuni za Uchaguzi tajwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Waziri Mkuu alieleze Bunge iwapo aliwasilisha maombi husika kwa Rais na nini majibu juu ya hatma ya uchaguzi husika. Serikali inayotawaliwa na CCM inapaswa kuhakikisha kwamba inaheshimu maoni ya wananchi juu ya Uchaguzi wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa ambao wametaka mabadiliko makubwa ya taratibu za uchaguzi huo kupitia mchakato wa mabadiliko ya Katiba.

Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kwamba Uchaguzi wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa na mfumo mzima wa Serikali za Mitaa siyo mojawapo ya mambo ya Muungano kwa hali ya saa. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya maamuzi na mabadiliko ya Kisheria kuwezesha uchaguzi huo kufanyika mapema kabla ya mchakato wa mabadiliko ya Katiba kukamilika ili kuhakikisha kwamba Uchaguzi huo unakuwa huru na wa haki.

Mheshimiwa Spika, Ifahamike kwamba mwanya huu wa kisheria wa Waziri kutunga kanuni ulitumiwa vibaya mwaka 2004 na kufanya kanuni hizo kutungwa kupendelea Chama kinachotawala na kuweka mianya ya hujuma za kiuchaguzi. Matokeo yake ni uchaguzi uliopita wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa kutokuwa huru na haki kutokana na upungufu mwingi ambao hata Serikali yenyewe iliukiri.

Mathalan, upigaji kura haukuwa wa siri, fujo katika Mikutano ya Uchaguzi, matayarisho kuwa hafifu, kuingiliwa na Maafisa na Watendaji wa Kata na Vijiji ambao walifikia hatua ya kuwatisha wananchi na kutotoa taarifa za muhimu za uchaguzi, kukosekana kwa Daftari la Wapiga Kura na uchaguzi kusimamiwa na chombo kisicho huru cha Kiserikali moja kwa moja, yaani Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, lakini zaidi kutokana na hujuma hizo wananchi wakalazimishwa kuongozwa na Viongozi wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa katika maeneo mengi wasiokuwa na uhalali wa kukubalika ambao wamekuwa kikwazo cha maendeleo na pia kusababisha migogoro ambayo ingeweza kuepukwa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, naomba hotuba yangu yote iingizwe kwenye *Hansard* na Kumbukumbu Rasmi. Lakini niendelee sasa katika ukurasa wa 27 na 28.

Mheshimiwa Spika, kasoro za utaratibu na kanuni za uendeshaji wa Serikali kwa Chaguzi za Serikali za Mitaa ni pamoja na kanuni kuelekeza

kwamba karatasi za kura kutokuwa na majina ya Wagombea na kwamba mpiga kura alilazimika kuandika mwenyewe. Hali hii ilichochea kuchelewa ama kuvurugika kwa mchakato wa upigaji na uhesabuji wa kura katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Spika, katika nchi ambayo takriban nusu ya wananchi wake hawajui kusoma na kuandika na sehemu kubwa ya wanaojua bado siyo kwa kiwango kizuri, uamuzi wa kutunga kanuni ambazo zinalazimisha Wapiga Kura wote waandike wenyewe majina kamili ya Wagombea, ulitoa mianya ya kuvurugika kwa uchaguzi huu na ukijirudia tena utasababisha athari zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kwa upande mwingine maelekezo ya uchaguzi yaliyotolewa na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda yalipingana na kanuni ambapo Ofisi yake imezitoa kuhusiana na dhamana ya Wagombea. Kanuni zitaka Mgombea awe amedhaminiwa na Chama cha Siasa. Hata hivyo, katika maelekezo, Ofisi ya Waziri Mkuu imekwenda mbali zaidi kwa kuongeza maneno mengine ambayo hayapo kabisa kwenye kanuni ya kwamba mgombea lazima awe amedhaminiwa na ngazi ya chini kabisa ya Chama chake.

Maelekezo hayo yalipingana kabisa na Katiba za Vyama shiriki ambazo zinaeleza bayana ni ngazi zipi zenye mamlaka ya kudhamini Wagombea. Maelekezo hayo potofu yalitumika kuwawekea pingamizi Wagombea wengi wa upinzani na kusababisha wengi kuenguliwa.

Mheshimiwa Spika, izingatiwe kuwa mfumo wa utawala wa nchi yetu unaanzia katika Vitongoji, Vijiji na Mitaa ambayo ina mamlaka kadhaa ya kiutendaji na kimaamuzi. Kuruhusu uchaguzi huu kuvurugika ama kuleta Viongozi wabovu, kama Taifa tutakuwa tumeweka msingi legelege wa utawala na demokrasia na athari zake zitaonekana katika kukwama kwa jitihada za kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu Tume Huru ya Uchaguzi na Maboresho ya Daftari la Wapiga Kura.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilieleza kwa kirefu jinsi ambavyo Serikali ina dhamira ovu dhidi ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, na hivyo inapoka haki za kikatiba za wananchi waliotimiza masharti ya kupiga kura ambao inakataa kuwaandikisha ili wasipige kura.

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilionyesha bayana jinsi ambavyo ilijitahidi kumuuliza Waziri Mkuu maswali Bungeni juu ya suala hili, na Waziri Mkuu

mara zote alionekana kutoa majibu ya jumla ambayo hayakukidhi haja ya tatizo.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba tangu Uchaguzi Mkuu wa 2010, kumefanyika chaguzi ndogo takribani nne za Ubunge katika Majimbo ya Igunga - Tabora, Arumeru Mashariki - Arusha, Kalenga – Iringa, na Chalinze Mkoani Pwani. Aidha, zimefanyika chaguzi za marudio za Madiwani takribani 90 katika Kata kadhaa hapa nchini kwa sababu mbalimbali. Katika chaguzi hizi, Daftari la Kudumu la Wapiga Kura halikufanyiwa marekebisho na hivyo kuwanyima wananchi wengi waliokuwa na sifa ya kuandikishwa na kupiga kura haki ya kushiriki katika chaguzi hizo.

Mheshimiwa Spika, licha ya wapiga kura waliotimiza masharti ya kupiga kura kunyimwa haki hiyo ya kikatiba kwa kutoboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura; jambo hili pia limesababisha migogoro isiyo ya lazima baina ya Vyama vinavyoshiriki katika chaguzi hizo na Tume ya Uchaguzi.

Katika chaguzi zote hizo za marudio, wastani wa waliojitokeza kupiga kura hawakufika asilimia 30 na hivyo kusababisha manung'uniko kuwa Tume ya Uchaguzi inashirikiana na Serikali na Chama cha Mapinduzi kuzuia walio wengi kutokupiga kura kwa maslahi ya Chama cha Mapinduzi.

Hadi leo, siyo Tume wala Serikali imeweza kutoa sababu za msingi za Wapiga Kura wengi kiasi cha wastani wa asilimia 70 kutokuweza kujitokeza na kupiga kura achilia mbali wale ambao hawajaandikishwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kambi Rasmi ya Upinzani imeshasema vya kutosha kuhusu uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura; na kwa kuwa Serikali haionyeshi umakini, kujali na dhamira ya dhati ya kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga kura, kwa kuwa chaguzi zote za marudio zilizofanyika baada ya mwaka 2010 zimefanyika bila daftarti la Wapiga Kura kufanyiwa maboresho, jambo ambalo limewanyima wananchi wengi haki ya kupiga kura; na kwa kuwa kufanya chaguzi bila kuboresha Daftari la Wapiga Kura kunafanya chaguzi hizo kukosa sifa ya kuwa huru na za haki; hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya mambo yafuatayo kabla ya Uchaguzi Mkuu ujao:-

(i) Kutoa Ratiba Rasmi ya Maboresho ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika Bunge hili;

(ii) Kuleta marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi ili kuondoa ukomo wa kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura wa mara mbili kwa kipindi cha miaka mitano na badala yake daftari hilo liwe huru wakati wote kuandikisha

Wapiga Kura wapya wanaotimiza masharti ya kupiga kura na kuingiza marekebisho ya taarifa za wapigakura wengine; *(Makofi)*

(iii) Kutenga Bajeti Maalumu kwa ajili ya Maboresho ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura; na

(iv) Kupanga Ratiba yenye kutoa muda wa kutosha wa uhamasishaji wa wananchi kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu uandikishji wa watu kwenye daftari la uraia unaofanywa kinyemela na Maablozi wa Nyumba Kumi wa Chama cha Mapinduzi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepata taarifa kwamba Mabalozi wa Nyumba Kumi wa CCM wanafanya zoezi la uandikishaji wa wananchi kwenye kitu kinachoitwa Daftari la Uraia. Uandikishaji huu unafanyika kinyemela na unaonekana kuwa na baraka za Serikali kwa kuwa fomu za usajili zinatumika zimetolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Taarifa tulizozipata ni kwamba Daftari hilo ndilo linategemewa kutumika katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa na pia litatumika katika uandikishaji wa wananchi kwenye Datari la Kudumu la Wapiga kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imeshtushwa sana na usajili huu kwa kuwa haufanywi na *NIDA* wala Tume ya Taifa ya Uchaguzi ambazo ndizo Mamlaka halali kisheria kufanya usajili ama kwa lengo la Vitambulisho vya Taifa au kwa ajili ya Wapiga kura. Tumeshtushwa zaidi kwa sababu kwa taarifa tulizopata, usajili huo unafanyika kibaguzi kwa kuwaruka wananchi ambao ni wa Wanachama wa Vyama vya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Waziri Mkuu atoe maelezo mbele ya Bunge hili kuwa ni nani aliyeamuru usajili huo ufanyike na ni kwa malengo gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uandikishaji wa wapiga kura kwa kutumia teknolojia ya *Biometric (Biometric Voter Registration)*. Katika hotuba yangu niliyowasilisha Bungeni Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2013/2014 nilisema kwamba, nanukuu; *"kuna mchakato wa maandalizi ya siri unaoendeshwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) wa kuandaa utambuzi wa Wapiga Kura kwa kutumia mfumo wa "biometric" kwa maana ya kumtambua mpiga kura kwa alama za mwili kama alama za vidole na au mboni ya jicho kama sehemu ya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu ujao wa 2015".*

Kwa mujibu wa taarifa tulizokuwa nazo wakati ule, ni kwamba tayari Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilishaanza maandalizi mengi ya msingi bila kushirikisha wadau. Naomba kurudia hapa; ilishaanza maandalizi mengi ya msingi bila kushirikisha wadau hasa Vyama vya Siasa, isipokuwa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, nilieleza pia kuwa teknolojia hii kwa siku za karibuni imetumika katika chaguzi nchini Ghana na Kenya. Kote huko ilifeli, na chupuchupu iingize MaTaifa hayo katika vurugu kubwa za uchaguzi. MaTaifa haya yalilazimika kurudia mfumo wa upigaji na kuhesabu kura kwa mkono, hali iliyosababisha hofu kubwa.

Mheshimiwa Spika, niliweka bayana pia kwamba, siyo kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani haiafiki matumizi ya teknolojia mpya kurahisisha na kuboresha mfumo mzima wa uchaguzi katika nchi yetu, bali inatambua athari kubwa zinazoweza kutokea siku za usoni kama suala lililo *"sensitive"* namna hii halitafanywa katika misingi ya uwazi na ushirikishwaji wadau muhimu kama Vyama vya Siasa katika hatua zote la tangu awali kabisa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sababu hizo, tuliitaka Serikali kutoa maelezo ya kina kuwa ni sheria gani iliyotungwa na Bunge inayoruhusu uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa mfumo huu wa *"biometric"* na pia ni bajeti ipi inatumika kutekeleza mpango huo? Aidha, tulihoji ni kwa nini mpango huo unafanyika kwa siri bila wadau wa siasa nchini kushirikishwa na kutoa baraka zao juu ya mpango huo?

Mheshimiwa Spika, pamoja na tahadhari zote tulizotoa hususan ushirikishwaji wa wadau katika kwanza kuifahamu hiyo *"Biometric Voter Registration – BVR"* na kuiridhia, Tume bado imeendelea kutenga wadau hususan Vyama vya Upinzani na kuendelea kushirikiana na Serikali ya CCM katika kuielewa *BVR*, kutengeneza mifumo yake ikiwemo zabuni za ununuzi wa vifaa na mifumo yake ya uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na ucheleweshaji mkubwa wa utekelezaji wa mfumo huu. Miongoni mwa sababu kuu ni kunyukana kwa makundi ndani ya Serikali, Tume ya Uchaguzi na wazabuni katika kugombea fursa ya kuuza mifumo hii mipya ya *BVR*.

Vigogo ndani ya Serikali wamekuwa sehemu ya kuchelewesha mpango huu kwa zaidi ya mwaka sasa. Japo kwa mwonekano wa haraka kutoka kwa Mamlaka ya Uthibiti wa manunuzi ya Umma, Taifa litaaminishwa kuwa rufaa kadhaa kuhusiana na kandarasi ya *BVR* inatokana na ushindani miongoni mwa Wazabuni, ukweli unaofichwa ni kuwa nyuma ya wazabuni hawa, wako Vigogo wa Serikali na familia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mazingira haya ni viashiria tosha vya uwepo wa uwezekano wa ufisadi mkubwa tena wa kutisha katika mfumo huu wenye malengo maovu makuu mawili:-

(i) Lengo la kutengeneza mfumo wenye usiri mkubwa utakaowezesha uchakachuaji wa kitaalam wakati wa uchaguzi; na

(ii) Lengo la baadhi ya vigogo kutengeneza mabilioni ya fedha kupitia mradi huu. *(Makofi0*

Mheshimiwa spika, kwa kuzingatia unyeti wa zoezi hili kwamba linaweza kuiingiza nchi katika machafuko makubwa, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iweke wazi mchakato mzima wa wazabuni na gharama halisi za mfumo huu sambamba na Makampuni yote yaliyohusika na ambayo bado yana wahusika katika zabuni hii ikiwemo sifa ya kila mzabuni.

Kama Serikali itashindwa kuweka wazi suala hili, basi Kambi Rasmi ya Upinzani itatangaza mgogoro na zoezi zima hadi hapo uwazi *(transparency)* na ushirikishwaji utakopokuwa dhahiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utawala bora na uajibikaji wa kiutendaji. Utawala bora ni pamoja na kutenda mambo kwa haki na kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizowekwa kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa shughuli kiutawala. Aidha, kudumisha demokrasia kunachagiza sifa za utawala bora.

Mheshimiwa Spika, kwa muda unaozidi mwaka mmoja sasa, kumekuwa na zuio la Vyama vya Upinzani kufanya shughuli zake katika Mikoa ya Lindi na Mtwara kwa kisingizio cha vurugu za zilizotokea mwaka 2013 wakati wananchi wakikataa bomba la gesi kujengwa kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Rais ndiye mwenye mamlaka ya kutangaza hali ya hatari katika nchi au katika sehemu yoyote ya nchi. Kwa kuzingatia hali iliyopo Mtwara na Lindi kwa sasa, ni wazi inaonekana kuna hali ya hatari ambayo imetangazwa kimya kimya kwa Vyama kuzuiwa kufanya shughuli za kisiasa huku kukiwa na ushahidi kuwa Chama Tawala, yaani CCM wanaendelea kufanya Mikutano yao katika maeneo hayo kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kwamba huu ni ubaguzi wa wazi kabisa baina ya CCM na Vyama vingine vya upinzani na ni ukiukwaji mkubwa wa misingi ya utawala bora katika nchi. Hivyo, inamtaka Waziri Mkuu kutoa kauli hapa Bungeni kuwa ni nani aliyetangaza hali hiyo ya hatari katika mikoa ya Lindi na Mtwara, kiasi cha

kuzuia shughuli za siasa katika Mikoa hiyo na ni sheria ipi imetumika kukandamiza haki ya demokrasia kwa kipindi kirefu hivyo cha muda wakati vurugu zilizotokea Mtwara na Lindi zilishakwisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, kwa sababu ya muda, naomba sasa niende mbele nizungumzie kuhusu gharama za uendeshaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia gharama za uendeshaji wa Serikali katika muktadha wa Rasimu ya Katiba inayotokana na maoni ya wananchi ambayo inapendekeza Mfumo wa Serikali Tatu.

Katika mjadala wa Sura ya Kwanza na Sita ya Rasimu ya Katiba, hoja kubwa iliyokuwa ikitumiwa na CCM na mawakala wao kupinga maoni ya wananchi ya Mfumo wa Serikali Tatu na kupenyeza ajenda yao ya Serikali Mbili ilikuwa ni kwamba Mfumo wa Serikali Tatu utaongeza gharama za uendeshaji wa Serikali na kwa maana hiyo utaongeza mzigo kwa wananchi ambao ni walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, licha ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba kufanya utafiti wa kina na kupendekeza Serikali ndogo ya Shirikisho na Taasisi chache za Muungano ambazo gharama zake ni ndogo kuliko mfumo wa Serikali mbili tulionao sasa, bado CCM na mawakala wao wameendelea kueneza *propaganda* miongoni mwa wananchi kuwa Serikali tatu zitakuwa mzigo mkubwa kwa wananchi jambo ambalo siyo kweli hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jambo la kushangaza sana, Serikali hii inayopinga Serikali Tatu kwa kisingizio cha gharama kubwa, ndiyo inayoendelea kugawa Mikoa na Wilaya za nchi yetu kila kukicha na hivyo kuongeza gharama za uendeshaji wa Serikali mara dufu kuliko ambavyo ingekuwa kwa uendeshaji wa Seriakali ya Shirikisho la Serikali Tatu zinazopendekezwa kwenye Rasimu ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, Kama Serikali ingekuwa inajali gharama, basi ingekuwa inafanyia kazi mapendekezo ya Kambi ya Upinzani tangu mwaka 2010 ambapo tuliishauri Serikali kupunguza matumizi ya kawaida na kuongeza fedha zaidi katika miradi ya Maendeleo. *(Makofi)*

Aidha, Serikali ingeacha kuendelea kugawa Mikoa na Wilaya kwani kwa kufanya hivyo ni kuongeza gharama za uendeshaji wa Serikali. Ni jambo la ajabu kabisa kwamba kwa jinsi Serikali hii isivyojali gharama za uendeshaji wa Serikali, hata Kata ya Mbagala sasa inapendekezwa kuwa Wilaya mpya ya Mbagala. *(Makofi)*

Ofisi ya Waziri Mkuu imeshindwa kumshauri Rais juu ya ugawaji wa Mikoa na Wilaya, matokeo yake kila kukicha tunajenga Makao Makuu ya Wilaya na Mikoa wakati fedha hizo tungeweza kuzielekeza kwenye miradi ya Maendeleo na huduma za jamii kama vile shule, hospitali na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kudhihirisha kwamba Serikali haina uchungu na gharama za uendeshaji wa Serikali na kwamba inatumia kivuli cha gharama ili kupinga maoni ya wananchi ya Serikali Tatu katika Rasimu ya Katiba, katika bajeti ya Shilingi trilioni 19.6 kwa mwaka huu wa fedha 2014/2015, Shilingi trilioni 14.2 sawa na asilimia 72.4 ni matumizi ya kawaida ya uendeshaji wa Serikali. Wakati ni Shilingi trilioni 5.4 tu sawa na asilimia 27.5 tu ndizo bajeti ya Maendeleo.

Fedha za maendeleo zilizotengwa hazifikii asilimia 35 ya bajeti yote kama ambavyo Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Taifa ambao umeasisiwa na Serikali hii hii ya Chama cha Mapinduzi unavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie matumizi mabaya ya vyombo vya habari vya Umma.

Mheshimiwa Spika, Vyombo vya Habari vya Umma ni mali ya wananchi wote bila kujali itakadi zao za kisiasa wala imani zao za kidini. Vyombo hivi vinatumia kodi ya wanachi na hivyo vinawajibika kutoa habari kwa wananchi wote bila ubaguzi wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, licha ya wajibu wa kutoa habari kwa usawa na bila upendeleo kuwa ni wajibu wa kikatiba, vyombo vya habari vya Umma kwa mfano Kituo cha Televisioni cha Taifa *(TBC1),* Redio ya Taifa (*TBC* Taifa) na hata Magazeti ya Serikali husan *Daily News* na Habari Leo, vimekuwa vikitumika kutetea misimamo na mitazamo ya upande mmoja wa Chama cha Mapinduzi (CCM) na kuvinyima fursa Vyama vyenye mitazamo tofauti. *(Makofi)*

Hii ni kwa sababu Serikali na hata baadhi ya Viongozi wa CCM wamekuwa wanaingilia masuala ya uhariri wa vyombo hivyo, kiasi cha wasimamizi wa vyombo kudhani wanaendesha vyombo vya CCM. Haya ni matumizi mabaya ya kodi za wananchi zinazoendesha vyombo hivyo, na ni dhuluma kwa wananchi wanaopaswa kuhudumiwa na vyombo hivyo kwa usawa bila kujali tofauti za kiitikadi, za kijamii au za kidini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatujalalamikia Gazeti la Uhuru kwa sababu tunafahamu ni gazeti la Chama cha Mapinduzi na hatuna ugomvi nalo likiandika habari za Chama cha Mapinduzi. Hatulalamikii vyombo vya habari binafsi kwa sababu vina uhuru wa kufungamana upande wowote mradi viandike taarifa ambazo ni za kweli. Lakini vyombo vya Serikali vya Umma

vinapotumika kupendelea upande mmoja vinaweka misingi mibaya ya chuki miongoni mwa jamii, jambo ambalo siyo jema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Vyombo vya Habari vya Umma vimekuwa na tabia ya kutoa habari chanya kwa upande wa Serikali na CCM lakini vimekuwa vikitoa habari hasi kwa upande wa Upinzani na mara nyingine kutotangaza kabisa habari chanya zinazotokana na kazi nzuri ya Upinzani. Jambo hili liliwahi kulalamikiwa na Kambi Rasmi ya Upinzani lakini bado ubaguzi katika kutoa habari unaendelea. *(Makofi)*

mfano hai wa ubaguzi unaofanywa na vyombo vya habari vya Umma ni pale ambapo Kituo cha Televisheni cha Taifa *(TBC1)* na Redio ya Taifa, *TBC* – Taifa vilipokatikasha matangazo yake ya moja kwa moja ya Bunge Maalum la Katiba wakati Mjumbe wa Bunge Maalum anayetokana na Chama cha Upinzani, Mheshimiwa Tundu Lissu alipokuwa akitoa ufafanuzi wa Maoni ya Wachache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sababu iliyotolewa kwamba kulikuwa na matatizo ya kiufundi haina mashiko kwa kuwa Kituo cha Televisheni cha Taifa kiliendelea kurusha matangazo mengine jambo linalothibitisha kwamba kulikuwa hakuna tatizo la kiufundi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ilipata taarifa kwamba Watendaji wa *TBC1* na *TBC* Taifa walipata maelekezo kutoka kwa Waziri wa Habari, Vijana Michezo na Utamaduni kwamba wakatishe matangazo ya moja kwa moja ya Bunge Maalum wakati Mheshimiwa Tundu Lissu akiwasilisha maoni ya wachache. Tunaitaka Serikali ilieleze Bunge hili ni kwa nini inaelekeza vyombo vya habari vya Umma kufanya kazi kwa ubaguzi ilhali vyombo hivyo vinatumia fedha za walipa kodi wa nchi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niende katika uwekezaji na uwezeshaji na mengine naomba taarifa iingie kwenye *Hansard* lakini nisome upande wa uwezezaji wananchi, yaani *empowerment*.

Mheshimiwa Spika, ngoja niokoa muda kidogo hapa.

Mheshimiwa Spika, suala la uwezeshaji wananchi kiuchumi pia halimaanishi kuwa Serikali itoe fungu la fedha kwa ajili ya shughuli za uwekezaji. Badala yake, Serikali ina wajibu wa kutoa fursa hata za upendeleo ikibidi, kwa kulinganisha na washindani wageni. Ni dhahiri wakipata haki ya miliki, wawekezaji Watanzania wana uwezo wa kutosha wa kuvuta mitaji kutoka makampuni makubwa na hata mashirika na Taasisi za fedha za Kimataifa.

Aidha, ieleweke vilevile kuwa hata wawekezaji wengi wageni wanaoaminika na Serikali hii, hutafuta mitaji toka Taasisi za fedha za kwao na Kimataifa baada ya kupewa vibali vya kuvuna rasilimali zetu kwa bei ya kutupa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, inashangaza kusikia kauli za Viongozi Waandamizi wa Serikali zinazovunja moyo wawekezaji hao wa ndani badala ya Serikali kuwa chombo cha uwezeshaji wa wazawa katika uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, wawekezaji wazawa ambao walionesha nia au wameendelea kuonesha nia ya kuwekeza katika miradi mbalimbali, wameendelea kukashifiwa, kudharauliwa na kudhalilishwa na kauli tata za Viongozi kuwa hawana uwezo.

Kwa mfano, kauli ya Waziri wa Nishati na Madini Prof. Sospeter Muhongo kuwa Watanzania hawawezi na hawana uwezo wa kuwekeza kwenye gesi na mafuta, hivyo wawekeze kwenye viwanda vya matunda, juisi, nyanya, na kadhalika ni kauli ambayo ilistahili kukemewa kwa nguvu zote na Serikali na yeye mwenyewe kuwajibishwa moja kwa moja aidha kwa kujiuzulu au kwa kufukuzwa kazi. Lakini cha kushangaza, Viongozi Wakuu wa Serikali walikaa kimya na wengine hata kushangilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu ni ushuhuda wa wazi kuwa kauli kuwa "Sekta Binafsi" ni "*engine*" ya kukua kwa uchumi kwao inamaanisha sekta binafsi ya kigeni. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawashangaa zaidi wafanyabiashara hawa wanaotukanwa hadharani kuwa ndiyo hao hao wafadhili wakubwa wa CCM hiyo hiyo inayowabeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kauli hizi za Viongozi Waandamizi wa Serikali za kuudhi hazitakiwi kufumbiwa macho kwa kuwa wapo katika Utumishi wa Umma kwa maslahi ya Watanzania. Ni dhahiri kuwa, wawekezaji wazawa wana wajibu wa kuona kuwa Watanzania hawaachwi nyuma na badala yake wanashiriki pia moja kwa moja katika Sekta mbalimbali za uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, ni lazima vile vile kama Taifa tukumbuke kwamba wawekezaji tunaowaona ni wa maana kutoka nchi za nje nao waliwezeshwa katika hatua za mwanzo za uwekezaji wao na ndiyo sababu leo wana uwezo wa kuwekeza mitaji mikubwa katika nchi yetu.

Kama hatutakuwa na mkakati wa makusudi wa kuwezesha wananchi wetu kwa sababu eti hawana mitaji ya kutosha, tutakuwa hakika hatujengi kizazi cha kesho cha wawekezaji wa ndani.

Mheshimiwa Spika, niende sasa namba saba, nizungumzie mapendekezo yetu ya nyuma na ahadi za Serikali. Nitazungumza kuhusu RERA *(Real Estate Regulatory Authority)*.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Kambi ya Upinzani kwa mwaka wa fedha 2011/2012 tuliitaka Serikali kuanzisha chombo kitakachoweka uratibu na usimamizi wa sekta ya majengo makubwa ya biashara ambayo inakuwa kwa kasi kubwa. Mamlaka hii siyo tu itasimamia haki za wapangaji, bali hata mapato ya Serikali na ubora wa majengo haya na huduma zake.

Tulipendekeza mamlaka hii ya udhibiti iitwe *"Real Estate Regulatory Authority."* Tunarudia tena kusisitiza ushauri wetu huu kwani Serikali inapoteza mapato bila sababu ya msingi kwa jeuri na kiburi cha kutokubali ushauri uliotoka upinzani.

Mheshimiwa Spika, ni vema Bunge Tukufu na na wananchi wetu wakaelewa kwamba Sekta ya Ujenzi sasa hivi inachangia *almost* asilimia 18 ya *GDP* katika Taifa, ni sekta kubwa na ina fedha nyingi sana. Sasa kama Serikali haiweki mamlaka ya...

**SPIKA:** Mheshimiwa, naomba usome!

**MSEMAJI MKUU KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU – MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Nilichombeza kidogo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa maelekezo yako.

**SPIKA:** Ahsante.

**MSEMAJI MKUU KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU – MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Ni kwa sababu tu ya unyeti wa jambo lenyewe.

Mheshimiwa Spika, kumbukumbu za taarifa rasmi za Bunge zinaonyesha kwamba katika hotuba ya *KUB* mwaka 2011/2012 tuliishauri Serikali kuhusu kuunda Tume ya kijaji ya uchunguzi wa vifo vya raia. Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali walikubali na wakaahidi kutekeleza hilo, lakini toka mwaka huo hadi sasa hakuna chochote kilichotekelezwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba Serikali haina dhamira yoyote ya kulitafutia ufumbuzi wa kudumu suala hili ambalo wananchi wamekuwa wakililalamikia kuhusu jamaa zao kuuawa na vyombo vya dola. Ni ukweli ulio wazi kwamba tangu kipindi hicho vimeripotiwa vifo

kadhaa, majina ya watu waliouawa yanapatikana katika Taarifa ya Haki za Binadamu ya mwaka 2013, ukurasa wa 22.

Mheshimiwa Spika, Maadam ahadi ni deni na wananchi wanaendelea kuuawa, tunaomba kwa mara nyingine tena kauli ya Waziri Mkuu kuhusiana na kadhia hii.

Mheshimiwa Spika, lingine mapitio ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kuangalia fedha za maendeleo kwa baadhi ya mafungu kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa mujibu wa randama, inaonyesha kuwa kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 37; Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Fungu 61; na Mfuko wa Bunge, Fungu 42 kwa pamoja zilitengewa jumla ya Sh. 54,729,392,000/= kwa fedha za maendeleo. Hadi Machi, 2014 kiasi ambacho tayari kilikwishatolewa ni Sh. 17,263,036,286/= sawa na asilimia 28.4 ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya ni kwamba kwa upande wa Tume ya Taifa, hakuna fedha yoyote ya maendeleo iliyotolewa hadi kufikia hiyo Machi, 2014. Kwa mwaka huu wa fedha 2014/2015 kwa mafungu hayo hayo inaonekana zimetengewa jumla ya Sh. 29,953,134,000/= zikiwa ni fedha za ndani na fedha za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwonekano wa matumizi ni dhahiri kwamba uwezo wa Serikali kutoa fedha za maendeleo siyo mkubwa na jambo hili limepelekea uwepo wa bajeti kubwa lakini utekelezaji wake ni mdogo sana. Mfano unaonekana kwenye Wizara hii inayoongozwa na Kiongozi wa Shughuli za Serikali. Je, hili ni kuwadanganya Watanzania au Serikali inajidhalilisha yenyewe au kuna fedha nyingine zinazotumika bila kupitia kwenye mfumo wa kuidhinishwa na Bunge? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa Muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mbowe.

**MSEMAJI MKUU KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA WAZIRI MKUU – MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba yote iingine kwenye *Hansard*. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**Hoja ya Msemaji Mkuu wa Serikali kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kama ilivyowasilishwa Mezani**

**HOTUBA YA KIONGOZI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI MHE.FREEMAN AIKAELI MBOWE (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA WAZIRI MKUU KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015**

(Inatolewa chini ya Kanuni ya 99 (9), ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2013)

---

## 1.0 MCHAKATO WA KATIBA MPYA NA MUSTAKABALI WA TAIFA

**Mheshimiwa Spika,** Nchi yetu ipo katika kipindi tete cha kikatiba na kisiasa. Mchakato wa kutunga Katiba Mpya kwa ajili ya nchi yetu ulioanza kufuatia hotuba ya Mh. Rais Jakaya Kikwete ya Mwaka Mpya 2011 uko katika hatari kubwa ya kuanguka na kuparaganyika.

Sehemu kubwa na muhimu ya wajumbe wa Bunge Maalum, yaani wale wanaounda Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA), wamesusia vikao vya Bunge Maalum kutokana na kile wanachoona kama njama za kulitumia Bunge Maalum kama chombo cha kupitishia matakwa ya kikatiba ya Chama cha Mapinduzi (CCM) na kutupa jalalani matakwa ya wananchi kama yalivyoainishwa na Rasimu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ilivyoandaliwa na kuwasilishwa bungeni na Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

Kwa sababu ya njama hizo, Bunge Maalum limegeuzwa kuwa uwanja wa matusi, vijembe, kauli za kibaguzi na vitisho dhidi ya wananchi wanaotaka mabadiliko ya msingi ya kikatiba na kisiasa, na ya muundo wa Muungano kati ya nchi mbili zinazounda Muungano huu, yaani Tanganyika na Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Wakati akitangaza kuanza kwa mchakato wa Katiba Mpya katika hotuba yake ya tarehe 31 Desemba, 2010, Rais Kikwete alisema maneno yafuatayo ambayo, kwa umuhimu wake, tunaomba kuyanukuu kwa kirefu:

> *"… Mwaka 2011, nchi yetu inatimiza miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara, miaka 47 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar na miaka 47 ya Muungano wa nchi zetu mbili. ... Kwa ajili hiyo ni vyema kuwa na Katiba inayoendana na mabadiliko na matakwa na hali ya sasa. Katiba ambayo italipeleka taifa letu miaka 50 ijayo kwa salama, amani, umoja na kuwepo maendeleo makubwa zaidi....*
> *"Ndiyo maana tukaamua kuanzisha mchakato huu na kwa ajili hiyo, nimeamua kuunda Tume maalum ya Katiba ... itakayoongozwa na*

*Mwanasheria aliyebobea, itakuwa na wajumbe wanaowakilisha makundi mbalimbali katika jamii yetu kutoka pande zetu mbili za Muungano. Jukumu la msingi la Tume hiyo litakuwa ni kuongoza na kuratibu mchakato utakaowashirikisha wananchi wote bila kubagua, vyama vya siasa, wanasiasa, wafanyabiashara, asasi za kiraia, mashirika ya dini, wanataaluma na makundi mbalimbali ya watu wa nchi yetu kote nchini, katika kutoa maoni yao juu ya wayatakayo kuhusu Katiba ya nchi yao.*
*"Baada ya kukamilisha kukusanya maoni, Tume itatoa mapendekezo yake yatakayofikishwa kwenye vyombo stahiki vya Kikatiba kwa kufanyiwa maamuzi. Baada ya makubaliano kufikiwa, taifa letu litapata Katiba mpya kwa siku itakayoamuliwa ianze kutumika....*

*"Ni matumaini yangu kuwa mchakato huo utaendeshwa vizuri, kwa amani na utulivu kama ilivyo sifa ya nchi yetu na mazoea yetu ya kujadiliana bila kugombana.... Pasiwepo kutukanana, kudharauliana, kushutumiana, kubezana, kuzomeana wala kushinikizana. Naomba washiriki waongozwe kwa hoja badala ya jazba. Tukiwa na jazba, hasira na kushinikizana kamwe hatutaweza kutengeneza jambo jema. Na inapohusu Katiba ya Nchi itakuwa hasara tupu. Haitakuwa endelevu na kulazimika kufanyiwa marekebisho mengi mwanzoni tu baada ya kutungwa."*

**Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza ahadi hiyo, Bunge lako tukufu lilitunga Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83 ya Sheria za Tanzania mnamo Novemba, 2011. Baadaye Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho mara tatu kati ya Februari 2012 na Desemba 2013. Aidha, Bunge lako tukufu lilitunga Sheria ya Kura ya Maoni, 2013. Vile vile, katika kipindi hicho hicho, Rais Kikwete aliteua Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

Kama alivyoahidi Rais, Tume hiyo iliongozwa na mwanasheria aliyebobea na ambaye aliwahi pia kuwa Mwanasheria Mkuu na Waziri wa Katiba na Sheria na Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Jaji Joseph Sinde Warioba. Na kama alivyoahidi Rais, wajumbe wa Tume hiyo walitoka katika makundi mbali mbali ya jamii kutoka nchi zote mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano. Wajumbe hao walijumuisha wanataaluma waliobobea, wanasheria, viongozi na watumishi wa umma waliolitumikia taifa katika nafasi za juu, viongozi wa kidini na wawakilishi wa vyama vya siasa na wa asasi za kiraia.

**Mheshimiwa Spika,** Kati ya Mei Mosi 2012 wakati Tume ya Mabadiliko ya Katiba ilipoanza kazi rasmi na tarehe 21 Machi, 2014, Tume hiyo ilipovunjwa rasmi, Bunge lako tukufu liliidhinisha jumla ya Shilingi bilioni 74.463 kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Tume. Katika kipindi hicho, Tume ilitembea nchi nzima kukusanya maoni ya Watanzania juu ya Katiba Mpya waitakayo. Tume

pia ilifanya rejea ya nyaraka nyingi kama zilivyoorodheshwa katika kifungu cha 17(4) cha Sheria; pamoja na kupitia taarifa mbali mbali zilizoandaliwa na wataalamu walioteuliwa na Tume kwa ajili hiyo.

Baadaye, kwa kuzingatia vyanzo hivi vya taarifa, tarehe 3 Juni 2013 Tume ilitoa Rasimu ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Rasimu hiyo nayo ilipelekwa kwa wananchi kwa ajili ya kutolewa maoni na wananchi, taasisi za kiserikali, asasi za kiraia, vyama vya siasa na watu mashuhuri. Aidha, Tume iliunda Mabaraza ya Katiba ya Wilaya na ya kitaasisi ili kutoa fursa kwa wananchi katika umoja wao kutoa maoni yao juu ya Rasimu ya Kwanza. Matokeo yake, Tume iliandaa Rasimu ya Pili ya Katiba ambayo iliwasilishwa katika Bunge Maalum na Mwenyekiti wa Tume, Jaji Warioba.

**Mheshimiwa Spika,** Vyombo vya habari mbali mbali hapa nchini vimemnukuu Waziri wa Fedha Mh. Saada Salum Mkuya akisema kwamba, hadi kuahirishwa kwake, Bunge Maalum limetumia zaidi ya Shilingi bilioni 27. Kama taarifa hizo ni za kweli itakuwa na maana kwamba katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, mchakato wa Katiba Mpya umetumia zaidi ya Shilingi bilioni 102. Hiki ni kiasi kikubwa mno cha fedha katika nchi ambayo shughuli mbali mbali za maendeleo na huduma za jamii zenye umuhimu mkubwa kwa ustawi wa wananchi zimekwama kwa kukosa fedha.

Hata hivyo, Mheshimiwa Spika, licha ya matumizi haya makubwa ya fedha za umma kwa ajili ya mchakato wa Katiba Mpya; na licha ya maneno ya Rais kwamba wajumbe wa Bunge Maalum wajadili Rasimu kwa hoja badala ya jazba, Rais Kikwete mwenyewe ndiye aliyeongoza mawaziri wake na viongozi wengine waandamizi na wajumbe wa CCM wa Bunge Maalum katika kujadili Rasimu kwa "… *kutukanana, kudharauliana, kushutumiana, kubezana, kuzomeana na kushinikizana.*"

Kauli na vitisho hivi vimetolewa hadharani sio ndani ya Ukumbi wa Bunge tu, bali pia hata katika nyumba za ibada bila kujali athari zake kwa jamii yetu yenye imani tofauti tofauti za kidini. Wajumbe wanaounda UKAWA wamekataa kuwa sehemu ya Bunge Maalum la aina hii na hawatarudi Bungeni hadi hapo dhima halisi ya Bunge hilo itakapopatiwa ufumbuzi.

Kama dhima hiyo itakuwa ni kutumia mwavuli wa Bunge Maalum ili kuendeleza mfumo wa kikatiba na muundo wa Muungano uliopo kwa sasa, basi wajumbe wa UKAWA hawatakuwa sehemu ya usaliti huo wa Watanzania. Hata hivyo, kama dhima ya Bunge Maalum itakuwa ni kujadili na kuboresha matakwa ya wananchi kama yalivyodhihirishwa na Rasimu ya Katiba na Taarifa ya Tume, basi wanachama wa UKAWA watakuwa tayari kurudi kwenye Bunge Maalum ili kuendelea na mjadala wa Rasimu hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Madai ya Katiba Mpya yana historia ndefu ikianzia miaka ya mwisho ya 1980. Mwaka 1990 Rais Ali Hassan Mwinyi aliunda Tume ya Rais ya Mfumo wa Chama Kimoja cha Siasa au Vyama Vingi iliyoongozwa na aliyekuwa Jaji Mkuu wa Tanzania, marehemu Francis Nyalali. Pamoja na mapendekezo mengine, Tume ya Nyalali ilipendekeza kutungwa kwa Katiba Mpya kwa ajili ya nchi yetu. Tume hiyo ilipendekeza pia muundo wa Muungano wa Serikali Tatu.

Baada ya mfumo wa siasa wa vyama vingi kurejeshwa mwaka 1992, vyama vya upinzani na makundi mbali mbali ya kijamii yaliendelea kudai kutungwa kwa Katiba Mpya. Hii ilitokana na kutoridhishwa na mfumo wa uchaguzi ambao haukuwa huru na wa haki, madaraka makubwa ya Rais, mfumo mzima wa usimamizi wa rasilimali za taifa pamoja na mapungufu mengi katika mifumo yetu ya utawala na uendeshaji wa Serikali.

Kwa kiasi kikubwa, mapendekezo ya Rasimu ya Katiba iliyowasilishwa na Tume yanakidhi mahitaji haya ya mabadiliko ya kimsingi katika mfumo wa utawala, usimamizi wa rasilimali za taifa na uendeshaji wa Serikali. Ni wazi, kwa hiyo, kwamba Rasimu hii inatoa fursa muhimu ya kutibu majeraha yetu kama taifa.

Kwa viongozi wa CCM, wakiongozwa na Rais Kikwete, kupotosha, kubeza na kukejeli mapendekezo haya ni kuthibitisha yale ambayo yaliwahi kusemwa na aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria Mh. Celina Kombani na baadaye kurudiwa na Mwanasheria Mkuu Mh. Frederick Werema kwamba Serikali ya CCM haioni haja ya kuwa na Katiba Mpya kwani iliyopo inatosha.

**Mheshimiwa Spika,** Tangu mchakato huu wa Katiba Mpya ulipoanza mwanzoni mwa 2011, CCM ilionyesha dalili zote za kutaka kuuteka na kuupotosha mchakato mzima. Suala la nafasi na ushiriki wa Zanzibar katika mchakato huu, na muundo wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba na utaratibu wa uteuzi wa wajumbe wa Tume yalikuwa masuala yaliyoleta mvutano mkubwa. Baadaye suala la muundo, idadi na utaratibu wa kuwapata wajumbe wa Bunge Maalum nayo yalileta mvutano mkubwa ndani na nje ya Bunge lako tukufu.

Hofu ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba CCM ingetumia mamlaka ya Rais ya uteuzi wa wajumbe wa Bunge Maalum kujaza makada wengi wa CCM katika Bunge hilo imethibitika kuwa ya kweli. Kwa utafiti wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kati ya wajumbe 201 wa Bunge Maalum walioteuliwa na Rais Kikwete, zaidi ya wajumbe 160 ni wanachama na viongozi wa CCM waliochomekwa kwenye Bunge Maalum kwa kutumia kivuli cha waganga wa kienyeji, taasisi za kidini, asasi za kiraia, taasisi za kitaaluma, watu wenye malengo yanayofanana, n.k. Ni dhahiri hatua hizi hasi zimechangia

kujenga mazingira ya kutokuaminiana na hivyo kuweka msingi mbaya kwa mchakato wenyewe.

**Mheshimiwa Spika,** Hata baada ya Bunge Maalum kuitishwa na kuanza kazi, CCM iliendelea kufanya hila za kuchakachua Kanuni za Bunge Maalum ili kupitisha hoja zao kirahisi. Hila hizo ziliposhindwa CCM ilitumia mabavu ya wazi kwa kulazimisha Mwenyekiti wake wa Taifa atumie kivuli cha Urais kusisitiza msimamo wa CCM na kutisha Wajumbe wa Bunge Maalumu kwamba wakipitisha muundo wa Serikali Tatu, kama ilivyopendekezwa na Tume aliyoiteua yeye mwenyewe, basi Jeshi la Wananchi wa Tanzania litapindua Serikali.

Hilo liliwezekana tu baada ya Mwenyekiti wa Bunge Maalumu kuchakachua Kanuni za Bunge Maalum ili kumwezesha Rais kuhutubia Bunge hilo baada ya Mwenyekiti wa Tume, kama njia ya kumwezesha Rais kuijibu Tume na kupinga Rasimu yake hadharani na kulazimisha maoni na msimamo wa CCM.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kadri ya ufahamu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, haijawahi kutokea kwa Mkuu wa Nchi na Amiri Jeshi Mkuu kuchochea jeshi lake kufanya mapinduzi ya kijeshi ili kuzuia matakwa ya wananchi juu ya Katiba Mpya kutekelezwa. Haijawahi kutokea kwa Rais na Mkuu wa Nchi kuwaasa wajumbe wa Bunge la Katiba kujadili hoja badala ya jazba halafu Rais na Mkuu wa Nchi huyo huyo kugeuka na kukejeli na kubeza Tume aliyoiteua yeye mwenyewe na hivyo kujenga mazingira ya wajumbe wa Bunge hilo "*… kutukanana, kudharauliana, kushutumiana, kubezana, kuzomeana na kushinikizana.*" Hapa ndipo CCM ilikoifikisha nchi yetu!

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji, kama Rais Kikwete hakuwa tayari kukubali maoni ya wananchi katika mchakato wa mabadiliko ya Katiba, kwa nini yeye na Serikali yake wameliingizia taifa hasara ya kutumia mabilioni ya fedha za walipa kodi wa Tanzania kugharamia mchakato wa Katiba Mpya ambao ni wazi yeye na chama chake hawako tayari kukubali matokeo yake?

**Mheshimiwa Spika,** Fedha zote zilizotumika kwa ajili ya gharama mbali mbali za Bunge Maalum hazikuidhinishwa na Bunge lako tukufu. Ukweli ni kwamba hadi sasa Bunge lako tukufu halijui bajeti yote ya Bunge Maalum, halijui fedha kiasi gani zimetumika kwa ajili ya matengenezo mbali mbali ya miundombinu ya Bunge hili, au kwa ajili ya posho, mishahara na stahili mbali mbali za wajumbe na watumishi wa Bunge Maalum hadi lilipoahirishwa tarehe 25 Aprili, 2014. Aidha, Bunge lako tukufu halina ufahamu wowote juu ya gharama za Bunge Maalum pale litakaporudi tarehe 5 Agosti, 2014, kuendelea kujadili Rasimu ya Katiba Mpya.

**Mheshimiwa Spika,** Bunge lako tukufu halina ufahamu huu kwa sababu, licha ya madai ya Wabunge, Serikali hii ya CCM haijawahi kuleta makadirio ya matumizi kwa ajili ya shughuli mbali mbali za Bunge Maalum. Mwaka jana wakati Bunge lako tukufu linajadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala iliagiza kwamba bajeti ya Bunge Maalum "… iletwe Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa." Agizo hilo la Bunge sio tu lilipuuzwa mwaka jana kwa Serikali hii ya CCM kutokuleta bajeti hiyo, bali hata mwaka huu agizo hilo limepuuzwa kwani bajeti ya Bunge Maalum haipo katika makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria!

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Mabadiliko ya Katiba inatamka wazi kwamba fedha zote zitakazogharamia mchakato wa Katiba Mpya zitatoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali. Ibara ya 136(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatamka kwamba *"fedha hazitatolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa ajili ya matumizi (isipokuwa) fedha hizo ziwe kwa ajili ya matumizi ambayo yameidhinishwa yatokane na fedha zilizomo katika Mfumo Mkuu wa Hazina ya Serikali na idhini hiyo iwe imetolewa na Katiba hii au Sheria nyingine yoyote; (na) fedha hizo ziwe kwa ajili ya matumizi ambayo yameidhinishwa ama na Sheria ya Matumizi ya Serikali iliyotungwa mahususi na Bunge au Sheria iliyotungwa kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 140 ya Katiba hii."*

Aidha, kwa mujibu wa ibara ya 136(3) ya Katiba, *"fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali hazitatolewa kutoka Mfuko huo kwa ajili ya matumizi ila mpaka matumizi hayo yawe yameidhinishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na pia kwa sharti kwamba fedha hizo ziwe zimetolewa kwa kufuata utaratibu uliowekwa kwa ajili hiyo kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge."*

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa vifungu tajwa vya Katiba, fedha kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Bunge Maalum zilitakiwa kuidhinishwa na Katiba au Sheria nyingine yoyote. Masharti haya yalitekelezwa kwa Bunge lako tukufu kutunga Sheria ya Mabadiliko ya Katiba iliyoidhinisha matumizi ya fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

Pili, fedha kwa ajili ya matumizi ya Bunge Maalum zilitakiwa kuidhinishwa na ama Sheria ya Matumizi ya Serikali iliyotungwa mahususi na Bunge au Sheria iliyotungwa kwa mujibu wa ibara ya 140 ya Katiba.

Ibara ya 140 inahusu Mfuko wa Matumizi ya Dharura unaoanzishwa kwa ajili ya mambo ya haraka na dharura ambayo hayakutazamiwa kutokea na ambayo hayakupangiwa fedha zozote za matumizi. Sharti hili halikutekelezwa.

Tatu, hata kama fedha za matumizi ya Bunge Maalum zingeidhinishwa kama inavyotakiwa na Katiba, bado matumizi hayo yalitakiwa kuidhinishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hili nalo halikutekelezwa.

Ukweli ni kwamba ingekuwa ajabu sana kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kuidhinisha matumizi ya fedha za Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali wakati matumizi hayo hayakuidhinishwa kwa mujibu wa Katiba.

Kwa sababu zote hizi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kupata majibu ya maswali yafuatayo:-

(i) Je, bajeti ya matumizi ya Bunge Maalum ni kiasi gani na kwa ajili ya matumizi gani?

(ii) Je, ni kiasi gani cha fedha hizo kimeshatumika hadi sasa na kwa ajili ya matumizi gani?

(iii) Je, ni nani aliyejadili na kupitisha bajeti hiyo?

(iv) Je, ni Sheria gani iliyotungwa na Bunge lipi iliyoidhinisha matumizi haya ya fedha za umma?

(v) Je, ni lini na kwa waraka gani Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliidhinisha matumizi haya?

**Mheshimiwa Spika,** Majibu ya maswali haya ni muhimu ili kuliepusha taifa letu na balaa la ufisadi na wizi mkubwa wa fedha za umma kama ilivyotokea mwaka 2005. Mwaka huo, kama inavyojulikana, mabilioni ya fedha za umma yaliibiwa kutoka katika akaunti ya kulipa madeni ya nje (EPA) ya Benki Kuu ya Tanzania kwa ajili ya kugharamia kampeni za Uchaguzi Mkuu za CCM na mgombea wake wa Urais. Makada wa CCM na viongozi waandamizi wa CCM na Serikali yake walishiriki katika ufisadi huo.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM itoe kauli rasmi mbele ya Bunge lako rasmi kuhusu giza hili lililogubika fedha za matumizi ya Bunge Maalum. Hii ni muhimu sio tu kwa sababu ni muhimu kuwa na uwazi katika matumizi ya fedha za umma, bali pia ili kuzuia wizi na ufisadi wa fedha za umma kwa kutumia kivuli cha mchakato wa Katiba Mpya ambao tayari umevurugwa na CCM, Serikali yake na viongozi wake waandamizi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mazingira ambayo Bunge Maalum limegeuzwa na CCM kuwa uwanja wa kuwazomea, kuwatukana, kuwatisha, kuwadhalilisha na kuwabagua kidini na kiasili yao, wajumbe wa Bunge hilo wanaotetea maudhui ya Rasimu ya Katiba iliyowasilishwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

Katika hali ambayo CCM imejaza makada wake ndani ya Bunge Maalum kwa kutumia kofia na vivuli mbali mbali vya kitaasisi ili kuhakikisha agenda yake ya kuendeleza mfumo wa kikatiba na muundo wa Muungano uliopo inatekelezwa.

Katika mazingira ambayo CCM inatumia wingi wake huo kupindua Rasimu ya Katiba iliyoandaliwa na Tume kufuatana na maoni ya wananchi. Katika hali ambayo wajumbe wa CCM katika Bunge Maalum wamebadilisha Kanuni za Bunge Maalum ili kuwawezesha kuchakachua maoni ya wananchi kama yalivyoakisiwa na Rasimu ya Tume, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuweka wazi msimamo wa wajumbe wake na wanachama wa UKAWA kwamba haitakuwa busara kwake kuendelea na mjadala wa Bunge Maalum wenye lengo la kupitisha mapendekezo ya kundi la viongozi wa CCM. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na wanachama wa UKAWA haiko tayari kuendelea kushiriki katika Bunge Maalum ambalo limejaa kauli za kibaguzi, kashfa, vijembe na matusi dhidi ya wajumbe wa UKAWA na dhidi ya wajumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, hasa Mwenyekiti wake Jaji Joseph Sinde Warioba.

**Mheshimiwa Spika,** Mjadala wowote utakaoendelea kuanzia sasa katika Bunge Maalum hautakuwa na uhalali wowote mbele ya macho ya Watanzania. Ni mchakato wa CCM, unaoendeshwa kwa fedha za umma na wanaCCM, kwa faida na matakwa ya CCM. Kinachoendelea sasa katika Bunge Maalum hakitajibu matatizo mbali mbali ya Muungano ambao umeigeuza Zanzibar kuwa koloni la Tanganyika na ambao umeivalisha Tanganyika joho la Jamhuri ya Muungano na ambao unatishia mahusiano kati ya wananchi wa nchi hizi mbili.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kwa niaba ya wanachama wa UKAWA, itaendeleza harakati za kudai Katiba Mpya yenye kujibu haja, matakwa na matumaini ya Watanzania walio wengi nje ya Bunge Maalum ambalo limetekwa nyara na CCM. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni itaendeleza harakati, nje ya Bunge Maalumu, zitakazowezesha kubadilishwa kwa muundo wa Muungano kwa kuivua Tanganyika koti la Muungano, kuipatia Zanzibar mamlaka kamili ndani ya Muungano na kujenga mahusiano ya hadhi na haki sawa baina ya Tanganyika na Zanzibar.

Kama ilivyoonekana wazi wakati wa mjadala katika Kamati mbali mbali za Bunge Maalum, licha ya kujaza makada na washirika wake, CCM haiwezi kupitisha matakwa yake ndani ya Bunge hilo kwa vile haiwezi kupata theluthi mbili ya idadi ya wajumbe wa kuiunga mkono kama inavyotakiwa na kifungu cha 26(1) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba na ibara ya 98(1) ya Katiba. Hii ndio sababu pekee iliyosababisha kuahirishwa kwa Bunge Maalum hadi mwezi Agosti ijayo bila ya kupiga kura ya maamuzi juu ya Sura za Kwanza na Sita za Rasimu zinazohusu muundo wa Muungano.

Kama CCM haijaweza kupata idadi ya wajumbe inayotakiwa na Sheria na Katiba ndani ya Bunge Maalum inayolitawala, itakuwa ni ndoto kupata idadi inayotakiwa na Sheria wakati wa kura ya maoni ya kuhalalisha Katiba Mpya isiyotokana na matakwa ya wananchi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawataka Watanzania wote wenye nia njema na nchi yetu, kujiandaa kwa ajili ya kura hiyo ili kuhakikisha kwamba ndoto na matumaini yao kuhusu Katiba Mpya hayapotezwi kutokana na hila za CCM na washirika wake.

## 2. KAULI ZA UCHOCHEZI NA UBAGUZI NJE YA BUNGE MAALUM

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kuhamisha mjadala wa Bunge Maalum la Katiba usijadili Rasimu ya Katiba iliyowasilishwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba na badala yake kujadili Rasimu ya Katiba ya Chama kimoja, CCM, nje ya Bunge Maalum, imeendeleza kauli za kichochezi na kibaguzi zinazoweza kuvunja amani.

Katika Mkutano wa Katibu Mkuu wa CCM Abdrahamani Kinana Unguja wa tarehe 4 Mei 2014, "Mnadhimu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar (BLW), Salmin Awadh Salmin ambaye ni Mjumbe wa Bunge maalum la Katiba, amesema wawakilishi wa CCM wanajiandaa kuwasilisha hoja binafsi kwenye Baraza hilo ili kuwapa nafasi wananchi waulizwe iwapo wanataka kuendelea na Serikali ya Umoja wa Kitaifa."

Madhumuni ya mchakato huo ni kuvunja serikali ya Umoja wa Kitaifa ambayo iliamuriwa iwepo na kura ya maoni ya Wazanzibari wote na imesaidia kuleta amani na utulivu Zanzibar.

Aidha, kauli ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Idd katika mkutano huo wa CCM kuwa Mhe. Ismail Jussa Ladhu, Mwakilishi wa Mji Mkongwe kuwa siyo raia wa Zanzibar ni ya kibaguzi, kichochezi na yenye kupandikiza chuki dhidi ya jamii watu wenye asili ya Kihindi. Ni kauli inayopaswa kulaaniwa na kilampenda amani popote alipo.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi rasmi ya Upinzani inapenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama hii sasa ndiyo Sera Mpya ya CCM na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuivunja Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar na kuibua hisia za ubaguzi?

Jeshi la Polisi lilishiriki katika mauaji yaliyotokea Zanzibar Januari 2001 na kwa mara ya kwanza kusababisha wakimbizi zaidi ya 2000 kutoka Zanzibar kwenda Kenya. Kauli za kuchochea kuivunja serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar zinatonesha vidonda na zinapandikiza mbegu ya chuki na vurugu inayoweza kusababisha maafa makubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Ikumbukwe Baraza la Wawakilishi kwa pamoja lilipeleka waraka kwenye Tume ya Mabadiliko ya Katiba na kupendekeza "kuwepo kwa mamlaka huru ya Zanzibar, mamlaka huru ya Tanganyika na mamlaka ya Muungano na iwekwe wazi maeneo, uwezo, nguvu, utendaji na mipaka ya kila mamlaka."

Kwa Kiswahili rahisi, mamlaka huru ya Zanzibar, mamlaka huru ya Tanganyika na mamlaka ya Muungano maana yake Serikali ya Zanzibar, Serikali ya Tanganyika na Serikali ya Muungano.

Kwa CCM na Serikali ya Muungano kuwabana Wawakilishi wa Zanzibar kubadilisha msimamo wao wakati wa Bunge maalum la Katiba ni kuendeleza taswira kuwa mambo ya Zanzibar yanaamuliwa Dodoma na kwa hiyo kuendelea kuudhoofisha Muungano.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mizunguko ya mikutano ya CCM na maandamano ya pikipiki kuhusiana na mchakato wa Katiba ndani ya Tanganyika na Zanzibar, kumeendelea kutolewa kauli za kutukana, kudhalilisha na hata kubeza viongozi mbalimbali wa vyama vingine na hata wasio na vyama wanaotofautiana kimsimamo au kimtazano na CCM.

**Mheshimiwa Spika,** Viongozi wa juu wa CCM na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanawajibika kukemea kauli hizi lakini hawafanyi hivyo na badala yake kuonekana ama kuzitoa, kuzikoleza au kuzishabikia bila kutathmini nafasi na wajibu wao wa kuliunganisha Taifa. Kitendo hiki siyo tu ni fedheha kwa Chama Tawala, bali ni ushuhuda wa aina gani ya viongozi tulio nao. Vikiruhusiwa kuendelea vitendo vya CCM vitaliingiza taifa letu katika mgogoro mkubwa wa kisiasa na hata maafa.

## 3. MCHAKATO WA KATIBA MPYA NA CHAGUZI ZA SERIKALI ZA MITAA NA UCHAGUZI MKUU WA 2015.

**Mheshimiwa Spika,** Iliyoonekana awali dhamira njema ya kupata Katiba aliyokuwa nayo Rais Jakaya Kikwete ilikuwa itupatie Katiba Mpya kwa Watanzania katika Mwaka 2014. Sheria ya Mabadiliko ya Katiba inalitaka Bunge Maalumu kujadili Rasimu ya Katiba Mpya na Maudhui yake kama iliyowasilishwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba na si vinginevyo.

Ni bahati mbaya kwamba, Rasimu ya Katiba Mpya imewekwa kando na mjadala wa katika Bunge Maalumu umejikita katika Mapendekezo ambayo hayamo katika Rasimu. Hali hii inapoteza uhalali wa Bunge Maalumu la Katiba, si tu kwa kuwa linakwenda kinyume na Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kifungu cha 25 lakini kwa sababu linakwenda kinyume na Matakwa ya wananchi

ambayo kwa ujumla wao yako katika Rasimu ya Katiba Mpya iliyowasilishwa na Tume.

**Mheshimiwa Spika,** Ni bahati mbaya zaidi kwamba baadhi ya wajumbe wa Bunge Maalumu la Katiba hasa kutoka kundi la walio wengi wamejivika jukumu lililokuwa la Tume ya Mabadiliko ya Katiba wakidai kupokea maoni mbadala ya wananchi, kitendo hiki ni kinyume na Sheria na ukiukwaji wa kiasi kikubwa wa haki ya wananchi ambao kwa ujumla wao walitoa maoni yao kwa Tume ya Katiba.

**Mheshimiwa Spika,** Nchi yetu inapaswa kuingia katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani Mwaka 2015. Ndoto ya Watanzania ilikuwa kutumia Katiba Mpya katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015.

Kama tutakwenda katika uchaguzi mkuu wa Mwakani bila Katiba Mpya tutaliingiza Taifa katika mgogoro mkubwa wa kikatiba yaani "Constitutional crisis" ambao utakuwa rahisi kuzaa machafuko haswa kipindi cha uchaguzi.

Katiba inayotumika sasa, Katiba ya Mwaka 1977, ina mapungufu mengi na haiwezi kutupatia uchaguzi ulio huru na wa haki katika mazingira ya sasa yanayojengwa na uzoefu wa chaguzi nne zilizopita chini ya mfumo wa vyama vingi.

**Mheshimiwa Spika,** Ni dhahiri vilevile kuwa kuna uwezekano mkubwa wa kufikia chaguzi zilizo mbele yetu bila kukamilisha upatikanaji wa katiba mpya yenye maridhiano. Kwa vyovyote vile, uhalali wa Katiba itakayokuwepo wakati huo wa uchaguzi ndiyo njia pekee ya kutokugeuza chaguzi za mbele kuwa kichocheo cha mpasuko mkubwa zaidi.

Tukienda katika Uchaguzi Mkuu Mwakani tukiwa katika mazingira tuliyonayo leo tutakwenda tukiwa tumegawika kama Taifa pengine kuliko wakati mwingine wowote katika historia ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kuna uwezekano mkubwa wa Uchaguzi Mkuu ujao wa 2015 kuwa chanzo cha machafuko makubwa ya kisiasa hapa nchini ikiwa Serikali itaendelea kupuuza mapendekezo ya marekebisho ya Sheria na Kanuni mbalimbali za Uchaguzi zilizolalamikiwa kwa muda mrefu.

Miongoni mwa mambo yaliyolalamikiwa na vyama vya siasa ni pamoja na daftari la kudumu la wapiga kura, marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi ya Mwaka 1985 ambayo imepitwa na wakati na hivyo kutokidhi mahitaji ya kisiasa ya sasa, na kuundwa kwa Tume Huru ya Uchaguzi.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na kutofanyika kwa marekebisho hayo, chaguzi zimekuwa zikifanywa kiholela bila utaratibu unaoeleweka kwa kutumia mwanya wa udhaifu au upungufu uliopo katika sheria na kanununi mbali mbali za uchaguzi ili mradi udhaifu au upungufu huo unakipa Chama cha Mapinduzi ushindi.

**Mheshimiwa Spika,** Mara kadhaa Serikali ilipoulizwa kuhusu marekebisho ya sheria na kanuni mbalimbali za uchaguzi imekuwa ikijibu kwamba tusubiri Katiba Mpya ambayo itatatua kero hizo. Ni kweli kwamba mchakato wa Katiba Mpya unaendelea, lakini umegubikwa na wingu zito la mivutano jambo ambalo ni kiashiria kimojawapo kwamba tunaweza tusipate Katiba Mpya kwa muda uliopangwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa kuna dalili na viashiria vya kutopata katiba mpya kabla ya uchaguzi mkuu wa 2015, na kwa kuwa hatutakuwa tayari kuingia katika uchaguzi mkuu kwa kutumia katiba ya sasa ambayo ndio chimbuko la matatizo ya ki-uchaguzi tuliyo nayo sasa; Hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza mbele ya Bunge hili ina mpango gani wa kuweka utaratibu wa mpito (transitional arrangements) kuelekea uchaguzi mkuu wa 2015 ikiwa uchaguzi huo utafanyika kabla ya Katiba Mpya kupatikana.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri kwa dhati kabisa kwamba, taratibu za mpito za kushughulikia masuala yote ya Uchaguzi Mkuu ziendelee kufanyika ili kama uchaguzi mkuu utafika kabla ya kuwa na katiba mpya basi kuwe na "fall-back position" ili kuinusuru nchi kuingia katika mtanziko ambao unaweza kuwa chanzo cha machafuko ya kisiasa.

**Mheshimiwa Spika,** Hatuwezi kuingia uchaguzi wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa kwa utaratibu uliopo leo.

Hatuwezi kwenda kwenye uchaguzi Mkuu mwakani na Tume ya Uchaguzi kama ilivyo leo ambayo haijawekewa vyombo vya kikatiba ikiwemo mifumo ya utendaji ambayo itahakikisha uhuru wa Tume unalindwa na haki kutendeka kwa wadau wote.

Hatuwezi tena kwenda kwenye Uchaguzi Mkuu mwakani wakati Matokeo ya Uchaguzi wa Rais hayawezi kuhojiwa Mahakamani na hoja ya mgombea huru haijapatiwa majibu. Hatuwezi kuingia katika uchaguzi ujao na daftari la wapiga kura lililopo leo.

Hatuwezi kulikubali daftari jipya litakalotengenezwa kama wadau wote hatutashirikishwa kikamilifu katika hatua zote za upatikanaji wake ikiwemo mifumo itakayotumika.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kurudia, Ni kweli, kama ilivyo kawaida, Serikali na CCM inaweza kupuuza tahadhari hizi na kulazimisha kwenda katika chaguzi hizi katika mazingira ambayo hayana muafaka kama inavyoonekana sasa katika Mchakato wa katiba Mpya.

## 3.1 UCHAGUZI WA SERIKALI ZA VITONGOJI, VIJIJI NA MITAA

**Mheshimiwa Spika;** Mwezi Machi 2014 Waziri Mkuu Mizengo Pinda alizungumza na vyombo vya habari na kueleza kwamba ameona dhahiri hatari ya kusogezwa mbele kwa Uchaguzi wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa kutoka Oktoba mwaka 2014 mpaka mwaka 2015.

Waziri Mkuu Pinda alieleza kwamba Uchaguzi huo ungesogezwa mbele kutoa nafasi kwa kazi zingine kuendelea hususan mchakato wa mabadiliko ya katiba. Waziri Mkuu Pinda alieleza kwamba angemwomba Rais Jakaya Kikwete kusogeza mbele uchaguzi huo.

Hata hivyo, wakati kauli hizo zikitolewa Kambi Rasmi ya Upinzani inazo taarifa kwamba maandalizi ya uchaguzi huo yanaendelea chini kwa chini kwa ajili ya uchaguzi huo kufanyika Oktoba mwaka 2014. Maandalizi hayo ni pamoja na mapitio ya Kanuni za Uchaguzi tajwa.

**Mheshimiwa Spika;** Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Waziri Mkuu alieleze Bunge iwapo aliwasilisha maombi husika kwa Rais na nini majibu juu ya hatma ya uchaguzi husika. Serikali inayotawaliwa na CCM inapaswa kuhakikisha kwamba inaheshimu maoni ya wananchi juu ya uchaguzi wa vitongoji, vijiji na mitaa ambapo wametaka mabadiliko makubwa ya taratibu za uchaguzi huo kupitia mchakato wa mabadiliko ya katiba.

Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kwamba Uchaguzi wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa na mfumo mzima wa Serikali za Mitaa sio mojawapo ya mambo ya Muungano. Hivyo, kwa kuzingatia rasimu kuwa iliyowasilishwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba katika Bunge Maalum imependekeza muundo wa Muungano wa Shirikisho lenye Serikali tatu, masuala ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa yanapaswa kuingizwa katika Katiba za Nchi Washirika za Tanganyika na Zanzibar.

Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya maamuzi na mabadiliko ya Kisheria kuwezesha uchaguzi huo kufanyika mapema baada ya mchakato wa mabadiliko ya Katiba kukamilika ili kuhakikisha kwamba Uchaguzi huo unakuwa huru na wa haki.

**Mheshimiwa Spika;** Izingatiwe kuwa chini ya sheria zetu, kanuni za chaguzi hizo hutungwa na Waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa na

Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Na kwa mujibu wa muundo wa sasa wa utawala wa Tanzania pamoja na kuwa na waziri wa nchi anayehusika na TAMISEMI, mwisho wa siku mwenye dhamana kamili ya "Wizara" hii ni Waziri Mkuu, ambaye kwa sasa ni Mheshimiwa Mizengo Pinda.

Itakumbukwa kwamba mwaka 2009 katikati ya mwezi Agosti baada ya kimya cha muda mrefu, kilichoambatana na shinikizo toka kwa wadau kutokana na serikali kuchelewesha kutoa kanuni tofauti na ahadi yake, hatimaye Waziri Mkuu Pinda kupitia Tangazo la Serikali (GN) namba 304 ya tarehe 21 Agosti 2009 alitoa kanuni na maelekezo kuhusu taratibu za uchaguzi husika yaliyotolewa kwa nyakati mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika;** Ifahamike kwamba mwanya huu wa kisheria wa Waziri kutunga kanuni ulitumiwa vibaya mwaka 2004 na kufanya kanuni hizo kutungwa kupendelea chama kinachotawala kwa kuweka mianya ya hujuma za kiuchaguzi. Matokeo yake ni uchaguzi uliopita wa vitongoji, vijiji na mitaa kutokuwa huru na haki kutokana na mapungufu mengi ambayo hata serikali yenyewe iliyakiri.

Mathalani upigaji kura haukuwa wa siri, fujo katika mikutano ya uchaguzi, matayarisho kuwa hafifu, kuingiliwa na maafisa na watendaji wa kata na vijiji ambao walifikia hatua ya kuwatisha wananchi na kutotoa taarifa za muhimu za uchaguzi, kukosekana kwa daftari la wapiga kura na uchaguzi kusimamiwa na chombo kisicho huru cha kiserikali moja kwa moja (Wizara ya TAMISEMI).

Kutokana na mapungufu hayo CCM ilishinda kwa asilimia 96 na kupata mtaji haramu wa kisiasa ambao ilianza nao kama hujuma katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2005 na kufanya uwanja wa ushindani wa kisiasa usiwe sawa. Na hivyo, CCM ikashinda kwa takribani asilimia 80 katika uchaguzi mkuu mwaka mmoja baadaye.

Lakini zaidi kutokana na hujuma hizo wananchi wakalazimishwa kuongozwa na viongozi wa vitongoji, vijiji na mitaa katika maeneo mengi wasio kuwa na uhalali wa kukubalika ambao wamekuwa kikwazo cha maendeleo na pia kusababisha migogoro ambayo ingeweza kuepukwa.

**Mheshimiwa Spika;** Ilitarajiwa kwamba marekebisho ya haraka yangefanyika, hata hivyo hakuna hatua za maana zilizochukuliwa kati ya mwaka 2005 mpaka 2008. Kesi iliyofunguliwa na vyama vya upinzani mwaka 2004 kuhusu kanuni na taratibu za uchaguzi wa vitongoji, vijiji na mitaa mpaka sasa ilibaki katika kizungumkuti. Kwa upande mwingine, Serikali ilikuwa ikiitisha mikutano na vyama na kuiahirisha bila maamuzi ya msingi kufikiwa kuhusu marekebisho yanayostahili kufanywa katika sheria na kanuni zinazosimamia

chaguzi husika, hali ambayo imeanza kujirudia tena kati ya mwaka 2011 na 2014.

**Mheshimiwa Spika;** Mwaka 2009, mwezi Februari ndipo serikali imesaini makubaliano na wadau kuhusu uchaguzi huu. Kwa kisingizio cha ufinyu wa muda, masuala ya msingi yaliyopaswa kufanyiwa marekebisho mengi hayapo kama sehemu ya makubaliano hayo. Kwa mara nyingine tena, serikali ilichelewesha muda na baadaye kutumia kisingizio cha muda kukwepa kufanya mabadiliko ya msingi ya kisheria ya kuhakikisha uchaguzi huu unakuwa huru na wa haki.

Kama ilivyotarajiwa kutokana na makubaliano hayo, yafuatayo iliamuliwe yasifanyiwe marekebisho kutokana na sababu mbalimbali zilizotolewa na serikali ikiwemo ufinyu wa muda. Kuhusu kilio cha miaka mingi cha wadau cha kutaka uchaguzi usimamiwe na Tume ya uchaguzi kama ilivyo katika baadhi ya nchi nyingine duniani; makubaliano yaliweka bayana kuwa uchaguzi utaendelea kusimamiwa na serikali kupitia waziri mwenye dhamana ya serikali za mitaa. Ndio maana kanuni ziliendelea kutungwa na waziri badala ya chombo huru. Katika kanuni hizo umri wa kugombea; umebaki kuwa miaka 21 badala ya kushuka mpaka 18. Wagombea binafsi; hawakuruhusiwa.

**Mheshimiwa Spika;** Mwito wa Vyama vya siasa kutaka viwezeshwe kutoa elimu ya uraia nao haukuzingatiwa. Serikali iliendelea kuweka msimamo kupitia maelekezo ya taratibu za uchaguzi husika kuwa jukumu la kutoa elimu ya uraia litaendelea kuwa la serikali.

Hoja ya kutaka uchaguzi wa madiwani uende sambamba na chaguzi zingine za mitaa nayo haikuwepo katika kanuni zilizotolewa na Waziri Mkuu Pinda. Uchaguzi wa madiwani uliendelea kuwa na uchaguzi mkuu mwaka 2010; hii ni kwa sababu suala hili linahitaji marekebisho ya kisheria na serikali ilishatamka wazi kwamba muda umeshakwisha wa kufanya marekebisho husika. Haya ni masuala nyeti ambayo wadau wengi walipenda yafanyiwe marekebisho lakini hakuna mabadiliko yoyote ambayo Serikali iliyafanya kuhusu masuala hayo katika kanuni zilizotungwa ambazo Waziri Mkuu Pinda alizitangaza.

**Mheshimiwa Spika;** Matokeo yake ni kuwa Waziri Mkuu Pinda na ofisi yake kuandaa Kanuni na taratibu za uchaguzi wa vitongoji na mitaa zilizo kinyume na misingi ya chaguzi huru na haki ambayo ni mhimili wa utawala bora. Ama kwa hakika mambo haya yanahitaji kutazamwa kwa kina na kwa haraka na wadau wowote ili kuepuka hali hiyo kujiridua na hivyo chaguzi za ngazi hiyo kugubikwa na vurugu zenye kutishia amani na demokrasia.

**Mheshimiwa Spika;** Kasoro hizo ni pamoja na kanuni kuelekeza kwamba karatasi za kura kutokuwa na majina ya wagombea na kwamba mpiga kura alilazimika kuandika mwenyewe. Hali ilichochea kuchelewa ama kuvurugika kwa mchakato wa upigaji na uhesabuji wa kura katika maeneo mengi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika nchi ambayo takribani nusu ya wananchi wake hawajui kusoma na kuandika na sehemu kubwa ya wanaojua bado si kwa kiwango kizuri, uamuzi wa kutunga kanuni ambazo zinalazimisha kwamba wapiga kura waandike wenyewe majina kamili ya wagombea ulitoa mianya ya kuvurugika kwa uchaguzi na ukijirudia tena utasababisha athari zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Baadhi ya upungufu Ofisi ya Waziri Mkuu iliukiri mnamo 11 Septemba 2009 kupitia barua yenye kumbukumbu Na. HB.114/126/01 kwamba maelekezo ambayo iliyatoa yalikiuka kanuni.

Mathalani, maelekezo yalisema wajumbe wa Halmashauri ya vijiji wanawake wa viti maalum watakuwa si chini ya 25%. Wakati ambapo Sheria Na. 19 ya mwaka 2009 inatamka kwamba idadi ya wanawake viti maalum katika halmashauri ya kijiji inatakiwa kuwa si chi ya theluthi moja ya wajumbe ambayo kwa vyovyote vile sio chini ya wanawake nane(8).

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwingine maelekezo ya uchaguzi yaliyotolewa na Waziri Mkuu Pinda yalipingana na kanuni ambazo ofisi yake imezitoa kuhusiana na dhamana ya wagombea. Kanuni zitaka mgombea awe amedhaminiwa na chama cha siasa. Hata hivyo, katika maelekezo Ofisi ya Waziri Mkuu imekwenda mbali zaidi kwa kuongeza maneno mengine ambayo hayapo kabisa kwenye kanuni ya kwamba mgombea lazima awe amedhaminiwa na 'ngazi ya chini kabisa ya chama chake'.

Maelekezo hayo yalipingana kabisa na katiba za vyama shiriki ambazo zinaeleza bayana ni ngazi zipi zenye mamlaka ya kudhamini wagombea. Maelekezo hayo potofu yalitumika kuwawekea pingamizi wagombea wengi wa upinzani na kusababisha waenguliwe.

**Mheshimiwa Spika,** Izingatiwe kuwa mfumo wa utawala wa nchi yetu unaanzia katika vitongoji, vijiji na mitaa ambayo ina mamlaka kadhaa ya kiutendaji na kimaamuzi.

Kuruhusu uchaguzi huu kuvurugika ama kuleta viongozi wabovu, kama taifa tutakuwa tumeweka msingi legelege wa utawala na demokrasia na athari zake zitaonekana katika kukwama kwa jitihada za kimaendeleo.

**3.2 TUME HURU YA UCHAGUZI NA MABORESHO YA DAFTARI LA WAPIGA KURA.**

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilieleza kwa kirefu jinsi ambavyo serikali ina dhamira ovu dhidi ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, na hivyo inapoka haki za kikatiba za wananchi waliotimiza masharti ya kupiga kura ambao inakataa kuwaandikisha ili wasipige kura.

Aidha Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilionyesha bayana jinsi ambavyo ilijitahidi kumuuliza Waziri Mkuu maswali bungeni juu ya suala hili, na Waziri Mkuu mara zote alionekana kutoa majibu ya jumla ambayo hayakukidhi haja ya tatatizo.

**Mheshimiwa Spika,** Ikumbukwe kwamba tangu uchaguzi mkuu wa 2010, kumefanyika chaguzi ndogo takribani nne za Ubunge katika Majimbo ya Igunga - Tabora, Arumeru Mashariki - Arusha, Kalenga – Iringa, na Chalinze mkoani Pwani. Aidha, zimefanyika chaguzi za marudio za madiwani takribani 90 katika kata kadhaa hapa nchini kwa sababu mbalimbali. Katika chaguzi hizi, daftari la Kudumu la Wapigakura halikufanyiwa marekebisho na hivyo kuwanyima wananchi wengi waliokuwa na sifa ya kuandikishwa na kupiga kura haki ya kushiriki katika chaguzi hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Licha ya wapiga kura waliotimiza masharti ya kupiga kura kunyimwa haki hiyo ya kikatiba kwa kutoboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura; jambo hili pia limesababisa migogoro isiyo ya lazima baina ya vyama vilivyoshiriki katika chaguzi hizo na tume ya uchaguzi.

Katika chaguzi zote hizo za marudio; wastani wa waliojitokeza kupiga kura hawakufika asilimia 30 na hivyo kusababisha manung'uniko kuwa Tume ya Uchaguzi inashirikiana na Serikali na Chama Cha Mapinduzi kuzuia walio wengi kutokupiga kura kwa maslahi ya CCM.

Hadi leo, siyo Tume wala Serikali imeweza kutoa sababu za msingi za wapiga kura wengi kiasi cha wastani wa asilimia 70 kutokuweza kujitokeza na kupiga kura achilia mbali wale ambao hawajaandikishwa kabisa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Kambi Rasmi ya Upinzani imeshasema vya kutosha kuhusu uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura; na kwa kuwa Serikali haionyeshi umakini, kujali na dhamira ya dhati ya kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga kura kwa kuwa chaguzi zote za marudio zilizofanyika baada ya mwaka 2010 zimefanyika bila daftarti la wapiga kura kufanyiwa maboresho, jambo ambalo limewanyima wananchi wengi haki ya kupiga kura; na kwa kuwa kufanya chaguzi bila kuboresha daftari la wapiga kura kunafanya chaguzi hizo kukosa sifa ya kuwa huru na za haki; hivyo basi; Kambi Rasmi ya

Upinzani inaitaka Serikali kufanya mambo yafuatayo kabla ya uchaguzi mkuu ujao:

(i) Kutoa Ratiba Rasmi ya Maboresho ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika Bunge hili;

(ii) Kuleta marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi ili kuondoa ukomo wa kuboresha Daftari la Kudumu la Wapigakura (wa mara mbili kwa kipindi cha miaka mitano) na badala yake daftari hilo liwe huru wakati wote kuandikisha wapigakura wapya wanaotimiza masharti ya kupiga kura na kuingiza marekebisho ya taarifa za wapigakura wengine;

iii. Kutenga Bajeti Maalumu kwa ajili ya Maboresho ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura; na

iv. Kupanga Ratiba yenye kutoa muda wa kutosha wa Uhamasishaji wa wananchi kujiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

### 3.3 UANDIKISHAJI WA WATU KWENYE DAFTARI LA URAIA UNAOFANYWA KINYEMELA NA MABALOZI WA NYUMBA KUMI WA CCM

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepata taarifa kwamba mabalozi wa nyumba kumi wa CCM wanafanya zoezi la uandikishaji wa wananchi kwenye kitu kinachoitwa Daftari la Uraia. Uandikishaji huu unafanyika kinyemela na unaonekana kuwa na baraka za Serikali kwa kuwa fomu za usajili zinatolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa tulizozipata ni kwamba Daftari hilo ndio linategemewa kutumika katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa na pia litatumika katika uandikishaji wa wananchi kwenye Datari la Kudumu la Wapiga kura.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani imeshtushwa sana na usajili huu kwa kuwa haufanywi na NIDA wala tume ya Taifa ya Uchaguzi ambazo ndizo Mamlaka halali kisheria kufanya usajili ama kwa lengo la Vitambulisho vya Taifa au kwa ajili ya Wapiga kura. Tumeshtushwa zaidi kwa sababu kwa taarifa tulizopata, usajili huo unafanyika kibaguzi kwa kuwaruka wananchi ambao ni wa vyama vya upinzani.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Waziri Mkuu atoe maelezo mbele ya Bunge hili kuwa ni nani aliyeamuru usajili huo ufanyike na ni kwa malengo gani.

## 3.4 UANDIKISHAJI WA WAPIGA KURA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA YA BIOMETRIC (BIOMETRIC VOTER REGISTRATION)

**Mheshimiwa Spika,** Katika hotuba yangu nilipowasilisha bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa mwaka wa fedha 2013/2014 nilisema kwamba; "kuna mchakato wa maandalizi ya siri unaoendeshwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) wa kuandaa utambuzi wa wapiga kura kwa kutumia mfumo wa "biometric" kwa maana ya kumtambua mpiga kura kwa alama za mwili kama alama za vidole na au mboni ya jicho kama sehemu ya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu ujao wa 2015".

Kwa mujibu wa taarifa tulizokuwa nazo wakati ule, ni kwamba tayari Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilishaanza maandalizi mengi ya msingi bila kushirikisha wadau, hasa vyama vya Siasa, isipokuwa CCM.

**Mheshimiwa Spika,** Nilieleza pia kuwa teknolojia hii kwa siku za karibuni imetumika katika chaguzi nchini Ghana na Kenya. Kote huko, ilifeli, na chupuchupu iingize mataifa hayo katika vurugu kubwa za uchaguzi. Mataifa haya yalilazimika kurudia mfumo wa upigaji na kuhesabu kura kwa mkono, hali iliyosababisha hofu kubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Niliweka bayana pia kwamba, si kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani haiafiki matumizi ya teknolojia mpya kurahisisha na kuboresha mfumo mzima wa uchaguzi katika nchi yetu, bali inatambua athari kubwa zinazoweza kutokea siku za usoni kama suala lilil "sensitive" namna hii halitafanywa katika misingi ya uwazi na ushirikishwaji wadau muhimu kama vyama vya siasa katika hatua zote la tangu awali kabisa.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na sababu hizo, tuliitaka Serikali kutoa maelezo ya kina kuwa ni sheria gani iliyotungwa na bunge inayoruhusu uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura kwa mfumo huu wa "biometric" na pia ni bajeti ipi inatumika kutekeleza mpango huo. Aidha, tulihoji ni kwa nini mpango huo unafanyika kwa siri bila wadau wa siasa nchini kushirikishwa na kutoa baraka zao juu ya mpango huo.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na tahadhari zote tulizotoa hususan ushirikishwaji wa wadau katika kwanza kuifahamu hiyo "Biometric Voter Registration – BVR" na kuiridhia, Tume bado imeendelea kutenga wadau hususan Vyama vya Upinzani na kuendelea kushirikiana na Serikali ya CCM katika kuielewa BVR, kutengeneza mifumo yake ikiwemo zabuni za ununuzi wa vifaa na mifumo yake ya uendeshaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kumekuwepo na ucheleweshaji mkubwa wa utekelezaji wa mfumo huu. Miongoni mwa sababu kuu ni kunyukana kwa

makundi ndani ya Serikali, Tume ya Uchaguzi na wazabuni katika kugombea fursa za kuuza mifumo hii mipya ya BVR.

Vigogo ndani ya Serikali wamekuwa sehemu ya kuchelewesha mpango huu kwa zaidi ya mwaka sasa. Japo kwa mwonekano wa haraka kutoka kwa PPRA yaani Mamlaka ya Uthibiti wa manunuzi ya Umma, Taifa litaaminishwa kuwa rufaa kadhaa kuhusiana na kandarasi ya BVR inatokana na ushindani miongoni mwa Wazabuni, ukweli unaofichwa ni kuwa nyuma ya wazabuni hawa wako Vigogo wa Serikali na Familia zao

**Mheshimiwa Spika,** Mazingira haya ni viashiria tosha vya uwepo wa uwezekano wa ufisadi mkubwa tena wa kutisha katika mfumo huu wenye malengo maovu makuu mawili:-

(i) Lengo la kutengeneza mfumo wenye usiri mkubwa utakaowezesha uchakachuaji wa kitaalam wakati wa uchaguzi; na

(ii) Lengo la baadhi ya vigogo kutengeneza mabilioni ya fedha kupitia mradi huu.

**Mheshimiwa spika,** Kwa kuzingatia unyeti wa zoezi hili kwamba linaweza kuiingiza nchi katika machafuko makubwa, Kambi rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iweke wazi mchakato mzima wa wazabuni na gharama halisi za mfumo huu sambamba na Makampuni yote yaliyohusika na ambayo bado yana wahusika katika zabuni hii ikiwemo sifa ya kila mzabuni.

Kama serikali itashindwa kuweka wazi swala hili, basi Kambi rasmi ya Upinzani itatangaza mgogoro na zoezi zima hadi hapo uwazi (transparency) na ushirikishwaji utakopokuwa dhahiri.

**3.5 UTAWALA BORA NA UWAJIBIKAJI WA KISIASA NA KIUTENDAJI**

**Mheshimiwa Spika,** Utawala bora ni pamoja na kutenda mambo kwa haki na kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizowekwa kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa shughuli kiutawala. Aidha, kudumisha demokrasia kunachagiza sifa za utawala bora.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa muda unaozidi mwaka mmoja sasa, kumekuwa na zuio la vyama vya upinzani kufanya shughuli zake katika mikoa ya Lindi na Mtwara kwa kisingizio cha vurugu za zilizotokea mwaka jana wakati wananchi wakikataa bomba la gesi kujengwa kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam.

**Mheshimwa Spika,** Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Rais ndiye mwenye mamlaka ya kutangaza hali ya hatari katika nchi au katika sehemu ya nchi.

Kwa kuzingatia hali iliyopo Mtwara na Lindi kwa sasa ni wazi kuwa inaonekana kuna hali ya hatari ambayo imetangazwa kimya kimya kwa vyama kuzuiwa kufanya shughuli za kisiasa huku kukiwa na ushahidi kuwa Chama tawala - CCM wanaendelea kufanya mikutano yao katika maeneo hayo kama kawaida.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kwaamba huu ni ubaguzi wa wazi kabisa baina ya CCM na vyama vingine vya upinzani na ni ukiukwaji mkubwa wa misingi ya utawala bora katika nchi. Hivyo, inamtaka Waziri Mkuu kutoa kauli hapa Bungeni kuwa ni nani aliyetangaza hali hiyo ya hatari katika mikoa ya Lindi na Mtwara kiasi cha kuzuia shughuli za siasa katika mikoa hiyo na ni sheria ipi imetumika kukandamiza haki ya demokrasia kwa kipindi kirefu hivyo cha muda wakati vurugu zilizotokea Mtwara na Lindi zilishakwisha.

**Mheshimiwa Spika,** Ni vyema ikaeleweka kuwa hitaji la kumtaka kiongozi wa kisiasa kuchukua hatua za uwajibikaji wa kisiasa, pale jambo linalosababishwa na uzembe wa ama yeye binafsi, watumishi walio chini ya mamlaka yake na hata mfumo anaousimamia, siyo jambo la chuki binafsi; bali ni kielelezo cha uongozi unaojali na kujutia, madhila yaliyosababishwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikipiga kelele ikiwataka mawaziri na watendaji wengine waandamizi wa Serikali hii kuwajibika kwa kujiuzulu kwa kushindwa kutimiza wajibu wao wa kusimamia vyema kazi za Serikali lakini kumekua na uzito mkubwa kuukubali utamaduni huu wa uongozi jambo ambalo limesababisha maovu kuendelea kufanyika na hivyo kuathiri ustawi wa Taifa.

## 3.6 OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA

**Mheshimiwa Spika,** Kwa nyakati mbalimbali kuanzia wakati wa Uchaguzi wa mwaka 2005 tumekuwa tukieleza kwamba Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na Mamlaka zingine zinazohusika za Serikali zimeshindwa kushughulikia matumizi ya fedha haramu kwenye siasa na fedha za umma zinazochotwa kifisadi kwa ajili ya kufadhili kampeni za CCM.

**Mheshimiwa Spika,** Ufisadi huo ulihusisha makampuni mbalimbali ambayo yalitumika kupitishia fedha zilizokwenda kwa baadhi ya wagombea na viongozi wa CCM. Aidha, Ufisadi huo ulifikia kilele chake pale ilipoelezwa hadharani

namna ambavyo Fedha hizo zilifadhili pia Kampeni za chama chenyewe cha CCM na mgombea wake wa Urais Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete.

Kama sehemu ya kudhibiti hali hiyo tukataka vile vile Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) aanze kukagua hesabu za vyama vya siasa. Hatimaye pamoja na sheria kumpa CAG uwezo wa kukagua hesabu za vyama vya siasa jukumu hilo halikutekelezwa kwa muda mrefu kwa sababu ambazo zilitokana na serikali kushindwa kutimiza wajibu wake kwa makusudi au kutokuona umuhimu wake.

**Mheshimiwa Spika;** kila wakati vyama vilivyotaka kukaguliwa CAG alivijulisha hakuwa na rasilimali za kuweza kutekeleza jukumu hilo.

Ni kwa bahati mbaya hata Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali na mashirika ya umma ilipofuatilia utekelezaji wa jukumu hilo ilishindwa kubainisha wazi kuwa kikwazo kilikuwa ni serikali na si vyama vya siasa.

Tunashukuru kwamba hatimaye sasa CAG amekagua hesabu za vyama vya siasa na tunatumaini kwamba amefanya hivyo kwa vyama vyote.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inataka hakikisho kutoka kwa Waziri Mkuu kwamba zoezi hilo litakuwa endelevu na hakutatokea tena taarifa kutoka kwa Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwamba ameshindwa kukagua mahesabu ya vyama vyote vya siasa kwa madai ya kukosa fedha au ufinyu wa bajeti.

Aidha, ukaguzi huu ni lazima uweke mkazo katika kufuatilia matumizi yote sio ya ruzuku pekee kwa kuzingatia kiwango cha matumizi makubwa ya fedha yanayofanywa hususan na CCM katika uendeshaji wa chama na katika kampeni za chaguzi ziada ya ruzuku ambayo chama hicho na vingine vinapokea.

Historia ya mapato yasiyojulikana vyanzo vyake wakati wa uchaguzi haipaswi kujirudia tunapoelekea kampeni za nchi nzima za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Kura ya Maoni ya Mabadiliko ya Katiba na Uchaguzi Mkuu wa Udiwani, Ubunge na Urais wa mwaka 2015.

**Mheshimiwa Spika,** Msajili wa Vyama vya siasa ana wajibu pia wa kudumisha mahusiano na vyama alivyovisajili. Tunatambua kwamba Baraza la Vyama vya siasa ni kati ya vyombo vyenye kuwezesha kukutana na kujadiliana. Hata hivyo, vipo vyombo vingine vyenye wajibu wa kuvikutanisha vyama vya siasa kuwezesha majadiliano yenye kuleta muafaka katika masuala mbalimbali.

Kati ya vyombo hivyo ni pamoja na Taasisi ya Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD) kilichoanzishwa na Vyama vyenye wabunge na kinachoshirikisha vile vile vyama visivyo na wabunge kwa lengo la kuvikutanisha bila kujadili tofauti za kisiasa katika masuala yenye maslahi mapana kwa Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi kama TCD zipo pia katika baadhi ya Nchi nyingine na kwa kutambua wajibu wa Taasisi hizo Serikali zao huzipatia ruzuku toka fedha za umma kuziwezesha kutekeleza wajibu unaochangia katika kukuza demokrasia na mustakabali mwema wa kisiasa katika nchi hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuthamini nafasi ya TCD katika muktadha huo Rais aliagiza kwamba Taasisi hiyo iweze kupatiwa ruzuku kutoka kwa Serikali. Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ikasaini Hati ya Maelewano (MOU) na TCD hata hivyo utekelezaji wa makubaliano hayo umekuwa ni wa kusuasua. Jambo hili Waziri Mkuu unalifahamu kwa undani, hivyo wakati umefika sasa wa kutoa kauli Bungeni sababu za utekelezaji huo kukwama.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, ni vizuri Vyama na wadau wa demokrasia wakaelezwa wazi kupitia majumuisho ya Mapito ya Utekelezaji wa Ofisi ya Waziri Mkuu kiasi cha ruzuku kilichotolewa kwa mwaka wa fedha 2013/2014 nje ya mchango wa matukio.

Pia, kiwango cha ruzuku kinachokusudiwa kutolewa kwa mwaka wa fedha 2014/2015 badala ya kusubiri tu mahitaji ya kuvikutanisha vyama yanapotokea masuala yanayohitaji maridhiano ndio umuhimu wa TCD unapoonekana.

Kwa upande mwingine Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa nayo inapaswa kuongezewa wataalamu na fedha iweze kuwa Kituo-Rasilimali kwa Vyama Vya Siasa (Political Parties Resource Centre) ili ilishiriki kikamilifu katika kuvijengea uwezo vyama na kuchangia katika maendeleo ya kisiasa yenye mchango katika uchumi wa nchi na ustawi wa wananchi.

## 4. GHARAMA ZA UENDESHAJI WA SERIKALI

**Mheshimiwa Spika,** Nitazungumzia gharama za uendeshaji wa Serikali katika muktadha wa Rasimu ya Katiba inayotokana na maoni ya wananchi ambayo inapendekeza mfumo wa Serikali Tatu.

Katika mjadala wa sura ya 1 na 6 ya Rasimu ya Katiba hoja kubwa iliyokuwa ikitumiwa na CCM na mawakala wao kupinga maoni ya wananchi ya mfumo wa Serikali tatu na kupenyeza ajenda yao ya Serikali Mbili ilikuwa ni kwamba mfumo wa Serikali tatu utaongeza gharama za uedeshaji wa Serikali na kwa maana hiyo utaongeza mzigo kwa wananchi ambao ni walipa kodi.

**Mheshimiwa Spika,** Licha ya Tume ya mabadiliko ya Katiba kufanya utafiti wa kina na kupendekeza Serikali ndogo ya Shirikisho na taasisi chache za Muungano ambazo gharama zake ni ndogo kuliko mfumo wa Serikali mbili tulio nao sasa, bado CCM na mawakala wao wameendelea kueneza propaganda miongoni mwa wananchi kuwa Serikali tatu zitakuwa mzigo mkubwa kwa wananchi jambo ambalo si kweli hata kidogo.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo la kushangaza sana Serikali hii hii inayopinga Serikali Tatu kwa kisingizio cha gharama kubwa ndio inayoendelea kugawa mikoa na wilaya za nchi yetu kila kukicha na hivyo kuongeza gharama za uendeshaji wa Serikali mara dufu kuliko ambavyo ingekuwa kwa uendeshaji wa Seriakali ya Shirikisho la Serikali Tatu zinazopendekezwa kwenye Rasimu ya Katiba.

**Mheshimiwa Spika,** Kama Serikali ingekuwa inajali gharama basi ingekuwa inafanyia kazi mapendekezo ya Kambi ya Upinzani tangu mwaka 2010 ambapo tuliishauri kupunguza matumizi ya kawaida na kuongeza fedha katika miradi ya Maendeleo.

Aidha, Serikali ingeacha kuendelea kugawa mikoa na Wilaya kwani kwa kufanya hivyo ni kuongeza gharama za uendeshaji wa Serikali. Ni jambo la ajaba kabisa kwamba kwa jinsi Serikali hii isivyojali gharama za uendeshaji wa Serikali, hata Kata ya Mbagala sasa inapendekezwa kuwa Wilaya Mpya!!!

Ofisi ya Waziri Mkuu imeshindwa kumshauri Rais juu ya ugawaji wa Mikoa na Wilaya, matokeo yake kila kukicha tunajenga Makao Makuu ya Wilaya na Mikoa wakati fedha hizo tungeweza kuzielekeza kwenye miradi ya Maendeleo na huduma za jamii kama vile shule, hospitali nk.

**Mheshimiwa Spika,** Ili kudhihirisha kwamba Serikali haina uchungu na gharama za uendeshaji wa Serikali na kwamba inatumia kivuli cha gharama ili kupinga maoni ya wananchi ya Serikali Tatu katika Rasimu ya Katiba.

Katika bajeti ya shilingi trilioni 19.6 kwa mwaka huu wa fedha 2014/2015, shilingi trilioni 14.2 sawa na asilimia 72.4 ni matumizi ya kawaida (ya uendeshaji wa Serikali) wakati shilingi trilioni 5.4 sawa na asilimia 27.5 tu ndio bajeti ya Maendeleo. Fedha za maendeleo zilizotengwa hazifikii asilimia 35 ya bajeti yote kama ambavyo Mpango wa Maendeleo wa Miaka mitano unavyoelekeza.

## 5. MATUMIZI MABAYA YA VYOMBO VYA HABARI VYA UMMA

**Mheshimiwa Spika,** Vyombo vya Habari vya Umma ni mali ya wananchi wote bila kujali itakadi zao za kisiasa wala imani zao za kidini. Vyombo hivi

vinatumia kodi ya wanachi na hivyo vinawajibika kutoa habari kwa wananchi wote bila ubaguzi wowote.

**Mheshimiwa Spika,** Licha ya wajibu wa kutoa habari kwa usawa na bila upendeleo kuwa ni wajibu wa kikatiba, vyombo vya habari vya umma kwa mfano Kituo cha Televisioni cha Taifa (TBC1), Redio ya Taifa (TBC Taifa), na hata Magazeti ya Serikali husan Daily News na Habari Leo, vimekuwa vikitumika kutetea misimamo na mitazamo ya upande mmoja wa Chama cha CCM, na kuvinyima fursa vyama vyenye mitazamo tofauti.

Hii ni kwa sababu Serikali na hata baadhi ya viongozi wa CCM wamekuwa wanaingilia masuala ya uhariri wa vyombo hivyo, kiasi cha wasimamizi wa vyombo kudhani wanaendesha vyombo vya CCM. Haya ni matumizi mabaya ya kodi za wananchi zinazoendesha vyombo hivyo, na ni dhuluma kwa wananchi wanaopaswa kuhudumiwa na vyombo hivyo kwa usawa bila kujali tofauti za kiitikadi, za kijamii au za kidini.

**Mheshimiwa Spika,** Vyombo vya habari vya Umma vimekuwa na tabia ya kutoa habari chanya kwa upande wa Serikali na CCM lakini vimekuwa vikitoa habari hasi kwa upande wa Upinzani na mara nyingine kutotangaza kabisa habari chanya zinazotokana na kazi nzuri ya Upinzani. Jambo hili liliwahi kulalamikiwa na Kambi Rasmi ya Upinzani lakini bado ubaguzi katika kutoa habari unaendelea.

**Mheshimiwa Spika,** Mfano hai wa ubaguzi unaofanya na vyombo vya habari vya umma ni pale ambapo Kituo cha Television cha Taifa (TBC1) na Redio ya Taifa, TBC –Taifa vilipokatikasha matangazo yake ya moja kwa moja ya Bunge Maalum la Katiba wakati Mjumbe wa Bunge Maalum anayetokana na chama cha Upinzani Mheshimiwa Tundu Lissu alipokuwa akitoa ufafanuzi wa maoni ya Wachache.

**Mheshimiwa Spika,** Sababu iliyotolewa kwamba kulikuwa na matatizo ya kiufundi haina mashiko kwa kuwa kituo cha Television cha Taifa kiliendelea kurusha matangazo mengine jambo linalothibitisha kwamba kulikuwa hakuna tatizo la kiufundi.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani ilipata taarifa kwamba watendaji wa TBC1 na TBC Taifa walipata maelekezo kutoka kwa Waziri wa Habari, Vijana Michezo na Utamaduni kwamba wakatishe matangazo ya moja kwa moja ya Bunge Maalum wakati Mheshimiwa Tundu Lissu akiwasilisha maoni ya wachache.

Tunaitaka Serikali ilieleze Bunge hili ni kwa nini inaelekeza vyombo vya habari vya umma kufanya kazi kwa ubaguzi ilhali vyombo hivyo vinatumia fedha za walipa kodi wa nchi hii.

## 6. UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI

### 6.1 UWEKEZAJI

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Ripoti ya Ufanyaji Biashara ya Benki ya Dunia ya mwaka 2014 inaonesha kuwa Tanzania imeporomoka kutoka nafasi ya 136 mwaka 2013 hadi nafasi ya 145 kati ya nchi 185 zenye mazingira bora ya kibiashara[4].

**Mheshimiwa Spika**, Ripoti hiyo, imetaja nchi nane bora Kusini mwa Jangwa la Sahara zinazofanya vizuri kuwa ni pamoja na Mauritius ya 20, Rwanda ya 32, Afrika Kusini ya 41, Botswana ya 56, Ghana ya 67, Zambia ya 83, Morocco ya 87 na Namibia ya 98.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa taifa lenye rasimali na utajiri wa kutosha kama la kwetu ni jambo la fedheha na la kushtua kwa kuwa bado tumejikuta tukishika mkia katika masuala ya kibiashara hata katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki huku mara nyingi tukijisifu kwa takwimu zisizo za kweli au za kutoka kwenye vyanzo visivyo na sifa na vingine vya kutengeneza kwa malengo hayo.

Na hii ni kwa sababu tumeshuka kwa nafasi 9 hali ambayo siyo nzuri kwa uchumi wa nchi. Haya ni matokeo ya kushindwa kwa Sera na mifumo mibovu ya uwekezaji ya Serikali ya CCM ambayo kwa muda wa miongo mitano sasa inashikilia dola.

**Mheshimiwa Spika,** Kama hiyo haitoshi ripoti hii inaeleza maeneo yenye changamoto ambayo yanachochea na kuchangia kushuka kwa ufanyaji wa biashara ni pamoja na upatikanaji wa mikopo, rushwa, mfumo wa utoaji na upatikanaji vibali, mazingira ya biashara mipakani, ulipaji kodi na usajili wa ardhi na mali.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kuwa Kituo cha Uwekezaji (**TIC**)kimeanzishwa mwaka 1997 ambapo ni takribani miaka 17 iliyopita na kinatakiwa kuwa sehemu moja ya kurahisisha masuala ya ufanyaji biashara nchini bado changamoto ya urasimu katika ufanyaji biashara unatajwa kama kikwazo nchini[2].

**Mheshimiwa Spika**, Kambi rasmi ya Upinzani bungeni inaitaka serikali kuhakikisha kuwa huduma katika kituo hicho zinaboreshwa na pia rushwa

inatokomezwa katika masuala ya kupata vibali na hati mbalimbali za biashara ili kujenga mazingira mazuri ya uwekezaji yenye tija kwa taifa kuliko sasa ambapo bado wawekezaji wengine wanashindwa hata kulipa kodi ya ardhi waliomilikishwa ili kuweza nchini[3].

### 6.2 UWEZESHAJI WA WANANCHI (EMPOWERMENT)

**Mheshimiwa Spika**, Ni dhahiri kuwa uwekezaji wa miradi mbalimbali hapa nchini umeweza kufungua milango ya fursa za ajira kwa wananchi. Ni malalamiko ya muda mrefu juu ya miradi ya uwekezaji nchini, kutotoa kipaumbele kwa nafasi za ajira hasa kwa wazawa. Malalamiko hayo si tu kuwa yamejenga uhasama kati ya wazawa na wageni, lakini pia yamechangia kwa kiasi kikubwa kukwama kwa programu mbalimbali za serikali ambazo zinalenga kujenga uwezeshaji wa kiuchumi wa wananchi wa maeneo husika.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya uwekezaji iliyotolewa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) inaonyesha kuwakulikuwa na ongezeko la ajira kwenye makampuni ya uwekezaji mwaka 2009 kufikia 83,879 kutoka 83,473 mwaka 2008. Hata hivyo idadi kubwa ya ajira ilikuwa kwa Watanzania ambao sio wataalamu[4].

**Mheshimiwa Spika**, Pia idadi ya wafanyakazi ambao sio Watanzania iliongezeka kutoka 752 mwaka 2008 mpaka 815 jambo ambalo ni kinyume cha Sheria ya uwekezaji ya mwaka 1997 ambayo inaruhusu wawekezaji kuleta wataalam nchini pale ambapo teknolojia inayotumika haina wataalam kama hao nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi ya Upinzani inaitaka serikali kutoa kauli na maelekezo mahsusi kuhusu uwepo wa idadi kubwa ya wafanyakazi ambao si wataalam nchini jambo ambalo linawanyima fursa vijana wengi wanaohitimu katika taasisi zetu za elimu.

**Mheshimiwa Spika,** Suala la uwezeshaji wananchi kiuchumi pia halimaanishi kuwa Serikali itoe fungu la fedha kwa ajili ya shughuli za uwekezaji. Badala yake, ina wajibu wa kutoa fursa – hata za upendeleo ikibidi - ; kwa kulinganisha na washindani wageni. Ni dhahiri wakipata haki ya miliki, wawekezaji Watanzania wana uwezo wa kutosha wa kuvuta mitaji kutoka makampuni makubwa na hata mashirika na taasisi za fedha za kimataifa.

Aidha, ieleweke vilevile kuwa hata wawekezaji wengi wageni wanaoaminika na serikali hii, hutafuta mitaji toka taasisi za fedha za kwao na Kimataifa baada ya kupewa vibali vya kuvuna rasilimali zetu kwa bei ya kutupa na Serikali ya CCM.

**Mheshimiwa Spika,** Inashangaza kusikia kauli za viongozi waandamizi wa Serikali zinazovunja moyo wawekezaji hao badala ya Serikali kuwa chombo cha uwezeshaji wa wazawa katika uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika**, Wawekezaji wazawa ambao walionesha nia au wameendelea kuonesha nia ya kuwekeza katika miradi mbalimbali, wameendelea kukashifiwa, kudharauliwa na kudhalilishwa na kauli tata za viongozi kuwa hawana uwezo.

Kwa mfano, kauli ya Waziri wa Nishati na Madini Prof. Sospeter Muhongo kuwa Watanzania hawawezi na hawana uwezo wa kuwekeza kwenye gesi na mafuta, hivyo wawekeze kweye viwanda vya matunda, juisi, nyanya, nk ni kauli ambayo ilistahili kukemewa kwa nguvu zote na Serikali na yeye kuwajibishwa moja kwa moja aidha kwa kujiuzulu au kufukuzwa kazi.

Lakini cha kushangaza, Viongozi Wakuu wa Serikali walikaa kimya na wengine hata kushangilia. Huu ni ushuhuda wa wazi kuwa kauli kuwa "Sekta Binafsi" ni "engine" ya kukua kwa uchumi kwao inamaanisha sekta binafsi ya kigeni.

Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inawashangaa zaidi wafanyabiashara hawa wanaotukanwa hadharani kuwa ndiyo wafadhili wakubwa wa CCM hiyo hiyo inayowabeza.

**Mheshimiwa Spika**, Kauli hizi za viongozi waandamizi wa Serikali za kuudhi hazitakiwi kufumbiwa macho kwa kuwa wapo katika utumishi wa umma kwa maslahi ya Watanzania. Ni dhahiri kuwa, wawekezaji wazawa wana wajibu wa kuona kuwa Watanzania hawaachwi nyuma na badala yake wanashiriki pia moja kwa moja katika sekta mbalimbali za uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inawasihi Watanzania wote wenye nia na dhamira ya dhati ya kuwekeza katika miradi mbalimbali nchini, kutokata tamaa kuhusiana na uwezo wa Watanzania kushiriki moja kwa moja katika kuendeleza rasilimali hizi. Na wala isifike mahala Watanzania wakaaminishwa ama kudanganywa kuwa ni dhambi kuwapendelea wazawa katika uwekezaji wa gesi asilia na mafuta, bali uamuzi kama huo uchukuliwe kuwa ndiyo njia mojawapo nzuri ya kushirikisha wazawa moja kwa moja katika kunufaika na rasilimali zao hizo.

### 6.3 UNUNUZI WA SAMANI ZILIZOTENGENEZWA NCHINI

**Mheshimiwa Spika,** Kwa muda mrefu sasa kumekuwa na msisitizo kuhusu ofisi na taasisi za serikali kununua samani zinazotengenezwa nchini. Ni dhahiri kuwa nchi zilizoendelea hazikufanikiwa kupiga hatua bila kushirikiana na

wafanyabiashara wa ndani hivyo samani za ndani zikinunuliwa kwa wingi pato la taifa litaongezeka kwani lita – stimulate sekta nyingine za uchumi ikiwemo ajira. Serikali lazima sasa ieleze ni wizara, taasisi na ofisi zake ngapi zimeanza kutekeleza tamko la Serikali la kuanza kutumia samani zilizozalishwa na viwanda vya ndani ya nchi?

## 7.0 MAPENDEKEZO YETU YA NYUMA NA AHADI ZA SERIKALI

### 7.1 RERA (Real Estate Regulatory Authority)

**Mheshimiwa Spika,** Katika hotuba ya Kambi ya Upinzani kwa mwaka wa fedha 2011/2012 tuliitaka serikali kuanzisha chombo kitakachoweka uratibu na usimamizi wa sekta ya majengo makubwa ya biashara ambayo inayokuwa kwa kasi kubwa.

Mamlaka hii siyo tu itasimamia haki za wapangaji, bali hata mapato ya Serikali na ubora wa majengo haya na huduma zake. Tulipendekeza mamlaka hii ya udhibiti iitwe "Real Estate Regulatory Authority." Tunarudia tena kusisitiza ushauri wetu huu kwani Serikali inapoteza mapato bila sababu ya msingi kwa jeuri na kiburi cha kutokubali ushauri uliotoka upinzani.

### 7.2 Uundwaji wa Tume Huru za Kimahakama

**Mheshimiwa Spika,** Kumbukumbu za taarifa rasmi za Bunge zinaonyesha kwamba katika hotuba ya KUB mwaka 2011/2012 tuliishauri Serikali kuhusu kuunda tume ya kijaji ya uchunguzi wa vifo vya raia. Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali walikubali na wakaahidi kutekeleza hilo, lakini toka mwaka huo hadi sasa hakuna chochote kilichotekelezwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba Serikali haina dhamira yeyote ya kulitafutia ufumbuzi wa kudumu suala hili ambalo wananchi wamekuwa wakililalamikia kuhusu jamaa zao kuuawa na vyombo vya dola. Ni ukweli uliowazi kwamba tangu kipindi hicho vimeripotiwa vifo kadhaa, majina ya watu waliouawa yanapatikana katika taarifa ya haki za binadamu ya mwaka 2013, uk. 22.

**Mheshimiwa Spika,** Maadam ahadi ni deni na wananchi wanaendelea kuuwawa, tunaomba kwa mara nyingine tena kauli ya Waziri Mkuu kuhusiana na kadhia hii.

**8.0 MAPITIO YA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU KWA MWAKA WA FEDHA 2013/14**

**Mheshimiwa Spika**, Naomba sasa kuangalia fedha za maendeleo kwa baadhi ya mafungu kwenye ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa mujibu wa Randama, inaonyesha kuwa kwa mwaka wa fedha 2013/14 Ofisi ya Waziri Mkuu, Fungu 37, Tume ya Taifa ya Uchaguzi; Fungu 61 na Mfuko wa Bunge, Fungu 42 kwa pamoja zilitengewa jumla ya Tshs. 54,729,392,000/- kwa fedha za maendeleo. Hadi Machi 2014 kiasi ambacho tayari kilikwishatolewa ni Tshs. 17,263,036,286/- sawa na asilimia 28.4 ya bajeti.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa bahati mbaya ni kwamba kwa upande wa Tume ya Uchaguzi hakuna fedha yoyote ya maendeleo iliyotolewa hadi kufikia hiyo Machi 2014.

Kwa mwaka huu wa fedha 2014/15 kwa mafungu hayo hayo inaonekana zimetengewa jumla ya shilingi 29,953,134,000/- zikiwa ni fedha za ndani na fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** Mwonekano wa matumizi ni dhahiri kwamba uwezo wa Serikali kutoa fedha za maendeleo si mkubwa na jambo hili limepelekea uwepo wa bajeti kubwa lakini utekelezaji wake ni mdogo sana. Mfano unaonekana kwenye Wizara hii inayoongozwa na Kiongozi wa Shughuli za Serikali. Je, hili ni kuwadanganya Watanzania au Serikali inajidhalilisha yenyewe au kuna fedha zingine zinazotumika bila kupitia kwenye mfumo wa kuidhinishwa na Bunge?

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bunge iliishauri Serikali katika vikao vyake iwezeshe Tume ya Uchaguzi ili iweze kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Katika maelezo ya Utekelezaji wa hoja hiyo, Serikali ilieleza kwamba kwa mujibu wa sheria za Uchaguzi, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatakiwa kuboresha daftari mara mbili kati ya uchaguzi mmoja na unaofuata.

Aidha, Tume itaandikisha watu wote watakaokuwa wametimiza umri wa kupiga kura katika uchaguzi Mkuu Oktoba, 2015. Awamu ya kwanza ya uandikishaji itafanyika mwezi Septemba hadi Desemba, 2014 na awamu ya pili itafanyika kati ya April na Agosti 2015.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inasema tayari imekwishatoa kiasi cha Tshs. Bilioni 39 kwa ajili ya maandalizi hayo. Fedha hizi hazikuwa katika bajeti ya Tume na hakuna maelezo yeyote ya ni wapi Tume au serikali ilichota fedha hizi. Kwa msingi huu, ni dhahiri ukaguzi wa matumizi kama haya utakuwa wa utata mkubwa kwa CAG na ni ushuhuda mwingine wa usiri mkubwa unaoendesha Tume ya Uchaguzi.

Aidha, Serikali imeshindwa kutoa mchanganuo wa kina wa namna fedha hizo zilivyotumika ili Watanzania na wadau wa Demokrasia waweze kujiridhisha kwa kazi zilizofanyika na thamani ya fedha hizo zilizokwishatolewa.

**Mheshimiwa Spika**, Randama inaonyesha kuwa kwa mwaka wa fedha 2014/15 Tume ya Taifa ya Uchaguzi imefanya makadirio ya Jumla ya kiasi cha shilingi 761,462,903,911.00 (US$476 Million) kwa ajili ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, Uendeshaji wa Kura ya Maoni na Uchaguzi Mkuu mwaka 2015.

Kati ya fedha hizo shilingi 296,551,542,711.00 (US$185.3 Milion) zimeombwa kwa ajili ya kuboresha Daftari la kudumu la wapiga kura na kiasi cha Sh. Bilioni 144 (US$90million) kwa ajili ya uendeshaji wa kura ya maoni na kiasi cha Sh. 323,277,260,150.00 (US$202 Million) kwa ajili ya uchaguzi mkuu, 2015.

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya kufanya uchambuzi wa kina, imebainika kwamba mchanganuo nuliotolewa na Serikali katika Randama, unatofautiana na ukokotoaji halisi kwa kiasi cha shilingi billion 2.4

Tofauti hii ni kubwa mno na inatia mashaka kuhusu kama kweli Serikali iko makini katika kutayarisha bajeti zake au pengine kuna mchezo mchafu uliofichika katika taarifa hii. Kumbuka kuwa kuna shs bilioni 39 tayari zimekwishatumika kwa mujibu wa taarifa ya Waziri wa Nchi, Sera na Uratibu Ofisi ya Waziri Mkuu ambazo chanzo chake hakina maelezo yeyote.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo la kutia mashaka ni kwamba randama hiyo hiyo fungu 61 jedwali no. 9 pamoja na jedwali no.10 fedha hizo zinazoombwa hazijaonekana katika majedwali hayo.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa maelezo kwani mfuko mkuu wa Serikali (consolidated fund) unaweza kuwa unatumika vibaya kutokana na ukweli kuwa matumizi yake hayakaguliwi na Mkaguzi wala kamati za hesabu za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, Naomba kuwasilisha.

**Freeman A. Mbowe**
**KUB na Msemaji Mkuu,**
**Ofisi ya Waziri Mkuu**
**6 Mei, 2014**

**SPIKA:** Ahsante. Kwa sababu nina mamlaka ya kuongeza dakika, namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani juu ya Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mtakatifu Thomas Mo, Mheshimiwa Selasini anasema Ibada ya Misa ipo saa 7.00 hii. Mheshimiwa Silinde endelea.

**Hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 kama ilivyosomwa Bungeni**

**MHE. DAVID ERNEST SILINDE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI, OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na uwezo wa kusimama mbele ya Bunge lako tukufu ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI kuhusu Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2014/2015, kwa mujibu wa kanuni za kudumu za Bunge, toleo la mwaka 2013, kanuni ya 99(9).

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ndiyo inayosimamia masuala yote ya Tanganyika kwa kuwa TAMISEMI siyo suala la Muungano. Hivyo basi, tunapozungumzia TAMISEMI, tunazungumzia Tanganyika inayotajwa kama Tanzania Bara ambayo msimamizi wake mkuu ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania asiye na mamlaka Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiki pekee ni kigezo tosha tu kwa nchi yetu sasa kuingia katika mfumo mpya wa Serikali tatu uliopendekezwa katika Rasimu Mpya ya Katiba ambao utatenganisha majukumu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tanganyika na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, lakini kubwa kuliko yote tutakuwa tumeheshimu maoni ya wananchi waliotuchagua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kizazi hiki kinatambua vyema wajibu wake na haki zake. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni itaendelea kutangaza na kuelimisha Umma juu ya wajibu wake kwa Serikali na haki zake ndani ya Serikali, hivyo juhudi za kuwaelimisha wananchi kudai haki ya kuheshimiwa na kuthaminiwa katika kuchangia uendelezaji wa mshikamano wa Taifa letu zitaendelea kufanywa na Vyama vyetu vya Upinzani Bungeni ili kuhakikisha wananchi wa Tanzania kutoka pande zote za Muungano kwa Zanzibar na Tanganyika wanatengeneza mustakabali wa ushirikiano katika Muungano wanaoutaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani bado inaamini Muungano huu utajengeka kwa kutoweka mbele maslahi ya upande mmoja ila kwa kuweka mbele maslahi ya pande zote za Muungano na kamwe haiko tayari

kuona Muungano ukivunjika bali ukiimarika zaidi katika uwepo wa Serikali huru ya Tanganyika, Zanzibar na Shirikisho.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI ni kiungo muhimu kati ya Wizara za Kisekta na Asasi mbalimbali za Serikali za Mitaa. Ofisi ya Waziri Mkuu inalo jukumu la kuhakikisha kuwa yanajengwa mazingira mazuri ya kuwezesha ushirikishwaji wa Umma kwa kuleta maendeleo katika Taifa letu.

Mambo muhimu yaliyo/yanayotarajiwa kuzingatiwa ni Utawala Bora na kuboresha huduma katika Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu ya kisera, Ofisi ya Waziri Mkuu ina majukumu nane ya kiutendaji yafuatayo:-

(1) Kuratibu na kusimamia Tawala za Mikoa ili ziweze kuzisaidia Halmashauri katika kutekeleza wajibu na majukumu yake;

(2) Kutayarisha na kusimamia Sera ya Maendeleo Vijijini;

(3) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Mijini;

(4) Kuendeleza Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa nchini ili ziweze kutoa huduma bora;

(5) Kuzijengea Serikali za Mitaa uwezo wa kusimamia mapato na matumizi;

(6) Kuboresha miundo, hali ya watumishi na mifumo ya kazi ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri;

(7) Kusimamia Asasi, Mashirika ya Umma na Miradi inayotekelezwa chini ya Ofisi ya Waziri MKuu – TAMISEMI;

(8) Kuratibu utekelezaji wa shughuli za hifadhi ya mazingira katika Serikali za Mitaa; na

(9) Kuratibu vita dhidi ya rushwa na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza wananchi kwa kina, ni kwa nini kumekuwa na ukiritimba mkubwa katika kutekeleza majukumu yake ili kuleta tija kwa wananchi na kupunguza malalamiko mengi yanayoikabili Wizara ya TAMISEMI, hususan katika kupunguza umasikini kwa wananchi wengi wanaoishi chini ya dola moja?

Mheshimiwa Spika, nizungumzi kuhusu Tume ya Waziri Mkuu kuhusu kushuka kwa ufaulu wa elimu ya Sekondari.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Awali, ya Msingi na Sekondari inayosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, kufuatia kutangazwa kwa matokeo ya mitihani ya Kidato cha Nne ya mwaka 2012 yaliyotangazwa na Serikali tarehe 18 Februari, 2013, ilibainika kuwa kiwango cha ufaulu kilishuka zaidi ikilinganishwa na mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, matokeo yaliyotangazwa yalionesha kwamba kati ya watahiniwa 367,756 waliofanya mtihani huo ni watahiniwa 126,847 tu ndio waliofaulu katika mtihani huo kwa daraja la I mpaka la IV sawa na asilimia 34.5 ya watahiniwa wote.

Mheshimiwa Spika, watahiniwa waliofaulu katika Daraja la I - III walikuwa 23,520 (6.4%) na Daraja la IV walikuwa 103,327 sawa na asilimia 28.1. Watahiniwa 240,909 sawa na asilimia 65.5 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani wa Kidato cha Nne mwaka 2012 walipata Daraja la Sifuri. Aidha, ilibainika kuwa ufaulu wa watahiniwa umekuwa ukibadilika na kushuka mwaka hadi mwaka katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, ufaulu wa kiwango cha juu ulikuwa wa mwaka 2004 ambapo watahiniwa 63,487 walitahiniwa na kati yao 58,876 sawa na asilimia 91.5 walifaulu. Ufaulu ulishuka hadi asilimia 50.4 mnamo mwaka 2010 ambapo watahiniwa 352,840 walifanya mtihani na kati yao watahiniwa 180,216 walifaulu. Ufaulu wa mtihani wa Kidato cha Nne mwaka 2012 ulilalamikiwa sana na wadau mbalimbali wa elimu na kuashiria kuendelea kupoteza imani na mfumo wa elimu na mafunzo nchini.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maoni yalionesha mshituko na mengine kuona matokeo hayo kuwa ni ishara ya mapungufu katika mfumo wa elimu wa nchi katika maeneo mbalimbali ikiwemo ubora wake. Kwa mantiki hii Mheshimiwa Mizengo Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliona ni busara kuunda Tume ili ifanye uchunguzi na kubainisha sababu za hali hii ya matokeo na kutoa mapendekezo juu ya kukabiliana navyo.

Mheshimiwa Spika, Tume ilipewa hadidu kuu sita za rejea kama ifuatavyo:-

(1) Kubainisha sababu za matokeo mabaya ya mtihani wa Kidato cha Nne mwaka 2012.

(2) Kubaini sababu za kushuka kwa kiwango cha ufaulu katika mitihani ya Kidato cha Nne mwaka 2011 na 2012.

(3) Kutathmini nafasi ya Halmashauri katika kusimamia elimu ya sekondari katika Halmashauri zake.

(4) Kuanisha sababu nyingine zinazoweza kuwa zimechangia hali hii ya matokeo.

(5) Kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua mara moja kwa watahiniwa 240,903 waliopata Daraja la Sifuri katika mtihani wa Kidato cha Nne mwaka 2012.

(6) Kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua kukabiliana na tatizo la mwenendo wa kushuka kwa kiwango cha elimu mara moja, kipindi cha muda mfupi, kati na kipindi cha muda mrefu.

Katika kila hadidu kuu hizi za rejea ziliambatana na hadidu mahsusi tano ambazo zipo kwenye ripoti sitazisoma, zitaingia kwenye *Hansard* kama zilivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wake hadidu hizi za rejea ziligusa maeneo makubwa yafuatayo:-

(a) Mitaala na mihtasari na ufundishaji;
(b) Udhibiti wa ubora katika elimu ya sekondari;
(c) Ugatuaji na uendeshaji wa elimu ya sekondari;
(d) Mitihani na uendeshaji wake;
(e) Masuala mtambuka; na
(f) Mapendekezo ya muda mfupi, wa kati na wa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Tume inaonyesha kuwa kwa vile Taasisi ya Elimu Tanzania *(TET)* ni waandaaji wa mitaala, wangehakiki mitihani iliyotungwa ili kuhakikisha kuwa inaendana na mitaala iliyopo. Uchunguzi umeonesha kuwa, mitihani iliyotungwa haikuhakikiwa na *TET* na wala *TET* haijawahi kufanya kazi hiyo ya kuhakiki mitihani inayotungwa na Baraza la Mitihani la Taifa *(BMT)*.

Mheshimiwa Spika, pia taarifa hiyo inaonesha kuwa hakuna uhakiki wa mitihani ambao umewahi kufanyika tangu vyombo hivi viwili vilipoanzishwa na sheria zake. Sheria za Taasisi hizi mbili hazielekezi uhakiki ufanyike vipi na kwa namna gani.

Vile vile, hakuna mwongozo wowote kutoka Ofisi ya Kamishna wa Elimu inayoelekeza jinsi Taasisi hizi zinavyoweza kushirikiana katika masuala ya mitaala na mitihani.

Mheshimiwa Spika, Uhakiki huu kama nilivyoeleza hapo, kama ungefanyika, ungeweza kusaidia katika kuamua aina ya tathmini inayotakiwa kufanyika katika mitihani ya Taifa.

Baraza la Mitihani Tanzania walikuwa na wasiwasi kuwa kuruhusu watu wengine kuhakiki mitihani, kungeongeza mianya ya kuvuja kwa mitihani hiyo. Lakini pia Makamishna wa Elimu wote wawili, yaani wa Tanzania Bara na wa Zanzibar pia ni Wajumbe wa *BMT* na hivyo ni sehemu ya maamuzi ya *BMT*. Katika hali hii inakuwa vigumu kwao kutoa maelekezo ya jinsi ya Taasisi mbalimbali zinavyoweza kushirikiana katika suala la mitihani.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa hiyo hiyo ya Tume ni kwamba mtaala ambao unatumika hivi sasa haukuwahi kufanyiwa majaribio, yaani *piloting* ili kubaini upungufu wake wala haukufanyiwa tathmini baada ya kumalizika mzunguko wa kwanza na sasa unakaribia kukamilisha mzunguko wake wa pili.

Kwa mantiki hii, mtaala huu unaweza kuwa umeathiri ufundishaji na ujifunzaji.

Pia matokeo ya mtihani ya Kidato cha Nne tangu ulipoanza mwaka 2005 hadi 2012. Mabadiliko haya yamefanywa bila ya Walimu wengi wa Bara na Visiwani Zanzibar kushirikishwa licha ya kupewa taarifa. Hii imefanya Walimu wengi wa Zanzibar kutokuwa na ufahamu wa kutosha wa mtaala wa kujenga ujuzi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji, kwa hali hii ya elimu, haya ndiyo Matokeo Makubwa Sasa? Je, matokeo ya mwaka uliopita kama yalivyotangazwa mwaka huu yana uhalisia wakati mazingira yaliyoshauriwa kufanyiwa kazi na taarifa ya Tume bado hayajabadilika?

Mheshimiwa Spika, elimu bora huanzia ngazi ya awali. Aidha, vyuo vya ualimu havifundishi mtaala wa Kuandika, Kusoma na Kuhesabu (KKK) kwa sababu ya ukosefu wa Walimu wa kutosha wanaojua kufundisha KKK na wale waliokuwa na ujuzi katika sehemu hii wengi wao wamestaafu. Vyuo vya Ualimu pia havifundishi somo la KKK na hivyo uwezekano wa kupata Walimu wa kutosha katika eneo hili ni mdogo. Licha ya KKK kutofundishwa taarifa pia zinaonesha kuwa hakuna vyumba vya madarasa na vifaa kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahitaji majibu, kwani nini Serikali imeshindwa kwa makusudi kuitoa taarifa ya Tume ya Waziri Mkuu kwa wananchi. Kama Walimu wenye taaluma ya kuwafundisha watoto Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) hawapo, ni kwa vipi Serikali inasema imefanikisha Mpango wa Matokeo Makubwa sasa kwa sekta ya elimu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maswali mengi yamekuwa yakijitokeza hasa hususani nani mwenye dhamana ya kusimamia elimu ya msingi baina ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi (WEMU) na TAMISEMI na mipaka yao. Kamishna na Kurugenzi husika bado zimekuwa zikitoa maelekezo mbalimbali ya kiutendaji kuhusu elimu ya msingi na wakati mwingine kwa masuala ambayo wahusika hawawajibiki moja kwa moja kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI nayo imeshindwa kusimamia baadhi ya mambo kwa ufanisi kwa sababu ya mipaka ya madaraka kutokuwa bayana, ama wakati mwingine kwa mipaka hiyo kutokueleweka kwa watendaji husika. Muundo wa Halmashauri ni changamoto. Kwa mfano, masuala ya elimu yanasimamiwa na Madiwani kupitia Kamati za Elimu katika eneo husika. Madiwani, pamoja na kutokuwa na utaalamu au mafunzo endelevu ya kuwajengea ufahamu katika elimu, wamekuwa wakitoa maamuzi mengi ambayo yamekuwa yakisababisha uendeshaji wa shughuli za elimu wakati mwingine kutoendana na maelekezo ya Sera, Taratibu, Kanuni na Minongozo inayotolewa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Hati ya Mgawanyo wa Majukumu iliyotolewa, Tume ilibaini kuwa kuna migongano katika usimamizi na utekelezaji wa majukumu kati ya Wizara ya Elimu na Mafunzo na TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani bado inaamini kwamba matatizo haya kama yalivyobainishwa na Tume iliyoundwa na Waziri Mkuu bado yapo, hoja ni kwa vipi utendaji unaweza kuwepo wakati mazingira bado ni tatanishi katika sekta ya elimu? Huu ndio udhaifu wa wazi wa Serikali kiutendaji lakini bado inadanganya wananchi kuwa mambo ni mazuri katika sekta ya elimu.

Mheshimiwa Spika, udhaifu katika Sera ya Uwezeshaji wa wananchi kiuchumu. Katika Ilani ya CCM ya mwaka 2010 - 2015 inazungumzia suala la Sera ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi kwa kuainisha kuwa Sera yetu ya Msingi ni kwamba wananchi wenyewe wamiliki na kuendesha uchumi wa nchi yao. Hata hivyo, ili wananchi wa Tanzania waweze kumiliki uchumi lazima wawe na maarifa ya kisasa. Watanzania walio wengi hawana maarifa ya uchumi wa kisasa, hawana mitaji na kukabiliwa na mazingira magumu ya kijamii yenye vikwazo vingi vinavyowafanya washindwe kushiriki katika uchumi wao. Ndio

maana ukabuniwa mkakati wa kuwawezesha wananchi kiuchumi ili nao waweze kushiriki katika uendeshaji wa uchumi huo.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya CCM ilitoa matumaini makubwa kwa wananchi kwamba ifikapo mwaka 2015 maisha bora kwa kila Mtanzania yatawezekana. Mipango ya Serikali inatoa matumaini makubwa kwa wananchi ifikapo mwaka 2015 ahadi zitakamilika. Maswali yanabaki kwa wananchi kuwa ahadi za Serikali kupitia mipango yake na ahadi za CCM wakati wa uchaguzi wa 2005 na 2010 zinasubiri mwaka 2015 wakati wa uchaguzi ndio zitekelezwe? Je, huo ndio utendaji wa Serikali ya CCM? Je, ni kwa nini Serikali ya CCM haichoki kudanganya na kuwahadaa wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuwaambia ukweli wananchi kuwa ahadi ya maisha bora kwa kila Mtanzania ifikapo mwaka 2015 haitekelezeki na imeshindikana na ilikuwa sera ya kuingilia madarakani tu. Pia isisite kuwaomba masamaha Watanzania kwa kuwaongezea kiwango cha umasikini na deni kubwa la taifa linalofikia trilioni 31. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matumizi mabaya ya fedha za umma. Kumekuwepo na hulka iliyoota mizizi ndani ya Serikali ya CCM katika matumizi mabovu ya fedha za umma. Wakati viongozi wakifanya juhudi za kutoa vitisho kwa wananchi wanapodai uwajibikaji wa viongozi, kwani viongozi hawaoni kuwa moja ya majukumu yao makubwa ni kudhibiti rushwa na matumizi mabaya ya fedha za umma. Kama Serikali isipolitazama hili kwa uzalendo zaidi na kuona kuna haja ya kufanya marekebisho ya mfumo huu unaoruhusu ufisadi mkubwa kuendelea yatakuwa ni sehemu ya mambo yanayoweza kuchochea kutokuwepo kwa utengamano katika nchi, kwa mwendo huu wa matumizi mabaya fedha za umma, matumizi mabaya ya madaraka na ufisadi Serikalini tusitegemee wananchi wataendelea kuvumilia kwa udhaifu huu wa Serikali ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taswira ya nchi katika huduma muhimu kwa jamii kwa sasa ni mbaya, kwani katika Halmashauri bado utoaji wa huduma muhimu kama afya, elimu, maji na miundombinu ya barabara imeendelea kuwa duni na ukisikiliza sababu zinazotolewa na Serikali ni vigumu sana kupata uhakika kwani tumekuwa tukikopa, tukikusanya mapato ya ndani na kupewa misaada ya kimaendeleo lakini vipaumbele vya kiutekelezaji ni posho na safari za viongozi wakubwa nje ya nchi, hii imepelekea kutofikishwa fedha katika miradi ya maendeleo na fedha nyingi kutumika katika mambo yasiyo na msingi na kulipana posho tu. Huu sasa ni wakati wa Watanzania kujiuliza ni lini sasa watapata maisha bora kwa nguvu mpya, ari mpya na kasi mpya kama sio kuwadanganya wananchi ili waendelee kuwapa kura za kubaki madarakani?

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri wa Fedha mwaka 2011 katika majadala wa bajeti wa kwanza tangu kuzinduliwa kwa Bunge la Kumi, Waziri wa Fedha akilihutubia Bunge lako juu ya masuala ya Serikali za Mitaa, aliliambia Bunge lako Tukufu nanukuu:-

*"katika mwaka 2010/2011, Serikali kuu imeendelea kuzipa uwezo Serikali za Mitaa wa kusimamia rasilimali watu na fedha ili ziweze kutoa huduma kwa wananchi kwa ufanisi".*

Mheshimiwa Spika, pamoja na maneno mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa Watanzania, pia alirejea taarifa za Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali na kukiri udhaifu wa Serikali juu ya usimamizi wa fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, naomba ninukuu sehemu ya hotuba ya Waziri wa Fedha alipozungumza juu ya udhaifu katika usimamizi wa fedha za umma, nukuu:-

"*taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2009/2010, inaonesha kutetereka kwa udhibiti na usimamizi wa fedha za umma katika Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa, ikilinganishwa na taarifa ya mwaka 2008/2009. Taarifa inaonesha kupungua kwa hati safi za ukaguzi zilizotolewa kwa Wizara na Idara za Serikali, kutoka asilimia 87 hadi asilimia 77, wakati hati zenye shaka zimeongezeka kutoka asilimia 10 hadi asilimia 20. Aidha, kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, hati safi za ukaguzi zimepungua kutoka asilimia 58 mwaka 2008/2009, hadi 48.5 mwaka 2009/2010, wakati hati zenye mashaka zimeongezeka kutoka asilimia 41 hadi asilimia 48.5*". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, huu ndio ulikuwa uthibitisho wa kukamilika kwa kauli mbiu ya ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umasikini unaowasibu wananchi wetu na mamilioni ya watu katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ni matokeo rushwa, watawala wabovu wasio wajibika kwa wananchi na uchumi ulio nyuma na tegemezi. Njia pekee ya kuondokana na uchumi huu unaozaa unyonge na shida katika jamii ni kujenga msingi wa utawala bora, uwajibikaji, kuondoa fikra za utegemezi kwa viongozi na watawala na kujenga uchumi wa kisasa ili kukuza uchumi na kuutokomeza umasikini hatua kwa hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya kwa takribani zaidi ya miaka 50 ya uhuru, watawala wetu wameshindwa kuondoa moja ya adui mkubwa umaskini ambaye amedumu hadi sasa. Ni ukweli ulio wazi Watanzania wasitegemee

kupata maisha bora kwani imekuwa kinyume huku wakija na misemo tofauti ya kupata kura za kuendelea kubaki madarakani.

Mheshimiwa Spika, wakati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere anasema:-

*"Lazima tukimbie wakati wenzetu (walioendelea) wanatembea".*

Mheshimiwa Spika, Ilani ya CCM ya mwaka 2005 imemnukuu Mwalimu kwenye usemi wake huu. Viongozi wetu wa sasa pamoja na kumnukuu Mwalimu na maneno yake haya mazuri yenye wosia mwema kwa taifa na kutaka tufanye kazi kwa bidii, tuwatumikie wananchi kwa uaminifu, tujenge uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma na kuheshimu utawala wa sheria, bahati mbaya viongozi wa CCM wamekuwa wakienda mrama kwa kuongeza kasi katika rushwa na ufisadi, kutowajibika kwa wananchi, kuendelea kutumia vibaya fedha za umma, kutoheshimu utawala wa sheria na kuongeza kasi ya kutafuta madaraka na kulumbana nani awe Rais, hiyo ndiyo kasi na mwendo wa kukimbia katika Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji ipi kasi mpya, ari mpya na nguvu mpya? Yako wapi maisha bora kwa kila Mtanzania? Iko wapi ari zaidi, kasi zaidi na nguzu zaidi? Yako wapi matumaini kwa Watanzania? Ziko wapi huduma bora za afya kwa Watanzania? Wapi elimu bora kwa Watanzania? Wapi huduma bora za maji kwa Watanzania? Wapi uchumi endelevu kwa Watanzania? Hatuwezi kufika wakutakako Watanzania kwa aina hii ya uongozi na sisi tunalo jukumu la kuwaongoza Watanzania kufikia wanakotaka kufika na kuambiwa watafika, lakini ni dhahiri nguzo ya utawala wa kidhalimu ni ujinga na woga wa wanaotawaliwa. Hivyo, CCM imeendelea kujenga Taifa la wajinga kwa lengo la kuendelea kukalia madaraka, hivyo ni mwiko kwa CCM kutoa na kuwezesha elimu bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa elimu ndio nguzo kuu ya maendeleo na nyenzo ya haraka na ya uhakika zaidi ya kujenga taifa la kisasa. Wananchi wasio na elimu au wenye elimu hafifu hawawezi kupata fursa za kumiliki na kuendesha uchumi, hawawezi kuiwajibisha Serikali yao na hawawezi kuwajibika. Kwa hivyo, kutoa fursa katika kupata elimu bora ni hatua ya kwanza na ya msingi katika kujenga taifa linalojitegemea na lenye uchumi imara na maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, katika kitabu cha Uongozi Wetu na Hatima ya Tanzania, Mwalimu Nyerere aliandika kwa kuelewa kuwa tatizo lililopo kwenye uongozi lilihusiana hasa na usugu (kiburi) cha viongozi yaani viongozi hawakuwa tayari kusikiliza na kubadili njia zao; waliamua kuendelea kwa mtindo wa 'maji ukiyavulia nguo sharti uyaoge'. Pia suala la uwajibikaji, Nyerere anataja kanuni moja muhimu sana kuizingatia kwa wakati huo na hata huko mbeleni yaani kwa

Tanzania ya sasa kwani yameonekana pia, kuwa "*lakini viongozi wetu Waheshimiwa baada ya kushindwa kwa aibu hivyo, hawataki kukubali matokeo ya kushindwa kwao*". Ni vizuri kuelewa vizuri sana dhana hii ambayo kila kiongozi angeielewa baadhi ya vitendo vya kizembe ambavyo vimeendelea visingekuwa vinavumiliwa au kuonewa haya kama tunavyoona hali halisi ya sasa ambapo mambo mabaya ya kudidimiza utu wa Mtanzania yanalindwa na dola kwa maslahi binafsi. Kutoka na udhaifu huu wa viongozi wa CCM kusimamia fedha za umma, wananchi viongozi wa CCM kuwa ni wajasiriamali zaidi katika matataizo ya wananchi tofauti na ilivyokuwa awali wakati wa uongozi wa Mwalimu Nyerere ambapo Viongozi walionekana ni majasiri wa maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa wito kwa Wabunge wa CCM na Mawaziri, ikumbukwe hakuna Mbunge hapa anayetoa fedha zake mfukoni kwa ajili ya kupanga utoaji wa huduma zote kwa wananchi. Wote hapa tunatumia kodi za wananchi kulipwa mishahara na posho lakini hatupangi sawia katika kuwahudumia wananchi, tunatizama mitizamo ya Chama cha Mapinduzi kuogopa kuiwajibisha Serikali kwa kuwatumikia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matumizi ya fedha za umma. Ni zaidi ya muongo mmoja sasa Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikitoa ushauri kwa Serikali juu ya kuboresha utendaji kazi kwa umma na kutumia vema fedha za wananchi, lakini cha kushangaza ushauri huu kwa Serikali hii ya CCM umekuwa ni mbaya kwani Serikali imekuwa haioni haja ya kuokoa fedha za umma kwa kuelekeza katika huduma muhimu kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, naomba mpaka ukurasa wa 28 iingie katika hotuba.

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara wadogo wadogo Machinga. Kumekuwepo migongano kwa muda mrefu kati ya Serikali na wafanyabiashara wadogo wadogo maarufu kama Machinga, pasipo kutambua msingi wa tatizo na kutafuta ufumbuzi wa kudumu, Serikali itaishia kutengeneza tatizo kubwa zaidi na kukuza mgogoro kati ya jamii hii na Serikali. Nchi yetu ni nchi chuuzi, bajeti ya Serikali imekuwa ikiendeshwa kwa mikopo, misaada na makusanyo. Huu ni uchuuzi wa Serikali ya CCM. Nchi kama hii haiwezi kukwepa Machinga ambaye anafanya biashara ya kutafuta wanunuzi waliko.

Mheshimiwa Spika, haihitaji utafiti wa kisomi juu ya mkakati wa Serikali kujenga *Machinga Complex* kuwa umeshindwa kutatua tatizo la Machinga katika jiji la Dar es Salaam peke yake. Haya ni mawazo ambayo tayari majaribio yake yameshindwa kufanya kazi nchini. Serikali ya CCM imeua viwanda vilivyoachwa na Mwalimu Nyerere ndio maana vijana wamekimbilia katika biashara ndogondogo ya Machinga. Hii ndio dhihaka kwa Mwalimu kuua

mema aliyotuachia, leo hii mpaka *toilet paper* tunagiza China, ni aibu kwa Taifa na ni aibu kwa Serikali ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nielekee kwenye mapitio ya bajeti. Katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2013/2014 hadi sasa kumekuwepo na changamoto mbalimbali katika kuhakikisha bajeti iliyotengwa inaheshimiwa kama ilivyoidhinishwa na Bunge hili na changamoto ni kutokana na kutokuheshimu maoni ya Bunge na mapendekezo ya Bunge. Pili ni hulka iliyojengeka na Serikali hii ya CCM ya kutoheshimu matatizo ya wananchi na maoni ya Watanzania. Pia ni dharau kwa Watanzania kwani CCM inaamini Watanzania wapo kwa ajili ya kudanganywa na kupewa ahadi zisizo na utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, wakati Kamati zikifanya vikao kwa ajili ya maandalizi ya bajeti hii ambayo tayari tumeingia kuijadili katika Bunge hili, taarifa iliyotolewa na Kamati ya *PAC* na *LAAC* na kunukuliwa na gazeti la *The Citizen* la tarehe 30 Aprili, 2014 kuwa taarifa ya utoaji wa fedha za maendeleo haukufikia asilimia 50 ya bajeti iliyopangwa kutekeleza miradi ya maendeleo. Taarifa inaonesha upungufu wa asilimia 60 ya fedha zilizopangwa kugharimia miradi ya maendeleo. Tafsiri yake ni kuwa si kipaumbele kuwapelekea wananchi huduma muhimu kama za afya, elimu, nishati, maji na huduma za kilimo kama pembejeo.

Mheshimiwa Spika, taifa hili wakati likiasisiwa na viongozi wetu wa kwanza hususani Mwalimu na Mheshimiwa Karume, walikuwa na kauli mbiu ya kupiga vita maadui watatu ambao ni maradhi, ujinga na umaskini, hii ilikuwa ni miaka ya 1960. Mwalimu katika uhai wake aliendelea kuona hawa ni maadui na kusisitiza kuwaangamiza. Pamoja na Serikali kulia juu ya uasisi wa Mwalimu katika baadhi ya mambo, ndani ya CCM haipo nia ya dhati ya kuasisi mambo yenye maslahi kwa wananchi, ila ipo nia ya kuasisi mambo ambayo yana maslahi kwa CCM na viongozi wake kama muundo wa Serikali mbili, kwani hadi sasa hatuoni vita dhidi ya umaskini kwa kupeleka fedha za miradi ya maendeleo vijijini ila zinaelekezwa katika safari za viongozi na maadhimisho ya sikukuu za kitaifa ambayo hayana tija kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, adui maradhi tunaweza kumuondoa kwa kuboresha huduma za afya, kasi ya uwekezaji katika miradi ya huduma za afya imekuwa ni kwa mazungumzo tu. Fedha zimekuwa zikipitishwa na Bunge lakini hakuna utekelezaji kwa maana ya fedha kupelekwa katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, Mwalimu aliwahi kusema namnukuu:-

*"nchi isiyokusanya kodi ni nchi corrupt (rushwa), Serikali yake hutumiwa na matajiri na Serikali hii huishia kufukuzana na vijitu vidogo vidogo barabarani". (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwalimu alitaka Serikali kuhakikisha inakusanya kodi kwa ajili ya kuendesha Serikali na kutoa huduma kwa wananchi. Mambo haya ya msingi Serikali hii ya CCM haitaki kuyaakisi kwa kuwa hayana mslahi kwao na hivyo kufanya Serikali kuwa watumwa wa matajiri. Serikali inatoa sababu za kutofikishwa fedha kwa wakati katika Halmashauri kuwa ni kutopata fedha kutokana na makusanyo ya kodi na kutopata fedha kutoka kwa wahisani wa maendeleo. Kama Serikali inategemea kuwapatia maendeleo wananchi wake kwa misaada na mikopo ya wahisani, hili ni janga kwa taifa kwani hakuna nchi iliyo tayari kuweka mipango ya maendeleo ya Tanzania na sio nchi zao. Mara zote tunasema maendeleo ya Tanzania yataletwa na Watanzania wenyewe na sio nchi nyingine.

Baada ya kusema maneno hayo, naomba zile kurasa kama ishirini ambazo sijazisoma maana hotuba yangu ni kurasa 46 yaingizwe katika *Hansard* ya Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI, MHE DAVID ERNEST SILINDE (MB) OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI KUHUSU MAKADIRIO YA MATUMIZI YA OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015**

**UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na uwezo wa kusimama mbele ya Bunge lako tukufu ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni, Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI kuhusu Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2014/2015, kwa mujibu wa kanuni za kudumu za Bunge, toleo la mwaka 2013, kanuni ya 99(9).

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM **TAMISEMI**) ndio inayosimamia masuala yote ya Tanganyika kwa kuwa TAMISEMI si suala la muungano, hivyo basi tunapozungumzia TAMISEMI, tunazungumzia TANGANYIKA inayotajwa kama Tanzania bara ambayo msimamizi wake mkuu ni Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania asiye na mamlaka Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika**, hiki pekee ni kigezo tosha kwa nchi yetu sasa kuingia katika mfumo mpya wa serikali tatu uliopendekezwa katika rasimu mpya ya katiba ambao utatenganisha majukumu ya serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tanganyika na serikali ya mapinduzi Zanzibar.Lakini kubwa kuliko yote tutakuwa tumeheshimu maoni ya wananchi waliotuchagua.

**Mheshimiwa Spika**, kizazi hiki kinatambua vema wajibu wake na haki zake, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni itaendelea kutangaza na kuelimisha umma juu ya wajibu wake kwa serikali na haki zake ndani ya serikali, hivyo juhudi za kuwaelimisha wananchi kudai haki ya kuheshimiwa na kuthaminiwa katika kuchangia uendelezaji wa mshikamano wa taifa letu zitaendelea kufanywa na vyama vyetu vya upinzani bungeni ili kuhakikisha wananchi wa Tanzania kutoka pande zote za muungano kwa Zanzibar na Tanganyika wanatengeneza mustakabali wa ushirikiano katika muungano wanaoutaka.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani bado inaamini muungano huu utajengeka kwa kutoweka mbele maslahi ya upande mmoja ila kwa kuweka mbele maslahi ya pande zote za muungano na kamwe haiko tayari kuona Muungano ukivunjika bali ukiimarika zaidi katika uwepo wa serikali huru ya Tanganyika na Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI ni kiungo muhimu kati ya Wizara za Kisekta na Asasi mbalimbali za Serikali za Mitaa. Ofisi ya waziri mkuu inalo jukumu la kuhakikisha kuwa yanajengwa mazingira mazuri ya kuwezesha ushirikishwaji wa Umma kwa kuleta maendeleo katika taifa letu, Mambo muhimu yaliyo/yanayo tarajiwa kuzingatiwa ni Utawala Bora na kuboresha utoaji huduma.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kutekeleza majukumu ya kisera, OWM - TAMISEMI, ina majukumu ya kiutendaji yafuatayo;

Kwanza, Kuratibu na kusimamia Tawala za Mikoa ili ziweze kuzisaidia Halmashauri katika kutekeleza wajibu na majukumu yake,

Pili, kutayarisha na kusimamia Sera ya Maendeleo Vijijini,

Tatu, Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Mijini,

Nne, Kuendeleza Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa nchini ili ziweze kutoa huduma bora,

Tano, Kuzijengea Serikali za Mitaa uwezo wa kusimamia mapato na matumizi,

Sita, Kuboresha miundo, hali ya watumishi na mifumo ya kazi ndani ya OWM - TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri,

Saba, Kusimamia Asasi, Mashirika ya Umma na Miradi inayotekelezwa chini ya OWM – TAMISEMI,

Nane, Kuratibu utekelezaji wa shughuli za hifadhi ya mazingira katika Serikali za Mitaa na mwisho Kuratibu vita dhidi ya rushwa na UKIMWI.

**Mheshimiwa Spika,** kambi rasmi ya upinzani bungeni inaitaka serikali kueleza wananchi kwa kina ni kwa nini kumekuwa na ukiritimba mkubwa katika kutekeleza majukumu yake ili kuleta tija kwa wananchi na kupunguza malalamiko mengi yanayoikabili wizara ya TAMISEMI hususani katika kupunguza umasikini kwa wananchi wengi wanaoishi chini ya dola moja.

**TUME YA WAZIRI MKUU- KUSHUKA KWA UFAULU WA ELIMU YA SEKONDARI**

**Mheshimiwa Spika**, Elimu ya awali, ya msingi na Sekondari inasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI**.** Kufuatia kutangazwa kwa matokeo ya mitihani ya Kidato cha nne ya mwaka 2012 (K4- 2012) yaliyotangazwa na Serikali tarehe 18 Februari 2013; ilibainika kuwa kiwango cha ufaulu kilishuka zaidi ikilinganishwa na mwaka 2011.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo yaliyotangazwa yalionesha kwamba kati ya watahiniwa 367,756 waliofanya mtihani huo ni watahiniwa 126,847 tu ndiyo waliofaulu katika mtihani huo kwa Daraja la I mpaka la IV sawa na asilimia 34.5 ya watahiniwa wote. Watahiniwa waliofaulu katika Daraja la I-III walikuwa 23,520 (6.4%) na Daraja la IV walikuwa 103,327 (28.1%). Watahiniwa 240,909 sawa na asilimia 65.5 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani wa Kidato cha nne mwaka 2012 walipata Daraja la Sifuri. Aidha, ilibainika kuwa ufaulu wa watahiniwa umekuwa ukibadilika badilika na kushuka mwaka hadi mwaka.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, ufaulu wa kiwango cha juu ulikuwa wa mwaka 2004 ambapo watahiniwa 63,487 walitahiniwa na kati yao 58,876 (91.5%) walifaulu. Ufaulu ulishuka hadi asilimia 50.4 mnamo mwaka 2010 ambapo watahiniwa 352,840 walifanya mtihani na kati yao watahiniwa 180,216 walifaulu. Ufaulu wa mtihani wa K4 - 2012 ulilalamikiwa sana na wadau mbalimbali wa elimu na kuashiria kuendelea kupoteza imani na mfumo wa elimu na mafunzo nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Baadhi ya maoni yalionesha mshituko na mengine kuona matokeo hayo kuwa ni ishara ya mapungufu katika mfumo wa elimu wa nchi katika maeneo mbalimbali ikiwemo ubora wake. Ni kwa mantiki hii Mheshimiwa Mizengo Pinda (MB), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliona busara kuunda Tume ili ifanye uchunguzi na kubainisha sababu za hali hii ya matokeo na kutoa mapendekezo juu ya kukabiliana navyo.

**Mheshimiwa Spika,** Tume ilipewa hadidu kuu sita (6) za rejea kama ifuatavyo;

(a) Kubainisha sababu za matokeo mabaya ya mtihani wa K4 - 2012.

(b) Kubaini sababu za kushuka kwa kiwango cha ufaulu katika mitihani ya K4 - 2011 na K4 - 2012.

(c) Kutathmini nafasi ya Halmashauri katika kusimamia elimu ya sekondari katika Halmashauri zake.

(d) Kuanisha sababu nyingine zinazoweza kuwa zimechangia hali hii ya matokeo.

(e) Kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua mara moja kwa watahiniwa 240,903 waliopata Daraja la Sifuri katika mtihani wa K4 - 2012.

(f) Kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua kukabiliana na tatizo la mwenendo wa kushuka kwa kiwango cha elimu mara moja, kipindi cha muda mfupi, kati na kipindi cha muda mrefu.

Hadidu kuu hizi za rejea ziliambatana na hadidu mahsusi tano (5) kama ifuatavyo:

(a) Mitaala na mihtasari:

(i) Kutathmini uwiano wa mitihani inayotungwa na Baraza la Taifa la Mitihani na uhakiki wa mitihani na maswali unaofanywa na Taasisi ya kukuza mitaala.

(ii) Kutathmini mihtasari iliyotumika kuwaandaa watahiniwa kuanzia K4 - 2012 kuanzia wakati wakiwa K1.

(b) Kutathmini kiwango na mazingira ya ufundishaji:

(i) Umahiri wa walimu kumudu maudhui ya masomo wanayofundisha (mastery of subject matter).

(ii) Mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

(iii) Matumizi ya vitabu na zana za kufundishia na kujifunzia.

(iv) Utoshelevu wa walimu kwa masomo.

(c) Kuangalia mfumo wa Upimaji na Tathmini ya mtihani:

(i) Kuoanisha utungaji wa mitihani na mihtasari iliyotumika kuwaandaa watahiniwa.

(ii) Kutathmini kiwango cha mitihani inavyoendana na masomo yaliyofundishwa (relevance and validity).

(iii) Kuangalia matumizi ya alama endelevu katika matokeo (Continuous Assessment).

(iv) Kutathmini mchakato mzima wa usahihishaji na kuangalia usahihi wa alama za karatasi ya majibu na matokeo.

(v) Kutathmini matokeo ya mfumo wa upangaji wa madaraja ya masomo kwa watahiniwa.

(vi) Kufanya ulinganifu kati ya matokeo ya mtihani wa K4 - 2012 na matokeo ya watahiniwa hao walipokuwa K2 mwaka 2010.

(d) Usimamizi na uendeshaji:

(i) Kutathmini viwango vya elimu, uzoefu na uwezo wa Wakuu wa Shule za sekondri kusimamia utoaji wa taaluma katika shule zao.

(ii) Kutathmini ufanisi wa mfumo wa nidhamu ya walimu.

(e) Maeneo mengine:

(i) Kutathmini mchango wa jamii na wazazi/walezi katika maendeleo ya watahiniwa.

(ii) Kutathmini hali ya mwamko wa jamii katika kufuatilia na kutilia mkazo suala la elimu kwa watoto.

(iii) Kutathmini uwajibikaji wa jamii/wazazi/walezi katika kuwasaidia watahiniwa kutoathirika na mmomonyoko wa maadili unaotokana na ukuaji wa utandawazi hususan Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

(iv) Kutathmini hali ya upatikanaji wa chakula cha mchana shuleni na mchango wake katika kuinua taaluma.

(v) Kutathmini athari ya mfumo wa mikondo miwili (double shift) uliopo hasa katika shule za Zanzibar katika ufundishaji.

(vi) Kuangalia athari za upungufu wa miundombinu kama vile majengo ya Shule, madarasa, maabara na maktaba katika ufundishaji.

Kwa ujumla wake, hadidu hizi za rejea ziligusa maeneo makubwa yafuatayo:

(a) mtaala, mihtasari na ufundishaji;

(b) udhibiti wa ubora katika elimu ya sekondari;

(c) ugatuaji na uendeshaji wa elimu ya sekondari;

(d) mitihani na uendeshaji wake;

(e) masuala mtambuka; na

(f) mapendekezo ya muda mfupi, wa kati na ya muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa taarifa ya tume inaonyesha kuwa kwa vile Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) ni waandaaji wa mitaala, wangehakiki mitihani iliyotungwa ili kuhakikisha kuwa inaendana na mitaala iliyopo. Uchunguzi umeonesha kuwa, mitihani iliyotungwa haikuhakikiwa na TET na wala TET haijawahi kufanya kazi hiyo ya kuhakiki mitihani inayotungwa na Baraza la Mitihani la Taifa (BMT).

**Mheshimiwa Spika,** Pia taarifa hiyo inaonesha kuwa Hakuna uhakiki wa mitihani ambao umewahi kufanyika tangu vyombo hivi viwili vilipoanzishwa na sheria zake. Sheria za taasisi hizi mbili hazielekezi uhakiki ufanyike vipi na kwa namna gani. Vile vile, hakuna mwongozo wowote kutoka Ofisi ya Kamishina wa Elimu inayoelekeza jinsi taasisi hizi zinavyoweza kushirikiana katika masuala ya mitaala na mitihani.

**Mheshimiwa Spika**, Uhakiki huu kama nilivyoeleza hapo, kama ungefanyika, ungeweza kusaidia katika kuamua aina ya tathimini inayotakiwa kufanyika katika mitihani ya taifa. BMT walikuwa na wasiwasi kuwa kuruhusu watu wengine kuhakiki mitihani kungeongezea mianya ya kuvuja kwa mitihani hiyo. Lakini pia Makamishna wa Elimu wote wawili yaani wa Tanzania Bara na wa Zanzibar ni wajumbe wa BMT na hivyo ni sehemu ya maamuzi ya BMT. Katika hali hii inakuwa vigumu kwao kutoa maelekezo ya jinsi ya taasisi mbalimbali zinavyoweza kushirikiana katika suala la mitihani[1].

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa taarifa hiyohiyo ya tume ni kwamba mtaala ambao unatumika hivi sasa haukuwahi kufanyiwa majaribio (piloting) ili

kubaini mapungufu yake wala haukufanyiwa tathmini baada ya kumalizika mzunguko wa kwanza na sasa unakaribia kukamilisha mzunguko wa pili. Kwa mantiki hii, Mtaala huu unaweza kuwa umeathiri ufundishaji na ujifunzaji, na pia matokeo ya mtihani ya K4 tangu ulipoanza mwaka 2005 hadi 2012. Mabadiliko haya yamefanywa bila ya walimu wengi wa Bara na Visiwani Zanzibar kushirikishwa licha ya kupewa taarifa. Hii imefanya walimu wengi wa Zanzibar kutokuwa na ufahamu wa kutosha wa mtaala wa kujenga ujuzi.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji, kwa hali hii ya elimu, haya ndiyo matokeo makubwa sasa? Je matokeo ya mwaka uliopita kama yalivyotangazwa mwaka huu yana uhalisia? wakati mazingira yaliyoshauriwa kufanyiwa kazi na taarifa ya tume bado hayajabadilika?

**Mheshimiwa Spika,** elimu bora uanzia ngazi ya awali**,** Aidha, vyuo vya ualimu havifundishi kuandika, kusoma na kuhesabu (KKK) kwa sababu ya ukosefu wa walimu wa kutosha wanaojua kufundisha KKK na wale waliokuwa na ujuzi katika sehemu hii wengi wao wamestaafu. Vyuo vya ualimu pia havifundishi somo la KKK na hivyo uwezekano wa kupata walimu wa kutosha katika eneo hili ni mdogo. Licha ya KKK kutofundishwa taarifa pia zinaonesha kuwa hakuna vyumba vya madarasa na vifaa kwa ajili hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi inahitaji majibu, kwani nini Serikali imeshindwa kwa maksudi kuitoa taarifa ya Tume ya Waziri Mkuu kwa wananchi. Kama walimu wenye taaluma ya kuwafundisha watoto kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK) hawapo ni kwa vipi Serikali inasema imefanikisha mpango wa Matokeo Makubwa sasa kwa sekta ya Elimu?

**Mheshimiwa Spika,** Maswali mengi yamekuwa yakijitokeza hasa kuhusu nani mwenye dhamana ya kusimamia elimu ya msingi baina ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi (WEMU) na TAMISEMI na mipaka yao. Kamishna na Kurugenzi husika bado zimekuwa zikitoa maelekezo mbalimbali ya kiutendaji kuhusu elimu ya msingi na wakati mwingine kwa masuala ambayo wahusika hawawajibiki moja kwa moja kwa WEMU.

**Mheshimiwa Spika**, TAMISEMI nayo imeshindwa kusimamia baadhi ya mambo kwa ufanisi kwa sababu ya mipaka ya madaraka kutokuwa bayana, ama wakati mwingine kwa mipaka hiyo kutokueleweka kwa watendaji husika. Muundo wa Halmashauri ni changamoto. Kwa mfano, masuala ya elimu yanasimamiwa na madiwani kupitia Kamati za Elimu katika eneo husika. Madiwani, pamoja na kutokuwa na utaalamu au mafunzo endelevu ya kuwajengea ufahamu katika elimu, wamekuwa wakitoa maamuzi mengi ambayo yamekuwa yakisababisha uendeshaji wa shughuli za elimu wakati mwingine kutoendana na maelekezo ya Sera, Taratibu, Kanuni na Minongozo inayotolewa.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na Hati ya Mgawanyo wa majukumu iliyotolewa, Tume ilibaini kuwa kuna migongano katika usimamizi na utekelezaji wa majukumu kati ya WEMU na TAMISEMI.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani bado inaamini kwamba matatizo haya kama yalivyobainishwa na TUME iliyoundwa na Waziri Mkuu bado yapo, hoja ni kwa vipi utendaji unaweza kuwepo wakati mazingira bado ni tatanishi katika sekta ya elimu? Huu ndio udhaifu wa Wazi wa Serikali kiutendaji lakini bado inadanganya wananchi kuwa mambo ni mazuri katika sekta ya elimu.

**UDHAIFU KATIKA KUTEKELEZA SERA YA UWEZESHAJI WA WANANCHI KIUCHUMI**

**Mheshimiwa Spika,** katika ilani ya CCM ya mwaka 2010 - 2015 inazungumzia swala la **SERA YA UWEZESHAJI WA WANANCHI KIUCHUMI** kwa kuainisha kuwa Sera yetu ya Msingi ni kwamba wananchi wenyewe wamiliki na kuendesha uchumi wa nchi yao. Lakini ili wananchi wa Tanzania waweze kumiliki uchumi lazima wawe na maarifa ya kisasa, Watanzania walio wengi hawana maarifa ya uchumi wa kisasa, hawana mitaji na kukabiliwa na mazingira ya jamii yenye vikwazo vingi vinavyowafanya washindwe kushiriki katika uchumi wao. Ndio maana ukabuniwa mkakati wa kuwawezesha wananchi kiuchumi ili nao waweze kushiriki katika uendeshaji wa uchumi wa kisasa.

**Mheshimiwa Spika,** ilani ya CCM ilitoa matumaini makubwa kwa wananchi kwamba ifikapo mwaka 2015 maisha bora kwa kila mtanzania yatawezekana, Mipango ya serikali inatoa matumaini makubwa kwa wananchi ifikapo mwaka 2015 ahadi zitakamilika, Maswali yanabaki kwa wananchi kuwa ahadi za serikali kupitia mipango yake na ahadi za CCM wakati wa uchaguzi wa 2005 na 2010 zinasubiri mwaka 2015 wakati wa uchaguzi ndio zitekelezwe? Je huo ndio utendaji wa serikali ya CCM? Je, ni kwa nini serikali ya CCM haichoki kudanganya na kuwahadaa wananchi?

**Mheshimiwa Spika**, Kambi rasmi ya upinzani bungeni inaitaka serikali kuwaambia ukweli wananchi kuwa ahadi ya maisha bora kwa kila mtanzania ifikapo mwaka 2015 haitekelezeki na imeshindikana na ilikuwa sera ya kuingilia madarakani tu. Na isisite kuwaomba masamaha watanzania kwa kuwaongezea kiwango cha umasikini na deni kubwa la taifa linalofikia trillion 31.

**MATUMIZI MABOVU YA FEDHA ZA UMMA**

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na hulka iliyoota mizizi ndani ya serikali ya CCM katika matumizi mabovu ya fedha za umma, wakati viongozi

wakifanya juhudi za kutoa vitisho kwa wananchi wanapodai uwajibikaji wa viongozi, kwani viongozi hawaoni kuwa moja ya majukumu yao makubwa ni kudhibiti rushwa na matumizi mabaya ya fedha za umma. Mhe spika, kama serikali isipolitazama hili kwa uzalendo zaidi na kuona kuna haja ya kufanya marekebisho ya mfumo huu unaoruhusu ufisadi mkubwa kuendelea yatakuwa ni sehemu ya mambo yanayoweza kuchochea kutokuwepo kwa utengamano katika nchi, kwa mwendo huu wa matumizi mabaya fedha za umma, madaraka na ufisadi serikalini tusitegemee wananchi wataendelea kuvumilia kwa udhaifu huu wa serikali ya CCM.

**Mheshimiwa Spika**, taswira ya nchi katika huduma muhimu kwa jamii kwa sasa ni mbaya, kwani katika halmashauri bado utoaji wa huduma muhimu kama afya, elimu, maji na miundombinu ya barabara imeendelea kuwa duni, na ukisikiliza sababu zinazotolewa na serikali ni vigumu sana kupata uhakika kwani tumekuwa tukikopa, tukikusanya mapato ya ndani na kupewa misaada ya kimaendeleo lakini vipaumbele vya kiutekelezaji ni posho za viongozi wakubwa na safari za nje ya nchi, hii imepelekea kutofikishwa fedha katika miradi ya maendeleo na fedha nyingi kutumika katika mambo yasiyo na msingi na kulipana posho, huu sasa ni wakati wa watanzania kujiuliza ni lini sasa watapata maisha bora kwa nguvu mpya,ari mpya na kasi mpya? Kama sio kuwadanganya wananchi ili waendelee kuwapa kura za kubaki madarakani?

**Mheshimiwa Spika**, katika hotuba ya waziri wa fedha mwaka 2011 katika majadala wa bajeti wa kwanza tangu kuzinduliwa kwa bunge la kumi, waziri wa fedha akilihutubia bunge lako juu ya maswala ya serikali za mitaa, aliliambia bunge lako tukufu nanukuu *"katika mwaka 2010/11, Serikali kuu imeendelea kuzipa uwezo Serikali za mitaa wa kusimamia rasilimali watu na fedha ili ziweze kutoa huduma kwa wananchi kwa ufanisi"* pamoja na maneno mazuri ya Mhe. Waziri wa fedha kwa watanzania pia alirejea taarifa za mkaguzi na mdhibiti mkuu wa hesabu za serikali na kukiri udhaifu wa serikali ya CCM juu ya usimamizi wa fedha za Umma.

**Mheshimiwa Spika,** naomba ninukuu sehemu ya hotuba ya waziri wa fedha alipozungumza juu ya udhaifu katika usimamizi wa fedha za Umma, nukuu ***"taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2009/10, inaonesha kutetereka kwa udhibiti na usimamizi wa fedha za umma katika Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa, ikilinganishwa na taarifa ya mwaka 2008/09. Taarifa inaonesha kupungua kwa Hati safi za ukaguzi zilizotolewa kwa Wizara na Idara za Serikali, kutoka asilimia 87 hadi asilimia 77, wakati hati zenye shaka zimeongezeka kutoka asilimia 10 hadi asilimia 20. Aidha, kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, hati safi za ukaguzi zimepungua kutoka asilimia 58 mwaka 2008/09, hadi 48.5 mwaka 2009/10, wakati hati zenye mashaka zimeongezeka kutoka asilimia 41 hadi asilimia 48.5"*** mwisho wa

kunukuu, huu ndio ulikuwa uthibitisho wa kukamilika kwa kauli mbiu ya ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya kama ilivyo katika ilani ya CCM ya mwaka 2005 – 2010.

**Mheshimiwa Spika,** Umasikini unaowasibu wananchi wetu na mamilioni ya watu katika nchi za Kusini mwa jangwa la Sahara ni matokeo rushwa, watawala wabovu wasio wajibika kwa wananchi na uchumi ulio nyuma na tegemezi. Njia pekee ya kuondokana na uchumi huu unaozaa unyonge na shida katika jamii ni kujenga msingi wa utawala bora, uwajibikaji, kuondoa fikra za utegemezi kwa viongozi na watawala, na kujenga uchumi wa kisasa ili kukuza uchumi na kuutokomeza umasikini hatua kwa hatua.

**Mheshimiwa Spika**, kwa bahati mbaya kwa takribani zaidi ya miaka 50 ya uhuru watawala wetu wameshindwa kuondoa moja ya adui mkubwa umaskini ambae amedumu hadi sasa, ni ukweli ulio wazi watanzania wasitegemee kupata maisha bora kwa ari, kasi na nguvu mpya kwani vitendo vimekuwa kinyume huku wakija na misemo tofauti ya kupatia kura za kuendelea kuishi madarakani pasipo maboresho ya hali za wananchi wa chini.

**Mheshimiwa Spika,** wakati mwalimu Julius Kambarage Nyerere anasema ***"Lazima tukimbie wakati wenzetu (walioendelea) wanatembea***" na ilani ya CCM ya mwaka 2005 imemnukuu mwalimu kwani usemi wake huu bado Viongozi wetu wa sasa pamoja na kumnukuu mwalimu na maneno yake haya mazuri yenye wasia mwema kwa taifa na kutaka tufanye kazi kwa bidii, tuwatumikie wananchi kwa uaminifu, tujenge uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma na kuheshimu utawala wa sheria, bahati mbaya viongozi wa CCM wamekuwa wakienda mrama kwa kuongeza kasi katika rushwa na ufisadi, kutowajibika kwa wananchi, kuendelea kutumia vibaya fedha za umma kutoheshimu utawala wa sheria na kuongeza kasi ya kutafuta madaraka na kulumbana nani awe rais hiyo ndio kasi na mwendo wa kukimbia kwa Chama cha mapinduzi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya upinzani bungeni inahoji ipi kasi mpya, ari mpya na nguvu mpya? Yako wapi maisha bora kwa kila mtanzania? Iko wapi ari zaidi, kasi zaidi na nguzu zaidi? Yako wapi matumaini kwa watanzania? ziko wapi huduma abora za afya kwa watanzania? Wapi elimu bora kwa watanzania? Wapi huduma bora za maji kwa watanzania? Wapi uchumi endelevu kwa watanzania?, hatuwezi kufika wakutakako watanzania kwa aina hii ya uongozi na sisi tunalo jukumu la kuwaongoza watanzania kufikia wanakotaka kufika na kuambiwa watafika, lakini ni dhahiri nguzo ya utawala wa kidhalimu ni ujinga na woga wa wanaotawaliwa, hivyo CCM imeendelea kujenga taifa la wajinga kwa lengo la kuendelea kukalia madaraka hivyo ni mwiko kwa CCM kutoa na kuwezesha elimu bora.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa elimu ndio nguzo kuu ya maendeleo na nyenzo ya haraka na ya uhakika zaidi ya kujenga taifa la kisasa. Wananchi wasio na elimu au wenye elimu hafifu hawawezi kupata fursa za kumiliki na kuendesha uchumi, hawawezi kuiwajibisha serikali yao na hawawezi kuwajibika. Kwa hivyo kutoa fursa katika kupata elimu bora ni hatua ya kwanza na ya msingi katika kujenga taifa linalojitegemea na lenye uchumi imara na maendeleo endelevu.

**Mheshimiwa Spika,** katika kitabu cha Uongozi Wetu na Hatima ya Tanzania Mwalimu Nyerere aliandika kwa kuelewa kuwa tatizo lililopo kwenye uongozi lilihusiana hasa na usugu (kiburi) cha viongozi, yaani viongozi hawakuwa tayari kusikiliza na kubadili njia zao; waliamua kuendelea kwa mtindo wa 'maji ukiyavulia nguo' lakini pia swala la Uwajibikaji Nyerere anataja kanuni moja muhimu sana kuizingatia sasa kwa wakati huo na hata huko mbeleni yaani kwa Tanzania ya sasa kwani yameonekana pia, kuwa "***Lakini viongozi wetu waheshimiwa baada ya kushindwa kwa aibu hivyo, hawataki kukubali matokeo ya kushindwa kwao***" Ni vizuri kuelewa vizuri sana dhana hii ambayo kila kiongozi angeielewa baadhi ya vitendo vya kizembe ambavyo vimeendelea visingekuwa vinavumiliwa au kuonewa haya kama tunavyoona hali halisi ya sasa ambapo mambo mabaya ya kudidimiza utu wa mtanzania yanalindwa na dola kwa maslahi binafsi.

## HUDUMA ZA AFYA

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na umuhimu wa sekta ya afya, swala la afya ni moja ya mambo muhimu yanayosimamiwa na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, hii ni kutokana na ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii katika nchi kutegemea hali nzuri za afya za wananchi wake, kutokana na umuhimu huo Kambi rasmi ya Upinzani bungeni inapenda kupata majibu ya serikali mbele ya bunge lako tukufu juu ya hali ya afya nchini ikiwa mipango ya serikali na ilani ya CCM ikizidi kuwadanganya watanzania na kuishia kutoa kauli kuwa bado tupo kwenye mchakato usio na mategemeo ya huduma bora za afya nchini.

**Mheshimiwa Spika**, ilani ya CCM ya mwaka 2005 na sio 2010 ilitamka kuwa ifikapo mwaka 2010 kutakuwepo na huduma bora za afya kwa kiwango kikubwa, pamoja na ahadi hiyo kwa wananachi CCM ilitoa takwimu za uboreshaji wa huduma za afya ifikapo mwaka 2010, moja ya maeneo ambayo yalipewa kipaumbele ni pamoja na kupunguza vifo vya mama na mtoto, katika suala la kupunguza vifo vya watoto wachanga ilani ya CCM iliazimia kutoa vifo 95 kwa kila watoto 1000 wanaozaliwa hai kutokana na utafiti wa mwaka 2002 hadi kufikia vifo 50 mwaka 2010, pamoja na Ilani ya CCM kupanga vifo 50 na sio kufuta kabisa vifo vya watoto, bado hadi sasa mwaka 2014 wameshindwa kufikia lengo lao la mwaka 2010, bado hatuwezi kukiri kuwa CCM ni dhaifu ila ni bingwa wa kutoa ahadi hewa kwa lengo la kubaki madarakani.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya shirika la watoto duniani UNICEF ya mwaka 2013 imetoa takwimu za vifo vya watoto hususani kwa Tanzania na kuonesha kasi ndogo sana ya upunguzaji wa vifo vya watoto wachanga, takwimu hizo zilizofanywa na UNICEF kuainisha kipimo cha utekelezaji wa malengo ya milenia kwa kuanzia mwenendo wa kufikia malengo ya milenia kuanzia mwaka 1990 hadi mwaka 2012 inaonesha vifo kutoka 47,000 hadi 39,000 hali ambayo inaonesha kuwa vigumu kwa Tanzania kufikia malengo ya milenia ifikapo mkwaka 2015.

**Mheshimiwa Spika**, ukisoma ilani ya CCM juu ya uboreshaji wa huduma ya afya kwa jamii utaonja matuimaini makubwa na kuona sasa Tanzania imefikia kiwango halisi kulingana na malengo ya milenia lakini ukalinganisha ilani hiyo na utoaji wa huduma za afya kwa wananchi kwa sasa bado ni kitendawili, cha kushangaza viongozi wa CCM hawalioni hili na kuwahadaa wananchi kuwa tupo kwenye mchakato wa kuboresha huduma za afya, mara tatizo ni mawaziri mizigo, na maneno mengi ya kuwatia matumaini watanzania na kuona huu ndio utawala sahihi.

**Mheshimiwa Spika**, pasipo kwenda mbali swala la huduma za afya limekuwa likiulizwa sana hapa bungeni, huu ni ushahidi wa kuonesha jinsi tatizo la afya liliovyokosa ufumbuzi chini ya serikali hii ya CCM inayojitambulisha kwa watanzania kuwa ni serikali sikivu.

**Mheshimiwa Spika**, hadi sasa tatizo la uchache wa vituo vya afya huenda ikawa sio hoja kwa sasa, kwani hata hivyo vichache vilivyopo matatizo yake ni makubwa zaidi kwani hakuna wataalam wa kutosha wa afya wa kutoa huduma za kitaalam kwa wananchi, pia hakuna madawa ya kuwezesha wananchi kupata ndani ya vituo hivyo, lakini cha kushangangaza ni pale tunapokutana hapa kama wabunge kwa ajili ya kupitisha bajeti ya serikali kwa kuangalia mahitaji ya wananchi na kinachofanyika huwa ni kinyume na matarajio ya wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa mwito kwa wabunge wa CCM na mawaziri, ikumbukwe hakuna mbunge hapa aneetoa fedha zake mfukoni kwa ajili ya kupanga utoaji huduma kwa wananchi, wote hapa tunatumia kodi za wananchi kulipwa mishahara na posho, lakini hatupangi sawia katika kuwahudumia wananchi zaidi tunatazama misimamo ya Chama cha mapinduzi kuogopa kuiwajibisha serikali kwa kuwatumikia wananchi zaidi.

**MATUMIZI MABAYA YA FEDHA ZA UMMA**

**Mheshimiwa Spika**, ni zaidi ya muongo mmoja sasa Kambi rasmi ya Upinzani imekuwa ikitoa ushauri kwa serikali juu ya kuboresha utenbdaji kazi kwa

umma na kutumia vema fedha za wananchi, lakini cha kushangaza ushauri huu kwa serikali hii ya CCM umekuwa ni mbaya kwani serikali imekuwa haioni haja ya kuokoa fedha za umma kwa kuelekeza katika huduma muhimu kwa jamii, katika taarifa ya mkaguzi mkuu wa hesabu za serikali zilizoishia mwezi juni 2012 inaonesha Malipo ya mishahara kwa Watumishi ambao hawako katika utumishi wa serikali na majina hayajafutwa katika Orodha ya mishahara kiasi cha Sh.82,372,936. Vilevile kuna mishahara kiasi cha Sh. 275,206,250.53 isiyolipwa kwa sababu mbali mbali haikurejeshwa Hazina kutoka katika halmashauri husika, tafsiri yake ni kwamba fedha hizi ziliingia katika mifuko binafsi, Huu ni UFISADI dhahiri kwa fedha za wananchi, tunaweza kupiga kelele juu ya uboreshaji wa maisha ya watanzania kama ilani ya CCM inavyosema, lakini yakabaki katika maandishi kwani haipo nia ya dhati ya kuwapa maisha bora watanzania walio wengi.

**Mheshimiwa Spika,** katika taarifa ya mkaguzi mkuu wa hesabu za serikali kwa mwaka 2012 inaonesha katika halmashauri Mishahara Isiyolipwa ambayo haikurejeshwa Hazina ilikuwa ni Sh.1,599,387,243 huku Agizo Na.79(5) la Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 2009 linaagiza kwamba, mishahara isiyolipwa inatakiwa ipelekwe benki ndani ya siku kumi (10) za kazi. Pia maelekezo kutoka Wizara ya Fedha ambayo yalitolewa kwa barua yenye Kumb. Na.EB/AG/5/03/01/Vol.VI/136 ya Agosti 31, 2007 ambayo inaelekeza kwamba mishahara yote isiyolipwa inatakiwa kurejeshwa Hazina kupitia kwa Katibu Tawala wa Mkoa. Kinyume na maagizo hayo, ukaguzi wa mishahara umebaini kwamba, kuna mishahara isiyolipwa ya kiasi cha Sh.1,599,387,243 katika Halmashauri 43 ambazo hazikurejeshwa Hazina kwa mujibu wa maelekezo. Hali hii inaweza kusababishwa na ukosefu wa uwajibikaji katika mishahara isiyolipwa ambayo inaweza kusababisha hasara katika Halmashauri husika.

**Mheshimiwa Spika,** Mishahara Iliyolipwa kwa Watumishi Waliostaafu, Walioachishwa zazi,Waliofariki jumla ya Sh.693,132,772 Wakati wa ukaguzi wa mfumo wa malipo ya mishahara na rejesta za mishahara isiyolipwa kwa mwaka wa fedha ulioishia 30Juni 2012 ilibainika kwamba, kiasi cha Sh.693,132,772 kililipwa na Halmashauri 43 ikiwa ni mishahara kwa watumishi ambao aidha wamestaafu,wamejiuzuru, wameachishwa kazi au wametoroka na majina yao yameendelea kuonekana katika mfumo wa malipo ya mishahara ya Halmashauri husika, huu sio ubadhirifu wa bahati mbaya ila ni dhamira ya serikali ya CCM kuendelea kuwafanya watanzania maskini ili CCM wabaki madarakani kuendelea kunufaisha familia zao, kwani kinachoandikwa katika ilani yao ni kinyume na kile kinachotendeka kwa wananchi wanaoahidiwa maisha bora.

**MAPENDEKEZO MABAYA YA KUONGEZA MAENEO MAPYA YA UTAWALA KATIKA MKOA WA DAR ES SALAAM**

**Mheshimiwa Spika;** Katika hali ambayo inadhihirisha kuwa 'ukiwa mwongo usiwe mwepesi kusahau', wabunge na viongozi wa CCM ambao walidai kwamba 'Serikali Mbili zatosha, Tatu za nini' katika Bunge Maalum kinyume na Rasimu ya Katiba iliyotokana na Maoni ya Wananchi wako mstari wa mbele kutaka ukubwa wa Serikali uongezeke.

**Mheshimiwa Spika**, Wabunge na Viongozi hao wa CCM walikataa Muundo wa Muungano wa Shirikisho la Serikali Tatu kwa kupotosha kwamba muundo huo ni wa kuongeza idadi ya marais kwa ajili ya kuwapa watu vyeo kutokana na uroho wa madaraka.

Wabunge na viongozi hao hao wa CCM wamekuja na mapendekezo mabaya ya kuongeza maeneo mapya ya utawala katika Mkoa wa Dar Es Salaam ambayo yana dhamira mbaya.

**Mheshimiwa Spika;** Mapendekezo hayo pamoja na kuongeza fursa za kugawana vyeo vya Kiserikali vya ukuu wa Wilaya yanaongeza mtandao wa makada wa CCM kwa kivuli cha kuwa Wakuu wa Nyongeza wa Wilaya kwa ajili ya kutumika kufanya shughuli za kisiasa za chama hicho baada ya kuafitia kuongeza kwa nguvu ya upinzani katika Manispaa mbalimbali za Jiji la Dar Es Salaam.

Katika mapendekezo hayo wanakusudia kuongeza Wakuu wa Wilaya katika Jiji la Dar Es Salaam kutoka watatu wa sasa na kuwa na Wakuu wa Wilaya wengine wawili kufanya Jiji hili kuwa na wakuu wa wilaya watano.

**Mheshimiwa Spika**, Mapendekezo hayo yaliyowasilishwa kwa barakoa ya 'kuanzisha wilaya mbili mpya' Jijini Dar Es Salaam yanapaswa kupingwa na wapenda demokrasia na maendeleo ndani na nje ya Bunge, mabaraza ya madiwani na vyombo vingine vya maamuzi.

**Mheshimiwa Spika**, Hii ni kwa kuzingatia kwamba kama hoja ni kubadilisha mfumo kwa ajili ya kuboresha utoaji huduma na ufuatiliaji wa maendeleo badala ya kufikiria 'maeneo mapya ya utawala' yanayoongeza 'watawala', mapendekezo yangekuwa ni kuongeza 'maeneo mapya ya kutoa huduma na kuwezesha uwakilishi wa wananchi katika upangaji na usimamizi wa miradi ya maendeleo'. Wananchi wanachohitaji ni huduma na miradi ya maendeleo za Halmashauri au Manispaa na si nyongeza ya idadi ya Wakuu wa wilaya ambao ni mzigo wa gharama usio wa muhimu kwa nchi na wananchi.

**Mheshimiwa Spika;** Waziri Mkuu anapaswa kujibu katika majumuisho kwa kuwa yeye ndiye mwenye madaraka na mamlaka kwa mujibu wa Ibara ya 52 ya Katiba ya Nchi ya udhibiti, usimamiaji na utekelezaji wa siku hata siku wa kazi

na Shughuli za Serikali; ikiwa mnaamini Serikali mbili zatosha, tatu za nini ni kwanini sasa hamjiulizi "Wakuu watatu wa Wilaya watosha, Watano wa nini?".

**Mheshimiwa Spika**, Mkuu wa Mkoa wa Dar Es Salaam amenukuliwa na vyombo vya habari kwa nyakati mbalimbali hivi karibuni akisema kwamba tarehe 22 Aprili 2014 kumewasilishwa kwenye Baraza la Ushauri la Mkoa (RCC) mapendekezo ya kuanzishwa kwa Wilaya Mpya za Ubungo na Kigamboni.

Lakini siku chache baadaye ameshiriki Mkutano wa CCM uliovikwa joho la Serikali na kudai kuwawakilisha wananchi wa Dar Es Saalam katika tukio la propaganda za "Serikali mbili zatosha, tatu za nini".

**Mheshimiwa Spika;** Itakumbukwa kwamba tarehe 25 Aprili 2014 kuelekea siku ya maadhimisho ya Miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar Mwenyekiti wa CCM Rais Jakaya Kikwete alipokea kilichoitwa matembezi ya vijana nchi nzima katika Viwanja vya Saba Saba Temeke.

**Mheshimiwa Spika**, Katika kupokea maandamano hayo yaliyoandaliwa na Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) Mwenyekiti wa CCM Rais Kikwete iliyosomwa risala na Katibu wa Vijana wa chama hicho ambayo pamoja na mambo mengine iliunga mkono msimamo wa CCM wa kupingana na Rasimu ya Katiba iliyotokana na maoni ya wananchi juu ya muundo wa Muungano wa Shirikisho.

**Mheshimiwa Spika**, Katika tukio hilo Rais alichanganya kwa pamoja majukumu yake ya kichama ya CCM na yale ya kiserikali ya Urais. Mwenyekiti huyo wa CCM alikuwa pamoja na Makamu Mwenyekiti wa CCM na Rais wa Zanzibar Ali Mohamed Shein. Katika tukio hilo mstari wa mbele alikuwa Katibu Mkuu wa CCM Abrahaman Kinana ambaye sekretariati yake iliratibu matembezi hayo ya kuwaghilibu vijana na watanzania kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika;** Mkuu wa Mkoa ametumia kisingizio kwamba mapendekezo hayo ni ya wabunge na vikao vya mabaraza ya madiwani. Kauli hiyo ya mkuu wa Mkoa ambayo ameitoa kiujumla jumla bila kueleza undani wa mapendekezo ya wabunge na mabaraza ya madiwani inaleta hisia kama vile wabunge wote na na madiwani wote wa katika Jiji la Dar Es Salaam wametoa mapendekezo na kuridhia kuongezwa kwa wilaya mpya mbili katika Mkoa huo.

**Mheshimiwa Spika;** Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Bunge anapaswa kujibu ni wabunge gani na wa chama kipi hao walitoa mapendekezo hayo ya kuongeza wakuu wa wilaya na waliyatolea wapi? Aidha, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anapaswa kujibu ni mabaraza gani na mawazo hayo yalitolewa na

madiwani wa chama gani ya kuomba kwamba kuandaliwa mapendekezo ya kuongeza Wakuu wa Wilaya Mkoa wa Dar Es Salaam.

**Mheshimiwa Spika**, Mkuu wa Mkoa anapaswa kujitokeza tena kwenye vyombo vya habari na kutoa ufafanuzi kwamba si wabunge wote wala mabaraza yote ya madiwani yametoa mapendekezo ya kuanzishwa kwa wilaya mpya mbili za Ubungo na Kigamboni katika Jiji la Dar Es Salaam.

Mkuu wa Mkoa awataje kwa majina wabunge waliopendekeza kuanzishwe wilaya mbili mpya na pia ayataje kwa majina mabaraza ya madiwani ambayo yamependekeza kuanzishwa kwa wilaya hizo mbili za Ubungo na Kigamboni.

**Mheshimiwa Spika;** Kambi Rasmi ya Upinzani inataarifa pia kwamba Wadau wa Kinondoni ambao ni wa vyama tofauti vya siasa ikiwemo vya upinzani, taasisi mbalimbali na wawakilishi wengine waliamua kwa kura 52 kuyakataa mapendekezo hayo ya kuanzisha wilaya mpya mbili katika Mkoa wa Dar Es Salaam dhidi ya kura 13 tu za waliotaka wilaya hizo mbili zianzishwe.

Wadau wa Wilaya ya Kinondoni kupitia Kikao hicho walichopendekeza ni kwamba kuanzishwe Halmashauri za Manispaa za Ubungo na Kigamboni kusogeza huduma za maendeleo kwa wananchi.

Wadau hao walipendekeza kwamba Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni abaki huyo huyo mmoja na atimize wajibu wa kuiwakilisha Serikali katika Halmashauri zote mbili za Kinondoni na inayopendekezwa ya Ubungo.

Hivyo hivyo kwa upande wa Temeke, Mkuu wa Wilaya abaki mmoja na afanye kazi za kuwaiwakilisha Serikali zinazohusu Manispaa zote mbili, ya Temeke na inayopendekezwa ya Kigamboni.

**Mheshimiwa Spika;** Msingi wa kuwa na Halmashauri za Manispaa za Ubungo ni pamoja na kuboresha ufanisi katika uwakilishi katika upangaji wa mipango ya maendeleo, ukusanyaji wa mapato na utekelezaji wa miradi ya maendeleo na pamoja na kupunguza msongamano katika upatikanaji wa huduma za Kimanispaa katikati ya Jiji.

Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo inayopendekezwa makao yake ya kutoa huduma yanapaswa yawe maeneo ya pembezoni ya Jiji la Dar Es Salaam mathalani katika miji ya viungani (Satellite Town) kama ule unaopaswa kuharakishwa kujengwa katika eneo la Luguruni katika kata ya Kwembe na maeneo ya Kibamba.

Aidha, kwa kuanzishwa kwa Mji mpya wa Kigamboni na kuanza kwa vyombo kama Mamlaka ya Kigamboni (Kigamboni Development Authority), ni muhimu kusogeza huduma za Kimanispaa na kuboresha ufanisi katika uwakilishi wa wananchi na usimamizi kupitia Manispaa mpya ya Kigamboni badala ya Temeke pekee kama ilivyo sasa.

Miundo na mifumo yote hii inapaswa kufanyika kwa kuzingatia pia mwelekeo wa sasa na wa baadaye kuhusu kasi ya ongezeko la watu katika jiji la Dar Es Salaam pamoja na kuongezeka kwa makazi na shughuli nyingine za uzalishaji ikiwemo vitega uchumi.

**Mheshimiwa Spika;** Tunapaswa kuanzia sasa kuanza kujadili kuhusu Dar Es Salaam ya miaka 50 ijayo badala ya kufikiria kwa malengo ya muda mfupi tu ya kuongeza idadi ya wilaya na kuongeza vyeo tu.

Malengo ya mapendekezo ya muundo na mfumo mpya wa uwakilishi wa wananchi, utoaji huduma na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo inapaswa kuwa ni yenye kuboresha maisha ya wananchi na sio kuongeza gharama zisizo za muhimu kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika;** Malengo yale ni yale yanayopaswa kuendana na kasi ya ukuaji wa Jiji la Dar Es Salaam. Lengo lingine liwe ni kuwezesha kupunguza msongamano wa huduma muhimu za kijamii katika maeneo ya katikati ya Jiji. Lengo hilo litachangia katika ufanisi wa Mkakati wa kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar Es Salaam. Kwa kupeleka mamlaka kwa wananchi na wawakilishi wao ufanisi wa kusimamia mipango miji kwa kuzingatia 'Mpango Mkuu (Master Plan) utaongezeka badala ya kuongeza tu Wakuu wa Wilaya kugawa kwa makada vyeo na kuongeza gharama kwa wananchi.

## KITUO CHA KIMATAIFA CHA MABASI AU AIBU/ADHA ZA KITAIFA NA UFISADI WA ULIOPINDUKIA.

**Mheshimiwa Spika;** Kituo Kikuu cha Mabasi Ubungo (UBT) kilifunguliwa rasmi tarehe 6 Desemba 1999 pamoja na mambo mengine uanzishwaji wa kituo hiki ulikuwa na dhumuni la kutoa huduma kwa wasafiri pamoja na watumiaji wengine kikiitwa kuwa ni cha Kimataifa na pia kuongeza mapato ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam. Katika kipindi cha kati ya mwaka 2004 mpaka 2008 kumeibuliwa tuhuma mbalimbali za ufisadi na upotevu wa mapato katika Kituo hicho zikiwemo zinazohusu Kampuni ya Smart Holdings ya Familia ya Kingunge Ngombare Mwiru; hata hivyo katika kipindi chote zimekuwa zikikanushwa na serikali na CCM.

**Mheshimiwa Spika;** Hatimaye Tarehe 15 Machi 2009 Waziri Mkuu Mizengo Pinda aliagiza ufanywe uchunguzi maalum (Special Audit) na Mdhibiti na

Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu makusanyo ya Kituo Kikuu cha Mabasi cha Ubungo (UBT) ili kuboresha mapato ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika**, Tarehe 28 Julai 2009 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Bw. Ludovick Utoh, alikabidhi ripoti hiyo kwa Waziri Mkuu ambayo pamoja na mambo mengine ilieleza kasoro za ukusanyaji wa ovyo na tuhuma za ubadhirifu wa mapato ya Kituo Kikuu cha Mabasi cha Ubungo. Hata hivyo, Ripoti hiyo ilifanywa kuwa Siri na Waziri Mkuu alipokabidhiwa katika hatua za awali na sehemu kubwa ya mapendekezo yake hayakutekelezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa wakati na kwa ukamilifu.

**Mheshimiwa Spika**, Kufuatia hali hiyo, Ofisi ya Waziri Mkuu ilifuatiliwa kwa maswali kwenye mkutano wa Nne wa Bunge Kikao cha Ishirini na Sita Tare 15 Julai 2011 na Mbunge wa Jimbo la Ubungo John Mnyika, nanukuu:

*"Mosi; Je, ni lini Serikali itaweka wazi taarifa hiyo?*

*Pili; Je, Serikali imechukua hatua gani juu ya kasoro zilizobainishwa kuhusu mikataba ya kampuni ya Smart Holdings, Rick Hill Hotel, Abood Bus Services, Clear Channel, Globe Accounting Services na Scandinavian Express Services, ambayo imesababisha hasara na upotevu wa mapato?*

*Tatu; Je, Serikali iko tayari kufuatilia na kuchukua hatua za haraka juu ya malalamiko yanayotolewa na ukusanyaji wa mapato unaofanywa sasa ili kunufaisha umma kikamilifu?*

**Mheshimiwa Spika;** akijibu maswali hayo kwa niaba ya Waziri Mkuu Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Miko na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) pamoja na mambo mengine alieleza kwamba hoja hizo zimeanza kufanyiwa kazi na Halmashauri ya Jiji.

Aidha, alieleza kwamba ili kuondoa kasoro zilizojitokeza katika Kituo hicho, Serikali inapitia upya mikataba ya makampuni na kuhuisha viwango vinavyotakiwa kukusanywa kulingana na sheria ndogo ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam inayosimamia ushuru huo.

**Mheshimiwa Spika;** Ofisi ya Waziri Mkuu ilieleza pia kwamba kwa wakati huo ukusanyaji wa ushuru ulikuwa unafanywa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kupitia kwa Wakala aitwae KONSAD INVESTMENT LIMITED ambaye alidai kwa makosa kuwa anakusanya ushuru huo kwa wastani wa shilingi milioni 4 hadi milioni 5.7 kwa mwezi wakati uhalisia ni kwamba kiwango hicho ni makusanyo ya siku moja.

**Mheshimiwa Spika**, Naibu Waziri alieleza pia kwamba kwa kuzingaia malalamiko yaliyopo, Serikali tayari ilibadilisha Menejimenti ya kituo na kuahidi kwamba ingeendelea kuboresha miundombinu yake. Ofisi ya Waziri Mkuu ililieleza Bunge kwamba katika Bajeti ya mwaka 2011/2012, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ilitenga kiasi cha shilingi milioni 85 kwa ajili ya kufanya matengenezo katika eneo la maegesho ya magari.

**Mheshimiwa Spika;** Ofisi ya Waziri Mkuu ikaahidi kwamba Mpango wa muda mrefu wa Serikali ni kukijenga upya kituo cha Mabasi kama ilivyoainishwa katika mpango wa biashara wa mwaka 2007. Kwa kiwango kikubwa Serikali haikutekeleza ahadi hiyo, na badala ya Kituo hicho kujengwa upya, kimebolewa zaidi bila ya maandalizi ya Kituo Mbadala kuanzia wakati huo.

**Mheshimiwa Spika;** maswali mawili ya nyongeza yaliulizwa kufuatia majibu hayo ya Serikali; nikiyanukuu: "katika majibu Naibu Waziri ameeleza kwamba mkandarasi KONSAD Investment anakusanya milioni Nne hadi milioni Tano kwa mwezi, lakini kwa mujibu wa taarifa zilizopo ni kwamba toka Mkandarasi aingie mkataba mwezi Oktoba mwaka 2010, kwa mujibu wa Mkataba alipaswa kukusanya shilingi milioni 5.6 lakini alifanya hivyo kwa siku mbili tu (mara mbili tu) baada ya hapo toka wakati huo Oktoba 2010 mpaka leo amekuwa hatekelezi mkataba na ameandika barua Ofisi ya Waziri Mkuu na inaelekea anakingiwa kifua kuutekeleza huu mkataba.

**Mheshimiwa Spika**, Mosi; Ningependa kupata kauli kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu na ninajua inafahamu hili jambo kwa undani, Je, iko tayari sasa kuiruhusu Jiji la Dar es Salaam liweze kuvunja huu mkataba ambao haunufaishi wananchi wa Dar Es Salaam?

Pili; Suala la udhaifu wa kimikataba wa kituo cha mabasi ya Ubungo ambayo yanahusisha vile vile sehemu ya eneo litakalohusiana na mradi wa mabasi yaendayo kasi ambayo linahusiana na Kampuni ya UDA yamefikia kiwango cha juu sana, ninaelewa kwamba ofisi ya Waziri Mkuu iliandika barua ya kusitisha taratibu za uuzwaji wa hisa za kampuni ya UDA ambazo zimeuzwa na upotevu wa mali nyingi; ninaomba kauli ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuhusiana na ufisadi uliopo kwenye kampuni ya UDA unaoendelea hivi sasa, na iko tayari kutoa maelekezo kwa Jiji la Dar es Salaam kuweza kusitisha taratibu zinazoendelea?".

**Mheshimiwa Spika**; akijibu maswali hayo ya nyongeza Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAWALA za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) aliahidi nikimnukuu *"hivi ninavyozungumza hapa sasa hivi, tumemwita Mkurugenzi Mtendaji Kingopi hapa Dodoma tukamuuliza hili analolizungumza hapa, wameniambia kwamba hili wameliona na wanalifanyia kazi…….kama ikiwezekana tukubaliane leo tukitoka hapa nimwuite Kingobi na wenzake tukae*

*na tuseme ni nini kilichotokea kwamba kiasi hiki sasa hakiendelei kukusanywa kama ilivyokuwa siku ya kwanza na siku ya pili kama anavyosema Mbunge*".

**Mheshimiwa Spika;** Kambi Rasmi ya Upinzani ina taarifa kwamba Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu hakutekeleza ahadi yake ya 'kumuita Kingobi na wenzake kukaa na mbunge' na matokeo yake ni kwamba hali katika kituo hicho ambacho si cha Jimbo la Ubungo bali ni cha kitaifa na kimataifa imezidi kuwa mbaya.

**Mheshimiwa Spika**, Katika hatua ya sasa baada ya sehemu kubwa ya Kituo kubomolewa, bado fedha zinaendelea kutozwa milangoni katika mazingira yenye mianya ya ufisadi; mapato hayo hayatumiki kuboresha vya kutosha huduma katika kituo.

Waziri Mkuu anapaswa kutoa maelezo ya sababu za kuendelea kutoza fedha mlangoni katika Kituo ambacho kimebomolewa na huduma nyingi za msingi hazipo tena.

**Mheshimiwa Spika;** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuacha kuendelea kusitisha kutoza kiingilio katika Kituo hicho chenye huduma mbovu. Badala yake mapato yaliyokusanywa mpaka hivi sasa pamoja na mkopo ambao tayari ulishakubaliwa kutolewa kwa ajili ya kujenga Kituo mbadala eneo la Mbezi vitumike kujenga Kituo mbadala kwa haraka wananchi waweze kupata huduma zinazostahili.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha, ikiwa Ofisi ya Waziri Mkuu na Halmashauri ya Jiji la Dar Es salaam wanasuasua kujenga Kituo mbadala basi katika kipindi hiki cha mpito matengenezo ya kutosha yafanyike katika Kituo kilichobaki kwa kuwa sasa inajulikana wazi eneo ambalo limebomolewa kupisha Mradi wa Mabasi yaendayo haraka (BRT) unaoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Wakala wa Mabasi ya Haraka(DART).

**Mheshimiwa Spika;** kwa sasa kituo hicho ni aibu na adha ya kitaifa kwa kuwa hali ya uchafu ikiwemo utiririkaji wa maji machafu ndani ya Kituo cha Mabasi ambayo yanatuama na hadi kubadilika rangi na kuwa ya kijani ambapo ni hatarishi kwa abiria na watu wanaofanya shughuli zao ndani ya kituo. Pia, kuna vyoo vichache ukilinganisha na idadi ya abiria na watumiaji wengine wa Kituo. Hali hiyo inaweza kusababisha magonjwa ya mlipuko.

**Mheshimiwa Spika**, Kituo hiki kwa sasa kinatia aibu na adha kuna usumbufu mkubwa sana kwa abiria na watumiaji wengine wa Kituo baada ya maeneo ya awali ya kupumzikia kwa abiria na wasindikizaji kwa sehemu kubwa kubomolewa. Aidha, huduma nyingi za msingi za abiria zilizokuwepo awali

zimeondolewa bila kuwepo kwa utaratibu mbadala wenye kupunguza adha kwa wasafiri na watumiaji wengine wa Kituo.

Katika Kituo hiki kuna malalamiko pia ya mawakala wa mabasi juu ya utaratibu uliowekwa ya kwamba ulipitishwa kwa kuhusisha wamiliki wachache wa makampuni ya mabasi na hivyo kuibua usumbufu kwa makampuni pengine pamoja na kupunguza ajira za waliokuwa wakifanya kazi na makampuni hayo.

**Mheshimiwa Spika**; Matatizo ya Kituo hiki kwa sasa yamevuka uwezo wa Halmashauri ya Jiji la Dar Es Salaam na ikiachiwa yenyewe bila mchango wa Serikali kuu aibu ni ya nchi kwa wasafiri wa Kimataifa na adha ni ya wananchi kwa ujumla toka Mikoa mbalimbali wanaotumia kituo hicho. Hatua za haraka zisipochukuliwa kuhusu hali hiyo tete na tata inaweza kusababisha maafa/majanga au kuibua kwa mgogoro/malalamiko baina ya Serikali na Wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, Itakumbukwa kwamba kwa nyakati mbalimbali mwaka 2012 Mkurugenzi na Meya wa Jiji pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Dar Es Salaam walinukuliwa wakisema kwamba Kituo hicho kingehamishiwa katika eneo la Mbezi Luis kuanzia Januari 2013 kupitisha ujenzi unaoendelea wa Mradi wa Mabasi yaendayo Haraka (DART) hata hivyo zaidi ya mwaka umepita bila ahadi hizo kutekelezwa.

**Mheshimiwa Spika;** Kwa upande mwingine, matatizo yanayoendelea sasa yangeweza kuzuilika iwapo mapendekezo yote ya hoja iliyowasilishwa mwezi Mei 2011 kuhusu kituo cha Ubungo yangetekelezwa kwa wakati na Halmashauri ya Jiji la Dar Es Salaam. Hivyo, Ofisi ya Waziri Mkuu inapaswa kuwahoji na kuwachukulia hatua waliozembea na kusababisha hatua kuchelewa kuchukuliwa kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, Ikumbukwe kwamba katika ya maazimio ambayo yalipendekezwa yapitishwe wakati huo ni kufanyika tathmini tangu mwaka huo wa 2011 kuhusu eneo ambalo lilitarajiwa kuchukuliwa na Mradi wa Mabasi yaendayo haraka (DART) hatua ambayo ingewezesha maandalizi ya kituo mbadala cha kudumu kufanyika kwa wakati. Matokeo yake ni Kituo cha Kimataifa cha mabasi kuwa ni aibu na adha ya Kitaifa huku ufisadi wa ukusanyaji wa mapato ya mlangoni ukiendelea. Aidha, ili kupunguza kiwango cha mabasi yanayotegemea kutumia Kituo cha Ubungo.

**Mheshimiwa Spika;** Serikali ieleze pia hatua iliyofikiwa katika maandalizi ya Ujenzi wa Kituo kingine ambacho iliahidi kingejengwa Bunju. Kwa upande mwingine, kwa ajili ya kuboresha huduma za mabasi ya kutoka Kusini mwa nchi, Serikali ieleze hatua iliyofikiwa katika kutekeleza ahadi ya muda mrefu ya kujenga Kituo eneo la Mbagala. Kwa sasa abiria kutoka Mikoa ya Kusini

wanaotumia maeneo madogo na yasiyo vituo muafaka kama Tandika Sudan wanapata adha kubwa. Aidha, kwa kuwa na Vituo katika Nchi kuu mbalimbali za kuingia Jijini, Serikali itakuwa imechangia pia katika kupunguza msongamano uliopo hivi sasa.

## PEMBEJEO ZA KILIMO

**Mheshimiwa Spika**, tatizo la pembejeo hasa mbegu limekuwa ni tatizo sana kutokana na ukweli kwamba kuna wamiliki wa makampuni yanayozalisha au kusambaza mbegu ni viongozi waandamizi wa Serikali au ni viongozi wa juu katika siasa, jambo hili limeendelea kulalamikiwa sana na wakulima lakini hakuna hatua zozote zinazochukuliwa na Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, kwa sasa karibu nusu ya wakulima Wilaya ya Hai na maeneo ya jirani wameathirika na kwa uotaji wa mbegu za mahindi zilizosambazwa na kampuni ya SEED CO namba 513 na namba 625, zilizoota chini ya asilimia 20, Wakulima waliothirika zaidi ni kutoka kata za Rundugai hasa kijiji cha Kawaya, Kata ya Masama na Kata ya Machame Weruweru Vijiji vya Mbatakero, Ngusero na longoi, Kwa tatizo hilo zaidi ya Ekari elfu moja zimeathirika. Pia kuna mbegu za nyanya aina ya *RIO GRAND* ambapo wakala wake ni DOLADAE ENTERPRISES wakulima wanaolima bustani wameathirika sana hasa wale wa Hai mjini.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya malalamiko haya kutoka kwa wakulima Halmashauri ilikiri uwepo watatizo hilo na kuahidi kulifanyia kazi kwani wamejiridhisha hasa kuwa mbegu hazioti.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze wananchi walioathirika na tatizo hilo watafidiwa je na lini? Kwani hasara tayari imeishaingia na msimu kwa sasa umepita na kwa suala kama hili ni dhahiri kwamba wakulima toka mikoa mbalimbali wanaathirika na tatizo hili la kutoota kwa mbegu lakini Serikali inakaa kimya. Kwa njia hii ni kwa vipi kilimo chetu kinaweza kuwa cha kisasa endelevu na cha kibiashara?

**Mheshimiwa Spika,** tatizo la mbegu kutokuota kwa msimu huu wa kilimo limekuwa ni kubwa sana hasa kwa wakulima wa pamba wilaya za Nzega na Igunga. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kupitia TAMISEMI kuwaeleza wakulima wa Pamba ambao kwa msimu huu wamepata hasara wanafidiwa vipi?

## WAFANYABIASHARA WADOGO WADOGO- MACHINGA

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwepo migongano kwa muda mrefu kati ya serikali na wafanya biasahara wadogo maarufu kama Machinga, pasipo

kutambua msingi wa tatizo na kutafuta ufumbuzi wa kudumu serikali itaishia kutengeneza tatizo kubwa zaidi na kukuza mgogoro kati ya jamii hii na serikali, nchi yetu ni nchi chuuzi, bajeti ya seriklali imekuwa ikiendeshwa kwa mikopo, misaada na makusanyo, huu ni uchuuzi wa serikali ya CCM, nchi kama hii haiwezi kukwepa machinga ambae anafanya biashara ya kutafuta wanunuzi waliko.

**Mheshimiwa Spika**, haihitaji utafiti wa kisomi juu ya mkakati wa serikali kujenga machinga complex kuwa umeshindwa kutatua tatizo la machinga katika jiji la dar es salaam peke yake, haya ni mawazo ambayo tayari majaribio yake yameshindwa kufanya kazi, nchi hii chini ya CCM imeua viwanda vilivyoachwa na Mwalimu Nyerere ndio mana vijana wamekimbilia katika biashara ndogondogo (Machinga) hii ndio dhihaka kwa Mwalimu kuua mema aliyotuachia, leo hii mpaka toilet paper tunagiza china, ni aibu kwa Taifa na CCM.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani imeshauri serikali ya CCM juu ya kukuza sekta zisizo rasmi na kuzirasimisha ili vijana waweze kujiajiri na kupata ajira rasmi, sasa tunaona CCM ni kichwa kisicho sikia mema, kimechoka, na kilichobaki kwa CCM ni kufisadi fedha za wananchi na kujilimbikiza mali kinyume kabisa na Matarajio ya waasisi wa taifa hili katika kujenga jamii yenye usawa jamii isiyo na matabaka ya kiuchumi na sasa tunaona wazi viongozi wanajenga jamii mbili tofauti katika nchi moja, wale walionancho na wasio nacho, na bila aibu kila siku CCM na serikali yake inatumia fedha kubwa kulipana posho na kuhonga watu kushinikiza misimamo ya CCM kugeuza matarajio ya wananchi wanyonge na kuweka maslahi ya vigogo wa CCM mbele.

**Mheshimiwa Spika**, Wito mkubwa kwa watanzania leo, kama wakubwa wanaungana kutetea maslahi ya wakubwa wenyewe, je wanyonge wasipo ungana na kutetea unyonge wao, wapi haki yao itatambuliwa na kupatikana? Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inawaomba wananchi kuunga mkono juhudi za ukombozi wa mnyonge dhidi ya chama cha mapinduzi ambacho kimekuwa kikiratibu mikakati ya kuendelea kujejnga taifa la wanyonge wengi wasio na fursa ya kupata haki katika taifa lao.

## MAPITIO YA BAJETI YA MWAKA 2013/2014

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2013/2014 hadi sasa kumekuwepo na changamoto mbalimbali katika kuhakikisha bajeti iliyotengwa inaheshimiwa kama ilivyoidhinishwa na bunge hili, na changamoto ni kutokana na kutokuheshimu maoni ya bunge na mapendeklezo ya bunge, lakini pili ni hulka iliyojengeka na serikali hii ya CCM ya kutoheshimu matatizo ya wananchi na maoni ya watanzania, pia ni dharau kwa watanzania kwani CCM

inaamini watanzania wapo kwa ajili ya kudanganywa na kupewa ahadi zisizo na utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika**, Wakati kamati zikifanya vikao kwa ajili ya maandalizi ya bajeti hii ambayo tayari tunmeingia kuijadili katika bunge hili, taarifa iliyotolewa na kamati ya PAC na LAAC na kunukuliwa na gazeti la The Citizen la tarehe 30 Aprili 2014, taarifa ya utoaji wa fedha za maendeleo haukufikia asilimia hata 50 ya bajeti iliyopangwa kutekeleza miradi ya maendeleo, taarifa inaonesha upungufu wa asilimia 60 ya fedha zilizopangwa kugharimia miradi ya maendeleo, tafsiri yake ni kuwa si kipaumbele kuwapelekea wananchi huduma muhimu kama za afya, elimu,nishati, maji, na huduma za kilimo kama pembejeo.

**Mheshimiwa Spika**, taifa hili wakati likiasisiwa na viongzoi wetu wa kwanza hususani Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alikuwa na kauli mbiu ya kupiga vita maadui watatu ambao ni Maradhi, Ujinga na Umaskini, hii ilikuwa ni miaka ya 1960, Mwalimu katika uhai wake aliendelea kuona hawa ni maadui na kusisistiza kuwaangamiza, Pamoja na serikali kulia juu ya uasisi wa mwalimu katika baadhi ya mambo, ndani ya CCM, haipo nia ya dhati ya kuasisi mambo yenye maslahi kwa wananchi, ila ipo nia ya kuasisi mambo ambayo yana maslahi kwa CCM na viongozi wake kama muundo wa serikali mbili, kwani hadi sasa hatuoni vita dhidi ya umaskini kwa kupeleka fedha za miradi ya maendeleo vijijini ila zinaelekezwa katika posho za viongozi na maadhimisho ambayo hayana tija kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, adui maradhi tunaweza kumuondoa kwa kuboresha huduma za afya, kasi ya uwekezaji katika miradi ya huduma za afya imekuwa ni kwa mazungumzo tuu, fedha zimekuwa zikipitishwa na bunge lakini hakuna utekelezaji kwa maana ya fedha kupelekwa katika maeneo husika.

**Mheshimiwa Spika**, mwalimu aliwahi kusema namnukuu ***"nchi isiyokusanya kodi ni nchi corrupt, serikali yake hutumwa na matajiri, na serikali hii huishia kufukuzana na vijitu vidogo vidogo barabarani"*** Mwalimu alitaka serikali kuhakiki inakusanya kodi kwa ajili ya kuendesha serikali na kutoa huduma kwa wananchi, mambo haya ya msingi serikali hii ya CCM haitaki kuyaakisi kwa kuwa hayana mslahi kwao, na hivyo kufanya serikali kuwa watumwa wa matajiri, Serikali inatoa sababu za kutofikishwa fedha kwa wakati katika halmashauri kuwa ni kutopata fedha kutokana na makusanyo ya kodi na kutopata fedha kutoka kwa wahisani wa maendeleo, kama serikali inategemea kuwapatia maendeleo wananchi wake kwa misaada na mikopo ya wahisani hili ni janga kwa taifa kwani hakuna nchi iliyo tayari kuweka mipango ya maendeleo ya Tanzania na sio nchi zao, mara zote tunasema maendeleo ya Tanzania yataletwa na Tanzania sio nchi nyingine.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

------------------------

**David Ernest Silinde (Mb)**
**Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI**
**6.05. 2014**

**SPIKA:** Nakushukuru.

Waheshimiwa Wabunge, niliongeza muda ili kusudi hotuba hizi za watu ziishe hapa na yote Mungu anajua lakini sasa ninasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi. (Kicheko)

*(Saa 7.16 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo asubuhi tumefanikiwa kumaliza hotuba mbalimbali za Kamati kuanzia Kamati zilizohusika na Wizara hii pamoja na hotuba za pande za upinzani. Sasa tunaanza utaratibu wetu tuliokubaliana kwamba tutakuwa tunajadili kwa muda wa dakika saba, dakika tano za mwanzo utapigiwa kengele kwamba zimebakia mbili halafu itapigwa ya pili. Naamini kabisa mtajipanga vizuri kutumia vizuri hizo dakika saba. Sasa kiwango cha uzuri mtajua ninyi wenyewe.

Waheshimiwa Wabunge, lakini wakati huohuo tunaendelea na utaratibu ambao tulikubaliana kwamba idadi ya wazungumzaji itakwenda kwa *ratio* ya watu waliomo humu ndani. Kwa hiyo, hizo *ratio* zimeshafanyiwa kazi. Kama kuna mtu anataka kubadili lazima awe kwenye orodha ile aliyoomba kwa kujaza fomu. Kama haupo kwenye orodha hiyo huwezi kufanya hivyo isipokuwa nafasi za Mawaziri. Nafasi za Mawaziri kama watasema watachukua dakika saba lakini katika idadi ya watu walewale waliotakiwa kuzungumza katika Wizara hiyo. Sio kwamba mkimchukua Waziri sasa mnaongeza pale, hapana! Kama idadi ya wazungumzaji ni 20 hata akija Waziri itabidi wawatoe watu wengine halafu huyo Waziri ajibu na yeye atatumia dakika saba labda iwe wakati wa kujibu hoja zake rasmi pale atapewa muda unaostahili lakini kama anachangia atachukua nafasi ya wale wengine katika kundi lilelile.

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na kwa sasa hivi naowaona humu ndani tutaanza na Mheshimiwa Shekifu atafuatiwa na Mheshimiwa Ndassa,

Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim na Mheshimiwa Moses Machali. Mheshimiwa Shekifu!

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mungu lakini pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia katika Bunge hili la bajeti kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, mimi sikutaka kugusia jambo lolote kuhusu siasa za Katiba lakini nimelazimika kwa kifupi sana nizungumzie masuala haya ambayo yanaonekana ni uchonganishi, maneno ambayo hayana msingi na yanatolewa pia kwa viongozi wetu. Kanuni zetu za hilo Bunge la Katiba na Bunge hili zinakataza sana kusema mambo ambayo hayana ukweli na hasa yanapowagusa viongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi sioni mahali ambapo Mheshimiwa Rais Kikwete amekosea kuzungumzia Katiba, ilikuwa nafasi yake si tu kama Rais lakini kama binadamu, alikuwa na haki ya kutoa hoja na kutuangaliza. Hata hivyo, Rais huyu ni wa Chama cha Mapinduzi, anatoka huko. Huwezi ukamtaja Kikwete nje ya Chama cha Mapinduzi na yeye hawezi akazungumza jambo nje ya Sera za chama chake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi sioni kosa, tunachosema Muungano udumu basi na ameshauri kwamba haya tunayoyaamua yanaweza kuangusha Muungano. Hata asiye wa kawaida hatuwezi miaka 50 tumekwenda tuache miaka 50 tuanze upya, hata mtu anayesoma darasa si busara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nisingependa nizungumzie sana lakini niwaombe wenzangu hawa hasa upinzani, mtoto akililia kisu mpe atakuja kujikata mwenyewe. Uvumilivu wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi sasa unaanza kutoweka. Hawawezi kuondoka humu ndani, watoke nje wawachanganye wananchi na wamekimbia Bunge la Katiba bado tuangalie tu tuwaone hivyo. Mimi naiomba Serikali, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kweli watu hawa waonywe na wasiposikia wawajibishwe kwa mujibu wa Sheria. Tupo ndani kwenye Katiba wala hatupo kuwachanganya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongee kwa kifupi, dakika saba ni chache sana, sasa nizungumzie bajeti yenyewe. Kwanza, mimi nashukuru sana hotuba ya Waziri Mkuu, pengine haya nitakayoyazungumza ni kuimarisha na kujaribu kushauri. Hotuba ya Waziri Mkuu ni hotuba mtambuka ambayo inataja maeneo mengi, nitaje machache. Kwanza, nishukuru ununuzi wa mazao kwa mwaka wa jana kwenye mfuko wetu wa akiba ya chakula. Kazi ilifanyika nzuri, mazao yamenunuliwa kwa wingi na ndio sera nzuri. Mazao yale yanunuliwe tuwe na akiba ndani ya nchi na tutashusha mfumuko wa bei. Mfano mzuri umejitokeza,

tumekuwa na vyakula ndani ya nchi, mfumuko wa bei umepungua. Kwa hiyo, utaratibu huu uendelee na naiomba Serikali ianzishe kwa kasi kubwa Shirika la Ununuzi wa Mazao mchanganyiko. Tukiamua hivyo tutaisaidia sana nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yako maeneo ambayo ningeomba kuelekeza hasa katika tawala za Mikoa. Mimi nimekuwa Mkuu wa Mkoa, ninaelewa matatizo yaliopo katika Mikoa lakini niseme utendaji wa Mikoa utaweza tu kuimarika kama mafungu yaliyotengwa yanapelekwa. Tatizo la kutopeleka bajeti ya fedha zilizokasimiwa kwenda kwenye maeneo husika, zinatuondelea uwezo wetu wa kuiongoza Serikali na Mikoa itarudi nyuma sana kama Serikali haitaendelea kupeleka hela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012/2013, nilisisitiza sana uanzishwaji wa Kamati ya Bajeti. Kamati hiyo ilianzishwa lakini sina uhakika kwamba kweli imepewa haki za kutekeleza wajibu wake kikamilifu kwa sababu hela zilizoahidiwa ni kidogo sana zimekwenda kwenye maeneo husika. Wilaya hazikupokea hela, Mikoa haikupokea hela na maendeleo ya nchi ni Mikoa si vinginevyo lazima kwenda kwenye Mikoa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni madeni makubwa ya watumishi. Watumishi wapewe fedha zao waweze kuwa na motisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu nizungumzie kidogo amani kimkoa. Niipongeze Kamati nayo imeandika vizuri sana. Nchi yoyote na chama chochote cha siasa kinahitaji kuwe na amani kwa wananchi wake. Kumekuwa na tabia ya ubabe kwa viongozi, niwaombe Wakuu wa Mikoa wenzangu, hawa *Ma-DC* hawa wengine wamezoea ubabe sana, ndio! Nisingependa kuwataja lakini mimi ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Tanga na sifurahishwi sana na uongozi wa Wilaya ya Korogwe, ubabe. Wananchi wanahitaji tuwastahi, tuwaelimishe, tuwape maelekezo ya haki na kama hawakuelewa tusiwaonyeshe kwamba sisi ndio watawala, ni lazima tuwaelekeze na tuwatawale maana kuongoza ni kuonyesha njia. Kama wewe huonyeshi njia, unakemea, unamweka Diwani mwenzako ndani, Kiongozi mwenzako unamweka ndani kwa sababu wewe una madaraka, hawa vijana madaraka haya wana yapata wapi? Mimi sijawahi hata kumtamkia mtu kwamba nitakuweka ndani katika uongozi wangu lakini hawa vijana wanazunguka wakisema nitakuweka ndani, nitakuweka ndani! Inafika mahali unamweka mwenzako, Diwani mzima unamweka ndani, hamuwezi mkakaa, utatawalaje? Kwa hiyo, katika utaratibu ule wa ubabe, uongozi wa pamoja unaondoka, nyufa zinakuwa kubwa, hatuwezi kutawala kwa nyufa hizi. Nimuombe Waziri Mkuu nilikwishamjulisha na akaniahidi hatua zitachukuliwa. Sasa mimi kwa kweli nisingependa sana kulalamika kwa sababu ni kiongozi najua kuvumilia, nimuombe sana hatua zichukuliwe.

**SPIKA:** Ahsante, dakika zako zimeisha.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja mara mia moja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Ndassa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nchi yetu inahitaji amani na utulivu. Niiombe Serikali kwa wale wenye mchezo wa kutengeneza vurugu au wanaotaka kutengeneza vurugu ichukue hatua bila kuchelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie ahadi za Mheshimiwa Rais Mkoa wangu wa Mwanza, Jimbo langu la Sumve na Wilaya ya Kwimba. Tunaishukuru Serikali kwa kutupatia maji ya Ziwa Victoria mpaka sasa, yameshafika Ngudu, tunaishukuru sana Serikali. Pia tuiombe Serikali kupitia Wizara ya Maji, ule mpango wa kutoa maji sasa Ngudu kwenda mpaka Sumve na wenyewe ufanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, ahadi ya Mheshimiwa Rais. Barabara ya kutoka Magu kwenda Hungumarwa nayo kwa sababu ni ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa kiwango cha lami na yenyewe naiomba Serikali itekeleze.

Mheshimiwa Spika, Kilimo Kwanza. Miaka miwili, mitatu ya nyuma kulikuwa na utaratibu wa kuleta matrekta kupitia JKT. Matrekta hayo yalikuja kwa mwaka mmoja, mwaka wa pili hakuna tena matrekta. Wananchi wengi wanahitaji matrekta sasa lakini hawajui matrekta wayapate wapi. Naiomba Serikali iwe na utaratibu mzuri matrekta yaweze kupatikana ili kilimo kiwe na tija.

Mheshimiwa Spika, mbegu za pamba. Msimu huu mbegu za pamba kutoka *Quton* hazikuota. Wananchi wanalalamika wamepata hasara, naiomba Serikali ifanye utaratibu wa kuwafidia wakulima wale ambao walinunua mbegu lakini mbegu hizo hazikuota. Naiomba sana Serikali ifanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, afya, huduma ya mama na mtoto ipo kero kubwa kwa upande wa kadi wanapokwenda kliniki wazazi hawa na watoto wanalazimishwa kununua kadi. Nimeshamwambia Waziri wa Afya tatizo hili ni kubwa sana, nafikiri ni nchi nzima. Niiombe sana Serikali ilitazame hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madawati kwenye shule za sekondari na shule za msingi. Serikali ina kigugumizi gani kuamua mara moja kwamba mwaka huu au miaka miwili tunataka tumalize tatizo la madawati kwenye shule za sekondari na za msingi? Kama unapeleka Walimu wa kutosha wa shule za sekondari na msingi lakini Walimu hawa wanaenda kukuta shule ambazo hazina madawati,

niiombe Serikali ipeleke madawati kwenye shule za msingi na sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Mwanza *Airport* ni tatizo, haueleweki. Mpaka leo tunasuasua tu. Kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri Mkuu kinazungumzia ukarabati, hivi ni ukarabati au ujenzi? Naomba nipate majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, madawa ya kulevya. Hii imekuwa sasa ni ngonjera tu, wanakamatwa dagaa lakini masangara hayakamatwi. Kama imeshindikana basi mseme biashara hii imeshindikana kuliko kuwasumbua hawa wadogo wadogo. Tatizo hili limekuwa ni kubwa, sasa hivi mnasema mtaleta Sheria, Sheria ipo lakini nani anaamua kuwakamata hawa wakubwa? Maana huu umekuwa ni wimbo tu, naomba Serikali ikishaamua jambo ilitekeleze.

Mheshimiwa Spika, michezo. Watanzania tupo milioni arobaini na tano, hivi hata mchezo mmoja tu wa kutupa hata mshale, tufe, hatuwezi! Wapo Wagogo mashuhuri sana kwa kurusha mishale, Wamasai akina Ole, hivi inashindikana kweli Tanzania hata kurusha mkuki, tufe, kukimbia inashindikana? Naomba tukitumie Chuo cha Michezo ya Malya ili kusudi tuweze kufanikisha suala zima la michezo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabla kengele haijalia, wale ndugu zetu niwapongeze kwa sababu nasikia Baraza lao la Mawaziri Kivuli watatangaza kesho, nawatakia kila la kheri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nakushuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshiwa Waziri Mkuu, naomba upite urudi kwenye nafasi yako. Napenda nimuite Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza atafuatiwa na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika bajeti ya ofisi ya Waziri Mkuu na ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI). Mimi ni Mjumbe wa Kamati inayoshughulikia TAMISEMI, napenda kwanza kuchukua nafasi hii kukushukuru kuweka Kamati hii kwa sababu kwa muda mrefu Serikali za Mitaa zilikuwa hazina Kamati ya kuzisimamia.

Mheshimiwa Spika, katika ziara zetu tumegundua mambo mbalimbali katika Halmashauri hizi ambapo ni pamoja na ubadhirifu mkubwa, usimamizi dhaifu wa miradi, migogoro mbalimbali katika Halmashauri kati ya Mameya, Madiwani na Wakurugenzi. Ni mambo mengi sana tumeyagundua mengine yamejitokeza katika taarifa yetu ya Kamati lakini mimi nitaongelea mambo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, naomba niongee kuhusu Mfuko wa Barabara. Halmashauri au Serikali za Mitaa zinazo barabara nyingi lakini ukitazama mgawanyo wa pesa za barabara, katika shilingi mia moja inayotolewa Serikalini basi Serikali Kuu hupata asilimia 70 na Halmashauri au Serikali za Mitaa hupata asilimia 30. Tuseme kwa kila shilingi mia *TANROAD* wanapata Sh.70 na Serikali za Mitaa zinapata Sh.30.

Mheshimiwa Spika, ukitizama sasa barabara ambazo zinatengenezwa katika Halmashauri ni kubwa kuliko tathmini ya awali. Kwa sasa hivi inakadiriwa kuwa Serikali za Mitaa zina barabara karibu 96 *square kilometers*. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali irudie upya na kutazama mgawanyo wa fedha hizi ikibidi Halmashauri zipelekewe mpaka asilimia 40. Sasa hivi zinatengeneza barabara ambazo sio imara yaani wanapitisha greda, hazina mitaro, hazina nini kwa sababu hazina uwezo. Zinaendelea kupata lawama kwamba zinatengeneza barabara mbaya lakini pesa wanazopata kwa kweli ni kidogo na kwa kweli tunaomba Waziri Mkuu hili jambo ulione kwa sababu kule ndio kuna wananchi.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa niongelee kuhusu usimamizi wa miradi katika Halmashauri. Upo udhaifu mkubwa wa kusimamia miradi katika Halmashauri na hasa Ma-*engineer* wetu. Tunaomba Serikali itazame upya ma-*engineer* hawa ambao wanadhalilisha taaluma yao. Hawasimamii miradi ipasavyo, unakuta miradi mingine imejengwa chini ya viwango na mingine kwa kweli haipendezi katika hali tunayoiona tunapokuwa katika ziara.

Mheshimiwa Spika, napenda niongee kwa haraka haraka maana dakika saba hizo ni kidogo kuhusu migogoro iliyoko katika Halmashauri. Ipo migogoro mingi mingine Waziri Mkuu unaijua lakini napenda nitoe maoni kidogo kuhusu mgogoro katika Manispaa ya Bukoba, Kagera. Mheshimiwa Waziri Mkuu ulileta maagizo yako lakini maagizo yako sasa yamegeuka ni kama umemwaga ugali watu wamwage mboga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo kesi zinaendelea na ipo michango mikubwa ya wakandarasi na watu wengine kuhakikisha kwamba wale Madiwani wasimamishwe Udiwani wao ili maagizo ya *CAG* yasiweze kutekelezwa. Kwa ufupi, naomba ufuatilie mgogoro huu kwa sababu Halmashauri hii ipo katika matatizo lakini hali ilivyo ni kwamba unamsimamisha Meya basi na yeye anahakikisha Halmashauri haifanyi kazi. Ndio taarifa hiyo, Waziri Mkuu naomba maagizo yako yatekelezwe kama ulivyoelekeza na usimamizi uwepo na naomba wewe ufuatilie kwa sababu wale ni watu wa chama chako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumegundua kwamba katika Halmashauri hizi licha ya usimamizi mbaya lakini pia hata fedha nyingi zinapotelea katika mikono ya watu. Ndiyo maana kwa msisitizo mkubwa sisi kutokana na taarifa yetu

tumeamua katika bajeti hii kwamba ni lazima Halmashauri zitenge asilimia sitini ya mapato yake kwenda katika miradi ya maendeleo.

Tunafanya hivyo kwa sababu tunaamini kwamba katika Halmashauri zipo pesa nyingi ambazo zinapotelea katika mikono ya watu na vyanzo vingine havitumiki. Ukienda katika Halmashauri unaweza ukakuta kuna vitabu viwili, kitabu kimoja cha watendaji, kitabu kimoja ni cha Serikali, hivyo pesa nyingi zinavuja. Kama pesa zote zitakusanywa wana uhakika wa kusimamia miradi ya maendeleo yao. Kama sisi TAMISEMI tutakuwa tumefanikiwa jambo hili basi hata Serikali Kuu itaiga kutoka kwetu iweze kutenga asilimia arobaini ya bajeti yake kwenda katika shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, niongelee suala la Serikali kununua chakula. Ni kweli tunashukuru Serikali inanunua chakula hasa Mikoa ya Kusini lakini yapo malalamiko mengi kwamba *NFRA* hailipi ushuru wa Halmashauri. Halmashauri zinadai pesa nyingi, Halmashauri ya Mkoa wa Njombe, Mkoa wa Ruvuma wanadai mabilioni ya pesa. Tunaomba Serikali kupitia Waziri Mkuu uhakikishe kwamba Halmashauri ambazo zinategemea kilimo katika kujiendeleza na katika kukusanya mapato yao waweze kupata mapato hayo. Tunasisitiza na kuomba Waziri Mkuu uingilie kati ili Halmashauri hizi ziweze kulipwa ushuru wake.

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapo niachie na wenzangu maana yake hizo dakika saba hazitoshi lakini naomba hayo yawe ndiyo mchango wangu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Masoud, atafuatiwa na Mheshimiwa Machali.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Waziri Mkuu. Katika kurasa zote 25 za hotuba yako Mheshimiwa Waziri Mkuu sijaona mahali popote ambapo umeonesha juu ya nidhamu ya matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko makubwa kama ripoti ya Mwenyekiti wa Hesabu za Serikali za Mitaa (*LAAC*) ambayo aliisoma mwezi Novemba 2013, kwamba kuna wizi, ubadhirifu na ufisadi wa hali ya juu na utovu wa nidhamu wa hali ya juu kwa Wakurugenzi na Watendaji na malalamiko ya kuwahamisha watendaji na Wakurugenzi wa Halmashauri moja baada ya kufanya ubadhirifu na ufisadi kuwapeleka Halmashauri nyingine. Waziri Mkuu, katika hotuba yako jambo hili halipo, je, sasa kuna usafi wowote? Naomba utakapofanya majumuisho utueleze kuna kesi ngapi zilizopo Mahakamani juu ya watendaji waliofanya wizi, ubadhirifu na ufisadi na nini hatua zinazochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atueleze juu ya hali ilivyo, juu ya demokrasia ilivyominywa katika Mikoa ya Lindi na Mtwara ambapo vyama vya siasa vya upinzani vimenyimwa fursa ya kufanya mikutano yake ya hadhara. Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992, Sura ya 258 imeruhusu juu ya jambo hilo, katika kifungu cha 11(1). Je, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hili mna mkakati gani wa ziada kuhakikisha kwamba Vyama vya Upinzani vinapata fursa ya kufanya shughuli zake za siasa katika Mikoa ya Lindi na Mtwara? Isionekane kwamba kesho kutwa kuna uchaguzi wa Serikali za Mitaa baadaye CCM ikapata nafasi kubwa ya kushinda mkaja hapa mkajisifia kwamba CCM inakubalika, kumbe mliminya kwa muda mrefu na kisingizio kwamba hakuna amani, siyo kweli, amani ipo. Mkoa wa Lindi haukuwa katika vurugu lakini nako kumepigwa marufuku kufanya shughuli za siasa. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuja hapa atueleze mkakati za ziada kuviruhusu Vyama vya Upinzani kufanya shughuli za siasa katika Mikoa ya Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, Ustawishaji wa Makao Makuu Dodoma (CDA). Chombo hiki kimeundwa kusimamia na kukuza makao makuu kwa lengo la kusaidia mpango wa Serikali kuweza kuhamia hapa Dodoma. Mwenyekiti wa Bodi ya *CDA* ni Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi. Kwa hili nalo la Serikali kushindwa kuhamia hapa Dodoma mtu wa kwanza kuulizwa ni Mheshimiwa Lukuvi. Mheshimiwa Lukuvi ndiye Mwenyekiti wa Bodi hii na kwa sababu ameshindwa, atueleze hapa mpango gani ambao unafanywa kuweza kuwahamisha baadhi ya maskini kuwapeleka maeneo mengine na hata fidia wasiweze kupewa. Naomba Mheshimiwa Lukuvi aliangalie suala hili ustawishaji wake wa Makao Makuu uwe ni ustawishaji wa kweli na usiwe ustawishaji ule wa kuwagawa na kuwachochea watu.

**SPIKA:** Kwa mujibu wa Kanuni zetu, Waziri yeyote anatamkwa kwa cheo chake. Maana ukisema Lukuvi sisi hatuelewi ni rafiki yako wa wapi.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera na Uratibu na Bunge, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, ni vema aangalie utaratibu ulio mzuri wa kuweza kustawisha Makao Makuu Dodoma na Serikali kuhamia Dodoma kuliko kustawisha chuki, ubaguzi ndani ya jamii kitu ambacho haileti taswira nzuri. Hili ni jambo kubwa, ni jambo zuri ambalo linapaswa kuangaliwa na yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, wahamiaji haramu wameanza kurudi Mkoa wa Kagera, Wilaya ya Karagwe na Misenyi na imebainika kwamba Watendaji wa Vijiji ambao wengi ni wa Chama cha Mapinduzi ndiyo wanaochukua rushwa katika Wilaya ya Karagwe na Misenyi. Kulikuwa na operesheni Tokomeza lakini baada ya operesheni hii fedha nyingi za Serikali zikatumika lakini watendaji hao hao sasa hivi wanatumia rushwa, hii imekuwa ni danganya toto. Serikali itueleze ina mkakati gani wa ziada kuhakikisha wahamiaji hawa haramu na Watendaji

wale wa Vijiji na Vitongoji katika Wilaya za Karagwe na Misenyi wanachukuliwa hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, mwisho, katika hali ambayo si ya kawaida suala ambalo nataka kulisisitiza kwamba Mkoa wa Lindi hakukutokea fujo yoyote kwa kipindi kile na kwa sababu wao ni miongoni mwa waliopata zuio la kufanya shughuli zao za kisiasa ni kwa nini basi Mkoa wa Lindi usipewe fursa ya kufanya shughuli zao za kisiasa kadri inavyowezekana? Jambo hili la kudhibiti Vyama vya Upinzani na umebakia muda mdogo kufanya shughuli za kisiasa kuelekea chaguzi za Serikali za Mitaa, halikubaliki. Ni vema Serikali ikae iangalie utaratibu mzuri wa kuweza kuviruhusu Vyama vya Upinzani kufanya shughuli zake katika Mikoa ya Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Spika, hili jambo siyo jambo la mchezo na siyo jambo la kubeza. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati akifanya majumuisho awaeleze Watanzania ni njia zipi utatumia kuwaruhusu Vyama vya Upinzani kufanya shughuli zake za kisiasa katika Mikoa ya Lindi na Mtwara? Isionekane Chama cha Mapinduzi Serikali za Mitaa wameshinda kesho kutwa wakajipatia sifa kumbe sisi mlituzuia kwa muda mrefu jambo ambalo halikubaliki. Mheshimiwa Waziri Mkuu, najua uwezo bado unao na kwa utaratibu wako ambao ninakuelewa nakuomba suala hili ulitafutie ufumbuzi unaostahili wakati huu kabla ya muda wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakapowadia.

Mheshimiwa Spika, baada ya haya machache, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimuite Mheshimiwa Machali!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa fursa nami nichangie kwenye hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naomba nijikite kwenye maeneo kama matatu tu ambayo ninaamini kwamba ndiyo tatizo kubwa ambalo linaikabili nchi yetu hususani Mkoa wa Kigoma. Nitaanza na sekta ya barabara. Ni aibu na maajabu kuona Serikali ikiwa inatenga bajeti kwa miaka minne mfululizo halafu hakuna hata shilingi moja iliyopelekwa na kazi ikafanyika, ni aibu na ni maajabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu wakati huo ilitenga kiasi cha zaidi ya bilioni sita kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kutoka Kigoma-Kidahwe-Kasulu-Kibondo-Nyakanazi haikutoka hata shilingi moja na wakazi wa Mkoa wa Kigoma tumedanganywa kwa mwaka huo. Mwaka uliofuata 2011/2012 zilitengwa shilingi bilioni mbili na milioni mia tatu hali kadhalika hata shilingi moja haikutolewa. Mwaka 2012/2013

zilitengwa shilingi bilioni tatu na milioni mia tano kwa ajili ya kuanza kuijenga barabara hiyo hakuna hata shilingi moja iliyotolewa. Mwaka huu ambao ni mwaka wa fedha 2013/2014 zimetengwa shilingi bilioni kumi na barabara ilikuwa imetangazwa tunaelekea mwisho wa mwaka hakuna kazi yoyote ambayo imefanyika. Serikali itaendelea kuwadanganya mpaka lini wakazi wa Mkoa wa Kigoma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ifike mahali, ni aibu kusema kwamba tuna Serikali ambayo iko makini na ambayo inawajali watu wake kwa kuendelea kuwapatia ahadi za uwongo uwongo. Ifike mahali watu wamuogope Mungu na waache kuwaahidi watu vitu ambavyo wameshindwa kuvitekeleza. Nitaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa kuwa mwaka jana alifanya ziara katika Mkoa wa Kigoma atueleze mchakato wa ujenzi wa barabara ya Kigoma-Kidahwe-Kasulu-Kibondo-Nyakanazi utakamilika lini nikiwa na maana ya barabara ile kuanza kujengwa. Ieleweke pia kwamba hata Kigoma kule ni Tanzania, si kwamba Tanzania ni maeneo mengine, tuna haki ya kuweza kujengewa barabara kwa kiwango cha lami kwa sababu ni wakazi wa Kigoma nao wanalipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutoa ahadi kwa miaka minne mfululizo, *fairness* iko wapi? Watueleze watu wa Kigoma wamekosea nini, kuna matatizo gani? Ninaomba kupata ufafanuzi ni nini hatma ya Wizara ya Ujenzi kuendelea kuwadanganya wakazi wa Kigoma barabara hiyo itajengwa kwa miaka minne mfululizo, bajeti inatengwa na barabara ilitangazwa kwamba ilikuwa *award* mzabuni mwaka jana mwezi wa nane wamekaa kimya ukiuliza wanasema tutajenga, tutajenga miaka minne inakwenda hakuna ambacho kimefanyika, nitaomba ufafanuzi kwa Serikali. Niseme kwamba tutaenda kuwaambia wakazi wa Kigoma mtazidi kupata taabu Chama cha Mpinduzi poleni sana, wanaelewa na wanaona ni kitu gani ambacho mnafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikimaliza hapo ni imani yangu nitakuwa nimeeleweka vizuri. Najielekeza pia kwenye sekta ya maji. Katika hali ya kusikitisha kuna mradi wa maji ambao hata mwaka jana nilizungumza unajengwa chini ya kiwango na Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya ziara Mkoa wa Kigoma na Jimboni kwangu Kasulu Mjini, Kijiji cha Nyumbigwa, nasikitika kiasi gani hatukuelewana katika lugha lakini naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba mradi ule baada ya kufungulia maji bomba zinapasuka na kulipuka kama vile ni mabomu kutoka ardhini. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nilizungumza lakini nilibezwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu ulishangazwa sana mimi kukueleza hatuna imani na mradi huu kwa sababu nyaraka zilifichwa. Wananchi wa kijiji cha Nyumbigwa wanaendelea kunipigia simu kupitia Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji, Serikali inachukua hatua gani dhidi ya wale wote ambao wamesababisha hasara kubwa, mradi wa zaidi

ya shilingi milioni mia nane, pesa zenyewe zimepatikana kwa shida kweli kweli na tumechukua muda mrefu mpaka mradi ule kuja kufikia hatua ya kuanza kujengwa lakini mradi huo inasikitisha sana inawezekana hatutautumia kwa muda mrefu. Tenki linavuja, mabomba yanapasuka, haiwezekani tukawa tunatafuta pesa kwa shida kama Taifa halafu matokeo yake watu wanafanya uchakachuaji, bidhaa zinazonunuliwa zinaonekana ni hafifu halafu tunawaacha watu, Wahandisi wa Maji, Wakurugenzi na watu wengine wanapiga *deal* Serikali mnawaangalia! Mnataka tuwaeleze namna gani ili kusudi muweze kutuelewa?

Mheshimiwa Spika, wananchi ni hawa, *BOQ*s nilieleza hapa zilifichwa. Mbunge anakwenda kuomba *BOQ* ili kuweza kufuatilia kwamba hivi huu mradi unajengwa kwa viwango vinavyotakiwa? Wale *beneficiaries* ambao ni wakazi wa kijiji ambao wanapelekewa maji wameomba *BOQ* wamenyimwa! Mnataka tuwaelezeje ili kusudi mtuelewe?

Mheshimiwa Spika, nitaomba kupata ufafanuzi nini hatma ya mradi ule wa maji katika kijiji cha Nyumbigwa ambao hata Mhandisi Mshauri leo hii ameshaondoka na mradi haujakamilika.

**SPIKA:** Ahsante muda umeisha.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba ufafanuzi katika maeneo hayo, mengine nitaandika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Serukamba ulitaka kusema nini?

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kumpa taarifa muongeaji aliyemaliza sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Wizara ya Ujenzi iko chini ya Kamati yetu. Barabara ya kutoka Kigoma mpaka Nyakanazi ni barabara ambayo imekuwa inajengwa kwa vipande vipande. Nimeamua kutoa taarifa hii kwa sababu Mheshimiwa Machali anataka kuwadanganya watu wa Kigoma kwamba jambo hili siyo la kweli wakati barabara ya kutoka Kidahwe mpaka Kasulu tayari imesainiwa, tumepata mkandarasi. Barabara ya kutoka Nyakanazi mpaka kuja Kasanda tayari imesainiwa na tumepata mkandarasi. Fedha ambazo zilitengwa mwaka jana na mwaka juzi zilisaidia katika kufanya *feasibility study*, kufanya *design* na sasa tunaanza ujenzi.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kumpa taarifa hiyo. *(Makofi)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, taarifa yake siipokei kwa sababu haina ukweli na nilikuwa Kamati ya Miundombinu nikiwa naye...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, ninyi mnaanza fujo sasa, nataka tujadili. Mheshimiwa Mchungaji naomba uendelee.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie. Nianze kwa kutoa pole kwa wakazi wa Manispaa ya Iringa na Vitongoji vyake kwa kufiwa na Kamanda makini Gervace Kalolo ambaye awali alikuwa ni Diwani wa CCM lakini baadaye alikimbia Chama cha Mapinduzi akaingia CHADEMA baada ya kuona kuna ufisadi katika Manispaa yetu. Niwape pole kwamba tumepotelewa na pengo lake ni gumu sana kuliziba na Mungu akipenda kesho tutakwenda kushiriki mazishi pale Iringa Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema Manispaa yangu ya Iringa Mjini tulijitahidi sana tukajenga Hospitali ambayo tuliamini kwamba itapunguza msongamano katika hospitali ya Mkoa ambayo ni ya Rufaa. Nashukuru kwamba kwa namna fulani Serikali ilitoa shilingi milioni mia tatu kusaidia ujenzi na maendelezo ya Hospitali ile. Lengo kubwa lilikuwa ni kupunguza msongamano katika hospitali ya rufaa, hospitali ile ya Manispaa ambayo wananchi wengi wa Manispaa ya Iringa wakienda katika hospitali ile wanapata matatizo makubwa kwa sababu kumuona Dokta unalipa shilingi elfu tano, usipopata matibabu kesho tena ukimwona ni shilingi elfu tano inakuwa ni tatizo kubwa kwa sababu Madaktari katika hospitali ya Rufaa wanaamini kwamba katika ile hospitali ya Manispaa kuna huduma zote.

Mheshimiwa Spika, ningeomba ofisi ya Waziri Mkuu iangalie kwa makini kuiboresha hospitali ya Manispaa ili tupunguze msongamano uliopo katika hospitali ya rufaa ambayo inahudumia maeneo mbalimbali likiwemo na Jimbo la Mheshimiwa Lukuvi na wengine wengi inawasaidia sana hii hospitali. Tulitoa maombi maalum katika hospitali hii ya Manispaa kuomba shilingi milioni mia tano lakini katika ombi hili hatujajibiwa. Ningeomba Waziri Mkuu uliangalie kwa makini suala hili ili tupate hizi shilingi milioni mia tano kwa ajili ya kujenga maabara ambayo itaweza kusaidia wakazi wa Manispaa ya Iringa.

Mheshimiwa Spika, naomba wakazi wa Manispaa ya Iringa, kuna propaganda zinazosema ukiwa Mbunge wa Upinzani huwezi kusikilizwa. Ili muoneshe kwamba hambagui mnatenda haki, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu ulifanyie kazi, naomba hizo milioni mia tano ziende katika hiyo hospitali ya Manispaa ili itatue tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni barabara. Hizi pesa za barabara ambazo mnazitoa ningeshauri muwe mnaangalia mazingira ya eneo na eneo.

Manispaa yangu ya Iringa ina milima na mabonde. Sasa mvua ikinyesha madhara yanayopatikana hayalingani na madhara ya maeneo mengine. Tulikuwa tunapata shilingi bilioni mia mbili mwaka huu mmetutengea shilingi milioni mia saba hazitoshi na Mji ule umekaa kimaendeleo, tunavyo vyuo vingi, ni Mji wa kihistoria. Ningeomba Ofisi ya Waziri Mkuu muangalie hizo pesa kwa sababu kuna mawe mvua ikinyesha inaharibu zaidi barabara hiyo. Mwanzo tulikuwa tunapata shilingi bilioni mia mbili sasa wametuletea shilingi milioni mia saba ambazo hazitoshi na sasa hivi barabara siyo nzuri ni kero kwa wakazi wa Manispaa ya Iringa.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambalo ningependa kulizungumza ni suala la matengenezo ya shule za msingi. Shule nyingi za msingi zimetelekezwa, mmejielekeza zaidi kwenye shule za sekondari lakini shule nyingi za msingi ni za kizamani nyingine zilijengwa toka wakati wa mkoloni hazijapata matengenezo ya kutosha. Kwa mfano shule ya Kitwiru katika Kata ya Kitwiru, shule ya Mkoga, Mawelewele, Mshindo, shule zile zina hali mbaya. Ningeomba pesa inayokuja isaidie kupunguza matatizo haya.

Mheshimiwa Spika, nimezungumza masuala ya hospitali, akina mama wengi wanapata matatizo, afya ya mtoto na mama bado ni shida, dawa hakuna, wazee ambao mliwaahidi kwamba mtawatibu bure hamjawatibu kama mlivyowaahidi. Naomba suala hili tuliangalie kwa kina, Mawaziri msaidie ili muoneshe kwamba hampendelei. Maana wengine wanasema eti maendeleo mnapeleka tu kwenye Majimbo ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la maji tuna matatizo kidogo lakini asilimia 95 Jimbo la Manispaa ya Iringa lina maji ya kutosha. Hilo naweza kusema nampongeza Waziri wa Maji ametusaidia kwa sehemu kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa watu wengine wamesimama wanazungumzia suala la amani na utulivu. Katika maeneo ya utawala bora ndugu zangu naomba niseme hii nchi ni ya wote. Kwa bahati mbaya amani na utulivu imekuwa ni kichaka, mnafanya maovu halafu mnakimbilia kwa watu na kusema amani na utulivu. Tunaomba amani na utulivu msituchokoze, msichokoze watu wakidai haki zao, tukiomba hela zisiibiwe, tukitaka haki mnaenda kwenye vyombo vya habari, mnasema amani na utulivu, mnatumia amani na utulivu kama *stepping stone* kuficha maovu yenu. Mwogopeni Mungu, hakuna mtu anayetaka kuvuruga nchi hii. Ninapodai haki au tunapodai haki msikimbilie amani na utulivu. Mmetuambia tusifanye mikutano Lindi na Mtwara lakini juzi juzi *First Lady* anaenda anafanya mikutano. Mnafanya mikutano ya Chama cha Mapinduzi halafu wengi mnajiita Wakristo mnamcha Mungu, tukidai hiyo haki mnasema amani na utulivu, kimekuwa ndiyo kichaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba tutende haki. Nyie mnaomcha Mungu ambao ni Wakristo na Waislam, Mungu anakataza kudanganya, tutende haki, tushirikiane wote kwa pamoja. Msibadilishe magoli kila wakati, tunapotaka kufunga kwenye goli lenu mnahamisha tena, amani na utulivu. Tukitaka tuwapige chenga kufunga mnahamisha goli, amani na utulivu. Hatuwezi kuendelea kwa stahili hiyo na hii ni ya wote. Mwisho wa siku katika vita vya kiraia hakuna atakayeshinda. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, niseme watu wanaokimbilia kusema nchi hii Jeshi litachukua, mimi niwaulize Mheshimiwa Lukuvi rafiki yangu na kaka yangu, kwani Jeshi likichukua wewe utakuwa wapi? Wewe utakuwa sehemu ya Jeshi? Si na wewe utakuwa raia? Kwa hiyo, wote tutaitikia nguvu ya Jeshi hiyohiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kukimbilia kwamba Jeshi litachukua nchi, kutisha watu, tusitishane. Tukae kama watu wazima ambao taifa limetuamini, tushirikiane wote kwa pamoja. Nimalizie kwa kusema, nina imani na Mawaziri kwamba tunapomalizia mwisho, pamoja na kwamba Serikali imechoka na imeshindwa, lakini kipindi hiki cha mwisho tusaidiane, tuwatumikie wananchi kama tulivyoahidi, maana yake ahadi nyingi hamjazimaliza. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ulianza kama Mchungaji ukamaliza sijui kama nani. Mheshimiwa Anna Abdallah. *(Kicheko)*

**MHE. ANNA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Naomba radhi sana sauti yangu siyo nzuri nina mafua lakini na mimi naomba nichangie hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kutokana na hotuba ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni pamoja na ile ya Msemaji wa Waziri Mkuu wa Upinzani, naomba tu niseme kwamba kutumia Bunge ni haki kuizungumzia mambo ya Bunge Maalum. Mmoja hapa anasema kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu ndiyo Tanganyika, kwa nini mmeondoka kwenye Bunge la Maalum, si mngekaa mkayasema hayo kule? S hata mkiyasema, sisi hatuna uwezo nayo, wala hatuwezi kuyajadili, habari za Bunge Maalum kuna mahali pake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri mambo mengine humu, kwa mfano mwingine anasema kwamba eti Rais Kikwete ndiye aliyewaongoza Mawaziri wake na Viongozi wa Serikali na wa CCM kujadili Rasimu kwa kutukanana, kudharauliana, kutuhumiana, kubezana na kadhalika na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme hivi, kwanza siyo vyema kutumia jina la Rais kwa mambo ambayo siyo ya kweli. Lini alituambia tutukanane? Humu

ndani hakuna upande unaoweza ukasema wenyewe haukutukana mwenzake. Iweje leo upande mmoja ndiyo unaumia zaidi wakati kila upande ulikuwa utukana matusi yao na maneno yao, yamo kwenye rekodi. Kwa hiyo, nasema wakati mwingine yule anayepiga kelele sana pengine ndiyo anataka kuhurumiwa zaidi lakini, mimi nafikiri jambo hili halifai na hapa siyo mahali pa Bunge la Katiba, hebu njooni, ingawaje mnasema hamtarudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mnasema lazima tufanye uchaguzi. Katiba Mpya hiyo mnayoitaka ya uchaguzi itapatikanaje? Ni huko kuzunguka huko Mikoani kwenda kusema mtaipata huko na kama vitisho hata humu humu kuna vitisho. Mnasema eti tutafanya uchaguzi, tutafanya mabadiliko, utafanyaje mabadiliko bila kuwa na Bunge? Kwani maana yake hatuijui? Kwa hiyo, mnaona Mheshimiwa Lukuvi aliyoyasema kuhusu Jeshi lakini kwenda kufanya mabadiliko ili kufanya uchaguzi kwa Katiba Mpya bila kutumia Bunge hiyo ni sawa, hiyo siyo vitisho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 30 Aprili, 2014 kule Dar es Salaam tulifanya kikao, mkatupa *overview* ya bajeti Waziri wa Fedha na mwenzake wa Mipango na Waziri Mkuu katika kumalizia akasema kwamba angeomba au anatarajia kwamba tutaingia katika bajeti mpya bila madeni. Hata hivyo, naomba nimhakikishie kwamba madeni tutakayoingia nayo katika bajeti itakayokuja ni makubwa mno. Kwa sababu tunao ushahidi kabisa kwamba katika baadhi ya maeneo hakuna hata senti moja ya miradi ya maendeleo iliyotolewa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kama mwaka huu tunaomalizia hela haikutoka, mwakani tena tutaweka. Sasa sijui tunatekeleza hii ambayo hatukutekeleza mwaka huu ama ndiyo tunafuta, tunaanza ya mwakani? Kwa kweli hili ni tatizo kubwa. Licha ya hivyo kuna madeni makubwa ya wafanyakazi mbalimbali. Sasa hivi wanazungumzia madeni zaidi ya Walimu, lakini kuna wafanyakazi mbalimbali wa Serikali wana madeni makubwa mno wanayodai. Sasa mimi sijui itakuwaje kuingia kwenye bajeti ijayo bila madeni hayo kwanza kufutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe katika kusema pale ile tarehe 30 ulizungumzia juu ya Sheria ya Bajeti, mimi naiunga mkono. Hata hivyo, nakuomba hivi, maadam umefanikiwa kubadilisha hata hii program nzima ya bajeti hii tuliyonayo sasa, ni kwa ajili ya *initiative* yako. Ninakuomba hii Sheria ya Bajeti kabla hatujafika bajeti ijayo tuwe tumekwishaipitisha na uanzishe mchakato wewe ndani ya Ofisi yako ili tuipitishe lakini tusiingojee Serikali kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kuhusu maafa. Mimi nashangaa, maafa nchi hii ni mafuriko, njaa lakini kuna watu wamepata maafa zaidi ya hapo. Mimi ni mmojawapo, tuliunguziwa nyumba tena na baadhi ya Wabunge humu

tuko wanne. Waliotusaidia angalau kwa chembe kidogo ni Wabunge wa CCM wenzetu, walichangishana wakatusaidia tukapata angalau shilingi milioni nne kila mmoja lakini hakuna mfuko wowote wa maafa uliotusaidia kwa jambo lolote mpaka hivi leo. Tumenyamaza mwisho tumeona jamani tuseme kunani? Kwa hiyo, tunaomba na hiyo mtujibu ili tuweze kujua tunakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu hata watu wenyewe waliofanya zile fujo hivi kweli Serikali haiwezi hata mtu mmoja ku-*pinpoint* kwamba ni wewe hamna yaani ni mambo ya ajabu sana. Kwa hiyo, tunaomba sana, mambo haya yaangaliwe.

Mheshimiwa Spika, mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Ngeleja atafuatiwa na Mheshimiwa Capt. Komba.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami naungana na wenzangu waliotangulia waliounga hoja hii mkono.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya asilimia 60 ya nguvu kazi ya Watanzania ni vijana. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, yako maelezo mazuri kuhusu uimarishaji wa Mfuko wa Vijana. Ombi langu, Serikali ione pamoja na wadau wengine zikiwemo sekta binafsi namna ya kuimarisha Mfuko huu wa Maendeleo ya Vijana kwa sababu ya umuhimu tu wa kundi hili lakini pia Mfuko wa Maendeleo ya Wakawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miaka mitatu iliyopita Serikali ilitupa habari njema kuhusu Kilimo Kwanza na moja ambayo yalijitokeza miaka miwili, mitatu iliyopita ilikuwa ni uanzishaji wa bima ya kilimo kwa ajili ya moja, ni kusaidia tu kupata fidia ama kuzima ama kuzuia hasara ya mazao ya wakulima lakini pia kuwawezesha kupata mikopo na mambo mengine ambayo yanaweza kuimarisha kilimo chao. Naomba ufafanuzi kwa sababu kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nafahamu tutakapofika pengine Wizara ya Kilimo tunaweza kupata maelezo haya lakini kwa sababu hotuba hii ndiyo hotuba elekezi kwa kweli, hotuba kiongozi kwenye hizi *sector ministries,* nilikuwa naomba, tupate ufafanuzi ili tujue.

Mheshimiwa Spika, nalisema hili kama alivyosema Mheshimiwa Ndassa, sisi wakulima wa pamba mwaka huu tumeathirika sana. Yako baadhi ya maeneo ambayo tumepata mbegu ambazo hazikuota na tunaamini kwamba kupitia mpango huo wakulima wa pamba wangeweza kunufaika pamoja na wakulima

wa mazao mengine. Kwa hiyo, tunaomba ufafanuzi kuhusu maendeleo ya uanzishaji wa bima ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kusema ni hili suala la *Airport* la Mwanza kwenye hotuba hii inajitokeza kama ni ukarabati. Hata hivyo, miaka yote tumekuwa tukiaminishwa kwamba ni matengenezo mahsusi kuimarisha ile *Airport* iwe *Airport* ya kimataifa na ukizingatia mahali ilipo tunaambiwa kwamba kile ni kitovu cha Ukanda wa Maziwa Makuu. Sasa taarifa inayojitokeza hapa ni ya ukarabati, nadhani ama pengine ni tatizo la uandishi, ni *typographic error,* basi tuna-*assume* kwamba limekosewa kiuandishi, lakini nia inayokusudiwa ni uimarishaji wa *airport* ya Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, msongamano wa magari Dar es Salaam. Tunaaminishwa na taarifa mbalimbali za kitakwimu kwamba uchumi wa Tanzania kwa zaidi ya asilimia 60 ama takriban asilimia 70 kwa ujumla wake unategemea na uwekezaji uliofanywa katika Jiji la Dar es Salaam. Sasa kama ukweli ndiyo huo, ombi langu pamoja na mambo ambayo tumekuwa tukiyasikia kwamba madhara ambayo tunayapata kama Watanzania wanaoishi Dar es Salaam ama wanaokuja kufanya shughuli zao kutokana na msongamano wa magari, natoa rai na kuishauri Serikali ifikirie kulifanya Jiji la Dar es Salaam kuwa Wizara Maalum. Ilishafanyika katika nchi zingine tunafahamu, kwa hadhi iliyonayo inastahili kabisa kupewa hiyo heshima ya kuwa Jiji Maalum ili tutenge fedha na rasilimali za kutosha kwa ajili ya kushughulikia maendeleo na kurahisisha namna ya watu kusafiri katika Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba ya wenzetu hapa imesema mambo mengi lakini kama walivyosema waliotangulia huu siyo mjadala wa Bunge Maalum. Hata hivyo, yapo mambo mazito yaamesemwa lazima tuyaseme hapa. Tusipoyasema hata kama ni kidogo madhara yake ni makubwa sana. Watanzania wataendelea kuaminishwa mambo ambayo siyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli wenzetu wamechepuka tena kwa mara nyingine kama kawaida yao katika mjadala. Kwa sababu mjadala huu ni wa bajeti wenzetu wamekuja na mjadala wa Bunge Maalum. Tuna fursa hiyo mwezi wa nane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo moja lililonifanya niongelee hii habari, ni ule ukurasa wa saba…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, naamini ni kengele ya kwanza hiyo? Kwa hiyo, kuna dakika mbili au tatu.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa saba tunaaminishwa katika taarifa hii kwamba eti katika lile kundi kwa mujibu wa Sheria la watu 201, Chama cha Mapinduzi kimechomeka makada wake kutumia kivuli cha Taasisi mbalimbali ikitajwa ya Waganga wa kienyeji, hilo kwa sababu Mheshimiwa Kingunge ni mtani wangu tunaweza kuliacha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini linalofuatia pale la hawa viongozi wa kidini, Taasisi za kidini, siamini kama tumefikia hapo Watanzania leo kutowaamini hata viongozi wa kiroho. Kama tumefikia hatua hiyo ni hatari kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamua kulisema hili ili Watanzania wafahamu na waelewe, maneno yanayotumika katika Bunge hili kwa Kambi ambayo tunaamini kwamba ndiyo inaweza kuwa na mawazo mbadala kwetu sisi tunaoongoza Serikali hii kwamba hata taasisi za kidini hizi haziaminiwi bali walichokileta hapa ni mjumuiko wa makada wa Chama cha Mapinduzi. Mimi nasema hili tuliangalie, Watanzania wafahamu tu waendelee kupembua mchele na pumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lingine hili ambalo Mheshimiwa Rais anatuhumiwa kwamba ameongoza kama alivyosema Mheshimiwa Mama Anna Abdallah, si sahihi hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, imesemwa sababu nyingine ukurasa wa 13 wa hii hotuba, eti sababu pekee iliyofanya tuahirishe ule mjadala wa Bunge Maalum ni kwa sababu ya hofu ya kutopata ile theluthi mbili lakini tunafahamu wote kwamba suala la mjadala wa bajeti ni suala la kikatiba. Sasa Watanzania hapa wanazidi kuelezwa mambo ambayo si sahihi na naamini kwamba hatustahili kuacha yaendelee hata kama siyo jukwaa lake.

Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Nitamwita Mheshimiwa Capt. Komba atafuatiwa na Mheshimiwa Chomboh halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Muhongo.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza hii hotuba ya Kambi ya Upinzani hii aliyosoma Mheshimiwa Mbowe, naichukua tu kama vile jamaa anapigana na mtu mwenye nguvu kubwa kapigwa, majeraha kapata usoni, sasa anamwambia mtu mshike huyo nitammaliza wakati kamalizwa yeye. Ndiyo hii hotuba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, CHADEMA wamemalizwa humu ndani, CUF wamemalizwa humu ndani, sasa wanakuja hapa kwenye Bunge la Muungano wanasema mshike huyo, tutamuua, rudini kule tukatwangane kule, hapa siyo

sehemu yake. Siyo sehemu yake kabisa, njooni mpate makonde kule. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kweli umefanya mambo mengi sana na Mawaziri Wakuu wengine waliotangulia Mwalimu Nyerere, Kawawa, sijui nani na wengine wote, mmefanya mazuri mengi tu. Wako Mawaziri Wakuu wengine watakachokumbukwa ni kuharibu nchi hii na kuvuruga nchi hii na kuleta kitu ambacho kinaitwa hovyo hovyo tu na yeye mwenyewe ni wa hovyo hovyo tu. *(Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, mimi niseme kabisa kwamba unaweza kuwa Jaji lakini ukawa Jaji wa hovyo. Unaweza kuwa Jaji lakini usiwe Jaji mzuri ukawa Jaji wa hovyo. Mimi nafikiri wako Majaji wengine wa hovyo pia, siyo wote lakini wapo wa hovyo. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa walikuwa wakiongea kwa sauti za juu)*

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, mimi niseme katika hii, mchango wangu wa leo narudi Nyasa…

**SPIKA:** Naomba uvumilivu, kama wengine wamewavumilia na wengine wavumilie. Huo ni mwanzo, uvumilivu. Mvumilie kama mlivyovumiliwa. Kwa hiyo, tunaendelea. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, hawa watashika mpira kwapani sasa hivi hapa wataondoka, vumilia yakuingie, usishike mpira, acha yakuingie vizuri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kule kwangu kuna madini Mchuchuma na Ngaka lakini yale ya Ngaka sisi wananchi wa Nyasa hayatusaidii kabisa, yanavuruga barabara, yanaleta mashimo kwenye barabara, yanaleta vifua kwa wananchi, yanaleta vumbi kwa watu. Kwa hiyo, naomba kabisa mkataba kati ya wale wanaochimba Ngaka na wananchi ueleweke vizuri, wananchi wanapata faida gani na wao wanapata faida gani lakini tunaona wao wanapata faida, wananchi tunapata hasara. Naomba mkataba ule uwe *reviewed* kabla.

Mheshimiwa Spika, meli Nyasa, yamesemwa mengi, Nyasa meli itakuja, Nyasa meli itakuja mpaka yule mama Rais wa kule ameichukua meli yake, kwa hiyo, hatuna meli. Naomba hili suala la meli mwakani ndiyo uchaguzi, isije

mpaka mwakani meli ile haijafika, itakuwa ni aibu kwetu. Tunaomba meli ile iliyoahidiwa hapa ije Nyasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika viwanja ambavyo vimeandikwa, kiwanja cha Songea mtasikia sasa hivi kitapata ajali ya ndege. Unapotua kiwanja cha Songea kuna mashimo kama vile barabara ya vumbi lakini kiwanja ni cha lami. Kwa hiyo, ndege ikitua inaruka hivi, sasa ikiruka hivi mimi nina hakika baada ya muda itakuwa ni balaa. Naomba sana wanaohusika na viwanja wakaukague uwanja ule na mara moja waufanyie kazi ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, redio na *TV*. Ni kweli Songea sasa Mbinga, Namtumbo na maeneo mengine redio inasikika vizuri sana, tunawapongeza sana kwa hili. Bahati mbaya sana jiografia ya kule ni ngumu kidogo kwa sababu kuna milima inaitwa *Livingstone Mountains* ambayo zinatenga kati ya nchi iliyo milimani na nchi iliyoko Ziwani. Kwa hiyo, watu wa Ziwani bado kilio chao ni kilekile. Milima inakinga mawimbi ya redio na televisheni, kule mwambao kote kule hawapati redio wala televisheni. Tumechoka kusikia lugha ya Kichewa ya Kinyasa. Naomba tuleteeni redio, mlete *buster* pale mlete TV wananchi wa Nyasa wafaidike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *REA,* tangu wametangaza nimeona tu mara moja yule M-Srilanka amekuja pale, mimi ndiyo mkandarasi miezi sita imepita mpaka sasa mkandarasi haonekani na kazi haiendi vizuri. Naomba waendelee ili watu wa Mbambabay waweze kupata umeme tena mwaka huu isizidi mwezi wa saba. Kwa sababu tuliahidiwa ni mwezi wa tatu na leo ni mwezi wa tano.

Mheshimiwa Mbunge… *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo ni Mbunge.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Kwani yeye si Mbunge jamani? *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Sawa kabisa.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana namna unavyoliendesha Bunge hili, uendelee hivyo hivyo, Mungu akubariki. Kwa sababu umekuwa ni mvumilivu, kwa kweli asubuhi kama wana CCM wasingekuwa siyo wavumilivu ile hotuba ilikuwa inawatukana tu, inawatukana tu, inawatukana tu lakini umekaa kimya na sisi tumekaa kimya. Naomba uwasihi hawa jamaa hivi tunavyokwenda sasa tunaanza kujibu maswali yale ambayo kwenye hiki kitu ya hovyo hovyo imeandika humu. Sasa wavumilie kwa sababu mimi nimeanza bashrafu…

**MBUNGE FULANI:** Makamanda bado.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Makamanda wenyewe bado hawajafika, kwa hiyo, wavumilie. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, wengine wako kulia kwangu, wengine kushoto kwangu, wengine wako mbele. Wavumilie kwa sababu tulivumilia muda mrefu kusikiliza hotuba ile ambayo haikutupendekeza masikioni.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Chomboh.

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Mimi nilikuwa nakwenda moja kwa moja kwanza kwa kuisihi Serikali isimamie vizuri bajeti ambayo imeshatoka ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wizara zote kwa ujumla. Tatizo letu Tanzania ni kwamba maamuzi yetu au mipango yetu tunashindwa kuisimamia vizuri matokeo yake kila siku mambo hayaendi sawa kama vile tulivyokusudia.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nijikite zaidi kunako suala la ajali nyingi zinazotokea Tanzania hasa kupoteza maisha ya raia wetu. Madereva wa mabasi, madereva wa malori, wamekuwa ni watu ambao sio waangalifu, wanazitumia vibaya leseni zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naishauri Serikali, ilete Muswada hapa Bungeni kwamba leseni za madereva sasa zikatiwe *insurance* na hususan wale madereva ambao wanaendesha magari ya kuchukua abiria, wanaendesha tu kwa sababu wana leseni lakini hawana uangalifu wala hawana hofu. Yeye roho yake moja lakini dereva mmoja anaweza akapoteza mamia na maelfu ya wananchi kwa sababu tu ya uzembe na kwenda mwendo kasi na kutozingatia sheria za barabarani.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ilete Muswada huo kwamba madereva au leseni sasa zikatiwe *insurance*. Itakapokuwa mtu anafanya kosa kwa mara ya kwanza leseni yake inapungua *points,* inapungua *points* mpaka ikifika pale ambapo anakuwa *disqualified,* anafutiwa leseni kabisa. Hiyo itawapa wao uchungu na kuweza kuchunga umuhimu wa leseni. Wakate leseni za magari, lakini kila dereva lazima leseni yake ai-*insure* na hiyo *insurance* ikiwa leseni kubwa ya mabasi, Serikali itapata mapato kwa *insurance* hizo, lakini pia kuwapa funzo na kuwapa usimamizi mzuri madereva.

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapo nije kwenye hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ukurasa wa 14. Alizungumzia kidogo suala ambalo juzi lilitokea kule Zanzibar siku ya Mkutano wa Chama cha Mapinduzi kwa

wananchi wa Zanzibar. Amedanganya kitu kimoja kusema kwamba, katika Mkutano Katibu Mkuu wa CCM, Abrahaman Kinana, alisema kwamba, anawashauri Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wapeleke Muswada wa kuweza kuwauliza wananchi kama wanataka tena Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Katibu Mkuu hakusema hilo, huo ni uwongo. Mimi nilikuwepo, aliyesema hilo ni Mnadhimu Salmin Awadh Salimin. Mimi nilikuwepo, Msemaji wa Kambi ya Upinzani kadanganya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia alizungumza kuhusu huyu mtu anaitwa Ismail Jussa. Mimi nataka kuwaambia hawa ndugu zangu, sio ninyi CHADEMA wala ninyi *CUF* wanaomjua Jussa kuliko ninavyomjua mimi.

Mheshimiwa Spika, Jussa akisema yeye Mzanzibari, akiulizwa Zanzibar kwenu wapi, atasema Makunduchi. Babu yake Mkuu Mzee Alaiya aliyetoka huko India akamzaa babu yake yeye anaitwa Selemani Alaiya Kikoko, akamzaa mama yake yeye anaitwa Jenna, wamekaa katika mtaa wetu sisi. Tunapendana na wazee wake, tunaheshimiana na tunakaa kama ndugu, hakuna ubaguzi. Jussa habaguliwi, Jussa anajibagua na hajibagui kwa ninyi tu, anajibagua mpaka kwa familia yake yenyewe; hiyo familia yake niliyoitaja pia anajibagua. Namjua Jussa toka hajazaliwa. Siku ya harusi ya yeye mama yake kuolewa mimi niko barazani anaolewa mama yake, nakuambia sasa, nakuambieni. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea kwa sauti za juu kuonesha kutokubaliana na mzungumzaji)*

**SPIKA:** Naomba uvumilivu. Kama wenzenu wasingevumilia hotuba ile isingesomwa.

**MBUNGE FULANI:** Watoke nje.

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Spika, haya ninayoyazungumza…

**SPIKA:** Nasema hivi, kama wangeanza kufanya kama mnavyofanya ninyi ile hotuba isingesomwa, sasa na nyie muwe na uvumilivu. Tunachosema kama wenzetu wangefanya mnavyofanya msingesoma, muwe na uvumilivu, mkubali kuvumilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Chomboh endelea.

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Spika, mimi siyatoi mbali nayatoa kwenye Kitabu hiki.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea kwa sauti za juu kuonesha kutokubaliana na mzungumzaji)*

**SPIKA:** Nitatoa watu sasa hivi, nitatoa watu nje.

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Spika, hiki ni kitabu alichosoma Mwenyekiti wenu wa Kambi ya Upinzani na Mwenyekiti wa UKAWA na ndio maana nikaona kuna umuhimu wa kuwaambia nani Jussa?

**WABUNGE FULANI:** Sawa kabisa.

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Spika, Jussa kawasaliti mpaka wazee wake yeye, waliomzaa yeye. Jussa amesimama mara mbili, amekwenda Jimboni kwangu amesema juzi ya Mkutano wenu wa UKAWA akanitaja mimi akamtaja na Mheshimiwa Salmin kwamba sisi ni wasaliti. Mimi nitamsaliti wazee wangu waliopokea wazee wake wakakaa pale Zanzibar? Mimi siumwi na Zanzibar kuliko yeye?

Mheshimiwa Spika, mnajidanganya, hamumjui Jussa. Jussa ni msaliti namba moja. Sisi Zanzibar, hasa Makunduchi, hatumbagui Muhindi hata siku moja, tunaishi kama ndugu na mimi nawaheshimu sana. Kwa taarifa yenu basi, mama yake Jussa mimi namheshimu, Mungu amrehemu kama dada yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaambieni tena, mimi wazee wake Jussa, kuanzia wajomba zake tunaheshimiana na ninachelea kusema sana kwa sababu nitakuwa kama najitukana mwenyewe, hamumjui Jussa, msidanganywe. Jussa ni mtu ambaye mimi ninamjua sana na nitamwambia sana nitakapofika Jimboni, hamumjui Jussa.

Mheshimiwa Spika, nimemaliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Muhongo.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia fursa hii.

Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote wanaonisikia, kuna tofauti kati ya uzawa na ubinafsi. Kuna tofauti kati ya uzawa na ubabaishaji. Kuna tofauti kati ya uzawa na wizi. Kwa hiyo, mtu ambaye

ananyemelea mafuta na gesi na madini kwa kisingizio cha uzawa, lazima tumwangalie historia yake na biashara yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kurudia tena nilivyosema, mimi ni Mtaalam, hata Wafadhili wenu wananitambua mimi ni Mtaalam, ni kwamba, hii biashara ya mafuta na gesi tusidanganywe na watu wanaotaka kuwa mawakala, hawana uwezo wa kifedha, hawana uwezo wa teknolojia. Kazi wanayotaka wapewe vitalu, wakimbie Uarabuni, waende India, watafute watu wenye fedha na teknolojia na ninawahakikishia haiwezekani na haitafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa wale wanaosema wazawa wana fedha, niliwahi kuwaambia wajitokeze, ndugu zangu mambo yanayotoka Wizara ya Nishati na Madini ninapoongea chukua kalamu na karatasi, chukueni humu ndani na walioko nje wachukue, wazawa. Tunafunga maombi tarehe 15 Mei, kama wewe una uwezo wa kifedha na teknolojia kwa nini upige kelele, uwape watu *imprest* waje ku-*retire* humu Bungeni, ni afadhali uende ukaombe huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maombi peke yake ni dola za Marekani 700,000 zisizorudishwa. Ninawaomba kesho tuonane *TPDC* na hizo fedha. Takwimu ambazo ni lazima ununue gharama yake ni Dola la Marekani milioni 3.5, tuonane kesho *TPDC*. Utafutaji, ukichukua *3D* kwa *square kilometer* moja, eneo utakalopewa, *one square kilometer,* ni kati ya dola 15,000 na dola 20,000. Kuchoronga kwenye maji ya kina kirefu, siku moja unatumia dola za Marekani 1,000,000, nani yupo Mtanzania? Huo ukweli ukitoka nje unakatisha nani tamaa? Unakatisha tama wezi na wababaishaji. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Kweli.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, tundu moja kulimaliza, tundu moja, unatumia sio chini ya dola 1,000,000 na ukishagundua gesi au mafuta hapo, unahitaji sio chini ya matundu 12 ni 12,000,000, ni nani ninayemkatisha tamaa mimi? Nijiuzulu na mambo ya kitaalam haya, haiwezekani! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, halafu ukishaigundua hiyo gesi, kuchimba, kujenga bomba kwenda nchi kavu utatumia sio chini ya dola 200,000,000.

**WABUNGE FULANI:** Ooooh!

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Rais hawezi kunitoa kwa sababu hiyo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hiyo nimemaliza, mafuta ndugu zangu nasisitiza hayupo Mtanzania mwenye fedha hizi labda kama anatudanganya anataka kuwa wakala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile duniani kote, kama ninyi mmesoma vizuri na mnazunguka dunia mnaijua, makampuni makubwa yanayotafuta gesi na mafuta duniani hayavuki 10. Hakuna mambo ya uzawa hapa kukatisha mtu tamaa, tunakatisha tamaa wezi na wababaishaji. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, haya nakuja Mererani. Sasa mafuta tu ni kina kirefu twende Mererani mahali ambapo ni vitu vya bei ya chini kabisa Mererani ndugu zangu kuna leseni 597, wanaolipa kodi ni 10 peke yake na kwa miaka sita kila mwaka wamelipa 5,000,000 fedha za Tanzania, hawa tunataka tuwatie moyo hawa wababaishaji hawa? Kwa nini hawalipi kodi zetu na hata yule aliyemfadhili kuja kutoa *imprest* yake wana migodi hawajalipa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, Serikali yetu imedhamiria kuwasaidia Watanzania. Juzi mmeona wachimbaji wadogo tunawapatia dola 50,000 na mwezi huu vilevile…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa!

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, anachukua dakika zangu huyu; utaniongezea muda, anachukua dakika zangu.

**MBUNGE FULANI:** Ana taarifa.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Hana taarifa. Haya mambo ya kitaaluma, hana taarifa huyo, hana taarifa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni kwamba Serikali sasa hivi inawawezesha wachimbaji wadogo na maeneo, niliwahi kusema hapa leseni za utafutaji wa madini nchi nzima 70%...

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Naomba aendelee Profesa.

**MBUNGE FULANI:** Mbona Serukamba ulimpa?

**SPIKA:** Ninaendesha Kikao mimi, sio mtu mwingine, naomba mkae. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mbona ulimpa Serukamba?

**SPIKA:** Haya, endelea Mheshimiwa, endelea Profesa.

**MBUNGE FULANI:** Muache akimaliza usimame.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mzee naye anataka ku-*retire* naye *imprest* hapa.

**SPIKA:** Endelea na wewe Profesa!

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, watu walio na leseni za kutafuta madini nchini 70% iko mikononi mwa Watanzania na tumeamua kuwafutia. Hawa wengine wanaolalamika ni ambao hawajalipa kodi kwenye migodi, wala hawalipi mafao ya wafanyakazi kwenye migodi na sasa tumeanza taratibu za kuwanyang'anya. Kufikia mwezi Aprili tulikuwa tumewanyang'anya leseni 174 na mwezi huu ninawanyang'anya leseni 78 na nyingine za uchimbaji 34 na kuwanyang'anya tumechukua kisayansi, tunaenda *latitude* kwa *latitude*. Tumeanzia *Lake Victoria* mpaka tutashuka *Lake Nyasa*. Kwa hiyo, ndugu zangu ambao mmeshika maeneo lazima mtanyang'anywa na maeneo watapewa wachimbaji wadogo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kafulila?

**TAARIFA**

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa napenda kutoa taarifa kwa mzungumzaji anayemaliza kwamba, katika ujenzi wa uchumi duniani kote uwe wa madini uwe wa gesi, nimesoma kitabu kinaitwa '*the Resource Curse*' yaani Laana ya Rasilimali, Bingwa wa Masuala ya Mijadala ya Utandawazi Duniani, Joseph **Stigris**, amesema kwamba moja ya nguzo muhimu sana ya kuhakikisha makampuni ya nje hayaibii wazawa lakini pia uchumi unasaidia wazawa ni ushiriki wa wazawa kwenye umiliki wa mali zao wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilipenda kutoa taarifa hiyo kwa Bunge lako Tukufu kwamba, hoja ya mitaji na ukubwa wa mitaji ni kweli lakini bado kama Serikali kwa sababu hii nchi ni ya kwetu kuna umuhimu wa kuona kwamba hoja ya ushiriki wa wazawa kwenye uwekezaji huu wa jambo hili muhimu ni jambo ambalo halipaswi kubezwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, Mtaalam Profesa, naomba ujibu?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba sisi Watanzania hayo unayoyasema tumekabidhi Shirika la Umma *TPDC,* kwa nini hulitaki? Hayo unayoyasema tumekabidhi Shirika la Madini *STAMICO.* Huyo Stigris umesema ni Mtaalam wa Uchumi Duniani na mimi ni Mtaalam wa Jiolojia Duniani. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea. Mheshimiwa Mabumba, atafuatiwa na Mheshimiwa Zambi.

**MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, napenda kwanza nizungumzie jambo ambalo sikutaka kulizungumzia kutoka kwenye hotuba ya Kiongozi wa Upinzani. Amesema hapa kwamba Tanzania Bara ambayo yeye ameiita Tanganyika ni mkoloni anayeitawala Zanzibar kwa nguvu lakini sifa ya koloni linapokuwa linatawala mahali huwa linateua Gavana. Napenda atuambie Gavana wa Tanganyika ambaye yuko Zanzibar ni nani? Kama hayupo basi afute kauli hiyo kwa sababu anadanganya wananchi, hakuna koloni, Zanzibar ni nchi huru, Zanzibar ina Rais kachaguliwa na Wazanzibari wote katika uchaguzi huru kabisa; hakuna koloni linaloitwa Zanzibar, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nianze kuchangia; naipongeza sana hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na pia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. Pia, naipongeza Serikali kwamba bajeti zetu sasa zinazingatia kwanza, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ambacho ndio Chama Tawala, lazima itekelezwe, pili MKUKUTA II, tatu Dira ya Taifa ya 2025, nne malengo ya Milenia na Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa.

Mheshimiwa Spika, mipango hii ni mizuri sana kulipeleka Taifa letu hatua ya mbele ya maendeleo lakini jambo moja niiombe Serikali, bajeti karibu zote asilimia kubwa ya fedha imepelekwa katika mishahara na matumizi mengineyo, fedha ya maendeleo imewekwa katika asilimia isiyozidi 20. Sasa ili kufikia mipango hii ambayo nimeitaja ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake ameielezea haiwezi kufikiwa iwapo asilimia chini ya 20 ndio fedha za maendeleo. Huwezi kuifikia Dira ya 2025, wala malengo ya Milenia, wala MKUKUTA au kutekeleza kwa ukamilifu Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, naiomba Serikali yangu iwekeze fedha nyingi katika miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia napenda niipongeze Kamati ya TAMISEMI chini ya uongozi wa Mwenyekiti Dokta Hamis Kigwangalla imeelekeza sasa

Mikoa yote nchini itenge 60% katika fedha za mapato ya ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Serikali itusaidie kuhakikisha kwamba Wakuu wa Mikoa wanapata nguvu ya kusimamia na kuwawajibisha Watendaji katika Halmashauri kwa sababu mara nyingi kumekuwa na upotevu wa fedha katika maeneo haya, kwa hiyo, hata lile lengo la kusimamia miradi ya maendeleo haliwezi kufikiwa. Naomba hii 60% itengwe lakini matumizi ya fedha kwa uadilifu yahakikishwe kwamba fedha hizi zinatumika vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, nataka nizungumzie kuhusu mauaji ya wanawake kama ambavyo hotuba imeripoti. Naomba sana Serikali yetu ilete Muswada hapa Bungeni, tutunge Sheria kali kwa wauaji ambao wanawaua akinamama hawa katika Mikoa yote. Unapouwa akinamama maana yake ni Taifa haliwezi kuongezeka na Wanaharakati waache kupinga. Tutunge Sheria ambayo itapeleka adhabu ya kunyonga hawa wauaji na Wanaharakati waache kufanya harakati za kupinga adhabu ya kunyonga wauaji kama hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia napenda nizungumzie uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Kwa vile takwimu za sensa 2012 zinaonesha idadi kubwa ya Watanzania ni akinamama, naomba Serikali ifanye maamuzi ya makusudi, iweke hela nyingi sana kusaidia akina mama popote hapa nchini. Kuwawezesha akinamama kiuchumi ni kuwezesha Taifa letu lote kwa sababu akina mama ndio wanaochukua mzigo mkubwa katika familia kulea watoto, kusomesha watoto, sasa tunapowawezesha kiuchumi, Taifa letu litahakikisha kwamba watoto wetu wanapata elimu lakini pia hali ya maisha ya wananchi itaboreka sana. Hivyo, naomba Benki ya Maendeleo ya Akina mama iwekewe hela za kutosha sana na urasimu uondoshwe, ili akinamama hawa waweze kupata mikopo na katika masharti nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie kuhusu sekta binafsi. Sekta binafsi ndiyo kinara katika kujenga uchumi popote duniani. Naomba mazingira mazuri yaendelee kuwekwa hasa mabenki yapunguze riba. Riba za sasa za asilimia ishirini hazisaidii wawekezaji katika sekta binafsi. Kwa hiyo, kuwe na fursa nzuri katika sekta binafsi kwa mabenki kuwa na riba nafuu lakini pia umeme usambazwe nchini kote ili viwanda vidogo vidogo vianzishwe. Pasipo umeme wa uhakika haiwezekani kuwa na sekta binafsi iliyoshamiri. Pia napendekeza vilevile katika sekta binafsi Serikali ipunguze pia gharama za umeme kwa sababu umeme ambao ni wa ghali si rahisi sana kuanzisha viwanda ambavyo vitatumia umeme…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja.

**SPIKA:** Sasa nitamwita Mheshimiwa Zambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Assumpter Mshama.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia kidogo. Kwanza naomba nitumie nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo amewasilisha mbele ya Bunge hili, hotuba ambayo imeelezea mambo mengi ambayo yanagusa maisha ya Watanzania lakini pia nipongeze na hotuba ambayo imesomwa na Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu lakini pia na hotuba zile ambazo zilisomwa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, mimi nimesimama kusema mambo machache kidogo na nimesikia wenzangu wakisema ni ukweli kwamba hili ni Bunge la bajeti wala siyo Bunge la Katiba lakini kwa sababu kuna mambo ambayo yamejitokeza na yanataka kuleta upotoshaji, ni vizuri mengine tukayasemea na Watanzania wakayaelewa.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimeshangaa na nilitaka nisimame wakati ule Kiongozi wa Kambi ya Upinzani akichangia lakini nikaona wacha amalize. Yako mengine ambayo wenzangu wameyasema nimeyasikiliza, hayo sitayarejea lakini naomba kwenye Kitabu kile cha Kambi ya Upinzani nirejee jambo moja na ikiwezekana hili jambo lipatiwe majibu au Kiongozi wa Kambi ya Upinzani basi atakiwe kutoa maelezo juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa kumi na moja wa kitabu chake, nataka niseme jambo moja katika alilolisema hapa, ameuliza maswali hapo juu anasema ili kuepusha Taifa letu na balaa la ufisadi na wizi mkubwa wa fedha za umma kama ilivyotokea mwaka 2005. Halafu akasema mwaka huo kama inavyojulikana mabilioni ya fedha za umma yaliibiwa kutoka katika akaunti ya kulipa madeni ya nje *EPA* ya Benki Kuu ya Tanzania kwa ajili ya kugharamia kampeni za Uchaguzi Mkuu za CCM na mgombea wake wa Urais.

Mheshimiwa Spika, taarifa kama hizi ni za upotoshaji mkubwa na sisi kama viongozi wa Serikali na Chama kinachotawala hatuwezi kunyamaza tukaacha kuyasemea hayo. Mimi nilikuwa naomba umtake Kiongozi wa Kambi ya Upinzani awathibitishie Watanzania maana anataka kuwaaminisha kwamba Rais wetu yupo madarakani kwa sababu ya fedha za wizi jambo ambalo haliwezi kuvumilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa nini wamenyamaza na jambo hili, mambo ya mwaka 2005 yanakuja leo mwaka 2014 kama huku siyo kutafuta sababu ni kufanya nini.

**MBUNGE FULANI:** Tumesema.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, hili tusikubali, tuombe lipatiwe majawabu na kama hana sababu basi akiri kwamba Rais wetu hayuko madarakani kwa sababu ya fedha za wizi. Tupo madarakani kwa sababu ya sera za Chama cha Mapinduzi kuaminiwa na Watanzania, sera za Chama cha Mapinduzi zinawaondoa Watanzania katika umaskini, sera za Chama cha Mapinduzi zinawapendeza wengi ndiyo sababu wanaweza wakatuchagua tukaendelea kuwa madarakani. Mimi naomba niwaombe viongozi wa Serikali sisi na ambao wako huko nje tuendelee kuchapa kazi ili Watanzania tuendelee kuaminiwa hasa sisi ambao tupo ndani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba niseme kwamba Kiongozi wa Kambi ya Upinzani anatabiria mabaya nchi hii. Anasema tunapoenda kwenye uchaguzi unaokuja kama hamna Katiba mpya hapataeleweka, amani itapotea, kwa nini unakuwa mganga au mtabiri wa kienyeji kuitabiria nchi mambo mabaya? Haiwezi kueleweka! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu anasema Katiba isipokuwepo, tumekuwa kwenye Bunge Maalum la Katiba wanakimbia wanakwenda nje Katiba itakamilika saa ngapi wakati ninyi mnakimbia mnakwenda nje? Katiba inaandikwa ndani humu mnakimbia mnaenda nje, tutaandika Katiba? Haiwezekani! Lazima tubaki humu ndani, tuzungumze pamoja halafu sisi siyo wa mwisho katika kuandika Katiba, wako Watanzania ambao watakwenda kupiga kura kukubali yale ambayo tutakuwa tumekubaliana humu ndani au kutokuyakubali. Sasa tunapotaka kwenda kwa Watanzania kuwaaminisha sijui kama tutapata Katiba ambayo inaandikwa mtaani.

Mheshimiwa Spika, naomba tuache kuwaaminisha Watanzania kwamba tusipopata Katiba mpya maana yake nchi itakwenda vibaya. Kama tunatabiria nchi mabaya basi sisi ni watu wabaya sana, ni watu wa ajabu sana. Naomba Watanzania wajue kwamba wakati mwingine viongozi wengine wa Kambi ya Upinzani pia hawana nia njema na nchi hii. Wangependa kuona nchi hii inatumbukia kwenye vurugu, nchi hii inatumbukia kwenye machafuko labda ndiyo itakuwa furaha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba niwaambie Watanzania, nchi hii itakapoingia kwenye vurugu, hawa viongozi wote watakimbia nje ya nchi lakini Watanzania ambao wako huko nje watabaki ndiyo wanaopata mahangaiko

hapa ndani. Kwa hiyo, tuwe waangalifu sana na kauli ambazo zinapotoshwa na Viongozi wa Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mimi nashangaa sana, anazungumza mdogo wangu Mheshimiwa Mbunge wa Mbozi Magharibi hapo, anasema eti ahadi za CCM zinasubiri mwaka 2015 lakini anasema tuliingia kwa gia ya ahadi za uwongo halafu tunasubiri mwaka 2015 ndiyo tutekeleze.

Mheshimiwa Spika, yeye mwenyee anajua kule Jimbo lake la Mbozi toka Tunduma kwenda Sumbawanga tumejenga barabara kubwa ya lami ambayo ilikuwa ahadi ya Chama cha Mapinduzi na wale wananchi wanafaidika, ile haioni lakini anasema tuliahidi uwongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ndugu zangu wa *TANESCO* kupitia *REA* wamepima mradi mkubwa wa umeme ambao utatoka Jimboni kwake Momba kwenda mpaka Mbozi, hayo yote hayaoni. Juzi juzi wamepeleka karibu shilingi milioni mia mbili za maji pale Tunduma kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji, hayo yote hayaoni anaona ni ahadi za CCM za kuwaingiza madarakani. Tuwaambie Watanzania ukweli, tusiseme kwa sababu tunaweza kusema. Kwa hiyo, ni vizuri tukawa wa kweli.

Mheshimiwa Spika, lakini Kiongozi wa Kambi ya Upinzani anasema kugawa maeneo anasema ni gharama zaidi eti kuliko kuwa na Serikali tatu. Hivi unapokuwa na shughuli nyingi katika eneo moja, ukajenga shule nyingi, ukajenga zahanati nyingi vyovyote haya ni majukumu ambayo yanahitaji pesa zaidi kwa ajili ya utekelezaji wake.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Ni ya mwisho?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Assumpter Mshama atafuatiwa na Mheshimiwa Rage.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika Bunge hili la bajeti.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mungu kunipatia wakati mzuri leo kuweza kuchangia. La kwanza kabisa ambalo ningependa

kuongelea, naipongeza Serikali na Ofisi ya Waziri Mkuu na ninaunga hoja mia kwa mia kwa kazi nzuri ambayo inaendelea kutendeka.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ningependa niongee kidogo juu ya Mheshimiwa Mbowe. Mimi kwa kweli nataka kusema kwamba jambo alilolifanya leo amedhihirisha kazi yake ile ya zamani. Nilikuwa ninauliza huu ni muziki gani unaopigwa maana tukiwa katika Bunge la bajeti anaongea Bunge la Katiba tukiwa kwenye Bunge la Katiba anatoka nje, sasa hilo disko sijui lilikuwa disko la namna gani, kwa kweli amepotosha umma kwelikweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye kilimo. Naipongeza Serikali kwa kweli kwa namna ambayo imeeleza lakini labda ningeomba nitoe ushauri kidogo. Ukiangalia ripoti ya Waziri Mkuu inasema kwamba hali ya chakula ni nzuri lakini kuna maeneo wananchi wanapata mlo mmoja. Niombe tu Serikali ingetusaidia ni namna gani inaweza kuelimisha wananchi wajue kwamba mazingira yamebadilika na wakati wa kupanda siyo wenyewe kama zamani na wakati wa kuvuna sasa hivi siyo kama ule wa zamani. Kwa hiyo, itolewe elimu ya kutosha ili wananchi wajue kwamba majira yaliyokuwa yanatumika zamani siyo yanayotumika leo. Kwa hiyo, hiyo itasaidia wananchi kupata mavuno ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni Kilimo Kwanza. Katika Kilimo Kwanza kuna kitu kinaitwa Mpango wa Kutekeleza kwa Matokeo Makubwa sijui hiyo ndiyo *Big Results Now* au na hiyo ni *slogan* nyingine imeanza sijaielewa lakini unapokuwa unaongelea Kilimo Kwanza wakati pembejeo zinatoka baada ya msimu, unaongelea Kilimo Kwanza kwamba tumeenda vizuri wakati unaona kwamba umetoa miche laki tatu na hamsini yenye thamani ya shilingi milioni mia moja na miche ya chai ya thamani ya shilingi milioni mia tatu kwa kweli hicho Kilimo Kwanza hakijawa Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Spika, Tanzania nzima kilimo kimeajiri watu zaidi ya 80% lakini hakijawekewa msisitizo kama ambavyo kimebeba jina lenyewe. Kwa hiyo, mimi ningeomba kwanza zile nafasi ambazo zilikuwa zimetolewa mwaka jana na mwaka juzi tukapata matrekta na pembejeo, ningeomba vitiliwe mkazo ili tuweze kuwa na zana hizo na ndipo kitakuwa Kilimo Kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongee juu ya elimu. Suala la elimu Tanzania limeonekana kabisa kama ni kitendawili. Kule kwenye Wilaya yangu ya Misenyi kuna Walimu waligawiwa mwaka jana lakini nataka nikuambie hivi tunavyoongea hata robo ya wale Walimu hawajafika. Tatizo ni kwamba tulipoomba hata katika bajeti iliyopita nilichangia nikaomba Serikali, kwa nini hatuweki posho ya mazingira magumu. Posho ya mazingira magumu itamfanya Mwalimu aende kufundisha Nkenge, itamfanya Mwalimu aende kufundisha Mtukula, aende kufundisha Kakunyu. Haiwezekani Mwalimu anayefundisha Dar

es Salaam analipwa sawasawa na mtu anayefundisha Kakunyu haitawezekana na ndiyo maana ukienda pembezoni elimu imeshuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee juu ya maji. Wilaya ya Misenyi tuna neema ya mito zaidi ya mitatu nyingine hata majina mengine yakitajwa watu wanacheka. Tunao Mto Ngono, tunao Mto wa Kagera, tunayo mito mingi lakini sisi Wilaya ya Misenyi ni Wilaya yenye miaka nane hatuna maji ya bomba na tuna Mto uko pale kwa nini Serikali haitupatii maji? Mimi niiombe Serikali itupatie maji kwa sababu Mungu alishatupa hiyo mito, tuitumie kwa kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa naongelea habari za *VICOBA*. Mimi nilipopata nafasi ya kuwa Mbunge nimeanzisha *VICOBA* kwenye eneo langu lakini nguvu ninayotumia kwenye *VICOBA* ni ya hela yangu kuitafuta mimi mwenyewe. Tumeshajaribu kuona kwamba *VICOBA* ni chombo kizuri kinachoweza kumuinua mwanamke na mwanaume katika uchumi, kwa nini hatuweki sera ya kusaidia hivi *VICOBA* ili kusudi wanawake wapewe nguvu waweze kufanya biashara na kusomesha watoto wao.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, namshukuru Waziri Muhongo kwa kunipa umeme Mtukula. Mtukula tangu imekuwepo sasa hivi ni mara ya kwanza umeme kuwaka. Niombe vile vijiji ishirini na nne alivyoniahidi, nikuombe sana unisaidie angalau mwaka huu kwenye bajeti hii viweze kupata umeme maana umenipa vijiji viwili na Mtukula ambavyo siyo sawa kwa vijiji ishirini na nne kupata vijiji viwili. Kwa hiyo, mimi nikuombe na nikushukuru kwa jambo hilo na ninakuamini kwa namna ulivyosema ni mtaalam mkubwa, nina uhakika majibu ya umeme yatapatikana nisaidie ili 2015 nione kama nitaweza kurudi, ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ndiyo lala salama yenyewe. Mheshimiwa Rage atafuatiwa na Mheshimiwa Leticia Nyerere.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote, napenda kuunga mkono mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, lakini kama walivyotangulia kusema wenzangu hotuba ya Kiongozi wa Upinzani haikuwa nzuri hata kidogo na kwa taarifa za kiintelijensia ambazo tunazo, baada ya kufanya vibaya kule Kalenga na Chalinze kesho wanatangaza Baraza lao jipya la Mawaziri Kivuli. Hii ni dhahiri kabisa kwamba wameshindwa kufanya kazi wao wenyewe. *(Makofi)*

**SPIKA:** Watakaokuwa wanavunja viti vyangu watachajiwa humuhumu. *(Kicheko)*

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Spika, mimi nina matatizo kama matatu makubwa katika Manispaa yangu ya Tabora na Mkoa wa Tabora. Tumekuwa tunaahidiwa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Manyoni kwenda Tabora, Nzega kwenda Tabora, Tabora kwenda Urambo mpaka Kaliua na hatimaye kuungana na ndugu zetu wa Kigoma. Kwa kweli kwa mujibu wa takwimu ambazo ninazo, mara ya kwanza barabara hizi zilitakiwa ziwe zimekamilika tarehe 29 Novemba, 2012 lakini zikaongezewa muda mpaka tarehe 3 Novemba, 2013.

Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha barabara ya kutoka Tabora kwenda Ndono angalau inatoa matumaini kwa kiwango cha 87% lakini barabara ya kutoka Ndono kwenda Urambo iko kwa 48%, barabara ya kutoka Tabora kwenda Puge 35% na barabara ya kutoka Nzega kuja Puge 29%. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka jana kabla ya bajeti Wabunge wote wa CCM wa Mkoa wa Tabora tulikuja ofisini kwako na ulishuhudia mama yangu Margaret Sitta ilibidi alie machozi na *pressure* ikampanda tukampeleka hospitali jioni. Kwa hiyo, tunaomba asije akalia tena na mwaka huu. Tunahakika kwa sababu ya busara zako basi barabara hizi zitapewa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo la maji Mkoa wa Tabora na hii inatokana na *geological report*. Maji chini ya ardhi ni aghalabu kupata katika Mkoa wetu wa Tabora. Kwa hiyo, maji ambayo tunayategemea ni kutoka Shinyanga kuja Tabora ambayo yanatokea *Lake Victoria*. Maji ya ya Ihelela yana uwezo wa kutoa kila siku lita milioni mia moja na ishirini na mradi ule umeigharimu Serikali ya CCM shilingi bilioni 253 lakini kwa zaidi ya miaka sita sasa maji yanayotumika ni lita milioni kumi na saba. Kwa hiyo, zaidi ya lita milioni mia moja na ushehe hivi hayatumiki hata kidogo. Kwa hiyo, utakuta kwamba Serikali inapoteza fedha nyingi kwa ku-*subsidize* uendeshaji wa ile kampuni ya KASHUWASHA. Mpaka sasa hivi KASHUWASHA imeshapata fedha kutoka Serikalini zaidi ya shilingi bilioni tano ambazo zingeweza kutosheleza kusambaza maji katika miji ya Nzega, Igunga, Tabora na Sikonge. Nina imani kabisa kwamba mradi huu ambao hauhitaji pampu yoyote kupiga maji kutoka Shinyanga kuyaleta Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa za kitaalam, kuna kitu wanaita *force of gravity*. Tuna Hospitali yetu ya Rufaa pale Kitete, sasa hivi tuna maafa mengi sana yanatokea kwa sababu hatuna Madaktari wa kutosha, hatuna Manesi wa kutosha, kulikuwa na Mkandarasi pale amepewa *award* ambaye kwa bahati mbaya ameshindwa kufanya kazi ile ya kupanua Hospitali ile tangu mwaka 2005 mpaka sasa. Pamoja na kwamba tunazo fedha zimetolewa na *African Development Bank* lakini mradi ule umesimama sasa kwa takribani zaidi ya miaka miwili na tunakosa Chuo ambacho kingetoa Madaktari wenye degree pamoja na Manesi. Kwa hiyo, nina imani kabisa kwamba Serikali suala hili italiangalia.

Mheshimiwa Spika, tuna mradi mkubwa wa bwawa la Inala, ningependa kuishukuru Serikali ya Japan kwa kupitia *JICA* wiki mbili zilizopita wametoa shilingi 595,000,000 kwa ajili ya kutengeneza lile bwawa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali Mkandarasi aliyekuwepo pale ameacha kufanya kazi sasa anadai shilingi 400,000,000 angepewa na yeye.

Mheshimiwa Spika, tunalo Shirika la Maji linaitwa TUWASA pamoja na wafanyabiashara wengine wa kawaida ambao wametoa tenda, nilifurahi Waziri Mkuu tulipokuwa naye Dar es Salaam alituahidi kwamba atahakikisha madeni yote yanalipwa. TUWASA wanaidai Serikali zaidi ya shilingi bilioni moja ambayo kama watalipwa huduma za maji katika mji wa Tabora zitabadilika sana kwa sababu mpaka sasa kwa mujibu wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Ibara ya 17(h), Tabora Mjini tulikuwa tufike 85% lakini tuko zaidi ya 95% sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono bajeti hii mia kwa mia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Nilisema baada ya wewe atakuja Mheshimiwa Leticia Nyerere, atafuatiwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza, naomba kuwatoa wasiwasi kwamba, sisi Wananchi wa Kwimba hatuna tatizo la kushughulikia Miradi ya Maendeleo, tunashirikiana wote kwa pamoja; naomba maji Mheshimiwa Waziri anayaleta, naomba vitabu Mheshimiwa Waziri anashughulikia, naomba Bwawa la Mahiga, Mheshimiwa Waziri Mkuu anashughulikia, ninaomba nyongeza ya Walimu Mheshimiwa Majaliwa ameniletea takribani Walimu 300 wa nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Walimu 300 bila vitabu ni sawa kuvaa suruali bila kufunga vifungo. Hivyo, niko hapa leo, nikimwomba tena Mheshimiwa Waziri awe mvumilivu na atuletee vitabu Wananchi wa Kwimba. Narudia tena, sisi Wananchi wa Kwimba, hatuna mchezo na maendeleo, tumelelewa vizuri na Viongozi wetu. Naomba nichukue nafasi nyingine kuwapongeza Viongozi wetu akiwemo Mkuu wa Mkoa Mheshimiwa Ndikilo ambaye ni mchakapakazi na sisi wote tunafuata nyayo zake. *(Makofi)*

Vilevile nichukue nafasi hii kumpongeza Mkuu wangu wa Wilaya, Mheshimiwa Suleiman Mzee, kwa umakini wake wa utekelezaji wa Mipango

yote ya Wilaya na Miradi yote. Nawapongeza sana, waendelee kunivumilia, kwa sababu nitaendelea kuwasumbua. Ninakiri kweli nimekuwa msumbufu, lakini mnisamehe nimefanya hivyo kwa manufaa ya Wananchi wa Kwimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie suala la tabia ya nchi. Kama tunavyofahamu, wote tumekuwa na tatizo jinsi tabia ya nchi inavyoendelea kubadilika, Wananchi tumekuwa hatuna miundombinu ya kutosha, barabara zinajaa maji. Nimeshuhudia wawekezaji ambao tunawavutia waje nchini, anakuja anafikia Serena Hotel, anatakiwa kwenda ng'ambo nyingine ya barabara, analazimika kuvua viatu. Unamwona anatembea na viatu mkononi, unaanza kushangaa kumbe kwa sababu barabara imejaa maji yanayofika hadi kwenye magoti.

Naomba kusisitiza Serikali ni lazima itambue kwamba, huwezi ukatatua tatizo la tabia ya nchi kwa kufukia mabonde haisaidii; ni lazima tuingie sasa kwenye teknolojia ya juu kama wenzetu Korea Kusini walivyofanya. Ninaishauri Serikali ijaribu kuwa-*consult* pengine watapata wazo. Tukiendelea na utatuzi wa tatizo kwa muda mfupi, nina hakika hata hao wawekezaji wote watakimbia.

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia kuzungumzia suala la kuchangia Miradi ya Maendeleo. Natoa wito kwa Wananchi wote wa Kwimba, kwamba, tuisaidie Serikali pia na hata Mbunge kama mimi ambaye napigania maendeleo tusaidiane, tunapoambiwa kuchangia Miradi ya Maendeleo wote tuchangie. *(Makofi)*

Naomba kunukuu usemi wa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alisema hivi; "Ukitaka kula, lazima ukubali kuliwa." Kwa hiyo, hakuna *free lunch, there is no free lunch,* Wananchi wote tuchangie katika shughuli za maendeleo kwa manufaa ya Wilaya yetu ya Kwimba, kwa manufaa ya Mkoa wetu wa Mwanza na kwa manufaa ya Taifa letu wote kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisingependa kugongewa kengele, naomba nimalizie kwa kusema kwamba, naipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwanza kabla hawajashangilia, nimesema naipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kutekeleza yale yote ambayo nimekuwa nikiyapigania Bungeni; nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Kushukuru ni kuomba si unaona na hiyo ndiyo siasa. *(Makofi)*

Sasa nilisema nitamwita Mheshimiwa Sakaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Capt. Chiligati.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru nami kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nataka nianze na makusanyo ya Serikali hasa Serikali za Mitaa. Tumeshuhudia kila mwaka Miradi mingi ya kwenye Halmashauri haitekelezwi kwa sababu mapato yanayokusanywa kwenye Halmashauri ni kidogo sana na Serikali za Mitaa zinategemea ruzuku tu ya Serikali kwa ajili ya Miradi yote ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tunategemea, mwaka jana hapa kwenye *Speech* ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, alizungumza kabisa ninayo hapa, alisema kwamba, Halmashauri zote Tanzania zilikusanya chini ya asilimia kumi ya matarajio yao waliyokuwa wameweka. Mwaka huu amekuja anatuambia kwamba, kumekuwepo na ongezeko la makusanyo ya mapato katika Halmashauri! Ninapoangalia *Speech* yake, ukiangalia mtiririko wa miaka 2010/2011 walikusanya kwa asilimia 92, 2011/2012 asilimia 62, 2012/2013 ikapanda kidogo asilimia 73, 2013/2014 asilimia 54. Sasa najiuliza mbona anasema mapato yanaongezeka wakati yanazidi kushuka?

Mheshimiwa Spika, matarajio wanayoyaweka ni madogo na hata hayo madogo wanayoyaweka bado hayafikii malengo. Ukiangalia *Speech* ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Halmashauri nyingi hazikufika hata nusu ya makusanyo. Haiwezekani kwa Tanzania yenye rasilimali kibao, *almost* kila Wilaya Tanzania inacho chanzo cha mapato, neema ambayo tumepewa kila Mkoa una vyanzo vya mapato, hawakusanyi na katika makusanyo kuna mianya mingi sana ya wizi wa fedha, lakini Serikali imeshindwa kusimamia Halmashauri zikusanye mapato kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo hapa nchini. Tumekuwa tunasema kila siku hapa na hata Hotuba ya *CAG* ya mwaka huu inasema kwa mwaka mmoja tu, Halmashauri zimepoteza shilingi bilioni 6.1; ni hela nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, upo udhaifu hata kinachokusanywa hakipelekwi benki kama inavyotakiwa. Mfumo wenyewe wa ukusanyaji hauleti marajio ya kuhakikisha fedha iliyokusanywa yote inafanya kazi inayotakiwa, kuna mianya ya wizi, kuna mianya ya rushwa, wafanyabiashara wakubwa hawalipi kodi wanapewa *ten percent* wanasamehewa kodi! Tutafika kwa utaratibu huu, Miradi haiendi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunataka Serikali ituambie mwaka jana Mheshimiwa Waziri Hawa Ghasia, alituambia wanaandaa utaratibu mzuri wa *e-Tax* utakaotumika inagundua vyanzo vya mapato lakini pia kuzibana Halmashauri

kuhakikisha kwamba wanakusanya vizuri. Mimi nikategemea mwaka huu angekuja na tathmini, kwa mwaka uliopita utaratibu wa *e-Tax* umefanikiwa kwa kiasi hiki. Ninachokiona kwenye *Speech* yake anatuambia mwaka huu tena tunategemea kuweka halmashauri kumi kwenye *e-Tax* kwa ajili ya kuweka utaratibu mzuri. Hakuna *consistency* na hili ni tatizo, ndiyo hatupigi hatua. Hatufanyi tathmini tunatamka kwenye makaratasi hakuna *implementation. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hilo ni tatizo, leo tunalalamika Mheshimiwa Rage kasema hapa, Barabara za Mkoa wa Tabora kwa miaka minane, Wananchi wanateseka. Leo Tabora haina reli, reli imebomoka hakuna treni inayokwenda kule, barabara zimevunjika, mvua hii kulala barabarani siku mbili ni kawaida kwa Wananchi wa Mkoa wa Tabora. Barabara zote angalau hata moja, Serikali ingesema angalau barabara moja Itigi - Tabora ikamilika, badala ya Wananchi kuteseka watumie moja. Itigi – Tabora haijakamilika, Nzega – Tabora haijakamilika, Tabora – Urambo hakuna, Uramba – Kaliua hakuna, tutaongea hivi mpaka lini? Tunaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuwa ana-*windup* atuambie ni lini Barabara za Mkoa wa Tabora zitakamilika, Wananchi wa Mkoa wa Tabora nao wajione ni sawa na Wananchi wengine ambao wamefunguliwa kwenye Mikoa yao?

Mheshimiwa Spika, niende kwenye Sherehe za Muungano; nakubali kulikuwa na kila sababu ya kuadhimisha miaka 50 ya Sherehe za Muungano, lakini nakataa gharama zilizotumika mwaka huu ni nyingi sana; haziendani na uchumi wetu, haziendani na umaskini wetu na haziendani na hali ya maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Haiwezekani wewe baba unafanya sherehe ya kuadhimisha miaka 20 ndoa yako unawalaza watoto wako njaa, huo ni ubinafsi wa hali ya juu. Tumefanya kufuru mwaka huu; nikashangaa kweli kabisa kati ya miaka ambayo nimeishangaa sherehe ni mwaka huu, kweli Serikali inakwenda kuchukua vyombo vya vita kokote vilipo inapeleka Dar es Salaam, kwa mtu yeyote makini anayewaza vizuri huwezi kuonesha vyombo vyako vya vita hadharani. Tena unatamba kabisa kwamba, tunaonesha kwa jinsi gani ambavyo tuna vyombo vingi; kwa faida ya nani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikashangaa kabisa mwenyewe …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Nilikuwa *busy,* kengele ya pili imeshagonga tunaendelea.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Ya kwanza Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Umemaliza, nasema imegonga kengele ya pili. Nilisema nitamwita Mheshimiwa Capt. Chiligati, atafuatiwa na Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed.

**MHE CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, nianze kwa kumpa taarifa Mbunge aliyeketi sasa hivi kwamba, utaratibu wa nchi kuonesha baadhi ya zana za kivita ni utaratibu wa kawaida Duniani na sisi siyo wa kwanza na kilichooneshwa pale ni sehemu ndogo tu ya mambo yaliyopo. *(Kicheko/Makofi)*

Nasema hii kwa uhakika kama Mjumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge.

**SPIKA:** Halafu hawajui kama wewe ni Captain.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Ya Captain sijasema, lakini ndiyo ilivyo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze kwa kutoa tahadhari kwamba, Waheshimiwa Wabunge wenzangu tusigeuze Bunge hili la Bajeti, likawa ni Bunge Maalum la Kutunga Katiba. Hili ni Bunge ambalo Wananchi wanataka kujua bajeti inatoa majibu gani kwa matatizo yao ya maji, afya, elimu, barabara na kadhalika. *(Makofi)*

Sasa nilishangaa sana asubuhi, Hotuba ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, katika ile saa moja karibu dakika thelathini na tano, zaidi ya nusu ya ule muda anazungumza mambo ambayo yalipaswa yazungumzwe kwenye Bunge la Katiba. Sasa badala mambo yale kuyazungumza kwenye Bunge la Katiba, akachukua timu yake akaweka mpira kwapani akatoka nje. Sasa leo badala ya kuzungumza shida za Wananchi bajeti inasemaje, zaidi ya dakika ya 30 karibu 40, hakuwatendea haki Wananchi kuzungumza mambo ya Bunge la Katiba. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ushauri wangu kwa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, mwezi wa nane, timu yake airudishe humu ndani, yale mambo yote tuyazungumze humu ndani na ni lazima tutoke na Katiba mpya, nzuri, tuwaoneshe Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nirudi kwenye mambo ya Wananchi. Uchumi tumeambiwa jana kwamba, unakua kwa asilimia saba kwa mwaka, lakini umaskini haupungui kwa kasi hiyo, umaskini unapungua kati ya asilimia moja mpaka mbili tu. Maana yake ni kwamba, yale maongezeko ya uchumi, mapato ambayo yanaongezeka, bado hayajawafikia Watanzania walio wengi. Watanzania wengi bado wanaendelea katika hali ya umaskini. Hii inasababisha

pengo kati ya wenye fedha matajiri na maskini linazidi kukua tena kwa kasi na hii ni hali ya hatari kwa umoja wetu, ni hali ya hatari kwa amani yetu, ni hali ya hatari kwa upendo wetu. Mkishakuwa na matabaka ya aina hiyo amani inatoweka na upendo unatoweka. Kwa hiyo, ushauri wetu kwa Serikali kwamba ili umaskini upungue, Bajeti ya Serikali tuielekeze kule ambako Wananchi wapo wengi, kwenye sekta inayobeba watu wengi, ndiyo hela zote ziende kule. *(Makofi)*

Nimewauliza Wajumbe wenzangu wa Kamati inayoshughulika na Sekta ya Kilimo; je, bajeti ya mwaka huu liko ongezeko ambalo litakwenda kubadilisha hali ya kilimo? Wameniambia haina tofauti kubwa na bajeti ya mwaka jana. Sasa hii habari siyo nzuri hata kidogo, ni habari ambayo inatufanya umaskini uendelee kupungua kwa asilimia moja, wakati Wananchi tunaambiwa uchumi unakua kwa asilimia saba. Ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba, hatujachelewa kuongeza bajeti ya kilimo, ili hela nyingi zaidi ziende kule kwa Wananchi asilimia 75 ndiyo wanaobebwa na kilimo, ndiyo wanaoajiriwa na kilimo.

Kamati ya Bajeti ya Mheshimiwa Chenge, naiomba sana itazame namna gani tunaweza tukaongeza bajeti ya kilimo ili isaidie wale wakulima, asilimia 75 ambao wako vijijini. Ninapendekeza tukipata nyongeza hiyo, tulenge maeneo manne ambayo yatabadilisha kilimo chetu, ambayo yataongeza kipato cha wakulima. Eneo la kwanza ni kilimo cha umwagiliaji, hela ziende kwenye umwagiliaji, kilimo cha kutegemea mvua ni kilimo cha pata potea, ni kilimo tulichokaa nacho kwa miaka hamsini hakijaleta tija, iende kwenye umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, hata maeneo kama Manyoni, kila baada ya miaka miwili au mwaka mmoja tunajipanga kwa Waziri Mkuu kuomba chakula cha msaada. Ardhi tunayo, tuna puga nzuri, ukame tu, kwa hiyo, kama tutajengewa mabwawa na mambo yetu yako kwa Waziri wa Kilimo na kwenye sekta yake nikipata nafasi nitalizungumza, tukipata mabwawa tukamwagilia, hatutapiga foleni tena Wilaya ya Manyoni kuomba chakula kwa sababu tutalima, tutavuna, hata mara mbili kwa mwaka. Kwa hiyo, eneo la umwagiliaji tulitazame na ninawashawishi Wabunge tutazame, ikija bajeti ya kilimo, tutazame kama kuna hela za kutosha kulima kilimo cha umwagiliaji au ni bajeti ambayo tunaendelea kutegemea kilimo cha mvua ambacho hakitufikishi popote.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni Maafisa Ugani; Ilani ya Chama cha Mapinduzi imesema kila kijiji kuwe na Afisa Kilimo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Dakika zimeisha.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nilisema nitamwita Mheshimiwa Rukia Kassim, atafuatiwa na Mheshimiwa Abbas Mtemvu.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuchangia katika Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ningependa kujielekeza kwenye hali ya uchumi. Kitabu hiki cha Mheshimiwa Waziri Mkuu, kinaelezea kuwa, uchumi wetu umekua, Pato la Taifa limeongezeka kwa asilimia saba na ukilinganisha na mwaka uliopita, kulikuwa na ongezeko la ukuaji wa asilima 6.9. Ninajiuliza hivi kama kweli uchumi umekua ni kwa nini Wananchi wanaishi katika maisha magumu, maisha ya umaskini uliokithiri? *(Makofi)*

Mimi nadhani ilikuwa Serikali ikae ifikirie ni namna gani ya kuwasaidia Wananchi wetu waweze kuondokana na umaskini huu. Kwa kweli hali waliyonayo watu wetu wanaishi kwa mlo mmoja kwa siku ni mbaya na inatisha, tusijione sisi tuko humu kwenye viyoyozi, lakini Wananchi wetu huko vijijini wanaishi maisha magumu sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naishauri Serikali ijielekeze katika Sekta ya Kilimo. Serikali ikijielekeza katika Sekta ya Kilimo, tutaweza kuwasaidia Wananchi wengi walioko vijijini wakwamke na umaskini huu. Mimi nashauri kuwe na mabenki ambayo yataweza kuwakopesha wakulima mikopo ambayo itakuwa na riba nafuu, waweze kununua matrekta, wajiendeleze kwa kilimo ili umaskini huu upungue.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoka hapo, niende kwenye Operesheni Tokomeza. Nimesoma katika Kitabu hiki cha Mheshimiwa Waziri sikuona popote walioelezea hali hii. Operesheni Tokomeza iliwaumiza Watanzania wengi, lazima tukubali ukweli kuwa wafugaji waliathirika na walipata umaskini wa hali ya juu. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuja kujibu hapa atuambie, je, wafugaji hawa waliokumbwa na umaskini kwa ajili ya Operesheni hii Serikali imewasaidia vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna watu ambao walibakwa, kuna akina mama walibakwa, wengine wamepata watoto kwenye Operesheni hii, kuna waliopata UKIMWI kwenye Operesheni hii, kuna wengine wamekuwa wajane na wengine wamekuwa walemavu pia. Kwa hiyo, kwa kweli Operesheni hii imeathiri baadhi ya Watanzania kwa kiasi kikubwa. Juzi tuliona katika vyombo vya habari, kuna Kamati ya Bunge ilienda kutembea Ngara, wakaona sehemu ambako kulikuwa na wafugaji walitekwa mifugo yao iliwekwa pale na mingi

ilikufa. Kwa kweli, Operesheni hii imewatia umaskini wa hali ya juu wenzetu wenye jamii ya ufugaji.

Nakuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, utuambie mmewasaidiaje na kama hukutuambia mmewasaidia vipi, ninakuhakikishia tunazuia Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, utuambie na wale wote waliosababisha maafa haya, je, Serikali ilichukua hatua gani na waliowajibishwa tuambiwe ni wangapi na waliofungwa tuambiwe, tujue kila kitu kisifichwe, ikawa sisi tunaendelea kukaa hapa bila ya kujua kinachoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo nijielekeze kwenye Mfuko wa Maafa. Ni juzi tu baada ya kutokea mafuriko tuliona kuna Watanzania wengi ambao waliathirika na mafuriko yale, watu walikuwa wanalala barabarani. Sasa tujiulize sisi tuna Serikali, tuna Uongozi kamili; je, watu wale walisaidiwa vipi? Kuna akina mama na watoto walikuwa wakilala katika mabarabara, tumewaona wengine nyumba zao zimekwenda kabisa, mali zimepotea. Je, Serikali ituambie imewasaidia vipi?

Mfuko huu wa Maafa, utumike pia kuzuia yale maafa yasitokee, kwa sababu kwa mfano, Jagwani, pale kuna daraja ambalo huwa linajaa mchanga maji yanapita juu yanaingia katika nyumba za watu, watu wanakosa makazi wanaathirika na wengine wanakufa. Sasa jambo hili linatokea hii ni karibu mara ya tatu, Serikali kwa nini haitumii Mfuko huu kukinga maafa yale yasitokee? Hivi kweli tunashindwa kuyatafutia namna yale maji yakaelekea kwingine yasiingie katika nyumba za watu?

Kuna watu waliohamishwa pale wakapelekwa Magwepande, wamekwenda kule hakuna miundombinu, hakuna chochote ambacho kitawasaidia. Wale ni binadamu siyo Komba. Komba ukimchukua huko mwituni ukimleta kwenye nyumba hawezi kuishi kwa sababu kazoea kukaa mwituni. Sasa wale ni binadamu, nao wapatiwe yale ambayo ni mahitaji muhimu kwa binadamu ili waweze kuishi kule Magwepande, lakini wasipelekwe kule kama wanavyopelekwa Komba mwituni. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kuna wengi niliwasikia hapa walikuwa wakijadili wanasema turudi tuje katika Bunge la Katiba. Mimi nakubali kuwa kweli turudi tuje tujadili hii Katiba, lakini tujadili Rasimu ile ambayo tuliletewa hapa na Tume ya Warioba, Rasimu ya Serikali Tatu. Ikiwa tunatoka kwenye malengo yaliyokusudiwa, Rasimu iliyoletwa na Serikali hatuijadili, tunajadili nyingine, tunatukanana, tunabaguana kwa makabila, hili jambo halifai. Mwalimu alituambia Tanzania haina kabila, tusibaguane kwa makabila, tujadili vizuri, tupate Katiba nzuri, ili twende nayo vizuri. Hata hivyo, ni kweli sisi sote tunaitakia kheri nchi hii na hatuna pa kwenda zaidi ni hapahapa kwetu.

Mimi nashauri tuache yaliyotokea pale, twende vizuri, tuje tujadili Rasimu lakini tujadili ile iliyoletwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naomba kukaa kitako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mtemvu, atafuatiwa na Mheshimiwa Ole Medeye!

**MHE. ABBAS ZUBERI MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Niseme kidogo japo Bi Rukia asipoteze wangu; mimi ni Mwenyekiti wa Wabunge wa Dar es Salaam, wale Wananchi waliohamishiwa Magwepande wana huduma nzuri, wamepewa mabati, wamepewa simenti na wana shule wamejengewa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nianze kwa Mheshimiwa Dada yangu Mama Hawa Ghasia, yuko Mhasibu ambaye alikuwa Ilala ...

**SPIKA:** Sema Waziri wa Nchi!

**MHE. ABBAS ZUBERI MTEMVU:** Waziri wa Nchi, dada yangu, yuko Mhasibu ambaye alikuwa Ilala akahamishiwa Mvomero, sasa nasikia mmemleta Temeke. Tunaomba sana sana mchukueni huyo Mhasibu.

Mheshimiwa Spika, niende ukurasa wa 56 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, inazungumzia suala la msongamano. Mimi nataka kumpa taarifa tu Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, taarifa ulizopokea siyo sahihi; Barabara ya Jet-Conner, Davis-Conner bado haijakamilika na barabara nyingi hazijakamilika.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, njia ya kuondoa msongamano Dar es Salaam, mwaka 2007/2008, RC akiwa Lukuvi na Kandoro, ulianzishwa mpango mzuri tu wa *ring road* na ulitusaidia sana kwa Mkoa wa Dar es salaam. Barabara zote ambazo zimetengenezwa sasa na ambazo ziko kwenye Mpango huu, ziko kwenye mpango huo wa *ring road,* Waziri akiwa Kawamba. Kwa hiyo, tunaomba sana, jaribuni kufuata ule Mpango tutafanikiwa. Katika taarifa hii hakuna jipya, sana sana inaonesha jinsi barabara zilivyochelewa.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la bodaboda. Sisi wengine tulijitoa tukawatafutia vijana uwezo wa kujiwezesha, lakini kitu cha kusikitisha, wale vijana sasa hivi wananyanyasika kupita kiasi. Uongozi wa Mkoa na Uongozi wa Jiji la Dar es Salaam, sisi Wabunge wa Dar es Salaam tunataka usafi, tunataka mji uwe mzuri, lakini utaratibu unaofanyika siyo utaratibu sahihi. Leo kuna vijana wa bodaboda karibu mia na kitu wako ndani, lakini kitu cha kusikitisha hata walemavu wamechukuliwa vitu vyao na wametiwa ndani! Inasikitisha sana sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunataka sana usafi lakini si kwa utaratibu

unaofanyika Dar es Salaam wa kuonea watu, vijana wa bodaboda wanatozwa shilingi laki tano.

Kitu cha kusikitisha wanaambiwa Wabunge wenu ndiyo wamepitisha sheria. Sisi hatukupitisha sheria ya kuonea, hatukupitisha sheria ya dhuluma, tulipitisha sheria, SUMATRA ndiyo walikuwa na utaratibu wa kupanga. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumesema hatukusikilizwa, tunakuomba sana utusimamie hilo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wananchi wa Temeke wamenituma, tulikuja kwako kuomba Kata tatu, kati ya Kata tisa zilizochukuliwa Kigamboni, tumekuomba Kimbiji, tukakuomba Pemba Mnazi, tukakuomba Kisarawe Two; hadi leo hatujapata jibu, Wananchi wanateseka. Ninajua Mbunge wa Kigamboni ataongea mengi, lakini Wananchi wanateseka, Wizara ya Ardhi hakuna majibu, tunashindwa kuelewa. Kwa hiyo, Wananchi wa Temeke wanaomba sana, utakaposimama uzungumzie zile Kata tatu.

Pia Wananchi wa Kurasini, ambao ulifika wewe mwenyewe, wanasikitika sana; wakati wa mvua hizi tulikwenda kuwatembelea, kufika kitandani kwake mpaka akanyage matofali. Inasikitisha sana. Wote tuliahidi, mwaka wangu wa nane nimeingia humu, nazungumzia Kurasini, Kurasini, lakini pale Mtoni Kijiji cha Wavuvi ni hivyo hivyo.

Jambo la kusikitisha na la kutisha ni *National Housing*. *National Housing* tulipitisha hapa mwaka 2007, Wananchi wale wa maghorofani wamilikishwe zile nyumba, lakini ulivyoingia Uongozi wa *Serengeti Boys* pale *National Housing* na Kamati, wakafanya mambo ya ajabu sana. Leo Wananchi wale wanaambiwa mwisho wa mwezi huu wahame; watakwenda wapi? Inasikitisha na wapo njiani wanakuja wanataka kukuona Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba sana uwapokee, uwasikilize.

Mheshimiwa Spika, liko suala la *EPZ* Kurasini. Tumelipa hela pale chungu nzima, lakini leo bado Wananchi wachache hawajalipwa; inasikitisha sana sana. Kwa hiyo, naomba Serikali hii sikivu itekeleze majukumu yake kwa utaratibu. Hata hivyo, kuna suala la maafa Dar es Salaam, kwenye Kamati yangu niliona ni Ilala pekee ndiyo imetengewa shilingi bilioni nne ponti tisa. Nilipoongea na Mheshimiwa Lukuvi, akaniambia taarifa ya Temeke na Kinondoni hazijafika. Nimeongea na Wakurugenzi wanasema taarifa wamepeleka Mkoani; sasa sijui kuna kitu gani!

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Lukuvi, tunaomba sana mtusaidie hilo, Kinondoni na Temeke waweze kupata pesa hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante na kengele imegonga. Nilisema nitamwita Mheshimiwa Ole-Medeye, atafuatiwa na Mheshimiwa John Cheyo!

**MHE. GOODLUCK JOSEPH OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Naomba nianze kwa kusema kwamba, naunga mkono hoja au Hotuba hii ya Mheshimwia Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nina kero kadhaa katika Jimbo langu. Kero ya kwanza, kuna Wananchi wa Kijiji cha Oldonyosambu ambao walihamishwa na Serikali mwaka 1984 ili kupisha uanzishwaji wa Kituo cha Jeshi letu la Ulinzi katika Kijiji hicho. Wananchi wale waliahidiwa kupewa ardhi, tangu wakati huo Wananchi hao wamekuwa wanatangatanga katika Mkoa wa Arusha, hawana ardhi, hawana pa kulima, hawana pa kuishi na hata wakifiwa hawana pa kuzika.

Tarehe 20 Machi, 2012, Mheshimiwa Waziri Mkuu, alitoa agizo kwamba, Wananchi wale wapatiwe ardhi katika eneo ambalo Jeshi litahama kupisha Wananchi, katika eneo la Moshono. Kwa bahati mbaya, uhakiki wa ardhi iliyoko eneo la Moshono umeonesha kwamba ardhi ile ni kidogo haiwezi kutosheleza mahitaji ya Wananchi wale hususan tukizingatia kwamba, wale ni wakulima na wako Wananchi zaidi ya 1,000.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, atusaidie Serikali ipate ardhi mbadala, Wananchi wale wapatiwe ardhi ili nao waweze kuishi kama Watanzania walio huru. Niliwazuia Wananchi wale wasije kwa sasa hivi kwa sababu waliahidi kwamba, wanataka kuja kumwona Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini nimewaambia wasubiri mpaka Mheshimiwa Waziri Mkuu amalize Hotuba yake ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, tunalo suala la ugawaji wa Wilaya ya Arumeru, ni jambo la siku nyingi sana, ni ombi la siku nyingi sana na ninakumbuka wakati wa mazishi ya Marehemu Mheshimiwa Sumari, mwaka 2012, Serikali ilituahidi kwamba, Wilaya ile itagawanywa. Tunakishukuru Chama cha Mapinduzi kilitekeleza ahadi yake ya kuigawa Wilaya ile kichama na imekwishagawanywa. Sasa naomba Serikali iigawe Wilaya ili kusogeza huduma za kiutawala karibu na Wananchi hususan wale wanaoishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha.

Wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha wanateseka sana kufuata huduma; kwa mfano, Wananchi wanaoishi Oldonyosambu au Oljoro

kwenda Usa kufuata huduma za kiutawala. Naomba sana Serikali itusaidie kuigawa Wilaya ile haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, suala la Madiwani; hivi tunapoketi hapa wanaotusaidia kazi Majimboni ni Madiwani. Tunaomba Waheshimiwa Madiwani walipwe mishahara na Wenyeviti wa Vijiji ambao wanafanya kazi saa 24 wapatiwe posho.

Mheshimiwa Spika, tuna ahadi za Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais, katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, alipofanya Mkutano wa Kampeni mwaka 2010 alituahdi kwamba, atatujengea barabara moja ya lami ambayo inajulikana kama Ngaramtoni - Sambasha. Ahadi hiyo bado haijatekelezwa, naomba Serikali iitekeleze.

Mheshimiwa Spika, ahadi nyingine ya Mheshimiwa Rais alituahidi kwamba, Serikali itaandaa Mpango Kamambe na fedha zitatengwa za kutekeleza mpango huo ili ifikapo mwaka 2015, kero ya maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha iwe ni historia isiwepo tena. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, asimamie utekelezaji wa ahadi hiyo ili Wananchi waweze kupata maji. Wilaya hiyo ya Arumeru ndiyo inayotoa maji yanayotumika Arusha Mjini, yanayotumika Monduli na Longido.

Mheshimiwa Spika, Wananchi hawa wamechoka kutunza mazingira ambayo ndiyo hifadhi ya maji wakati wao hawanywi maji. Tunaomba Serikali itekeleze ahadi za Mheshimiwa Rais ili Wananchi waweze kupata maji. Wamenituma Wananchi wale nimpelekee Mheshimiwa Waziri Mkuu salamu na ninayo hapa zawadi waliyonipa nitamkabidhi Mheshimiwa Waziri Mkuu sasa hivi. Wameniambia zawadi hiyo ni shukrani kwa ahadi za Mheshimiwa Rais, lakini bado wanayo matumaini ya kwamba, ahadi hiyo itatekelezwa kwani hivi sasa wanaendelea kuishi kama mababu zao wa Karne ya 19 walivyoishi.

Mheshimiwa Spika, suala la maafa limekuwa ni jambo linalojirudia katika Taifa letu. Ukija ukame tuna maafa, yakija mafuriko tuna maafa, suala kubwa hatujajipanga kama Taifa. Tuna Kitengo cha Maafa, Kitengo kile naomba kibadilishwe majukumu na kirekebishwe ili kiweze kufanya kazi kubwa zaidi. Nashukuru wamekuwa wakitusaidia sana kila tunapopata maafa. Mwaka huu tuna mafuriko, tumepeleka maombi tunaomba tusaidiwe ili Wananchi ambao wamekumbwa na mafuriko na wameathirika hata kupoteza uhai tuweze kupata msaada wa kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, nashauri ifuatavyo: Kitengo kile cha Maafa kwanza kibadilishiwe *scope of work*, kiwe *reformed*, badala ya kushughulika na *disaster* kishughulike na *risk management*. Kwa maana ya upeo wake wa kazi upanuke, kishughulike na *mitigation* na kila Wizara, kila Mkoa na kila Wilaya, iwe na Sera

na mkakati wa kukabiliana na maafa, yaani kuzuia na kukabiliana na maafa. Moja ya maeneo ambayo nashauri ifanyike, tujenge mabwawa makubwa ya kukinga na kuzuia maji ya mvua ili badala ya kuondoka na kwenda kusababisha maafa na kuelekea baharini, yatumike kwa ajili ya kilimo, yatumike kwa ajiliya kunywesha mifugo, kwa ajili ya kunywa na kufuga samaki.

Mheshimiwa Spika, naomba nimkabidhi Mheshimiwa Waziri Mkuu zawadi yake!

**SPIKA:** Funga hiyo simu wape *page girls* ndiyo wapeleke siyo wewe.

Mheshimiwa John Cheyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Zaynab Vullu!

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Bajeti hii ya Waziri Mkuu. Kwanza, kwa maoni yangu, Bajeti hii ya Waziri Mkuu ndiyo Bajeti ya Watu wa Tanganyika. Hii ndiyo Serikali yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nimesikitishwa sana kuona katika shilingi trilioni nne za mwaka jana, ni asilimia 60 tu ndiyo imeenda kwa TAMISEMI. Mimi naona hii ni *failure* au ni makosa makubwa kwa Serikali kutoweza kuwapelekea Wananchi fedha ambayo wanahitaji kwa ajili ya maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, tumezungmza sana juu ya umaskini na maendeleo, ukweli ni kwamba, mpaka hivi sasa hatuwezi tukapunguza umaskini kwa Wananchi walio wengi ambao ni wakulima kwa sababu mbili. Jambo la kwanza hakuna anayezungumza juu ya uhaba wa ardhi katika vijiji. Tuna asilimia kubwa ya Wananchi wana uwezo wa kuweza kulima lakini hakuna mahali pa kulima. Ni vizuri sasa tuangalie, nchi hii ni moja kama kuna maeneo ambayo Wananchi wanaweza kuhamia wakalime kama sisi Wasukuma tunachotaka ni jembe na ardhi basi, tutakuchapia kazi. Haya mambo ya kuzia watu wasihame kutoka sehemu moja kwenda nyingine haiwezi ikatusaidia. Hili ni jambo ambalo ni muhimu sana. *(Makofi)*

Jambo la pili, hatuwezi kuendelea kutegemea kilimo cha mvua. Mambo ya mvua hatujui tabia nchi maji yatakuja lini na yanaweza kuja yakawa mengi. Hatuwezi kuendelea kwa njia hiyo, Serikali iangalie hili jambo.

Mheshimiwa Spika, nataka kutoa shukrani, maji kule Nkoma, Bwawa la Nkoma, sasa Mradi unajengwa. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa kutimiza hiyo ahadi, endelea mpaka huo Mradi ukamilike. Pia ninashukuru umeme umeanza kwenda Itilima, nashukuru kwa hilo lakini tunaona nguzo tu kutoka Ng'wamapalala kwenda Ng'warushu ambapo ndiyo tuna Hospitali ya Wilaya. Tunaomba kama ni nguzo basi zifike na umeme ufike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, kwa sisi ambao ni Wilaya mpya, tunahitaji msaada mkubwa sana wa Serikali. Kwanza, tunahitaji watumishi walio imara, siyo watumishi ambao kila siku wanatafuta sababu kwa nini Mradi haujafanyika. Mimi sasa hivi katika fedha ndogo tu ambayo tunapewa kwa ajili ya Jimbo, nimeweza kufungua njia nyingi sana kule kijijini. Tangu tumepata Mkurugenzi mpya, kila siku tunaambiwa fedha ya Mbunge sijui iko Bariadi, sijui fedha ya Mbunge iko wapi, mpaka hivi sasa Miradi mingi imesimama!

Namwomba Mkuu wa TAMISEMI, niangalizie hilo jambo, kama huyo Mkurugenzi hatufai, basi tuletee mtu ambaye anajua kuchapa kazi ili tujenge Wilaya mpya, ambayo itahakikisha Wananchi wanapata maendeleo kwa haraka zaidi.

Jambo lingine, tunasikitika kuona Wilaya yetu haina Hospitali ya Wilaya. Hospitali ambayo tulikuwa tumeichagua ile ya Nkoma, tuliyopewa na *World Vision,* mpaka hivi sasa hatujapewa barua kuonesha hiyo sasa itakuwa Hospitali ya Wilaya angalau kwa muda. Kwa hiyo, naomba upande wa TAMISEMI, mhakikishe tunapata vifaa vyote, tunapata waganga wa kutosha kwa ajili ya Hospitali ile ili iweze kufanya kazi ya kuhudumia Wananchi na ndiyo maana ya kusogeza huduma karibu kwa Wananchi.

Bado nataka kusisitiza kwamba, ili tuweze kusaidia watu wa vijijini, Serikali iweke fedha za kutosha kwa ajili ya barabara vijijini. Barabara vijijini ndizo ambazo zitaondoa umaskini katika Taifa letu na ndiyo zitakazofungua biashara za Wananchi katika sehemu mbalimbali. Bila kuwa na barabara vijijini, Wananchi hawawezi kuuza mazao yao kwa urahisi.

Jambo la mwisho ninalotaka kusema, nimeelezwa hapa kwamba, Serikali imetumia zaidi ya bilioni 4.8 kwa ajili ya mbegu ya pamba, lakini mbegu hizo hazikuota! Matokeo yake zimeleta umaskini mkubwa katika *Sukuma Land*, matokeo ni kwamba mwaka huu hata Halmashauri hazitaweza kupata fedha ya kutosha ya ushuru, kwa sababu zao la pamba litakwenda chini. Tunachotaka basi, Serikali itafute fedha ya kuwafidia wakulima ambao hawakupewa mbegu nzuri.

La pili, Serikali pia iwaongezee sehemu mbalimbali, Bariadi, Itilima na sehemu zingine zinazotegemea pamba, ruzuku zaidi. Kwa sababu ilikuwa ni uamuzi wa Serikali kuwashurutisha watu kutumia mbegu ambazo hazijajaribiwa.

Maoni yangu ni kwamba, mbegu isiwe lazima, twende polepole, mbona kuna mbegu za mahindi zinajaribiwa mwaka huu, zinajaribiwa mwaka unaokuja, mpaka watu wanazoea. Hivi ni siri gani kwa upande wa pamba kila kinachokuja ni lazima na lazima ifanyike kwa wakati huo? Tumechoka ulazima

wa kila kitu, lazima uwe na mkataba, ni lazima uuzie watu mbalimbali kwa ajili ya mazao, hali hii inatuletea umaskini.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Zaynab Vullu, atafuatiwa na Mheshimiwa Yahya Kassim Issa.

**MHE. ZAYNAB MATITU VULLU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote, nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, aliyenijalia leo hii na mimi nachangia katika Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, mengi yamezungumzwa kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu, lakini nilikuwa naomba nipatiwe ufafanuzi wa mambo yafuatayo:-

La kwanza, tumesema kuwe na uwiano wa jinsia na hili limeanzia katika shule zetu za msingi za awali. Hadi kufikia mwaka 2007, uwiano wa kijinsia katika shule zetu ulikuwa asilimia 68 na lengo ifikapo mwaka 2015, tufikie asilimia 100. Sasa ni mkakati gani ambao umewekwa kuhakikisha 2015 inafikia hiyo asilimia 100, lakini pia kuna mkakati gani uliowekwa kuangalia mdondoko wa wanafunzi wa kike! Hii inafanya ongezeko la ile idadi ya wanawake katika hayo maendeleo inarudi nyuma. *(Makofi)*

Sasa nataka kusikia ni mkakati gani ambao umewekwa katika hilo maana elimu ndiyo inamsogeza mtu kufikia hatua fulani? Serikali imejipanga vizuri katika 50 kwa 50 kwenye ngazi za Uongozi wa Kiserikali, kwenye Mashirika ya Umma na sehemu mbalimbali, lakini sijaona mkakati uliowekwa wa kufikia 50 kwa 50 kwenye uchumi kwa wanawake. *(Makofi)*

Wanawake wengi ni wakulima na wengine wanafanya biashara ndogondogo, hivi lengo la Serikali kuona wanawake kila siku wapo katika biashara zile za K tatu, KKK, Kufuma, Kushona na Kupika, tunataka watoke huko waende mbele. *(Makofi)*

Sasa nataka kuona Serikali imejipanga vipi katika kuhakikisha wanawake wakulima watapatiwa mikopo ama pembejeo. Halikadhalika wenye biashara ndogondogo na wao wafikiriwe ili twende sambamba. Tunapozungumzia kumwinua mtu kiuchimi basi tuliangalie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, vifo vya akina mama na watoto pamoja na juhudi za Serikali, bado asilimia inayozungumzwa na hali halisia ya vijijini, kuna utofauti. Ni vyema tukaangalia hiyo yote inasababishwa na nini.

Serikali inafanya juhudi kubwa na ina uhakika wa kuhakikisha maendeleo ya Wananchi wake, lakini bado naomba nipatiwe ufafanuzi katika hilo. Hawa wanawake ndiyo tunaotarajia kwenye chaguzi zijazo na wao waingie katika nafasi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kuweka 50 kwa 50, kwa maana kwenye uchaguzi wanawake na wanaume, lakini sikuona kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu igusie hilo, na mwaka huu tuna chaguzi za Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji na mwakani panapo uhai na uzima, tunaingia kwenye chaguzi kuu. Sasa ningeomba Serikali ituambie, imejipangaje katika kufikisha hilo lengo la 50 kwa 50? Imejitahidi, tulikuwa kwenye 16, tukaenda 23, sasa hivi tuko kwenye asilimia 33 na tumesema tunataka tusonge mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba watakaokuja kuzungumza wanieleze hilo wamelipangaje. Sisi tunataka kuona Serikali inasonga mbele, tunataka kuona maendeleo yetu wote wawili yanafanana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nizungumzie suala la barabara. Huko nyuma nakumbuka niliwahi kuzungumzia Barabara ya Morogoro. Matokeo yake, yale niliyoyasema juzi yamedhihiri. Niliomba Serikali iweke bajeti ya kutengeneza barabara ya kutoka Mzenga, ile ya zamani iliyokuwa inakwenda Morogoro, ili kuondoa msongamano au ikitokea dharura yoyote. Juzi tumeshuhudia mamia kwa mamia ya magari yamekwama kwenye Daraja la Ruvu. Hili ni tatizo kubwa, chombo kimoja tu kilichotegenezwa ndiyo kina mlango mmoja tu wa kuingilia na kutokea ni chupa. Sasa leo barabara haiwezekani na tuna nchi kubwa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba hilo Serikali iliangalie na itupatie majibu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nilikuwa nasikiliza Hotuba ya Kiongozi wa Upinzani, ninavyomjua mimi bwana yule, anaposimama majukwaani, sauti anayoitoa si ya kawaida, lakini leo ameongea kwa utaratibu mno! Sasa sijui alikuwa anaonesha nini, maana yale aliyokuwa akiyaongea na yanayotakiwa yazungumzwe humu ndani hayafanani. *(Makofi)*

Sijui ndiyo maana sauti ikawa ndogo, *Allahu Yaalam,* lakini ninachotaka kusema, kule kwetu sisi kuna ndege akiimba anasema *sambinigwe*, yaani maana yake bado kidogo ningeanguka. Ndiyo wimbo unaoimbwa humu ndani. *(Kicheko)*

Daftari la Wapiga Kura linakuwa baya pale tu wenzetu wanaposhindwa, lakini wakishinda lile Daftari halina hasara! Wameshinda Arumeru Mshariki kwa asilimia 72, Daftari hilo hilo, na wao wamo humu ndani daftari hilo hilo; ndiyo yule ndege yule *sambinigwe*. Hilo ni neno la Kizaramo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante, lakini nafikiri nimeeleweka, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** *Sambinigwe!*

**SPIKA:** Haya mmepata msamiati. *(Kicheko)*

Sasa nitamwita Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, atafuatiwa na Mhehsimiwa Chatanda.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia muda huu. Kwanza, kuna haja ya kutoa pongezi kwa jitihada zinazofanywa katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Tukubali kwamba, wanajitahidi, lakini ni kawaida ya Uongozi, mwenzake akikamata dhamana anamwona kama uwezo hana, lakini kwa kweli uwezo upo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila zuri halikosi kasoro; kuna matatizo makubwa sana yanajitokeza katika Halmashauri zetu ya ubadhirifu wa fedha. Muda mrefu nipo katika sehemu hizi, utendaji hauridhishi kwa watu wetu! Kitu ambacho kinasikitisha zaidi, muda wa kustaafu mfanyakazi yeyote unaeleweka na inafika hadi mtu kufariki, lakini utakuta kwa miezi sita au mwaka mzima zinakwenda fedha kwa mtu yule; ni kitu cha kustaajabisha sana.

Kwa hiyo, kuna haja ya kwa waangalifu na ningependa kushauri au kutoa mapendekezo katika Halmashauri zetu. Kwanza, ningependa Wakurugenzi wapewe angalau meno kwa Watendaji wao. Kama Watendaji au Mkurugezi, hana uwezo wa kumchukulia hatua yoyote mtendaji wake, kwa kweli heshima ya utendaji haitakuwepo. Kwa hiyo, kuna haja ya kuangaliwa hili japo kwa sheria ndogondogo nazo kidogo zimlinde ili aweze kufanya kazi yake vizuri. *(Makofi)*

Natumaini hili moja litachukuliwa zaidi, lakini hata Mkaguzi wa Ndani, awe mbali na Ofisi za Mkurugenzi na apatiwe usafiri ili aweze kufanya kazi zake vizuri. Haiwezekani kuwa wewe unamtegemea mtu, unafanya kazi, bila shaka hisani kidogo inapotokea utakuwa huna nzuri ya kufanya kazi yako.

Vilevile Serikali au Halmashauri, iangalie uwezekano wa kutekeleza Miradi kwa awamu, badala ya kutekeleza Miradi mingi kwa wakati mmoja. Ina maana lazima pawe na *choice*, kwamba, lazima tufanye hiki na mwaka mwingine tuweze kufanya hivi. Kwa kufanya pamoja ndiyo inasababisha hatuwezi kukamilisha Miradi yetu na tunakwama njiani.

Vilevile Halmshauri zitengeneze mifumo thabiti ya usimamizi na ufuatiliaji wa Miradi inayotekelezwa katika ngazi za Kata na Vijiji. Hii vilevile itasaidia, lakini pia na Serikali iangalie upya utaratibu wake wa kotoa ukomo wa bajeti *(Budget Ceiling),* kwani inapelekea bajeti nyingi kutokuwa na uhalisia. Mambo kama haya tunaweza kuyaangalia zaidi, yatatusaidia katika utendaji na katika sehemu zetu husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho Wabunge wengi hawalizungumzi, nalo ni kuhusu UKIMWI! Nina ushahidi mzuri sana, hata wakija madaktari hapa hatuendi kupima. Ushahidi ninao mzuri, nipo muda mrefu kwenye Bungeni hili. Hapo utaona kuna maambukizo mapya, katika ukurasa wa 85, watu 1,261,931 wenye VVU, watu 669,730 wamepatiwa dawa.

Mheshimiwa Spika, kwa mwenendo tunaokwenda, hatuwezi kufaulu kuweza kuondoa maradhi haya, ni bora tukose mtu mmoja tuepushe watu 100, tutafanikiwa. Mimi naona kuna haja hivi sasa kuchukua hatua kutokana na vitendo viovu vya uzinzi itatusaidia. Suala la kwamba, tunawapa watu dawa, baadaye mtu mmoja yule unamwona yuko *strong* na unamhisi kama hana maradhi, lakini ana maradhi na anaambukiza, haitusaidii! *(Kicheko/Makofi)*

Hivi sasa tuna miaka kama 34 na maradhi haya na bado yanaendelea. Hawa watu 1,261,931 niliosema, angalia watu hawa kila mmoja afanye uasi kwa mtu mmoja tunapata milioni ngapi! Madhali unawapa dawa hatuwezi kufanikiwa, tutazidisha maradhi kwa njia hii. Lazima tutafute uwezekano halisia utakaotusaidia, hakuna kitu kimoja kinachosaidia au sehemu yoyote ya dini zetu inayoashiria mambo maovu.

Kwa hiyo, mimi nahisi kubwa kupinga mambo maovu. Kuna maeneo mbalimbali tunayajua ya madanguro, mbona hatuchukui hatua! Mambo haya ndiyo ya kuchukua hatua. Kusema huyu nampa dawa, huyu anaambukiza, kwa hiyo, haitatusaidia. Haya hatusemi ukweli, unaona hata watu hawapigi makofi, hayakuwapendeza haya! Haya hayakuwapendeza watu, lakini huu ndiyo ukweli ulivyo. Kwa njia tuyayokwenda Serikali inazidi kuchangia. Ukishakuwa na maradhi huwezi kusema wewe mtendaji wa kazi mzuri, siyo kweli. Wewe ni mgonjwa isipokuwa unaambukiza na ukiambukiza wewe mtu mmoja unaambukiza watu mia, inakwenda tu, hii si hali nzuri wala haitusaidii. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, Serikali lazima itafute taratibu halisi za kufanikisha mambo haya ili tuepukane na maradhi haya. Toka 1980, walikuwa watu kama milioni, ilikuwa haijafika watu milioni, leo tuna wangapi na dawa mnatoa. Itafika wakati hao wahisani hawataleta dawa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Wewe peke yako umesema acheni michepuko! *(Kicheko)*

Nilisema nitamwita Mheshimiwa Chatanda, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari.

**MHE. MARY PIUS CHATANDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza, naomba niipongeze *TBC* kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuwahabarisha na kuwaburudisha Wananchi, wakiwemo UKAWA, ambao kwa ushahidi kabisa walipofanya mkutano kule Kibandamaiti, *TBC* ilionesha *live*.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri tukaipongeza *TBC* kwa kazi wanayoifanya na wenzetu hawa wanaendelea kuoneshwa, kwa hiyo, waendelee kuiunga mkono *TBC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upelekaji wa fedha za maendeleo kwa Wakuu wa Mikoa; mapato yasipokusanywa kikamilifu, ni lazima kutasababishwa Miradi ya Maendeleo kutotekelezwa kama ilivyokusudiwa. Vilevile, ahadi mbalimbali za Viongozi wa ngazi ya Kitaifa hazitatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, utatuzi na ufumbuzi wa masilahi ya wafanyakazi, mikopo kwa wanawake na vijana, haitapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi, madai sugu ya walimu ambao wameendelea kuwa wavumilivu, watulivu na wasikivu kwa muda wote, kushindwa kutatuliwa.

Mheshimiwa Spika, hivyo, ninashauri wale wenzetu waliokabidhiwa dhamana za kukusanya mapato, wafanye kazi hiyo kwa ukamilifu ili kutekeleza Miradi iliyopo, pamoja na kugharimia yale yote ambayo nimeyatamka katika maelezo yangu.

Mheshimiwa Spika, katika hili suala la walimu, huu Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa, naomba uanze kuwanufaisha sasa walimu kwa kuwaondolea kero zao. Vilevile naishauri Serikali, kama inawezekana irudishe *teaching allowance*, ilikuwa inawasaidia sana walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo tutakuwa tumetoa motisha kubwa kwa walimu na kutoa morali ya kuweza kufanya kazi zao vizuri. Vile vile lipo tatizo la waalimu wastaafu. Wakishastaafu walimu hawa, walio wengi hawalipwi nauli za kurudi makwao. *PSPF* imejitahidi sana kuwalipa *cheque* zao. Sasa unapowalipa *cheque* za mafao bila kuwapa nauli ya kurudi makwao,

unakuwa huwatendei haki. Niwaombe sana, katika suala la nauli, pamoja na kwamba *PSPF* wanawapa *cheque* zao kwa wakati, basi lipatiwe ufumbuzi ili nao waweze kupata nauli za kurudishwa makwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la upatikanaji wa maji safi na salama; nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitaishukuru Serikali kupitia Benki ya Dunia *(World Bank),* ambayo imekamilisha Mradi wa Maji Kata ya kwa Mndolwa Korogwe Mjini, ambao unahudumia vijiji viwili. Wananchi wamerejesha kwa Serikali yao kwa sababu Mradi huu ulikuwa umeahidiwa toka 2005. Hata hivyo, ninawashukuru watu wa *World Bank,* wanaendelea na kata ya Magunga na kwa Msisi na maendeleo yake yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, naendelea kuomba katika Mpango huu wa Maendeleo Makubwa Sasa, uendelee kusimamia kuhakikisha sasa maji safi na salama yanapatikana kwa Wananchi wote. Tumefanya kazi kubwa ya kuboresha barabara zetu, sasa tufanye kazi kubwa ya kuhakikisha maji yanapatikana ili Wananchi hawa waweze kupita kwenye barabara zile wakiwa na afya nzuri, wakienda kufanya biashara wawe na afya nzuri. Kwa hiyo, naomba katika Mpango huu sasa tuingie kwenye utaratibu wa upatikanaji wa maji safi na salama, kama ambavyo tumefanya kazi kubwa kwenye barabara.

Mheshimiwa Spika, suala la asilimia tano za mikopo ya wanawake na asilimia tano kwa vijana; zipo baadhi ya Halmashauri hazitengi fedha kwa ajili ya ile mikopo ya vijana na wanawake. Niwaombe Wakurugenzi wahakikishe wanatenga asilimia hiyo tano kwa ajili ya wanawake na vijana ili watu hao waweze kujikomboa kiuchumi. Siyo kwamba, Bunge liliweza kupitisha utaratibu huo kama mapambo, hapana, tunataka Wananchi hawa waweze kujikomboa kiuchumi kupitia mikopo hiyo ili waweze kuendesha shughuli zao ambazo wanazikusudia na kujikomboa kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kumejengeka tabia ya kuanzisha Miradi. Serikali imeanzisha Mradi wa Jengo la Utawala Chuo cha Uuguzi Magunga pale Korogwe. Jengo lile tangu limeanzishwa lina miaka minne sasa halijawahi kutengewa fedha. Naiomba Serikali, kwa sababu wale wakufunzi, walimu, wanakaa kwenye darasa ambalo inabidi watoto walisomee, lakini wanafunzi wale wanasomea kwenye bwalo la chakula kwa sababu walimu wako kwenye darasa lao. Sasa naiomba Serikali, kama upo uwezekano katika bajeti ya mwaka huu wakifikirie kile Chuo pale Magunga ili kiweze kukamilisha Jengo lao la Utawala.

Mheshimiwa Spika, nashukuru ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. KHATIB ALI HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa uungwana mkubwa nilionao, napenda kumpa taarifa mchangiaji aliyemaliza kuchangia hivi punde kwamba, *TBC Taifa* haikutangaza Mkutano wa Kibandamaiti. *TBC* kama kuna nyingine, lakini hii ya Nkamia tunayoijua haikutangaza Mkutano wa UKAWA. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. MARY PIUS CHATANDA:** Mheshimiwa Spika, niliona *TBC*.

**SPIKA:** Ukimaliza kusema taarifa ni ya kwake anajua yeye mwenyewe. Tunaendelea, nilisema Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari, atafuatiwa na Mheshimiwa Msabaha!

**MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami nitachangia machache tu.

Kwanza, napenda niipongeze Serikali kwa kuendelea kutatua kero zinazowakuta Wananchi kwa lengo kubwa kabisa la kufanya maisha yao yaboreke na shughuli zao za kila siku ziwe rahisi.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mwakyembe, kwa kazi nzuri aliyoifanya. Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa *Terminal Three* tuliuasisi muda mrefu, kuona sasa hivi utekelezaji wake umeanza sisi tumefarijika sana. Kwa sababu tunajua uwanja wa ndege ni muhimu sana. Nilikuwa najiuliza, hivi baada ya mvua zote hili zilizonyesha, madaraja kukatika na barabara zote kuharibika, isingelikuwa viwanja vya ndege kuwa imara na kufanya kazi yake tungelifanya nini? *(Makofi)*

Nichukue nafasi hii nimshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa sababu ameona Mradi huu una maana, una faida kiuchumi na una tija kwa Wananchi na hasa utaboresha utalii. Angeliweza kusema niuache huu niu-*shed* kidogo nitafute Mradi mwingine, lakini nashukuru kwamba zile *efforts* tulizozifanya sasa zinazaa matunda.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda niseme nimefurahi sana kuona sasa tumemaliza *feasibility study* na *design* ya reli ya kuunganisha Arusha na Musoma. Ni suala la muda mrefu na tulilizungumza muda mrefu sana, kila siku tulikuwa tunaambiwa hakuna pesa. Sasa ni vizuri basi tuthubutu, kwa sababu wenzetu wa Kenya wanavuna magadi kule kwa muda mrefu sana na sisi ilikuwa ni hadithi tu. Nina uhakika Mheshimiwa Mwakyembe atalishughulikia hili na tuone faida ya Reli ya Arusha na Musoma.

**SPIKA:** Mheshimiwa siyo Mwakyembe nafikiri ni Waziri wa Uchukuzi.

**MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Waziri Mwakyembe ninamshukuru sana, namwomba tu sasa baada ya *design* apewe pesa kwa ajili ya kujenga Reli ya Arusha – Musoma. Ni vizuri tuthubutu kwa sababu hii ndiyo miundombinu itakayotusaidia kuboresha uchumi wetu.

Ujenzi wa Reli ya Isaka Kigali ni muhimu sana. Tunafurahi kwamba, *feasibility study* imemalizika na usanifu tayari umekamilika, basi Serikali tuache kigugumizi kuipatia fedha; kama hatuwezi basi angalau tuwaruhusu Mheshimiwa Waziri akope ili reli hii ijengwe na tufungue njia katika kanda zinazohusika.

Mheshimiwa Spika, siku zote tulikuwa tunasema umuhimu wa kujenga Reli zetu za TAZARA na Reli ya Kati. Kutokana na kwamba, tunatia msukumo zaidi kwenye barabara na wafadhili hawapendi sana kusaidia reli kwa sababu *infrastructure* inachukua hela nyingi sana na wakitusaidia sisi tunaweza kujikomboa sana kiuchumi. Niombe tu Mheshimiwa Waziri, ajitahidi kwa kadiri atakavyoweza, Miradi hii ikikamilika tutakuwa tumefungua sana maeneo yetu kiuchumi, tutarahisisha Wananchi wetu wanaolima kusafirisha mazao yao na wakati huo huo tutaboresha uchumi wa nchi yetu.

Nilisema niyaseme hayo machache, kwa sababu tuliyafanyia kazi na tumemwona Mheshimiwa Waziri naye kayachukua kwa uzito wake, nampongeza sana, namwombea mafanikio mema.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Nilisema nitamwita Mheshimiwa Msabaha, atafuatiwa na Mheshimiwa Ignas Malocha!

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi nichangie Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kwanza kabisa, niwapongeze Wabunge wa CCM kwa kupoteza muda mwingi kujadili Hotuba hii ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Naona ni namna gani ilivyowagusa na ninaomba Serikali, mambo yote mazuri yaliyomo kwenye Hotuba hii, myachukue myafanyie kazi kwa ajili ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 14, kuna mambo ambayo Mheshimiwa Chombo, alipotosha humu ndani. Ibara ya tatu, alitajwa Mheshimiwa Awadh Salmin ndiye ambaye alitajwa huku, naomba Mheshimiwa Chombo airudie na aisome vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, mchango wangu nitauelekeza kwenye msamaha wa kodi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, huu msamaha wa kodi

imekuwa ni kero, tunapoteza pesa nyingi kwenye misamaha ya kodi. Sasa hivi tuangalie ni namna gani ya kubana hii misamaha ya kodi irudi Serikalini ili tupate kutatua mahitaji yetu. Sasa hivi ukiangalia bajeti, wahisani hawatuchangii vya kutosha katika bajeti yetu. Kwa hiyo, tuangalie vyanzo vyetu vya mapato ni namna gani ya kuvidhibiti ili tupate bajeti ambayo ni tegemezi na si bajeti ya ombaomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuna Sheria ambayo ilikuwa inatumika, Sheria ya Wahujumu Uchumi, Sheria hii sijui kama ina meno; na kama ina meno ni wahujumu uchumi wangapi wameshughulikiwa ambao wanalitafuna Taifa hili. Tunaangalia, watu wengi wanaona kama Wabunge ndiyo wenye fedha, lakini kuna watu kila mtu akilala akishasoma kidogo Serikali ikimsomesha, anawaza namna ya kuiibia Serikali, lakini hawa ambao wanahujumu uchumi tunawashughulikia vipi Mheshimiwa Waziri Mkuu?

Naomba unipe majibu wakati wa majumuisho yako na kama Sheria hii haina meno iletwe hapa Bungeni tuangalie ni namna gani tutaipa meno ifanye kazi kama ilivyokuwa inafanya wakati wa Marehemu Mheshimiwa Edward Moringe Sokoine, aliyekuwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, tunaangalia sasa hivi umaskini umekithiri vijijini. Ukienda sasa hivi mvua zinavyonyesha watu wanasimama mpaka asubuhi nyumba zinavuja. Kwa kweli tuangalie hawa ambao wamejilimbikizia mali kwa njia ya rushwa, kwa njia ambazo siyo za halali, tuchukue mali hizi na tuwapelekee mayatima, tupeleke kwa maskini, tupeleke kwa walalahoi ambao wako vijijini, ambao hawapati hata mlo wa siku moja.

Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu uthubutu kama Mwalimu Nyerere alivyothubutu. Upole wako naujua, umesoma Misheni, umelelewa Misheni na haukuwa Padri, lakini umekuja kwenye siasa, naomba uwawajibishe Mawaziri wako ambao wako kila Wizara. Waziri ambaye hafanyi kazi katika Wizara yake umwajibishe vya kutosha. *(Kicheko)*

Leo tukiangalia Tanzania tunaongoza, kuna ombaomba wengi, kuna wazee wengi wanalala kwenye mitaro, kuna watoto kila kukicha hatujui wanatokea wapi. Tunatakiwa tuangalie watoto hawa wanatoka wapi, watoto hawa wana baba au kuna akina baba ambao wanakimbia watoto? Na kama kuna akina baba ambao wanakimbia watoto wao na wana uwezo, tunatakiwa tuwadhibiti ili tupunguze janga la taifa, watoto wa mitaani wamekuwa wengi. *(Makofi)*

Tuangalie wazee, wazee wamekuwa kero hata kwa wageni ambao wanakuja Tanzania kwa kuombaomba. Tukienda nchi za wenzetu, leo hii watu wasiojiweza wanalipwa na Serikali. Mimi siku moja nilikuwa Korea kwenye treni,

akapita mtu ambaye anaombaomba, lakini mtu yule kaoga vizuri. Walichokisema, wakasema Serikali ya Korea inawalipa watu wote, hata kama ni mwendawazimu, hata kama ni mlemavu wote wanalipwa. Kwa nini sisi Serikali yetu hii isiangalie na tuna vyanzo vingi vya mapato na tuna rasilimali nyingi hapa lakini zinaishia kwenye mifuko ya watu. Ufisadi ndiyo mkubwa, kila mtu anaangalia ni namna gani nitaiibia Serikali watoto wangu wasome vizuri, nile vizuri, nipande gari zuri; hasemi ni namna gani nitaitumikia Serikali na Wananchi wangu!

Mheshimiwa Spika, tuangalie sasa hivi imefika wakati wa kutokomeza mafisadi na sheria hii ya wahujumu uchumi ifanye kazi, kama haifanyi kazi naomba ifanye kazi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko mengi kwenye Vyuo Vikuu. Mimi nipo kwenye Kamati ya Miundombinu, tunapitisha bajeti, lakini tukiangalia Vyuo Vikuu vingi havipati ile bajeti kwa wakati mwafaka. Watoto wa maskini ambao wanasoma Vyuo Vikuu ile mikopo imekuwa haiwafikii kwa wakati mwafaka. *(Makofi)*

Hii ni kero na tuwadhibiti jamani hawa ambao wana uwezo wasichukue zile pesa za kuwasaidia watoto wa wakulima wapate na wao kusoma katika nchi yao.

Mheshimiwa Spika nashukuru, haya machache naona yameeleweka mpaka kilemba changu kimevuka. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante. Nilisema nitamwita Mheshimiwa Malocha, atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Mwambu kama yupo.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii. Kwanza, nichukue fursa hii kutoa pole kwa Wananchi wa Sumbawanga Vijijini na Chama cha Mapinduzi kwa ujumla, kwa kupotelewa na Katibu wa CCM Wilaya ya Sumbawanga, ambaye amefariki leo Mjini Mbeya. Mwenyezi Mungu, aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi; *amina.*

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu nataka nijielekeze kwanza katika malengo ya makusanyo ya Serikali Kuu na Halmashauri za Wilaya. Rekodi zinaonesha mfululizo wa miaka mingi makusanyo ambayo tunapanga wenyewe, tunasimamia wenyewe, hatujafikia lengo hata siku moja. Kwa maana hiyo, kama hatujafikia lengo tusitegemee muujiza wa kutekeleza Miradi tuliyopanga, matatizo yataendelea kuwepo siku hadi siku. Lazima tujielekeze katika kusimamia vizuri makusanyo tuliyoyapanga wenyewe.

Cha ajabu, inaonesha hata katika Halmashauri, wanapanga bajeti, wakileta huku Serikali Kuu inapangua inaweka ukomo kuthibitisha kwamba, ina uwezo wa kutoa zile fedha lakini haitoi. Sasa unashindwa kuelewa mnapanga wenyewe halafu hamtekelezi; ni jambo la ajabu sana na msitegemee muujiza kuleta maendeleo kama hatukusanyi kodi. Kwa hiyo, nasisitiza, Serikali ijipange vizuri katika kusimamia makusanyo. Vilevile yawezekana tunakusanya halafu makusanyo yanavuja, nalo mliangalie; mimi sitegemei kama makusanyo yote yanayokusanywa yanaingia kwenye kihenge kama inavyostahili. Jambo hilo lazima tuliangalie upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nataka nizungumzie suala la ardhi. Sisi wote tunafahamu kwamba, ardhi ni mkombozi wa wakulima, wafugaji, wavuvi na wachimbaji wa Miradi ya Madini. Kati ya Watanzania milioni 45, karibu Watanzania 39,000,000, sawa na asilimia 86.7 wanategemea kilimo na shughuli mbalimbali kutokana na ardhi. Cha ajabu, karibu kila kona ya nchi imejaa migogoro ya ardhi; wafugaji na wakulima, wakulima na wawekezaji. Cha ajabu Serikali inachukua hatua pale milipuko inapotokea watu kuuana au kugombana! Kwa nini tusiweke utaratibu wa kueleweka nchi nzima kuondokana na tatizo hili ambalo linajitokeza mara kwa mara? Tunataka mpaka nchi hii ije iingie kwenye migogoro mikubwa ya ugomvi au mapigano ya hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, ningeishauri Serikali ijaribu kuliangalia suala hili, huko mbele tunakokwenda litatuletea matatizo makubwa sana. Watu wanaohusika na usimamizi wa mambo haya, wanapaswa kuweka mipango thabiti katika kukomesha jambo hili.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna jambo moja linanisikitisha sana; katika Jimbo langu kuna mgogoro wa ardhi katika chamba la Malonje. Jambo hili limechukua muda mrefu sana, limezungumzwa mara kadhaa, Viongozi wamekuja kule wamezungumza mara kadhaa; amekuja Katibu wa CCM Taifa amezungumza, Wananchi wamemlalamikia; amekuja Makamu wa Mwenyekiti CCM Taifa; imekuja Kamati ya Ardhi ya Bunge; na Mheshimiwa Rais naye akapata taarifa akatoa agizo kwa Waziri mwenye dhamana kwamba, anamwagiza kumaliza tatizo hilo haraka iwezekanavyo kwa namna yoyote ile; iwe ni kumfidia mwekezaji au ni kwa namna yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha tangu Mheshimiwa Rais ametoa agizo hilo, sasa hivi miezi 11 imepita, Waziri ambaye ameteuliwa na Rais huyu hajafika hata kwenye eneo au Naibu wake hajafika hata kwenye eneo. Hivi tunataka kumuweka Rais katika msimamo upi? Hivi nchi hii itaheshimiwa na nani kama Rais hawezi kuheshimika, anatoa maagizo miezi 11 inapita hakuna uekelezaji; nchi hii sasa itaheshimikaje? Rais ametoa agizo na Wabunge mlisikia alipoagiza

kwamba, anataka ardhi irudishwe mikononi mwa Wananchi kwa namna yoyote ile, iwe ni kwa kufidiwa au kwa namna yoyote.

Sasa ni miezi 11 hata Waziri mwenye dhamana hajakanyaga hata kwenda kutoa ushauri mnategemea nini? Rais huyo ataheshimikaje kama Wateule wake hawachukui hatua?

Ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, jambo hili uje ulitolee ufafanuzi Wananchi wajue. Kama Serikali haiwezi kuwasaidia basi wajue watafute njia yoyote au mimi nikawahamasishe wafanye maandamano waje ofisini kwako.

**WABUNGE FULANI:** Hapana. *(Kicheko)*

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Ndiyo, kwa sababu suala hili limechukua muda mrefu, Wananchi wanazidi kuumia, wanapata madhara na wanazidi kuwa maskini. Hii Serikali ina maana gani kama Rais wa nchi anatoa agizo halafu wa chini yake hatekelezi maana yake ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba Waziri Mkuu aje anitolee ufafanuzi ni kwa nini Kiongozi mwenye dhamana hataki kuchukua hatua hata kufika kwenye eneo husika kutoa ushauri anafikiria nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ninalotaka kuzungumzia ni ahadi ya Rais. Asubuhi wakati nikiuliza swali nimeeleza ahadi ya Rais aliyoitoa mwaka 2010 wakati wa Uchaguzi Mkuu. Alitoa ahadi ya kujenga zile barabara mbili; Kalambanzite – Ilemba na Miangalua – Chombe, kwa kuziwekea lami. Sasa hivi tunaelekea karibu mwaka wa mwisho na Bajeti hii ndiyo hii ya mwisho sisi kama Wabunge kuisimamia, sasa ni muujiza gani utakaokuja kutekeleza zile ahadi za Rais! Tufike mahali kuwe na chombo mahususi cha kufuatilia maagizo au ahadi za Rais na kuhakikisha zinatekelezwa; vinginevyo, inakuwa ni aibu kwa Serikali, ni aibu kwa Viongozi.

Mheshimiwa Rais, alitoa ahadi ya umeme, ninashukuru Waziri mwenye dhamana na jambo hili anajitabidi na tumeahidiwa kwamba, umeme utawekwa. Kwa jinsi tunavyomfahamu na jitihada zake na usomi wake, tuna imani naye, lakini tunataka jambo hili lisifike mwaka 2015. Tunaenda kwenye Uchaguzi, umeme uwe umeshaenea katika Wilaya zote ambazo zina matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ninaona muda wako wa kuzungumza umekwisha.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Oh! Ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa ninaomba nimwite Mheshimiwa Salome Daudi Mwambu, atafuatiwa na Mheshimiwa Andrew Chenge.

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niseme machache kuhusiana na Hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Kwa kweli, Mheshimiwa Waziri Mkuu kama Serikali, Serikali imejipanga na inatekeleza mambo katika Mikoa yote na Wilaya zake. Wote hapa kila mtu kaguswa, kama upungufu upo basi utakuwa unaenda unamalizwa taratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninapenda nizungumzie kuhusu hizi Wilaya mpya. Wilaya mpya nyingi hazina uwezo wa kujiendesha, kwanza, miundombinu ni hafifu, maji hamna. Kwa mfano, Wilaya yangu ya Mkarama, tunajenga Makao Makuu Ndukuti, hatuna maji, hayo Makao Makuu tutayajengaje? *(Makofi)*

Tunaomba sana Serikali iliangalie hilo, itupie macho katika hizi Wilaya mpya. Vilevile magari hatuna, huwezi kuamini hata gari la ukaguzi wa shule hatuna na ndiyo maana Wilaya yangu ilifanya vibaya mwaka 2013, kwa sababu hatuna miundombinu, magari ya kutufikisha kule mashuleni na kwenda kukaguliwa. Nimesikia eti kuna magari mapya Wizara ya Elimu inanunua; chondechonde, ninaomba Wilaya ya Mkarama tupewe gari la ukaguzi, kwa sababu hata Mkurugenzi hana magari pale, ana gari moja tu tutafanyaje kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakumbuka Mheshimiwa Rais mwaka 2010 katika ahadi zake alisema, hizi Wilaya mpya, atahakikisha zinafanana na Wilaya za zamani. Sasa sisi majengo hatuna, magari hatuna, tutaendaje ili tufanane na wenzetu? Ninaliomba hilo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, afuatilie, ili na sisi tufanane na wenzetu.

Suala lingine, ninapenda nizungumzie kuhusu ardhi. Pamoja na kuwa Kitengo cha Ardhi kitakuja, lakini sisi kuna tatizo moja kubwa la ardhi, nalo linahusiana na haya mapori ya hifadhi. Nina ndugu zangu Wahdzabe, wako takribani watu 1,000 wamebakia, kile kizazi kitafutika. Ninaomba wapatiwe makazi yao ya kudumu, waache kuingiliwa na Makabila mengine. Tatizo lao au kitu ambacho hatufanani na sisi, wao wanakula nyama hawali vyakula vingine, ukimlazimisha anaugua. Sasa hawa binadamu ni lazima tuhakikishe wanatendewa haki na Serikali. *(Makofi)*

Wale watu wanaowavamia waondoke haraka sana. Suala hili nilishawahi kuchangia, ninairudia tena baada ya kuona hakuna kinachoendelea. Ninaomba Serikali ifikirie, kimebaki kizazi hiki tu cha Wahdzabe, ninaweza nikasema katika Afrika, sasa tusiwapoteze hawa watu. Wana mchango mkubwa Serikali ikiwatumia, wanajua dawa za asili nyingi mno. Serikali ikipeleka Wataalam wake watajifunza. Jamani wako *useful.* Nao ni watu na wana faida katika jamii, kwa hiyo, ninaomba Serikali iwaangalie. *(Makofi)*

Akina mama wanahangaika, pamoja na Mfuko wangu wa Jimbo, ninahangaika lakini hela inakuwa haitoshi. Hawana mahali pa kuzalia.

Mheshimiwa Spika, sasa tumeshawafundisha maendeleo, wanajua wakiugua au wanapotaka kujifungua wanaenda hospitali au kwenye kituo cha afya, lakini ndiyo unakuta hatuna majengo ya kuwahifadhi wale watu. Tunatakiwa Serikali iwasogezee huduma zote ziwe karibu na lile Pori lao la Hifadhi, ambalo Serikali imewatengea, lakini bado wanavamiwa, wanaingiliwa.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa nafasi hii uliyonipa.

Mengine ni kuhusu Wilaya yangu kwa ujumla. Wilaya ya Mkarama ni changa, tunaomba sana majengo ya watumishi. Watumishi hawana majengo, ofisi hatuna. Tumeanzisha ofisi kwa kuazima azima tu, kukodi kodi, mara leo muambiwe hapa ondokeni mwenye nyumba anataka kugeuza nyumba yake kuwa *Guest House.* Tutafika wapi katika utendaji huu wa Serikali? Tunaomba katika Bajeti hii pesa itengewe ili tuweze kujengewa majengo na sisi tuweze kujiendesha kama Wilaya nyingine.

Mheshimiwa Spika, watumshi nalo ni tatizo. Watumishi wengi hawapo, tunaomba tupelekewe watumishi. Nina imani Mkurugenzi wangu na Afisa Utumishi wamepeleka matatizo tuliyonayo katika upande wa Watumishi, Watendaji wa Serikali, ninaomba. Vilevile Wilaya yangu imekaa msambao, ninaomba katika huu mgawanyo wa kuongeza Kata na Vijiji tulivyoomba tufikiriwe, kwa sababu jiografia imekaa ya msambao. Unakuta kutoka Makao Makuu ya Kata mpaka kwenda kwenye Vijiji, siyo chini ya kilometa 60 mpaka 70. Sasa ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. SAL0ME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Andrew Chenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Msolla.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Nitamke kwamba, ninaiunga mkono hoja ambayo ni Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu; ni Hotuba nzuri na ina mambo mengi ambayo yanatoa mwelekeo kwa maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hotuba ya Mheshimwia Waziri Mkuu katika ukurasa wa 21, amesema yale ambayo ni ya msingi sana kuhusu ukuaji wa uchumi. Tunafanya vizuri, asilimia 7.0 katika mwaka 2013, lakini anasema wazi na huu ndiyo ukweli Mheshimiwa Spika na kwa Watanzania wote; ukuaji huu bado ni wa chini sana kama tunataka tupambane na umaskini. Amelisema wazi kwamba, lazima ukuaji wa uchumi wetu ufike asilimia 8 na zaidi, na siyo uwe wa siku moja au mwaka mmoja, lazima tuufanye kwa mfululizo na ndiyo maana nchi nyingi zimefanikiwa kwa namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, tuna Sera nzuri, lakini na yeye Mheshimiwa Waziri Mkuu anakiri, katika Hotuba yake ukurasa wa 22 anasema. "Mheshimiwa Spika, njia ya uhakika ya kuliwezesha Taifa kuwa na uchumi imara na wa kisasa, unaohimili ushindani katika Masoko ya Kikanda na ya Kimataifa, ni kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji."

Mheshimiwa Spika, tatizo tulilonalo katika nchi yetu kwa bahati mbaya, Sera ni nzuri, lakini ni sisi wa kwanza kuvuruga tena mazingira ya wawekezaji nchini. Tukilitambua hili, mengi ya makosa ambayo tunayafanya kila mwaka hasa katika mfumo wa kodi, tunaweza tukafikia kiwango cha ukuaji wa uchumi wa juu zaidi ya sasa hivi. *(Makofi)*

Ninaipongeza Serikali kwa maeneo hayo ambayo imeanzisha huu utaratibu wa kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Lazima pia tuangalie upande wa pili wa shilingi, matumizi ya Serikali yetu bado ni makubwa mno. Ni vyema tukaangalia katika Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na Serikali za Mitaa, tumesoma Taarifa ya Kamati, tunaona *trend* ya matumizi ni kubwa mno, lazima tuliangalie suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtu kwao; ninaishukuru Serikali kwa kazi nzuri, Makao Makuu ya Mkoa wa Simiyu ni Bariadi. Bariadi ni mji unaokua haraka sana, unapanuka haraka sana na una wakazi wengi; kwa maana hiyo tunahitaji uamuzi au *support* ya makusudi katika kupata huduma za Wananchi wetu. Tumeleta maombi Serikalini, TAMISEMI.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, ametembelea Bariadi na viongozi wake wamefika Bariadi. Bariadi, kuna mito na vijito vingi sana vinavyopita katika maeneo ya mji. Kwa hali ilivyo, Halmashauri ya Mji na hata kidogo ya Wilaya, hawataweza kujenga madaraja katika eneo la Mji wa Bariadi. Ndiyo maana tuna ombi kubwa kwa upande wa Mto Gabasingija unaotoka Sekondari ya

Chenge, kwenda Nyaomata, tunahitaji tuwe na daraja pale. Mto Ndoba na Mto Bariadi. Kwa sababu maeneo ambayo tunayalenga sisi katika kutoa huduma kwa Wananchi wetu ni haya. Tukiyashughulikia haya, hali katika Mji wa Bariadi na *environ* zake itabadilika haraka sana.

Mheshimiwa Spika, lipo ombi lingine la siku nyingi na labda kwa sababu Waziri Mkuu alipopita juzi, hata Mheshimwia Rais, hakupata nafasi kwenda kutembelea maeneo mengine zaidi ya yale waliyopita; lakini eneo la daraja katika Mto Duma, eneo linaloitwa Gibishi, Serikali imewekeza pale zaidi ya shilingi 300,080,000, lakini ukifika pale utaona aibu. Mimi ninaomba Serikali tuoneshe uchungu wa kodi za Wananchi.

Eneo hili litapendeza ikiwa Daraja hili la Gibishi tutalikamilisha na tutatenga fedha katika mwaka huu ujao wa fedha. Ombi langu ninarudia mtu kwao, Daraja la Gibishi na Madaraja ambayo tumeomba ya Gambasingija, Ndoba na Bariadi, ili Serikali iweze kuzisaidia Halmashauri ya Wilaya pamoja na ya Mji wa Bariadi kwa hali ambayo kama Makao Makuu ya Mkoa mpya wa Simiyu, angalau uendane na hali ya kuonesha kwamba ni Makao Makuu ya Mkoa wetu wa Simiyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Nimalizie kwa kusema, ninaunga mkono hoja hii. Ninawaomba pia Ndugu zangu, jamani mmeyasema mengi, lakini mimi ninawafahamu, tukifanya kazi kwa faida ya Tanzania, tunaweza lakini siyo katika haya maneno ya kurushiana vijembe.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Profesa Msolla, atafuatiwa na Mheshimiwa Bwanausi!

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nitoe shukrani zangu za dhati kwa kunipa nafasi hii, ili niweze kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. La pili, nitamke wazi kwamba, ninaunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambayo kusema ukweli imegusa maeneo mengi ya muhimu ya kimaendeleo na huduma za kijamii. *(Makofi)*

Nianze kuchangia kwa kuanza na eneo moja la kundi la Wafanyakazi na ambao wapo katika Serikali za Mitaa. Hawa ni ndugu zetu Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji, ambao wanafanya kazi nyingi sana, ukitaka kuitisha mkutano ni wao na wanaosimamia maendeleo ni wao. Hawa watu wanafanya kazi kwa kujitolea. Ninafikiri umefika wakati waanze kufikiriwa wapate hata kifuta jasho na hasa ukizingatia kwamba, Mwenyekiti wa Kijiji ama Kitongoji anafanya kazi na Mtendaji, Mtendaji huyu analipwa mshahara, lakini Mwenyekiti wake halipwi

kitu chochote. Ninaiomba Serikali iangalie uwezekano wa watu hawa kuwapa moyo kwa kuwalipa angalau posho kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile hili linakwenda sambamba pia kwa Madiwani. Ninajua miaka mitatu iliyopita tulizungumza sana juu ya posho ya Madiwani, kwa kweli haijafika mbali sana. Ukizingatia kwamba, hawa ni katika yale mafiga matatu na tunafanya kazi kwa pamoja, ni vizuri nao wakafikiriwa waweze kuwa na moyo wa kufanya kazi zaidi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012, nilileta hoja hapa Bungeni ya kuomba huduma ya Hospitali Teule ya Itunda na nikapewa majibu yaliyokuwa yananipa moyo. Nilisema huduma katika Hospitali ya Itunda siyo nzuri na ile ndiyo Hospitali Teule ya Wilaya ya Kilolo. Tulisema tulikuwa hatuna mashine za *X-Ray,* hatuna gari la *ambulance,* wala chumba cha kuhifadhia maiti, yaani *mortuary*. Licha ya ahadi tulizopewa mpaka leo hali ile ni mbaya na ni hospitali inayohudumia watu wengi sana. Ukizingatia kwamba, sehemu ile ipo jirani na Mlima wa Kitonga ambako kunatokea ajali nyingi sana za magari na wengi kimbilio lao ni katika Hospitali Teule ya Itunda. Ninaiomba sana Serikali, izidi kuweka mipango iisaidie hii Hospitali Teule ya Itunda.

Tatu, ni kwamba, wiki hii tunaidhinisha Wiki ya Elimu, lakini kwa ujumla elimu yetu katika nchi kama walivyotamka wengi, inazidi kushuka. Vijana wengi ufaulu wao umekuwa duni na tunazidi kuzalisha mbumbumbu wengi sana. Ni vyema katika wiki hii ambayo tunatathmini mafanikio na changamoto, tukaangalia mambo mbalimbali ili kuboresha elimu yetu kwa sababu huo ndiyo urithi wa kuaminika kwa vijana wetu.

Hivi karibuni nimesikitishwa sana na utaratibu wa kupanga madaraja uliowekwa na Wizara. Kwamba, kwa ujumla utaratibu umebadilika; kwa mfano, *Division One* ilikuwa *point 7 - 17,* hiyo haikubadilika. Ukienda kwenye *Division Two* imepanua na kusogeza zaidi wale ambao kwa kweli huko nyuma hawakuwa katika madaraja hayo. Kwa kufanya hivyo, tunazidi ku-*accommodate* vijana ambao ufaulu wao siyo mzuri. Kwa mfano, *Division Two* zamani ilikuwa *point* 18 – 20, sasa ni 18 – 24; *Division Three* ilikuwa *point* 21 – 25 sasa ni 25 – 31; *Division Four* ilikuwa *point* 26 – 33 saa ni 32 – 42 na sifuri ilikuwa *point* 34 – 35, sasa ni 43 – 49. Tulichofanya ni kupanua wigo ili hata wale ambao walikuwa nje ya ufaulu wa kawaida waingie huko wapate madaraja.

Mheshimiwa Spika, tunachofanya ni kwamba, tunajidanganya, tunazalisha kundi la vijana ambao hawatakuwa washindani katika siku zote za baadaye na hasa ukizingatia tunaishi katika Dunia ya utandawazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba, Wilaya ya Kilolo imeleta maombi Serikalini ya kugawiwa Kata na Vijiji na vilevile kupandisha hadhi ya Mji

Mdogo wa Ilula uwe na Halmashauri yake ili kuongeza na kusogeza huduma zaidi kwa Wananchi. Mji wa Ilula unakua kwa haraka sana na ni mji wa kibiashara na hauwezi kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Tumefikisha maombi hayo na vigezo vyote vimetekelezwa, ni imani yangu kwamba, Serikali italitazama jambo hili kwa jicho la huruma na kutupatia fursa hiyo.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, nataka kuzungumzia juu ya huduma ya nishati na hasa umeme. Nashukuru kwamba, sehemu mbalimbali katika Wilaya ya Kilolo tumepata umeme, lakini kuna maeneo mengi ambayo mpaka leo licha ya ahadi zilizotolewa, umeme haujafika. Maeneo hayo ni pamoja na Shule za Sekondari za Udzungwa, Maria Consolatha, Kijiji cha Kibaoni, Luganga, Ilole, Imalutwa, Kimamba, Kidika, Msosa, Image, Boma la Ng'ombe, Kitelewasi, Idegenda, Ng'ang'ange, Viwenge na Mwatasi. Tunaomba sana Wizara inayohusika, kwa sababu hivi vijiji vyote vipo katika Mpango na vimekaa kwa muda mrefu, Wizara itusaidie ili watu wapige hatua katika maeneo ya siku hata siku.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nilisema namwita Mheshimiwa Bwanausi, atafuatiwa na Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale!

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nianze kwa kuthibitisha kwamba, mimi naunga mkono kwa asilimia mia moja Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ningejikita kwenye suala zima la udhibiti wa bajeti zetu. Ushahidi upo kabisa kuonesha jinsi ambavyo Serikali yetu bado haina udhibiti katika suala zima la bajeti. Mimi nashauri kwamba, lazima tuwe na chombo kinachosimamia Bajeti ya Serikali. Kwa kuiachia tu Wizara ya Fedha ifanye maamuzi peke yake bila kuwa na chombo kingine, hii inaweza ikapelekea kuwalaumu Wizara ya Fedha lakini lazima tuwe na chombo ambacho kitakuwa kinadhibiti.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kabisa kwamba, kama hatutakuwa na nidhamu ya fedha tunazokusanya na jinsi ya kuzigawa, tutajikuta kila mwaka tunapitisha bajeti ambayo hatimaye Miradi mingi haitatekelezwa kwa sababu fedha hazifiki kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka kulieleza ni kwamba, kutokana na fedha kutofika katika maeneo husika ya Miradi kwa Wananchi, tumepata matatizo makubwa; kwa mfano, Barabara ya Kibiti Lindi. Taarifa

tulizozipata hivi punde, kwa sababu tuna ndugu zetu wako pale ambao wamekwama, hali za wagonjwa ambao wametoka katika maeneo mbalimbali kuja kwenye Hositali ya Rufaa ni mbaya. Vilevile zipo taarifa ambazo hatujazithibitisha rasmi kwamba, tayari kuna Wananchi wawili wamefariki Dunia pale. Kwa hiyo, hiyo inathibitisha jinsi gani ambavyo Serikali ingeweza kutoa fedha za kumalizia kile kipande cha kilomita 15, huenda madhara haya ambayo Wananchi wanayapata wasingeyapata.

Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, asimamie upatikanaji wa fedha za kumalizia eneo lililobaki la kilomita zisizozidi 15 kutoka Malendegu hadi Somanga. Uzuri wote wa barabara ya lami uliotengenezwa unaharibiwa kwa kipande cha kilomita 15 tu. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu atalisimamia jambo hili kuhakikisha sasa fedha zinatolewa kwa Mkandarasi amalizie eneo lile.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine ambayo imekuwa inawakatisha tamaa Wananchi wa Mikoa ya Kusini ni barabara ya kutoka Mtwara – Tandahimba – Newala – Masasi. Barabara hii ni ya kiuchumi, lakini Mheshimiwa Rais, aliahidi kwamba kabla hajamaliza kipindi chake, atakuwa ameshaweka Jiwe la Msingi la ujenzi wa barabara hiyo. Kwa hiyo, naiomba Serikali ihakikishe ahadi aliyoitoa Mheshimiwa Rais, inatekelezwa kwa kuweka katika Mpango ili mwakani barabara hii ianze kutekelezwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala la Miradi ya Maji. Wewe ni shahidi na Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kwamba, maji ni suala nyeti kwa Wananchi wetu na ni suala ambalo linawagusa karibu Watanzania wote katika Majimbo yote. Tuna Miradi ambayo tumeipitisha kwenye bajeti ya mwaka jana, lakini upatikanaji wa fedha katika Miradi hii ni mdogo mno. Kwa mfano, katika Jimbo langu la Lulindi, Mradi wa Maji wa Chiwambo, kwenye bajeti yetu tulitengewa shilingi bilioni 3.1, lakini hadi sasa Wakandarasi wako *site* na fedha zilizotolewa ni shilingi milioni 231 tu kwenye Mradi wa bilioni tatu. Kwa hiyo, ningeomba Serikali katika kipindi hiki kilichobaki, tuhakikishe fedha zinakwenda ili Mradi ambao unatekelezwa na utaweza kuwasaidia Wananchi kwa takribani Kata kumi katika Jimbo lile uweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kuchangia ni suala la maafa yaliyotokea Masasi. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni shahidi, ametutembelea na kuona athari kubwa iliyotokea katika Wilaya ile. Mimi naishauri Serikali iangalie kwa jicho la huruma ili kuhakikisha magari ambayo tumeyapoteza pale na majengo yetu yapate fedha ili yapatikane magari mapya na pia yale majengo tuweze kuyakarabati ili Halmashauri ya Wilaya ya Masasi au Wilaya ya Masasi kwa ujumla iweze kutekeleza wajibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sana pamoja na janga hili tulilolipata, lakini tuna janga lingine la marufiko. Barabara za Wilaya ya Masasi kuanzia Mjini Masasi na maeneo yote ya Vijijini hazipitiki. Kwa sasa hivi barabara ya kutoka Newala kwenda Masasi eneo la Kijiji cha Mbuyuni magari yamekwama pale. Naiomba Serikali ifanye kila njia inayowezekana kuhakikisha barabara hizi ambazo zimeathirika kutokana na mafuriko zinapatiwa fedha ili shughuli za maendeleo kwa Wananchi ziweze kuendelea kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, nisingependa kugongewa kengele, napenda kurudia kuunga mkono Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Ahsante sana. *(Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Limbu, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Faith Mitambo.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, na mimi nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi niweze kutoa mchango wangu katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Kabla sijasahau, naomba nijaribu kutoa taarifa kwamba, nimekuwa nikipokea simu nyingi na meseji nyingi ambazo zinaeleza kwamba, Walimu wamechelewa sana kupata mishahara yao. Naomba Serikali kama kuna hali hiyo basi ifanye bidii ya kuwalipa Walimu mishahara yao, kwa sababu mpaka sasa hivi bado hawajapata hasa huko Mbeya.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kuchangia katika Hotuba hii. Jambo la kwanza, naomba nijaribu kuzungumzia suala ambalo limejitokeza katika vyombo vya habari hasa kuhusu mafuta. Katika Hotuba ya Waziri Mkuu, ukurasa wa 70, ameelezea sana mambo ya lishe na kwamba, katika mafuta kuna mafuta mengine yanawekewa virutubisho ili watu waweze kupata *vitamin* inayohitajika. Juzi tu tumesikia katika vyombo vya habari wanasema mafuta yote ambayo yamewekwa barabarani, yakikaa muda mrefu kwenye jua ukiyatumia mafuta hayo basi unapata matatizo ya kansa au magonjwa kadha wa kadha. Naomba Serikali itoe tamko, kwa sababu mafuta hayo ni mengi na yamesambaa katika njia zote, huko kwangu Mbeya na kila mahali. Sasa kama watu wataendelea kuyatumia na kumbe yanaleta kansa na vyombo vya habari vimetangaza kwamba kuna magonjwa kama hayo, ni vizuri Serikali ingewaeleza Wananchi.

Mheshimiwa Spika, siyo hapo tu, siku za nyuma au mwaka jana, walitangaza kwamba, mafuta ya ubuyu pia yana matatizo hayo hayo. Kwamba, ukiyanywa unapata matatizo. Ninaiomba Serikali ichukue nafasi sasa ya kutangaza kutueleza Wananchi, kwa sababu mafuta hayo mpaka sasa hivi

yapo hapo nje yanauzwa. Naomba Serikali iwaeleze Wananchi mafuta hayo yanafaa kutumika au vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mwingine ni kuhusu barabara. Kule kwangu, kwanza niwape pole Wananchi ambao wamepata tabu sana na hasa Wananchi wa Milima ya Mporoto kutoka Isyonje kwenda mpaka Makete, ile barabara ambayo inapita katika Hifadhi maalum kabisa katika nchi hii ni mbaya wala haipitiki, watu wanalala njiani. Naomba pamoja na kwamba, nilimweleza Naibu Waziri na nimejaribu kuongea na watu wa *TANROADS,* lakini bado Wananchi wananipigia simu mno, naomba ile barabara kama nilivyoomba siku zote na kwa sababu ni barabara ambayo inapita katika Mbuga au Hifadhi ya Taifa kwa nini isifanyiwe mpango wa kujengwa iwe barabara ya lami?

Isitoshe hivyo, sehemu hiyo ya Milima ya Mporoto ndiyo sehemu muhimu kwa kilimo cha viazi katika nchi hii. Ukitoka Mporoto mpaka Makete na Njombe ni eneo muhimu sana kwa kilimo cha viazi, lakini barabara ni mbaya mpaka wanashindwa kuvisafirisha na ndiyo maana bei ya viazi inapanda kwa sababu vinachukua muda mrefu njiani. Kwa hiyo, naomba Serikali iifikirie hiyo barabara na siyo tu kwa viazi, kwa sababu ya umuhimu wake kwamba, inapita katika Hifadhi ya Taifa. Naomba Serikali ifikirie kutujengea barabara nzuri ya lami ili watalii wengi waweze kufika kule na Taifa lipate fedha au mapato.

Pia, naomba kuuliza hivi Benki ya Dunia ambayo inashughulikia kufadhili Miradi ya Maji inafanya kazi bado? Kwa sababu ukienda katika Wizara utakuta Waziri anahangaika kutafuta fedha huku na huko; je, hii Benki ya Dunia imesimama kufadhili Miradi hii? Miradi mingi imeanza kutekelezwa na wengine wamefikia 60% mpaka 70%, 30% mpaka 40%, lakini bado hawapati fedha. Hakuna fedha ya kuwalipa Wakandarasi ambao wanatakiwa kumaliza kazi. Naomba bajeti hii iangalie kabisa au kama hakuna bajeti hiyo basi zitafutwe fedha kuhakikisha hii Miradi ambayo tayari imeanza kutekelezwa ikamilike ili tunapoingia mwaka kesho tuone watu wanapata maji. Kwa hiyo, naomba sana kwamba Serikali ingefikiria mambo hayo.

Jambo lingine ambalo naomba nichangie ni kuhusu viwanja vya michezo kwa kila Halmashauri. Inaelekea michezo kweli inatiliwa nguvu lakini bado viwanja tunashindwa kuwa navyo. Ingelikuwa ni vizuri Serikali iweke umuhimu na isisitize kwamba, kila Halmashauri iwe na uwanja wake wa michezo kwa ajili ya Wananchi wake, kuliko ilivyo hivi sasa. Hilo ndiyo ombi langu, naiomba Serikali maana hii kazi siyo kubwa sana ya kutengeneza uwanja wa michezo. Naomba Serikali iliangalie suala hili ili Wananchi wajipatie nafasi ya kwenda kwenye michezo, kila Halmashauri angalau iwe na kiwanja ambacho kitasaidia kuwaweka vijana hao.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kuzungumzie ni upimaji wa viwanja katika Miji. Mbalizi sasa hivi ni Mji Mdogo, naomba Mji ule upimwe ili watu wajenge kwa usahini na kufuata ramani. Isije ikawa baadaye wanajenga holela na kama ilivyotokea Dar es Salaam mafuriko na kadhalika, kwa sababu watu wanajenga holela, hakuna sheria ambayo inazuia na kuwapa nguvu Halmashauri, kila mtu anajenga anavyotaka. Kwa hiyo, naomba Mji wa Mbalizi upimwe viwanja ili unapoendelea na kukua basi uwe na sehemu yake ambayo watu wanaweza kujipatia viwanja wajenge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nasema sitaki nigongewe kengele. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Limbu, atafuatiwa na Mheshimiwa Faith Mitambo, nafikiri Mheshimiwa Dunstan Mkapa atafikiwa.

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia.

Kwanza, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Napenda niishukuru Serikali na hususan Wizara ya Nishati na Madini, kwa kutandaza na kusimika nguzo za umeme pamoja na nyaya kutoka Kisesa katika Jimbo la Magu kupitia Ihushi, kupita Sese, kupita Itandula na Kikundi mpaka Kayenze. Nashukuru sana tayari nguzo zimesimama na nyaya zimepita, tatizo sasa umeme haujashushwa katika vijiji nilivyovitaja vya Ihushi, Sese, Itandula na Kikundi. Naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, usukume hizo nyaya Wananchi wasiendelee kuziona, umeme uweze kushuka.

Pili, naishukuru Serikali kwa kufanya jitihada kubwa za kupatikana fedha kwa ajili ya maji kwa Mji wa Magu. Taarifa nilizonazo, fedha kutoka *European Union* tayari zipo Wizara ya Fedha na mtekelezaji wa Mradi huu ambaye ni MWAUWASA (Mamlaka ya Maji Safi na Majitaka katika Jiji la Mwanza), ndiyo wanatekeleza Mradi wa Maji katika Mji wa Magu. Naiomba Serikali, Mheshimiwa Waziri Mkuu, atoe msukumo Mradi huu utekelezwe haraka. Kama utakumbuka, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ulikuja Uanja wa Magu wa Mwanankanda, ukatoa Hotuba na ukaahidi na Mheshimiwa Rais alikuja na akasema Wananchi wa Magu msimguse Mbunge, hili ni langu sasa nakwenda nalo. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, usaidie kusukuma ahadi hiyo ya kwako na ya Mheshimiwa Rais ili utekelezaji uweze kwenda kasi kwa sababu fedha sasa zipo tayari.

Napenda nishukuru pia jibu la Waziri wa Maji, jana bahati mbaya nilichelewa kufika, ameahidi kwamba, maji ya kwenda katika Kijiji cha

Nyangh'anga, Buhumbi na Iseni, utatekelezwa katika mwaka ujao wa fedha. Mradi huu umekuwa wa muda mrefu sana na ninaamini kwamba, Wananchi wa vijiji hivi vitatu sasa watafurahia ahadi ya Serikali kwamba, mwaka ujao wa fedha Mradi huu utaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la Mkataba wa Ramsar. Kuma Mkataba wa Ramsar, Ramsar ni mji mdogo uliopo Irani. Mkataba huu ulisainiwa mwaka 1971 na nchi yetu ilikuja kuridhia Makubaliano haya ya Kimataifa miaka 30 baadaye, mwaka 2000.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanauwana, wakulima na wafugaji wanauwana. Amezungumza Mheshimiwa John Cheyo hapa kwamba, wakazi wa kutoka mikoa ambayo ina wakazi wengi, hawana maeneo ya kilimo, hawana maeneo ya kuchungia mifugo yao, wanakwenda maeneo mbalimbali, walikwenda mpaka Ihefu wakafukuzwa wakapelekwa Lindi wakapoteza mali nyingi.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna Mkataba huu wa Ramsar, ambao katika nchi yetu umetenga maeneo manne; kuna eno la Kilombero, kuna eneo la Lake Natron, eneo la Malagarasi Myoyovi na Rufiji, Mafia, Kilwa, Ramsar Site.

Mheshimiwa Spika, maeneo haya niliyoyataja chini ya Mkataba huu, kwa pamoja ukiyajumlisha ukubwa wake, ni sawa sawa na nchi hizi ukizijumlisha kwa pamoja; Rwanda, Swaziland, Mauritius, Comoro, Seychelles na Mayote. Eneo hili linalojumuisha tu huu mkataba mmoja wa Ramsar, ujumlishe hizi nchi ninazozitaja, nchi sita, ukubwa wa eneo hili; Rwanda, Swaziland, Mauritius, Comoro, Seychelles na Mayote. Sasa sisi ni matajiri sana wa nchi, wa ardhi, tuna-*afford* kuhifadhi eneo lote hili kwa ajili ya Mkataba wa Ramsar ambao tuliusaini.

Mheshimiwa Spika, sawa, mimi sipingani na uhifadhi, lakini inabidi Mikataba mingine tuiangalie upya. Pale Kilombero kwenye Hifadhi ya Morogoro, kuna mnyama mmoja anaitwa Sheshe, sijui anaitwaje kwa Kizungu, sijui Puku, sijui kitu gani. Watu wanakufa, wanakosa mahali pa kuchungia kwa sababu tu ya mnyama mdogo anaitwa Sheshe mmoja na faida yake kimataifa sijaijua vizuri ni nini hasa. Mheshimiwa Waziri Mkuu, watu walipigana wakauwana na uliahidi kwenda kuusuluhisha mgogoro ule, kwa sababu kuna watu waliotoka Mwanza, wametoka Shinyangana sehemu nyingine wako kule na kuna wengine wameuwawa na wengine wamepoteza mifugo wanaambiwa mfugo lazima ipungue.

Mheshimiwa Spika, kuna Mikataba mingine haingii akilini. Sisi ni matajiri wa ardhi kiasi kwamba, tunakuwa *so generous* Kimataifa, ku-*commit* ardhi yenye ukubwa wa nchi hizi sita nilizozitaja. Hifadhi katika nchi hii, jumla tuna hifadhi

eneo linalolingana na nchi ya Uganda, nilishalisema hili huko nyuma. Tuna-*conserve* eneo linalolingana na nchi ya Uganda nzima ni hifadhi. Sawa, wakati tunahifadhi wakati ule tulikuwa hatuko wengi, matatizo hayakuwa mengi. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwenye Hotuba yako ukurasa wa 46 mpaka 48, umezungumzia mambo ya ardhi na umeahidi kuyafanyia kazi.

Mojawapo ya mambo ambayo mimi ninashauri; Serikali iliangalie upya suala hili, eneo hili lipunguzwe ili watu wapewe maeneo haya mengine yapunguzwe, wanyama wahamishwe wasogezwe mbali ili wafugaji na wakulima watengewe maeneo. Kila mahali kila siku kuna migogoro ya wakulima na wafugaji. Hivi tumeshindwa na ardhi tunayo kubwa hivi? Tunatenga eneo kubwa kwa ajili ya Ramsar tu, Mkataba mmoja!

Mheshimiwa Spika, mimi haingii akilini kwangu na kwa sababu haingii akili kwangu, naomba niishie hapo. Ahsante kwa kuniruhusu. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Haya! Maana yake umesusa, umefanyaje! *(Kicheko)*

*Okay!* Nilisema nitamwita Mheshimiwa Faith Mitambo, atafuatiwa na Mheshimiwa Dunstan Mkapa.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Awali ya yote, naomba niunge mkono Hotuba hii ya Waziri Mkuu kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, naomba niende ukurasa namba 44 wa Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Katika ukurasa wa 44, *paragraph* ya 60, amezungumzia masuala ya wanayamapori, vilevile amezungumzia mapato yanayotokana na uwindaji na masuala ya vitalu katika Halmashauri 38.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu ametaja kwamba, Halmashauri hizi 38 katika mwaka 2013/2014, zimeweza kupata jumla ya bilioni 8.7 kama mgawo wao wa asilimia 25.

Mheshimiwa Spika, ningependa kufahamu katika hili; Wilaya ya Liwale ni wadau wakubwa sana wa Hifadhi ya *Selous Game Reserve*. Sasa kwenye hizi fedha zilizotajwa hapa bilioni 8.7 ningependa kufahamu Wilaya ya Liwale kama wadau wamepata kiasi gani na pengine atakapofanya *winding-up* ya Hotuba yake, ningependa kujua ametumia *criteria* gani katika kugawa hizi pesa.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 52 Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia masuala ya mawasiliano na takwimu zake zimeonesha kwamba, katika Sekta ya Mawasiliano kuna *improvement*. Amezungumza kwamba, mwaka 2005 Watanzania waliweza kumiliki jumla ya *line* za simu milioni

2.96, lakini kufikia 2013 Watanzania wamemiliki *line* za simu milioni 27.45. Mimi nimeshindwa kuelewa kama kweli kwa kumiliki simu kunaonesha *improvement* yoyote katika Sekta ya Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wengi sana na hasa katika Wilaya yangu ya Liwale, wanamiliki *sim cards*, hizi *line* za simu, lakini wako vijijini na katika maeneo ambayo wanakaa wanamiliki *lines* za simu lakini hakuna mawasiliano. Watanzania wengine pia wanamiliki simu wakiwa vijiji lakini maeneo wanayokaa hayana mawasiliano. Wanatumia *sim cards* zile siku zote zinakaa mfukoni na simu zao walizonunua zinakaa mfukoni, wanazitumia tu wanapofika maeneo ya mjini ambako kuna mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, sasa ningependa kumwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na takwimu zake nzuri hizi, bado niendelee kumwomba kwamba, aendelee kutia mkazo kwenye Sekta hii ya Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, tunaenda ukurasa wa 55, Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia mafanikio yaliyopatikana katika ujenzi wa barabara na vilevile ujenzi wa madaraja. Mimi nafikiri ni sawa kabisa takwimu alizotoa ni kweli, lakini kwa upande wa Liwale wakisikia takwimu hizi ninazozizungumzia masuala ya madaraja, masuala ya barabara, kwa kweli hawataelewa.

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Nangurukuru kwenda Liwale na barabara ya kutoka Liwale kwenda Nachingwea hazipitiki kabisa, hali yake ni mbaya sana. Mimi mwenyewe nimepita kwenye barabara hizi hivi karibuni na nilipita kusudi kutokea Nangurukuru kwenda Liwale, nimekwama nimekaa porini muda wa siku mbili, magari hayapiti kabisa. Sasa takwimu hizi kidogo kwa sisi hazitufurahishi, tunaendelea kuiomba Serikali iendelee kuongeza nguvu na hasa katika Sekta hii ya Ujenzi na hasa Mawasiliano ya Barabara.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye masuala ya elimu: Masuala ya elimu vilevile yametolewa pale takwimu, maendeleo ya Sekta ya Elimu wamezungumzia. Mimi nataka nizungumzie hasa Idara ya Sekondari. Idara ya Sekondari wamezungumzia kwamba, kumekuwa na *improvement* ya upelekaji wa vitabu, *improvement* ya upelekaji wa vifaa vya maabara na mambo kadha wa kadha. Ninakubaliana labda kwa upande wa walimu, lakini kuna sekondari ambazo mwanafunzi hata ukimwambia *test tube* sasa hivi haijui, hata ukimwambia *burette* haifahamu.

Leo mnazungumza kwamba mnapeleka vifaa vya maabara vya kutosha kwa sekondari, sekondari hizi ni zipi? Sekondari nyingi sasa hivi zinafanya *alternative to practical* badala ya kufanya *practical* kwa sababu vifaa vya maabara hakuna. Sasa mimi ninakataa kabisa *statement* hii.

Mheshimiwa Spika, twende kwenye shule zile ambazo zilikuwa *giant schools* miaka ile tunazifahamu, nimeongea hili nimeongea na kuongea. Shule zile ambazo zilikuwa *giant schools* mimi ningeomba zingerudi Wizara ya Elimu, kwa sababu sasa hivi zina mazingira mabaya mno, siyo zile tunazozifahamu.

Kwa nini zile shule zote zenye *"A" Level,* kuanzia *Form One* mpaka *Form Six* tusizirudishe Wizara ya Elimu, tubakiwe na zile shule zingine zinazobakia. Shule hizi zina hali mbaya pamoja na ripoti hii iliyoandikwa hapa, pamoja na takwimu hizi zilizoandikwa hapa, tukichukua hali halisi ya shule zote, acha shule ambazo zina *"A" Level*, hata shule zetu za Kata. Mimi ni Mbunge wa Jimbo, nina shule 16 kwangu na ninatembelea kila shule, hakuna hivyo vifaa vya maabara, mnapeleka wapi mbona mimi sivioni? Mnapeleka bajeti ya milioni moja kununua vifaa vya maabara, mnapeleka bajeti ya milioni moja kununua vitabu; watanunua vitu gani?

Mheshimiwa Spika, bado ninaendelea kupingana na suala hili, ninamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aendelee kusimamia Sekta hii ya Elimu, pamoja na Mawaziri wanaohusika na Elimu na Mawaziri wa TAMISEMI. Bado ni kweli takwimu hizi zinawekwa hapa, lakini hali halisi iliyoko kwenye sekondari zetu za kule vijijini haiko sawa sawa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa asilimia 100. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Dunstan Mkapa, ndiye wa mwisho kwa leo. Mheshimiwa Mkapa yupo?

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Yupo!

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba na mimi nitoe shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Awali ya yote, naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali katika suala zima la miundombinu katika Wilaya yangu ya Nanyumbu. Kumejengwa barabara ya lami kutoka Masasi mpaka Mangaka, niliomba barabara ya lami kutoka Mangaka mpaka Mtambaswala, mkandarasi yuko *site*. Niliomba vilevile barabara ya kutoka Mangaka kwenda Tunduru, mkandarasi yuko *site* na zote hizi zitajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kuna barabara moja ambayo Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ijengwe kutoka pale Nangomba kwenda Nanyumbu kwa kiwango cha

lami. Naiomba sana Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, kabla Mheshimiwa Rais hajamaliza muda wake, barabara hii ijengwe.

Mheshimkiwa Spika, pamoja na hayo, barabara hizi ambazo zinajengwa sasa hivi za kutoka Mtambaswala kwenda Mangaka na Mangaka kwenda Tunduru bado Wananchi hawajalipwa fidia. Wamenituma kwamba, Mbunge tunaomba ukatuulizie hizi fidia tutalipwa lini wakati mkandarasi amekwishafika *site* na sisi hatuwezi kuhama mpaka tulipwe fidia zetu na ndipo tuweze kuondoka.

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba kuishukuru Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini, kwa kutuletea umeme wa uhakika katika Wilaya yetu ya Nanyumbu. Shahidi mkubwa atakuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye alikuja pale kwa ajili ya uzinduzi wa Mradi huu. Na mimi naishukuru sana Serikali kwa niaba ya Wananchi wa Nanyumbu.

Mheshimiwa Spika, kumetokea tatizo dogo ambalo ni kubwa kwa Wananchi wa kawaida kwamba, sasa hivi gharama za kuunganisha umeme wanalalamika kwamba zimepanda na kufikia hadi laki nne. Kwa Mwananchi wa kawaida kuweka nguzo kufikia laki nne kwa kweli hataweza. Naomba sana Wizara ya Nishati ya Madini kupitia Waziri Mhongo, atusaidie kupunguza gharama hizi ili Wananchi wa kawaida waweze kuzimudu.

Mheshimiwa Spika, tatizo la maji: Naishukuru tena Serikali kwa kutuletea baadhi ya Miradi katika Vijiji vya Nandembo, Chivirikiti, Chipuputa, Lukwika na Sengenya ambako sasa hivi kuna Miradi ya Maji. Bado tatizo ni kubwa hasa katika Vijiji vya Nangomba, Nakopi, Michiga, Likokona na Mikangaula. Hapo Mikangaula kulikuwa na Mradi wa *TASAF* wa kujenga bwana, lakini naona ule Mradi sasa hivi umekufa na Wananchi hawajui hatima yao kuhusu upatikanaji wa maji katika Kata hiyo ya Mikangaula.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa walimu na miundombinu mingine mingine ya elimu: Hata Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Ripoti yake ameliona tatizo hili, amesema ukaguzi pia umebaini kuwa shule za msingi na za sekondari zina upungufu wa walimu ambao huathiri sana ubora wa elimu.

Tatizo hili katika Wilaya yangu ya Nanyumbu ni kubwa sana, ndiyo maana kiwango cha elimu kiko duni kwa sababu kuna uhaba mkubwa wa walimu, kuna uhaba mkubwa wa madarasa, kuna uhaba mkubwa wa nyumba za walimu na kuna uhaba mkubwa wa madawati. Yote haya yanasababisha kushuka kwa kiwango cha elimu katika Wilaya ya Nanyumba. Vilevile ukosefu wa *hostel* za wanafunzi hasa wasichana, umesababisha watoto wengi kupata mimba; wengi wanapanga mitaani, huko wanarubuniwa, kuna vishawishi vingi.

Kwa hiyo, naiomba sana Serikali ilione jambo hili ili iweze kutujengea *hostel* za wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, afya: Tuna uhaba mkubwa wa zahanati. Tuna vituo vya afya vitatu katika Wilaya nzima na zahanati 15. Naomba kupitia Bunge lako Tukufu, nimshukuru Balozi wa Japani, kwa sababu niliwaomba wanijengee zahanati moja, wamenikubalia na ujenzi umeanza katika Kijiji cha Chipuputa. Naishukuru sana Serikali ya Japani na Mungu awabariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, posho za Madiwani zimesemwa hapa, lakini napendekeza sasa waanze kulipwa mishahara minono angalau inayofanana fanana na Udiwani. Pia posho kwa Watendaji wa Vijiji na wa Vitongoji, imezungumzwa hapa na Mheshimiwa Profesa Msolla, amezungumzia jinsi wanavyosaidia watu hawa katika Vijiji vyetu na Vitongoji vyetu.

Mheshimiwa Spika, *ceiling* kwenye bajeti: Kwenye bajeti kuna kitu kinaitwa *ceiling*. Mimi sioni sababu, naona kuna uharibifu mkubwa wa fedha watu wanaanzia vijijini mpaka Halmashauri, Halmashauri wanakuja mpaka Dar es Salaam wanajifungia huko maofisini, sijui wanakaa hotelini, pesa nyingi, mafuta yanatumika, lakini mwisho wa siku unaambiwa *ceiling* yako hii hapa. Kwa nini wasipelekewe tu *ceiling* wakaanza kupanga bajeti yao kutokana na hiyo *ceiling*? Ni gharama kubwa mno. *(Makofi)*

Nimekuta pale Dar es Salaam karibu Wilaya zote ziko pale, Halmashauri zote, lakini baadaye wanaambiwa wewe *ceiling* yako hii hapa. Faida yake nini? Tunapoteza muda, tunapoteza rasilimali, lakini mwisho wa siku tunapewa kiduchu. Kwa hiyo, naomba sana Serikali sasa hivi iangalie tuanzie kwenye *ceiling* ndiyo turudi chini.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, nashukuru.

Waheshimiwa Wabunge, nashukuru sana kwa kazi mliyoifanya kwa siku ya leo. Kinachohitajika daima katika siasa ni uvumilivu. Kujitia ushabiki wa kelele tu haisaidii, ni vizuri kuwa na uvumilivu, maana ukisema ujue na wenzio watajibu. Sasa hili nalo mlielewe, uwe na moyo wa kukubali, unayoyasema utajibiwa, ndiyo utaratibu.

Sasa naomba tuelewane kitu kimoja; kuna wengi walikuwa wanaomba kutoa taarifa wakati mzungumzaji mmoja mmoja alikuwa anazungumza, sikuwapa nafasi mpaka baadaye alimaliza. Unajua dakika saba ukimwingilia mtu, utavuruga hata kile anachotaka kukisema na taarifa ni ya kwako wewe wala siyo lazima umwingilie mtu. Kwa hiyo, ndiyo maana mimi nitakuita baada

ya mzungumzaji kumaliza, maana dakika zake saba amejenga hoja yake amemaliza, wewe toa taarifa yako, sawa. Kusema nitaruhusu, dakika zile ni chache, ukim-*interrupt* mno katika dakika tano, kwa kweli yule atapoteza hata anachotaka kukisema hataeleweka. Kwa hiyo, tuvumiliane kwa mtindo huo, hatuna muda wa kutosha. *(Makofi)*

Kwa sababu sasa hivi tunamhoji *Prime Minister* kila kitu tunachotaka siku tatu, kesho hakuna kipindi cha maswali ya *Prime Minister* asubuhi, mtaendelea kumhoji hapa hapa wote kadiri mnavyotaka dakika saba saba. Kwa hiyo, kesho msije mkaamka usiku, kipindi kile hakitakuwepo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru tena, niwatakie jioni njema. Ahsante sana kwa uvumilivu na mjadala mzuri. Tuonane kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.00 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,*
*Tarehe 8 Mei, 2014 Saa Tatu Asubuhi)*